ISO 9001:2015 Certified

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI
MACHI 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ukaguzi House, 4 Barabara ya Mahakama, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya upepo "Ukaguzi" Simu: +255 (026) 2161200-9, Barua pepe: ocag@nao.go.tz Tovuti: www.nao.go.tz

**Kumb. Na. CGA.319/421/01** **27 Machi 2025**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma.

Nawasilisha kwa unyenyekevu,

**Charles E. Kichere**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Mamlaka**

Mamlaka na majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu zinazoimarisha Imani kwa Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Kauli Mbiu**

Kuwa Taasisi yenye kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

## Misingi ya Maadili

**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo:** Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo

**Kufanya kazi kwa uadilifu:** Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadilina sheria katika utoajiwa huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo:** Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi staiki

**Kufanya kazi kwa utaalam:** Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi** Tunahimiza, kuvumbua na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwaajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa ushirikiano:** Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje

# YALIYOMO


KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI .......... i

YALIYOMO .......... ii

ORODHA YA MAJEDWALI .......... iv

ORODHA YA VIELELEZO .......... vii

ORODHA YA VIAMBATISHO .......... viii

VIFUPISHO .......... ix

SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI xiii

MUHTASARI .......... xv

SURA YA KWANZA .......... 1

MAELEZO YA AWALI .......... 2

SURA YA PILI .......... 3

HATI ZA UKAGUZI .......... 4

SURA YA TATU .......... 6

HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA .......... 7

SURA YA NNE .......... 10

MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI .......... 11

SURA YA TANO .......... 16

USIMAMIZI WA MAPATO NA DENI LA SERIKALI .......... 17

SURA YA SITA .......... 32

USIMAMIZI WA UNUNUZI .......... 33

SURA YA SABA .......... 50

SEKTA YA MIUNDOMBINU .......... 51

SURA YA NANE .......... 63

SEKTA YA MAJI .......... 64

SURA YA TISA .......... 83

SEKTA YA AFYA .......... 84

SURA YA KUMI .......... 92

SEKTA NYINGINE .......... 93

SURA YA KUMI NA MOJA .......... 106

USIMAMIZI WA MIFUKO MAALUMU NA MIFUKO MINGINE....................... 107
SURA YA KUMI NA MBILI ............................................................ 117
BALOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI .............................................. 118
SURA YA KUMI NA TATU ............................................................ 126
USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU, MISHAHARA NA MAFAO YA WASTAAFU .. 127
SURA YA KUMI NA NNE ............................................................... 141
USIMAMIZI WA MALI ................................................................. 142
SURA YA KUMI NA TANO ............................................................ 151
MAJUKUMU YA UTAWALA NA UANGALIZI...................................... 152
SURA YA KUMI NA SITA.............................................................. 162
VYAMA VYA SIASA..................................................................... 163
VIAMBATISHO.......................................................................... 170

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za Ukaguzi ........................................ 5

Jedwali Na. 2: Hali ya utekelezaji kwa Wizara, Idara na Wakala na Vyama vya Siasa ........................................ 8

Jedwali Na. 3: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ........................................ 8

Jedwali Na. 4: Mapendekezo ya Ukaguzi Yaliyobaki kwa Muda Mrefu ........................................ 9

Jedwali Na. 5: Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ........................................ 9

Jedwali Na. 6: Utendaji wa Bajeti ........................................ 12

Jedwali Na. 7: Uchambuzi wa Makusanyo ya Ndani ........................................ 12

Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa Mikopo ........................................ 13

Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Makusanyo ya Kodi Tanzania Bara ........................................ 17

Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa Makusanyo ya Kodi Zanzibar ........................................ 18

Jedwali Na. 11: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ........................................ 20

Jedwali Na. 12: Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa la Tanzania na Nchi Zingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Minne ........................................ 21

Jedwali Na. 13: Kesi za Kodi Ambazo Hazijatatuliwa Tanzania Bara ........................................ 23

Jedwali Na. 14: Kesi za Kodi Zilizopo katika Mahakama za Kodi Zanzibar ........................................ 23

Jedwali Na. 15: Kutokuzingatia Sheria za Kodi ........................................ 27

Jedwali Na. 16: Taasisi Zilizokusanya ya Mapato Nje ya Mfumo wa Mapato ... 28

Jedwali Na. 17: Mwenendo wa deni la Ndani ........................................ 30

Jedwali Na. 18: Mwenendo na Mseto wa Deni la Nje ........................................ 30

Jedwali Na. 19: Orodha ya Taasisi zenye Miradi Iliyotelekezwa ........................................ 35

Jedwali Na. 20: Orodha ya Taasisi zenye Miradi Iliyocholewa Kuanza ........................................ 36

Jedwali Na. 21: Orodha ya Taasisi zenye Malipo ya Awali Yasiyo na Dhamana 37

Jedwali Na. 22: Taasisi zilizofanya Ununuzi bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni ........................................ 41

Jedwali Na. 23: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi Mdogo bila taarifa kwa bodi ya zabuni ........................................ 41

Jedwali Na. 24: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi kwa Kutoa Zabuni kwa Wazabuni Maalumu na Njia ya Mzabuni Mmoja Bila Kuwa na Sababu Mahsusi za Kutumia Njia Hizo ........................................ 43

Jedwali Na. 25: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi bila Mikataba ........................................ 44

Jedwali Na. 26: Taasisi zilizokuwa na Mikataba Isiyopekuliwa na Wanasheria 45
Jedwali Na. 27: Orodha ya Taasisi ambazo Zimechelewa Kupokea bidhaa .... 47
Jedwali Na. 28: Bodi za Mabonde ya Maji Zilizo na Vibali vya Matumizi ya Maji Vilivyoisha Muda Wake ........ 66
Jedwali Na. 29: Mamlaka za Maji zilizoshindwa kukidhi Mahitaji ya Maji kwa Wateja ........ 67
Jedwali Na. 30: Maji Yasiyozalisha Mapato ........ 68
Jedwali Na. 31: Wateja Wasio na Mita za Kupima Maji ........ 69
Jedwali Na. 32: Upungufu wa Usambazaji wa Maji ........ 72
Jedwali Na. 33: Upungufu katika Miundombinu ya Usambazaji wa Maji ....... 72
Jedwali Na. 34: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vyenye kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ........ 73
Jedwali Na. 35: Orodha ya CBWSOs zenye Gharama za Uendeshaji Zilizozidi Mapato ........ 74
Jedwali Na. 36: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji ambavyo Havikufikia Lengo la Kusambaza Maji Vijijini ........ 77
Jedwali Na. 37: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji visivyofunga mita za maji........ 78
Jedwali Na. 38: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji visivyofanya vipimo vya ubora wa maji ........ 80
Jedwali Na. 39: Ucheleweshaji wa kulipwa kwa madai ya mfuko wa taifa wa bima ya afya ........ 87
Jedwali Na. 40: Kutoteketezwa kwa Dawa Zilizopita Muda ........ 89
Jedwali Na. 41: Hospitali za Rufaa za mikoa zilizo na Wataalamu wa Afya bila Leseni za Kufanya Kazi ........ 90
Jedwali Na. 42: Watoahuduma bila Leseni Halali ........ 90
Jedwali Na. 43: Ada/Tozo za Mafuta kwa mwaka 2023/24........ 107
Jedwali Na. 44: Fedha za Ukarabati Zilizotumwa Balozini ........ 122
Jedwali Na. 45: Mwenendo wa Ulipaji wa Kodi za Pango kwa Miaka Mitatu . 124
Jedwali Na. 46: Orodha ya Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Makato ya Kisheria ya Mishahara ........ 128
Jedwali Na. 47: Orodha ya Taasisi Zilizoshindwa Kufanya Programu za Utangulizi na Uelekezaji ........ 129
Jedwali Na. 48: Orodha ya Taasisi Zenye Taarifa Zisizo Sahihi za Watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS)........ 131

Jedwali Na. 49: Orodha ya Taasisi zenye Watumishi Wanao Kaimu katika Nafasi ya Uongozi kwa Zaidi ya Miezi Sita ............................................... 132

Jedwali Na. 50: Orodha ya Taasisi zisizo na Muundo wa Utumishi ulioidhinishwa ............................................................................... 134

Jedwali Na. 51: Orodha ya Taasisi Zenye Masurufu Yasiyorejeshwa .......... 136

Jedwali Na. 52: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa .............. 137

Jedwali Na. 53: Majalada yaliyochelewa kuandaliwa na kuwasilishwa ....... 139

Jedwali Na. 54: Taasisi zenye Mali Zisizokuwa na Nambari ya Utambulisho. 143

Jedwali Na. 55: Balozi zenye Mali zisizokuwa na Nambari ya Utambulisho .. 144

Jedwali Na. 56: Balozi ambazo hazikuongeza au kurekodi mali za Serikali katika Mfumo ................................................................... 145

Jedwali Na. 57: Orodha ya Taasisi zenye Viwanja Vinavyokosa Hati Miliki .. 147

Jedwali Na. 58: Mali zilizokabidhiwa kwa serikali ambazo hazijafanyiwa maamuzi ................................................................... 148

Jedwali Na. 59: Majengo chakavu katika Hospitali na Balozi .................. 149

Jedwali Na. 60: Taasisi Zisizo na Bodi za Usimamizi ............................ 153

Jedwali Na. 61: Taasisi zenye Bodi Zilizokwisha Muda wake ................... 153

Jedwali Na. 62: Taasisi zisizo na Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi ....... 156

Jedwali Na. 63: Orodha ya Mamlaka zisizo na Wakurugenzi Watendaji ...... 157

Jedwali Na. 64: Taasisi zenye Idadi Ndogo ya Vikao vya Bodi................. 159

Jedwali Na. 65: Taasisi zenye Upungufu katika Kamati za Ukaguzi ........... 160

Jedwali Na. 66: Vyama vya Siasa Vilivyokusanya Mapato Pungufu ............ 164

Jedwali Na. 67: Vyama vya Siasa ambavyo Havikuwasilisha kwenye Akaunti za Benki Michango ya Wanachama Wake............................................ 165

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Matumizi ya Serikali kulingana na Wapokeaji .................. 14
Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Matumizi ya Serikali kwa Makundi ............ 14
Kielelezo Na. 3: Makusanyo ya Kodi Tanzania Bara ................................ 18
Kielelezo Na. 4: Makusanyo Halisi ya Kodi Zanzibar ............................... 19
Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa ............. 20
Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali ........................ 29

## ORODHA YA VIAMBATISHO


Kiambatisho Na. I: Hati za Ukaguzi na Hitimisho la Utekelezaji wa Sheria .. 170

Kiambatisho Na. II: Taasisi Zilizopokea Fedha Zaidi ya Bajeti ................ 185

Kiambatisho Na. III: Malipo yasiyo na Idhini ya Mabadiliko ya Bajeti ......... 186

Kiambatisho Na. IV: Madeni ya Mapato Yasiyokusanywa ........................ 188

Kiambatisho Na. V: Orodha ya Taasisi zenye Madeni kwa Kazi Zilizofanyika 189

Kiambatisho Na. VI: Taasisi zenye Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Miradi..... 198

Kiambatisho Na. VII: Taasisi Zisizokuwa au Kuzingatia Mipango ya Ununuzi. 200

Kiambatisho Na. VIII: Ununuzi bila Kutumia Mfumo wa Kielekitroni .......... 201

Kiambatisho Na. IX: Ankara za Maji Zisizokusanywa............................ 203

Kiambatisho Na. X: Upotevu wa Mapato Kutokana na Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Afya ............................................................. 206

Kiambatisho Na. XI: Mapato Yasiyokusanywa kutoka kwa Kampuni za Bima ya Afya na Mifuko ya Fidia.......................................................... 207

Kiambatisho Na. XII: Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mradi wa BBT 2023/24 ............................................................ 209

Kiambatisho Na. XIII: Orodha ya Magari na Vifaa Chakavu Balozini ........... 210

Kiambatisho Na. XIV: Taasisi zenye Madeni ya Watumishi...................... 212

Kiambatisho Na. XV: Orodha ya Taasisi Zenye Nafasi za Kazi Zilizo Wazi.... 220

Kiambatisho Na. XVI: Taasisi Zisizokuwa na Mpango wa Matengenezo ya Mali ........................................................................ 221

Kiambatisho Na. XVII: Ofisi za Balozi Zisizokuwa na Mpango wa Matengenezo ya Mali ....................................................................... 223

Kiambatisho Na. XVIII: Mali Zisizotumika na Zilizochakaa bila Kufanyiwa Matengenezo wala Kuuzwa ..................................................... 223

Kiambatisho Na. XIX: Taasisi ambazo Hazikuweka au Kurekodi Mali Zao Kwenye Mfumo....................................................................... 225

Kiambatisho Na. XX: Taasisi Zenye Upungufu katika Usimamizi wa Viatarishi ........................................................................ 227

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| AGITF | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo |
| APRM | Mpango wa Kujitathmini wa Nchi za Afrika |
| BAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Babati |
| BBT-YIA | Jenga Kesho iliyo Bora- Uanzishaji Kilimobiashara kwa Vijana |
| BITs | Mikataba ya Uwekezaji baina ya Nchi mbili |
| BOQ | Jedwali la Mchanganuo wa Kazi na Bei |
| BRELA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| CAP | Sura |
| CAT | Mahakama ya Rufaa |
| CBMS | Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti Kuu |
| CBWSO | Chombo cha Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii |
| CFS | Hesabu Jumuishi za Serikali |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama cha Ukombozi wa Umma |
| CUF | Chama cha Wananchi |
| DCEA | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya |
| DLUFPs | Mifumo ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya |
| DVTCs | Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya |
| DM | Demokrasia Makini |
| DMI | Chuo Cha Bahari Dar es Salaam |
| DP | Democratic Party |
| DPP | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| DRC | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo |
| EFD | Mashine ya Kutoa Risiti za Kielektroniki |
| EMDF | Mfuko wa Maendeleo ya Uchimbaji Madini |
| ETS | Stempu za Kielekitroni za Kodi |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| FAO | Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GDP | Pato la Taifa |
| GePG | Mfumo wa Serikali wa Kukusanya Mapato |
| GN | Tangazo la Serikali |
| HCMIS | Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu |
| ICC | Chama Cha Kimataifa cha Biashara |
| ICHF | Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii Iliyoboreshwa |
| ICSID | Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji |
| ICU | Kitengo cha Uangalizi Maalumu wa Wagonjwa |

| | |
|---|---|
| IFAD | Shirika la Kimataifa la Fedha kwa Maendeleo ya Kilimo |
| IWRM | Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Pamoja |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| JPY | Fedha ya Kijapani |
| JWTZ | Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania |
| LGA | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| MCT | Baraza la Madaktari |
| MDAs | Wizara, Idara na Wakala |
| MFA&EAC | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| MNRT | Wizara ya Maliasili na Utalii |
| MoM | Wizara ya Madini |
| MoU | Mkataba wa Maelewano |
| MT | Kipimo cha Uzito Katika Mfumo wa Metri |
| MTEF | Mfumo wa Bajeti wa Muda wa Kati |
| MUSE | Mfumo wa Uhasibu Serikalini |
| Na. | Namba |
| NCC | Baraza la Taifa la Ujenzi |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| NGOs | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NIDA | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| NIDC | Kituo cha Taifa cha Utunzaji Data na Mfumo kwa njia ya Kimtandao |
| NIRC | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| NRW | Maji Yasiyo na Mapato |
| NWF | Mfuko wa Taifa wa Maji |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| OBGY | Daktari wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi |
| OMC | Kampuni za Uagizaji wa Mafuta |
| OSHA | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi |
| OWM-KVAU | Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira, na Watu Wenye Ulemavu |
| PAC | Kamati ya Hesabu za Serikali |
| PAPs | Watu Walioathiriwa na Mradi |
| PBPA | Mamlaka ya Ununuzi wa Pamoja wa Mafuta ya Petroli |
| PMG | Mlipaji Mkuu Serikalini |
| PMO | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| POPI | Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji |
| PO-PSMGG | Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| PSSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma |

| | |
|---|---|
| RAS | Katibu Tawala wa Mkoa |
| R. E | Toleo Lililohuhishwa |
| REA | Wakala wa Nishati Vijijini |
| RFB | Bodi ya Mfuko wa Barabara |
| RITA | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini |
| RRH | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa |
| RUWASA | Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini |
| RVTC | Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa |
| Sh. | Shilingi ya Kitanzania |
| SOPs | Kanuni na Taratibu za Uendeshaji |
| SQA | Udhibiti Ubora wa Shule |
| STAMICO | Shirika la Madini la Taifa |
| TAA | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania |
| TACAIDS | Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania |
| TAEC | Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania |
| TAHPC | Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala |
| TAMISEMI | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TANROADS | Wakala wa Bararaba Tanzania |
| TARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini |
| TASAC | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TBA | Wakala wa Majengo Tanzania |
| TEITI | Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia |
| TEMESA | Wakala wa Ufundi na Umeme |
| TFS | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| TOR | Hadidu Rejea |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TRAB | Bodi ya Rufaa ya Kodi |
| TRAT | Tume ya Rufaa ya Kodi |
| TVCs | Vocha za Hazina |
| TWPF | Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania |
| UDP | United Democratic Party |
| UMD | Union for Multiparty Democracy |
| UNESCO | Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| USD | Dola za Marekani |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| VLUFPs | Mifumo ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji |
| WCF | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi |

| | |
|---|---|
| WFP | Shirika la Chakula Duniani |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| WSSA | Mamlaka za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira |

## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti Kuu ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Ripoti hii inatoa tathmini ya taarifa za fedha, uzingatiaji wa sheria, na ufanisi wa kiutendaji wa taasisi za Serikali Kuu, ikiwemo Wizara, Idara, Wakala za Serikali, Mfuko Mkuu wa Hazina, pamoja na taasisi nyingine za umma.

Ninapongeza Serikali, chini ya uongozi wa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kujitoa kwake kuimarisha uwajibikaji, uwazi, na ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma. Pia, natoa shukrani zangu kwa uongozi wa taasisi zilizokaguliwa kwa kushirikiana nasi na kutoa taarifa muhimu zilizowezesha kukamilisha ukaguzi huu.

Matokeo na mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii yamelenga kuboresha utawala bora, nidhamu katika usimamizi wa fedha, na uzingatiaji wa mifumo ya sheria inayotumika. Ingawa ninatambua juhudi zilizofanywa na baadhi ya taasisi kuboresha nidhamu katika usimamizi wa fedha, nimebaini maeneo muhimu yanayohitaji hatua za haraka katika mifumo ya ndani ya udhibiti, utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato, ununuzi, na usimamizi wa deni la serikali.

Ninawasihi maafisa masuuli, bodi, na mamlaka za usimamizi kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti, kupunguza athari za vihatarishi, na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, nalisihi Bunge na wadau wengine muhimu kuyatumia matokeo yaliyomo katika ripoti hii kuboresha usimamizi wa fedha za umma, miundo ya utawala, na kuhakikisha uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kutekeleza jukumu lake la kikatiba kwa kiwango cha juu cha taaluma, uhuru, na uadilifu ili kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na manufaa ya wananchi wote.

Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kujituma na kutumia taaluma yao katika kusaidia ukamilishaji wa ukaguzi.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## MUHTASARI

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Inahusisha tathmini ya kifedha na kiutendaji kwa Wizara, Idara, Wakala 532, Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, Vyombo vya Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii, pamoja na taasisi nyingine za sekta ya umma. Ripoti hii imebainisha changamoto na mapendekezo ili kuboresha usimamizi na uwajibikaji.

### (i) Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya hati za ukaguzi 532 zilitolewa. Kati ya hati hizo, hati 531 (99.8%) zilikuwa hati zinazoridhisha, na moja (0.2%) ilipata hati mbaya.

### (ii) Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Miaka ya Nyuma Pamoja na Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka iliyopita ilibaini kuwa kati ya mapendekezo 8,430, mapendekezo 2,893 (34%) yalitekelezwa kikamilifu, 3,513 (42%) yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, 880 (10%) hayakutekelezwa, na 1,144 (14%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati au yalijirudia katika ukaguzi wa mwaka huu.

Uhakiki wa utekelezaji wa maagizo 123 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ulionesha kuwa maagizo 31 (25%) yalitekelezwa kikamilifu, 91 (74%) yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, na moja (asilimia moja) haikutekelezwa.

### (iii) Uandaaji na Utekelezaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Serikali ilikusanya Sh. trilioni 46.503, zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 44.388, ikiwa ni ongezeko la makusanyo ya Sh. trilioni 2.115. Hii ni sawa na ongezeko la 11% ikilinganishwa na Sh. trilioni 41.880 zilizokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2022/23.

Kati ya kiasi kilichokusanywa, makusanyo ya ndani yanayotokana na kodi, makusanyo yasiyotokana na kodi, na makusanyo ya serikali za mitaa yalichangia bajeti kwa Sh. trilioni 29.933 (64%). Kiasi kilichobaki cha Sh. trilioni 16.570 (36%) kilitokana na misaada na mikopo.

### (iv) Usimamizi wa Mapato na Deni la Serikali

Tathmini ya mapato ya kodi kwa mwaka wa fedha 2023/24 ilibaini kiasi cha Sh. bilioni 609.77 bilioni hakikukusanywa kutokana na matumizi ya viwango vilivyopitwa na wakati vya Ushuru wa Bidhaa kwa vinywaji baridi vyenye kaboni. Aidha, ukaguzi wa mafuta yaliyotangazwa kusafirishwa kupitia bomba la TAZAMA ulibaini kuwa lita 14,459,706.19 za mafuta zenye thamani ya Sh. bilioni 12.55 hazikufika kwenye maeneo yaliyokusudiwa, hali hii inaongeza uwezekano wa uuzaji wa mafuta hayo ndani ya nchi usio halali bila kulipwa kodi.

Vilevile, deni la Serikali, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024 lilikuwa Sh. trilioni 97.35, likijumuisha deni la ndani la Sh. trilioni 31.95 na deni la nje la Sh. trilioni 65.40, likiongezeka kutoka Sh. trilioni 82.25 trilioni katika mwaka wa fedha 2022/23. Ingawa Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ya mwezi Desemba 2024 inathibitisha kuwa deni la serikali la Tanzania bado linahimilika, baadhi ya viashiria kama uwiano wa kulipa deni na mauzo ya nje (11.7%) na uwiano wa deni na mapato (14.5%) vinakaribia viwango vya ukomo vya 15% na 18% mtawalia.

### (v) Usimamizi wa Ununuzi

Ukaguzi wangu wa ununuzi na usimamizi wa mikataba kwa mwaka wa fedha 2023/24 ulibaini upungufu wa kimfumo, usimamizi usioridhisha wa fedha, na ukosefu wa uangalizi madhubuti, hali iliyosababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi, kuongezeka kwa gharama, na hasara kubwa za kifedha.

Taasisi za umma zilikuwa na madai ya malipo yasiyolipwa yenye jumla ya Sh. trilioni 4.56, ambapo Sh. trilioni 3.53 zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, jambo lililosababisha ucheleweshaji wa miradi na migogoro ya kisheria. Wizara ya Ujenzi (Fungu Na. 98) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) zilikuwa na madai yanayotokana na riba ya Sh. bilioni 55.55 kutoka kwa wakandarasi kutokana na ucheleweshaji wa malipo, hali iliyoathiri matumizi ya fedha za umma.

Usimamizi usioridhisha wa mikataba uliathiri miradi 136 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.34, huku ucheleweshaji ukiwa kati ya 1% hadi 92%. Aidha, miradi 41 yenye thamani ya Sh. bilioni 558.63 iliachwa bila kukamilika kutokana na upungufu wa fedha, matatizo ya kifedha kwa wakandarasi, na mipango duni ya utekelezaji wa miradi. Malipo ya awali yenye jumla ya Sh. bilioni 141.09 pia

yalicheleweshwa, jambo lililozuia utekelezaji wa miradi na kusababisha madai kuongezeka.

Vilevile, nilibaini ucheleweshaji wa malipo ya fidia yenye jumla ya Sh. bilioni 27.81 kwa watu walioathiriwa na miradi (PAPs), hali iliyosababisha kusimama kwa miradi ya miundombinu na kuiweka serikali katika hatari ya kesi za kisheria na gharama za riba za ziada. Pia, Sh. bilioni 20.67 za malipo ya awali yasiyo na dhamana kwa miradi ya maji ziliongeza hatari ya kifedha kutokana na usimamizi duni wa mikataba.

### (vi) Sekta ya Miundombinu

Nilibaini kufanyika kwa upembuzi yakinifu usioridhisha kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kulisababisha kuvunjwa kwa mkataba wa Sh. bilioni 38.36 kwa barabara ya Ibanda-Kiwira Port Trunk Road kutokana na nyaraka za udanganyifu kutoka kwa mkandarasi, jambo lililosababisha hasara ya kifedha ya Sh. bilioni 13.72. Vilevile, ucheleweshaji wa malipo ya serikali kuongezwa kwa muda wa mikataba katika mradi wa barabara ya Nachingwea-Ruangwa-Nanganga ilisababisha hasara ya kifedha ya Sh. bilioni 1.79.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa katika mizani minne, magari 26,300 yalipita bila kupimwa uzito katika mizani. Hii ilitokana na changamoto za kiutendaji kama vile kukatika kwa umeme, kuharibika mara kwa mara kwa vifaa, na matatizo ya urekebishaji wa mizani, jambo lililodhoofisha utekelezaji wa kanuni za udhibiti wa mizigo na kuongeza gharama za matengenezo ya barabara.

Upungufu katika Mfumo wa Vibali Maalumu vya Mizigo ulisababisha vibali 792 kutumika zaidi ya mara moja katika vituo 41 vya mizani, hali iliyosababisha upotevu wa mapato ya Sh. milioni 41.18. Vikwazo vya bajeti pia viliathiri matengenezo ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA), ambapo kulikuwa na upungufu wa Sh. trilioni 1.43 kwa ajili ya matengenezo ya barabara, na kusababisha kusimamishwa kwa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 495.24. Migogoro na watoa huduma kuhusu upatikanaji wa taarifa za mizani ilizuia juhudi za utekelezaji.

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilikumbwa na changamoto za kifedha, ikiwa na madeni yasiyolipwa ya Sh. bilioni 3.98 kutokana na mradi wa nyumba za Bunju na migogoro ya bei iliyochelewesha mauzo ya nyumba 471 katika mradi wa nyumba wa Magomeni.

TEMESA inamiliki na kuendesha vyombo 32 bila kuwa na Cheti cha Usalama na Ustahili wa Safari Baharini kutokana na ukosefu wa mwongozo wazi wa kisheria, hali iliyoongeza mashaka juu ya usalama wa vyombo hivyo.

Aidha, mradi wa kivuko cha Nyamisati wenye thamani ya Sh. bilioni 9.5 ulicheleweshwa kwa miezi 14 kutokana na matatizo ya idhini ya michoro na mapungufu katika ufanisi wa mkandarasi.

### (vii) Sekta ya Maji

Mpango wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Maji (IWRM) umechelewa kuandaliwa kwa miaka 15, hali inayodhoofisha usimamizi wa maji na kuongeza hatari ya uhaba wa maji na uharibifu wa mazingira. Aidha, vyanzo vya maji 2,989 havijalindwa, na hivyo viko hatarini kuvamiwa na kukauka.

Pia, makusanyo ya Sh. bilioni 2.01 yanayotokana na vibali vya matumizi 1,795 hakikukusanywa kutokana na matumizi ya vibali vya maji viliisha muda wake, huku kampuni 36 za uchimbaji wa visima zikifanya kazi bila leseni kutokana na ushirikiano usioridhisha kati ya Wizara ya Maji na BRELA, jambo lililoongeza hatari ya uvunaji wa maji kupita uwezo wa chanzo na uchafuzi wa maji.

Upatikanaji wa maji mijini ulifikia 90% kufikia Juni 2024, lakini bado kulikuwepo na upungufu wa lita bilioni 26.29 katika mamlaka 16 za Majisafi na Usafi wa Mazingira (WSSAs). Zaidi ya hayo, maji yasiyozalisha mapato (NRW) yenye thamani ya Sh. bilioni 8.75 yalirekodiwa kutokana na uvujaji wa mabomba chakavu, huku wateja 2,203 wakiwa hawana mita za maji, hali iliyoathiri ukusanyaji wa mapato.

Katika maeneo ya vijijini, huduma za maji zilifikia 79.6%, lakini visima 642 kati ya 900 vilivyopata maji ya kutosha wakati miundombinu ya visima vyote ikiwa bado haijakamilika kikamilifu kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, Sh. bilioni 8.32 zililipwa bila makubaliano ya utendaji, hali inayoweza kuongeza hatari ya usimamizi usioridhisha na kuweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maji iliyokusudiwa.

Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) vilikabiliwa na upungufu wa maji wa 73%, miundombinu chakavu, na hasara ya Sh. bilioni 2.05 kutokana na upotevu wa maji usiolipiwa. Vilevile, mita 15,606 za maji hazikuthibitishwa, na Sh. bilioni 3.74 za mapato hazikukusanywa, hali iliyozorotesha mtiririko wa kifedha.

Changamoto za ubora wa maji pia zilibainika. Maji ya mabwawa yasiyopimwa yalitumiwa kwa matumizi ya binadamu, huku ukosefu wa ufuatiliaji wa ubora wa maji katika migodi ya dhahabu ukiweka afya za jamii hatarini. Aidha, vyombo 11 vya CBWSOs vilishindwa kufanya vipimo vya ubora wa maji, hali iliyohatarisha usalama wa maji. Vilevile, miongozo ya kitaifa ya ufuatiliaji wa ubora wa maji ya kunywa imepitwa na wakati, na ukosefu wa usimamizi wa maabara binafsi za kupima maji umeathiri utekelezaji wa kanuni za udhibiti wa ubora wa maji.

### (viii) Sekta ya Afya

Tathmini ya ukaguzi ilibaini changamoto za ufanisi katika sekta ya afya zinazohusiana na utoaji wa huduma, utekelezaji wa kanuni, na usimamizi wa fedha. Ukosefu wa kiunzi cha kisheria kinachosimamia uchangiaji na upandikizaji wa viungo vya binadamu unaoongeza ukiukwaji wa taratibu. Aidha, hospitali nne za Rufaa za Mikoa (RRHs) hazikufanyiwa Tathmini Huru za Utendaji wa Hospitali (EHPA), jambo ambalo limepunguza uwezo wa kutathmini huduma na kuboresha ubora.

Vilevile, ilibainika udhaifu katika usimamizi wa mapato, ambapo Sh. bilioni 9.64 zilipotea kutokana na madai ya bima yaliyokataliwa na Sh. bilioni 6.81 zilizobaki hazikukusanywa kutoka kwa watoa huduma za bima ya afya, hali ambayo imeathiri uwezo wa kifedha wa hospitali kutoa huduma muhimu za afya. Zaidi ya hayo, ucheleweshaji wa malipo ya NHIF yenye jumla ya Sh. bilioni 5.63 umeongeza mzigo kwa shughuli za hospitali.

Pia, ilibainika kutokufuata kanuni za leseni, ambapo wataalamu 84 wa afya na taasisi 50 za mafunzo zilifanya kazi bila leseni halali, hali ambayo inaathiri ubora wa huduma, usalama wa wagonjwa, na uangalizi wa kanuni. Aidha, dawa zilizokwisha muda wake zenye thamani ya Sh. bilioni 1.41 zilikuwa bado hazijateketezwa katika hospitali 11, jambo ambalo linaweza kuwa hatari kwa afya na mazingira.

### (ix) Sekta Nyingine

Ukaguzi uliangazia sekta nyingine ikiwemo Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Madini, Nishati, Elimu, pamoja na Ardhi. Masuala muhimu yaliyowasilishwa ni pamoja na usimamizi wa fedha, utawala, uzingatiaji wa sheria, na upungufu wa ufanisi wa utendaji.

- **Sekta ya Madini na Nishati**

Serikali imepata hasara ya Dola za Marekani milioni 147 kama fidia kwa kampuni za uchimbaji madini zilizoathiriwa na matumizi ya marekebisho ya Sheria ya Madini ya 2010. Kati ya kiasi hicho, dola milioni 117 zimelipwa na kubaki salio la dola milioni 30 ambazo hazijalipwa. Matokeo haya yanaashiria hatari kubwa za kifedha, ikiwemo uwezekano wa malipo yasiyo na tija yanayotokana na mchakato huu.

Zaidi ya hayo, Wakala wa Ununuzi wa Mafuta hajatekeleza uratibu wa bei ya mafuta kwa Kampuni za Uuzaji wa Mafuta tangu Machi 2024, na kushindwa kukusanya michango kutoka kwa Kampuni za Uagizaji wa Mafuta zenye gharama za chini za uingizaji au fidia kwa zile zinazoendesha katika bandari zenye gharama kubwa kama Mtwara na Tanga. Matokeo yake, Kampuni za Uagizaji wa Mafuta katika bandari hizi zinakutana na gharama kubwa bila fidia, jambo linaloweza kupunguza faida yao, kuzuia ushiriki wao katika biashara ya mafuta, na hatimaye kuathiri ugavi wa mafuta na bei zake nchi nzima.

- **Ardhi, Kilimo, na Mifugo**

Kamati ya Mawaziri wa Sekta ilibaini vijiji 975 kote Tanzania vinavyokutana na migogoro ya matumizi ya ardhi. Ingawa serikali ilianzisha mpango wa kutatua migogoro hii mwezi Septemba 2019 na lengo la kumaliza ifikapo mwaka 2022, vijiji 729 pekee (75%) vimeweza kutatua migogoro yao, na vijiji 246 (25%) bado havijatatuliwa. Kutotatuliwa kwa migogoro hii kuna hatari ya kuathiri mshikamano wa kijamii, kusababisha kuzorota kwa uchumi, na kuzuia maendeleo katika maeneo yaliyoathiriwa.

Zaidi ya hayo, masoko ya upili ya mifugo yenye thamani ya Sh. milioni 502.58 bado hayafanyi kazi kutokana na tathmini kutofanyika ipasavyo kabla ya kupendekeza shughuli za ujenzi. Vilevile, malipo ya fidia kwa migogoro ya ardhi bado hayajalipwa, ambapo Sh. bilioni 21.95 bado hazijalipwa kati ya Sh. bilioni 68.43 zilizokadiriwa kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi na jamii zinazoizunguka maliasili. Ucheleweshaji huu unaweza kusababisha malalamiko, uvamizi zaidi, na uwezekano wa ongezeko la riba kutokana na kutolipwa ndani ya kipindi cha zaidi ya miezi sita.

### (x) Usimamizi wa Mifuko Maalumu na Mifuko Mingine

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Fedha haikuwasilisha jumla ya Sh. trilioni 1.14 kati ya Sh. trilioni 2.59 zilizokusanywa kwa ajili ya REA, NWF, RFB, na RF. Hali hii imeathiri uwezo wa Mifuko na Wakala, kufadhili miradi muhimu, na kusababisha ucheleweshaji wa maendeleo ya miundombinu na kupunguza ufanisi wa utendaji.

Pia, kiasi cha Sh. bilioni 2.58 kinachodaiwa kutokana na mikopo iliyotolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kipo katika hatari ya kutokurejeshwa. Hali hii imesababisha ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo mipya kwa vikundi vingine vya vijana vinavyohitaji, hivyo kuathiri malengo ya Mfuko. Vilevile, mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.28 ilitolewa kwa vikundi vya vijana kabla ya kupatiwa mafunzo na mwongozo, jambo ambalo linaongeza hatari ya wanufaika kutumia vibaya fedha hizo na kufanya urejeshaji wa mikopo kuwa mgumu zaidi.

Zaidi ya hayo, Sh. bilioni 7.01 kati ya Sh. bilioni 11.13 zilizohamishiwa kwa taasisi nne za serikali katika Mkoa wa Manyara kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyoathiriwa na maporomoko ya udongo katika Wilaya ya Hanang hazijatumiwa. Hali hii inakwamisha matumizi sahihi ya rasilimali na urejeshaji wa huduma muhimu katika jamii.

### (xi) Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

Ukaguzi ulibaini nchi mbili hazikuweza kutekeleza kanuni ya utoaji huduma kwa uwiano sawa (reciprocity) ambapo mnamo mwezi Machi na Novemba 2024 Serikali ya Tanzania iligawa ekari tano za ardhi katika eneo la Mtumba, Dodoma kwa Serikali ya Jamhuri ya Uturuki na kiwanja kilichopo Ihumwa, Dodoma kiligawiwa kwa serikali ya Kuwait. Hata hivyo, serikali za Jamhuri ya Uturuki na serikali ya Kuwait bado hazijaweza kugawa ardhi kwa Ubalozi wa Tanzania huko Ankara na Kuwait licha ya maombi kadhaa kuwasilishwa kwa nchi hizo. Hii ni kinyume na Ibara ya 2 ya Mkataba wa Vienna juu ya Mahusiano ya Kidiplomasia ya mwaka 1961, ambayo inataka mahusiano ya kidiplomasia kati ya mataifa wenyeji na ofisi za balozi kuanzishwa na kufanyika kwa ridhaa ya pande zote mbili. Hii inadhoofisha kanuni ya usawa, inadhoofisha uhusiano wa kidiplomasia, na huongeza gharama za uendeshaji kwa Balozi za Tanzania, hasa katika suala la gharama za pango kwa ajili ya ofisi na makazi.

Pia fedha za matumizi zenye thamani ya Sh. bilioni 148.89 kutoka Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwenda balozini zilicheleweshwa, ikiwa na uchelewaji wa wastani wa mwezi mmoja kwa mwaka mzima. Uchelewaji huu uliathiri uwezo wa kifedha wa balozi za Tanzania nje ya nchi katika kutimiza majukumu kwa wakati.

### (xii) Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mishahara na Mafao ya Wastaafu

Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi 22 hazikuwasilisha makato ya kwa mamlaka husika yenye jumla ya Sh. bilioni 1.34, hatua hii inaweza kuathiri usalama wa kifedha wa watumishi na kuwaweka waajiri katika hatari ya kupewa adhabu za kisheria.

Masuala ya usimamizi wa watumishi yalibaini tofauti za takwimu katika mfumo wa HCMIS kwa watumishi 283 katika taasisi nane kasoro hizo ni kama vile tarehe za kuzaliwa zilizo kwenye mfumo kutolingana na zile zilizo kwenye nambari za utambulisho wa taifa za watumishi na kuwapo kwa tarehe moja ya uthibitisho na kupandishwa cheo. Pia, kuwapo kwa nafasi za kukaimu kwa muda mrefu kwa watumishi 106 katika taasisi 15. Aidha, madai ya watumishi ambayo hayajalipwa ya Sh. bilioni 274.80 kutoka taasisi 205 yalibainika, hii inaashiria ucheleweshwaji katika kushughulikia stahiki za watumishi.

### (xiii) Usimamizi wa Mali

Ukaguzi ulibaini upungufu katika usimamizi wa mali katika taasisi mbalimbali. Jumla ya taasisi 15 na balozi tano hazikuwa na msimbo wa mali zenye thamani ya Sh. bilioni 9.92, huku taasisi 47 na balozi 12 zikiwa hazijaorodhesha mali zao katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS). Hali hii inadhoofisha usimamizi na uwajibikaji, na kufanya iwe vigumu kufuatilia na kudhibiti rasilimali za umma kwa ufanisi.

Zaidi ya hayo, taasisi 31 na balozi 14 hazikuwa na mipango ya matengenezo wa mali wanazomiliki, hivyo kusababisha uchakavu wa mapema wa mali na kuongezeka kwa gharama za matengenezo. Vilevile, balozi tano na hospitali tatu ziliripoti kuwa na majengo yaliyochakaa, hali inayohatarisha usalama na kuongeza gharama za matengenezo. Pia, taasisi 34 zilikua na mali zilizochakaa ambazo hazitumiki na zilizopitwa na wakati, ambazo hazijatengenezwa wala kuuzwa hivyo kuongeza rekodi za hesabu na kuchukua nafasi muhimu pale zilipohifadhiwa. Taasisi 18 hazina hati miliki ya ardhi wanazomiliki, hivyo kusababisha kutokuwa na uhakika wa umiliki ambao unazuia maendeleo na uwezekano wa kupata mapato.

### (xiv) Majukumu ya Utawala na Usimamizi

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika utekelezaji wa majukumu ya kiutawala, udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi katika Wizara, Idara na Ofisi za Wakala. Taasisi 23 hazikuwa na bodi za usimamizi, bodi 10 hazikufanya mikutano inayohitajika, na Mamlaka 14 za Majisafi na Usafi wa Mazingira zinafanya kazi bila Wakurugenzi Wasimamizi.

Vilevile, Baraza la Mpango wa Kujitathimini kwa Nchi za Afrika (APRM), liliteuliwa mwaka 2006 likiwa na wajumbe 20, ila kwa sasa lina wajumbe wanne pekee ambao wametumikia baraza hilo kwa miaka 18 bila kuongezewa muda wa nyongeza, kuweka ukomo wa muda na akidi, jambo linalobainisha mapungufu ya kiutendaji.

Aidha, Ukaguzi ulibaini mapungufu katika kamati za ukaguzi na usimamizi wa vihatarishi ambapo, kuwapo kwa kamati za ukaguzi zisizo na ufanisi katika taasisi tisa, kutokuwapo kwa kamati za ukaguzi katika taasisi tano, na kukosekana kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika taasisi tano. Nilibaini taasisi 19 hazikuwa na mifumo ya udhibiti wa vihatarishi, Taasisi 18 zilikuwa na mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa viatarishi, ikiwa ni pamoja na kutokuwapo kwa sera za udhibiti wa vihatarishi, kutofanyika kwa tathmini ya vihatarishi, na kutokuwapo kwa waratibu wa vihatarishi.

### (xv) Vyama vya Siasa

Ukaguzi ulibaini upungufu katika usimamizi wa fedha, utawala, na mali ndani ya vyama vya siasa. Upungufu wa mapato ulibainika, ambapo vyama kumi vya siasa vilishindwa kukusanya Sh. milioni 133.26 kutoka kwa michango ya wanachama na ruzuku, hali iliyopunguza uwezo wao wa kifedha. Aidha, Sh. milioni 31.7 za michango hazikuwekwa benki, jambo lililokiuka matakwa ya kisheria na kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha.

Mapungufu ya utawala yalionekana, ambapo vyama vya Demokrasia Makini (DM) na National Reconstruction Alliance (NRA) havikuandaa mikutano ya kisheria, hali iliyokiuka Kanuni ya 24(1) ya Kanuni za Baraza la Vyama vya Siasa ya mwaka 2019 na kudhoofisha utawala bora.

Changamoto za umiliki wa mali zilibainika, ambapo mali ya NCCR Mageuzi yenye thamani ya Sh. milioni 145.06 na magari 10 ya CUF yenye thamani ya Sh. milioni 274.93 bado yalisajiliwa kwa majina ya watu binafsi badala ya Bodi za

Wadhamini wa vyama hivyo, hali inayosababisha hatari za kisheria na kudhoofisha udhibiti wa kifedha. Mapungufu haya ya usimamizi wa fedha na utawala yanadhoofisha uwajibikaji, ufanisi wa kiutendaji, na uthabiti wa vyama vya siasa.

# SURA YA KWANZA




# Maelezo ya Awali

# MAELEZO YA AWALI

## 1.1 Utangulizi

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala, Mfuko Mkuu wa Serikali, Hesabu jumuifu za Serikali, Vyama vya Siasa, na Vyombo vya Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii.

Ripoti hii ina sura 16, ambazo zinajumuisha maoni ya ukaguzi, utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita, usimamizi wa vihatarishi, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya utawala na usimamizi, utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na matumizi, usimamizi wa rasilimali watu, na ufanisi katika utendaji. Pia, inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa vyama vya siasa kwa mwaka wa fedha 2023/24.

## 1.2 Malengo ya Ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa hati iwapo taarifa za fedha zilitayarishwa kwa kuzingatia viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha. Pia, ukaguzi ulilenga kupitia na kutathmini ufuataji wa sheria za ununuzi pamoja na sheria ya bajeti, kanuni, na miongozo husika.

## 1.3 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (ISSAIs) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (INTOSAI), pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vilivyotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Ukaguzi na Uhakiki (IAASB). Mbinu za ukaguzi zilijumuisha hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukagua nyaraka, kufanya mahojiano, kuchambua taarifa na kutembelea maeneo husika.

## 1.4 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha ukaguzi wa taarifa za fedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, uzingatiaji wa sheria, kanuni, sera, na ufanisi katika utendaji kwa wizara, idara na wakala (MDAs) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Ukaguzi ulijumuisha tathmini ya usimamizi wa bajeti, ukusanyaji wa mapato, udhibiti wa matumizi, michakato ya ununuzi, usimamizi wa mali, usimamizi wa rasilimali watu, na mifumo ya utawala. Vilevile, ukaguzi ulitathmini hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita na ufanisi wa mifumo ya ndani ya usimamizi wa vihatarishi.

# SURA YA PILI




# RIPOTI ZA UKAGUZI

## Hati za Ukaguzi

# HATI ZA UKAGUZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa muhtasari hati za ukaguzi wa taarifa za fedha zilizotolewa kwa Wizara, Idara na Wakala (MDA) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Hati za ukaguzi hutoa tathmini huru ya kama taarifa za kifedha zilizoandaliwa na MDAs zimeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha na kutoa picha sahihi ya hali yao ya kifedha na utendaji ya MDA. Sura hii pia inaangazia mwenendo wa matokeo ya ukaguzi katika miaka ya fedha ya hivi karibuni na kubainisha masuala muhimu yanayoathiri ubora wa uwasilishaji wa taarifa za fedha za MDAs.

## 2.2 Aina za Hati za Ukaguzi

Baada ya kufanya uchambuzi na tathmini ya vielelezo vilivyotumika kuandaa taarifa za fedha, kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo zinaweza kutolewa. Aina hizo za hati zinategemea na kupatikana kwa ushahidi unaojitosheleza kuthibitisha ubora na usahihi wa taarifa inayowasilishwa katika taarifa za fedha. Aina hizo za hati ni kama ifuatavyo:

**Hati inayoridhisha:** Aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata ushahidi na vielelezo vya kutosha na kuthibitisha kwamba taarifa za fedha ni sahihi na zimeandaliwa kwa kufuata viwango kubalifu vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha. Aina hii ya hati ndio inayotazamiwa zaidi na inaonesha kiwango kikubwa cha kuaminika na usahihi wa taarifa za fedha.

**Hati yenye shaka:** Aina hii ya hati hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa kwa dosari moja au zaidi ya moja ambazo kwa ujumla wake ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha. Pia, aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi hakupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

**Hati mbaya:** Aina hii ya hati hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha kuwa dosari moja au zaidi ya moja au kwa ujumla wake zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kubwa na zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kusababisha taarifa hizo kutokuwa sahihi.

**Kushindwa kutoa maoni:** Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha kumuwezesha kutoa maoni ya ukaguzi. Katika hali hii, mkaguzi atahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea kutokana na

dosari zisizogundulika za taarifa za fedha zinaweza kuwa kubwa na zinaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za fedha. Katika mazingira nadra sana yenye shaka mbalimbali, mkaguzi anaweza kushindwa kutoa maoni hata kama amepata ushahidi wa kutosha kuhusiana na shaka husika.

## 2.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka Husika

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya hati za ukaguzi 532 zilitolewa. Kati ya hati hizo, hati 531 (99.8%) zilikuwa hati zinazoridhisha, na moja (0.2%) ilipata hati mbaya. Katika mwaka wa fedha husika hakukuwa na hati yenye shaka na kushindwa kutoa maoni.

Chama cha Siasa cha National Reconstruction Alliance (NRA) kilipata hati mbaya kutokana na mapungufu makubwa na uwepo wa makosa ya kimsingi yaliyobainika kwenye taarifa zake za fedha.

## 2.4 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Mwenendo wa hati zilizotolewa kwa miaka minne mfululizo tangu mwaka 2020/21 hadi mwaka 2023/24 umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1** na maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za Ukaguzi**

| Aina ya Hati ya Ukaguzi | 2023/24 | 2022/23 | 2021/22 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|
| Inayoridhisha | 531 | 471 | 323 | 315 |
| Yenye shaka | 0 | 1 | 10 | 5 |
| Mbaya | 1 | 1 | 2 | 5 |
| Kushidwa kutoa maoni | - | 2 | 1 | 2 |
| **Jumla** | **532** | **475** | **336** | **327** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi*

## 2.5 Hitimisho kuhusu utekelezaji wa Sheria

Kwa upande wa utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 313 zilikuwa na utekelezaji kamili wa sheria ya ununuzi, huku 200 zikitekeleza kwa upungufu. Aidha, taasisi 362 zilifuata Sheria ya Bajeti na Miongozo ya Bajeti, huku 151 zikionesha upungufu. Uchambuzi huu haujumuishi vyama vya siasa 19 na Hesabu Jumuifu ya Serikali, kwani sheria za ununuzi na bajeti hazitumiki kwa taasisi hizi. Taasisi hizo zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. I.**

# SURA YA TATU



# Hali na Utekelezaji wa mapendekezo ya Miaka Iliyopita

# HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

## 3.1 Utangulizi

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ni msingi muhimu wa kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kuboresha utawala, na kuhakikisha uwajibikaji katika Wizara, Idara, na Wakala (MDAs). Sura hii inatoa tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi za miaka iliyopita, ikibainisha kiwango ambacho Wizara, Idara, na Wakala (MDAs) zimechukua hatua madhubuti kushughulikia mapungufu yaliyoainishwa na kutekeleza marekebisho stahiki. Uchambuzi huu umeonesha mapendekezo yale yaliyotekelezwa kikamilifu, yaliyo katika utekelezaji, na yale ambayo bado hayajatekelezwa, ikielezea changamoto zinazojirudia na maeneo yanayohitaji maboresho zaidi. Vilevile, sura hii inatathmini mwenendo wa utekelezaji katika miaka ya fedha iliyopita ili kupima maendeleo yaliyopatikana na ufanisi wa mifumo ya ufuatiliaji katika kuhakikisha utekelezaji endelevu wa mapendekezo ya ukaguzi.

Sura hii pia inaeleza hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) yaliyotolewa katika miaka ya fedha iliyopita. Uchambuzi umeonesha maagizo yale yaliyotekelezwa kikamilifu, yaliyo katika utekelezaji, na yale ambayo bado hayajatekelezwa, ukitoa uelewa kuhusu changamoto zinazoendelea na maeneo yanayohitaji uangalizi zaidi.

Ninatambua juhudi za Mlipaji Mkuu wa Serikali na maafisa masuuli katika kushughulikia mapendekezo yangu na kutekeleza maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwani hatua hizi zinachangia kuimarisha utawala bora na uwajibikaji ndani ya taasisi za umma.

## 3.2 Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita

Katika mwaka wa ukaguzi, nilihakiki taarifa za ukaguzi za wizara, idara na wakala (MDAs) 514 na vyama vya siasa 19. Ukaguzi wangu ulitathmini hali ya mapendekezo ya ukaguzi 8,141 yaliyotolewa kwa wizara, idara na wakala, na 289 kwa vyama vya siasa. Kati ya mapendekezo 8,141 ya ukaguzi yaliyohusu wizara, idara na wakala (MDAs), 2,819 (35%) yalitekelezwa kikamilifu, 3,461(42%) yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, 767 (9%) hayakutekelezwa kabisa, 293 (4%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati, na 801 (10%) yalirudiwa kutokana na umuhimu wake kuendelea kuwapo.

Vilevile, kati ya mapendekezo 289 yaliyohusu vyama vya siasa, 74 (26%) yalitekelezwa, 52 (18%) yalikuwa katika hatua za utekelezaji, 113 (39%)

hayakutekelezwa, 8 (3%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati, na 42 (14%) yalirudiwa kutokana na umuhimu wake kuendelea kuwapo.

Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa wizara, idara na wakala (MDAs) na vyama vya siasani kama unavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 2: Hali ya utekelezaji kwa Wizara, Idara na Wakala na Vyama vya Siasa**

| Kundi | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yaliyo chini ya utekelezaji | Mapendekezo hayajatekelezwa | Mapendekezo yamerudiwa | Mapendekezo yamefutwa kutokana na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wizara, idara na wakala (MDAs) | 2,819 | 3,461 | 767 | 801 | 293 | 8,141 |
| Vyama vya siasa | 74 | 52 | 113 | 42 | 8 | 289 |
| **Jumla** | **2,893** | **3,513** | **880** | **843** | **301** | **8,430** |

***Chanzo**: Taarifa za Ukaguzi za Mwaka 2023/24*

Uchambuzi wa jumla wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika wizara, idara na wakala (MDAs) pamoja na vyama vya siasa umebainishwa katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi**

| Mwaka wa Fedha | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo yaliyo chini ya utekelezaji | Mapendekezo hayajatekelezwa | Mapendekezo yamerudiwa | Mapendekezo yamefutwa kutokana na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 2,893 | 3,513 | 880 | 843 | 301 | 8,430 |
| 2022/23 | 2,946 | 2,725 | 617 | 668 | 366 | 7,342 |
| 2021/22 | 2,380 | 2,506 | 1,104 | 637 | 320 | 6,947 |
| 2020/21 | 5,290 | 6,032 | 3,548 | 1,166 | 1,143 | 17,179 |
| 2019/20 | 2,308 | 2,441 | 1,257 | 621 | 333 | 6,960 |

***Chanzo:** Taarifa za ukaguzi mwaka 2023/24*

Wakati baadhi ya taasisi zimefanikiwa kutekeleza mapendekezo ya mwaka uliopita, zikionesha dhamira ya uzingatiaji wa miongozo na utawala bora, nyingine hazijatekeleza ipasavyo. Hali hii imepelekea changamoto sugu za utawala, kifedha na kiutendaji kuendelea kudumu.

Uchambuzi wa mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayajatatuliwa kwa muda mrefu unaonyesha kuwa mapendekezo 281 yamebaki bila kutekelezwa kwa zaidi ya miaka mitano, ikiwa ni pamoja na 17 ambayo hayajatatuliwa kwa zaidi ya muongo mmoja. Uchambuzi huu unaonyeshwa katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Mapendekezo ya Ukaguzi Yaliyobaki kwa Muda Mrefu**

| Hali | > Miaka 5 | > Miaka 10 | Jumla |
|---|---|---|---|
| Chini ya utekelezaji | 209 | 12 | 221 |
| Haijatekelezwa | 55 | 5 | 60 |
| **Jumla** | **264** | **17** | **281** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi za Mwaka 2023/24*

### 3.3 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilibaini kuwa, kati ya maagizo 123 yaliyoripotiwa katika ripoti zangu za miaka iliyopita, 31 (25%) yalitekelezwa kikamilifu, 91 (74%) yanaendelea kutekelezwa na 1 (1%) halikutekelezwa. Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali unaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 5: Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali**

| Mwaka wa Fedha | Maagizo yaliyotekelezwa | Maagizo yaliyo chini ya utekelezaji | Maagizo hayajatekelezwa | Maagizo yamerudiwa | Maagizo yamefutwa kutokana na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 31 | 91 | 1 | 0 | 0 | 123 |
| 2022/23 | 38 | 43 | 5 | 1 | 9 | 96 |
| 2021/22 | 35 | 113 | 22 | 1 | 1 | 172 |
| 2020/21 | 347 | 294 | 147 | 0 | 34 | 822 |
| 2019/20 | 130 | 101 | 17 | 0 | 11 | 259 |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi Mwaka 2023/24*

Mwenendo wa utekelezaji wa maagizo ya PAC katika miaka mitano ya fedha iliyopita unaonyesha mabadiliko katika maendeleo ya utekelezaji, ikiwa na viwango tofauti vya mwitikio miongoni mwa taasisi. Licha ya maboresho haya, juhudi endelevu zinahitajika ili kuhakikisha kuwa maagizo yanayoendelea kutekelezwa yanakamilishwa kikamilifu, hivyo kuimarisha utawala, uzingatiaji wa sheria, na mifumo ya usimamizi wa fedha.

# SURA YA NNE




# Maandalizi na Utekelezaji wa Bajeti

# MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI

## 4.1 Utangulizi

Bajeti ya Serikali ni nyenzo muhimu ya kugawa rasilimali kwa vipaumbele vya taifa na kuboresha ustawi wa jamii. Bajeti hii huandaliwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa (2021/22–2025/26), pamoja na Miongozo ya Mpango na Bajeti ya kila mwaka.

Bajeti ya mwaka 2023/24 ilizingatia kupunguza umaskini na kuleta ajira kwa kuwekeza katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, ujenzi, usafirishaji, na utalii ili kuimarisha ukuaji wa uchumi.

Ili kuongeza mapato na kudhibiti nidhamu ya kifedha, Serikali ililenga kuboresha ukusanyaji wa kodi kupitia mifumo ya TEHAMA, kupunguza misamaha ya kodi, kuimarisha taasisi za umma, na kuvutia uwekezaji kupitia hati fungani za serikali. Kwa upande wa matumizi, hatua zilihusisha kupunguza gharama kupitia TEHAMA, kuboresha usimamizi wa miradi, kufanya kaguzi kwa wakati halisi, na kurekebisha sheria za ununuzi ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha.

Sura hii inatathmini utendaji wa bajeti kwa kulinganisha makusanyo yaliyopangwa na halisi, kuchambua mchango wa vyanzo mbalimbali vya mapato, kutathmini utendaji wa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na kubainisha maeneo yanayohitaji maboresho.

## 4.2 Muhtasari wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia Sh. trilioni 44.388 kutoka kwenye makusanyo ya ndani, misaada, na mikopo. Makusanyo ya ndani yalijumuisha kodi, makusanyo yasiyo ya kodi, na makusanyo ya Serikali za Mitaa, huku misaada ikiwa ni msaada wa bajeti na ufadhili wa miradi kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mikopo ilitokana na mikopo ya ndani, mikopo ya nje yenye masharti nafuu, na mikopo ya nje isiyo ya masharti nafuu.

Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni 2024, kiasi halisi kilichokusanywa kilikuwa Sh. trilioni 46.503, ikizidi lengo kwa Sh. trilioni 2.115 (5%). Makusanyo ya ndani yaliendelea kuwa chanzo kikuu cha fedha, yakichangia Sh. trilioni 29.933 (64%) ya makusanyo yote **Jedwali Na. 6** linaonyesha muhtasari wa makusanyo yaliyopangwa na halisi, pamoja na tofauti zilizojitokeza

**Jedwali Na. 6: Utendaji wa Bajeti**

| Chanzo cha Bajeti | Kiasi cha Bajeti (Sh. Trilioni) | Kiasi kilichokusanywa (Sh. Trilioni) | (Upungufu)/Ziada ya Makusanyo (Sh. Trilioni) | % ya (Upungufu)/Ziada ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|
| Makusanyo ya Ndani | 31.381 | 29.933 | (1.448) | (5) |
| Misaada | 1.111 | 0.644 | (0.467) | (42) |
| Mikopo | 11.896 | 15.926 | 4.03 | 34 |
| **Jumla** | **44.388** | **46.503** | **2.115** | **5** |

*Chanzo*: *Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2023/24*

Sehemu ifuatayo inatoa uchambuzi wa kina wa kila chanzo cha bajeti ikilinganishwa na makusanyo halisi.

### i. Makusanyo ya Ndani

**Jedwali Na. 7** linaonesha utendaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kulinganisha na makadirio ya bajeti, likisisitiza tofauti katika mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, na ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

**Jedwali Na. 7: Uchambuzi wa Makusanyo ya Ndani**

| Aina ya Makusanyo ya Ndani | Kiasi cha Bajeti (Sh. Trilioni) | Kiasi kilichokusanywa (Sh. Trilioni) | (Upungufu)/ Ziada ya Makusanyo (Sh. Trilioni) | % ya (Upungufu)/ Ziada ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|
| Makusanyo ya Kodi | 26.725 | 26.065 | (0.660) | (2) |
| Makusanyo Yasiyokuwa ya Kodi | 3.512 | 2.636 | (0.876) | (25) |
| Makusanyo ya Serikali za Mitaa | 1.144 | 1.232 | 0.088 | 8 |
| **Jumla** | **31.381** | **29.933** | **(1.448)** | **(5)** |

*Chanzo*: *Taarifa ya Fedha ya Mfuko Mkuu*

### ii. Misaada

Misaada, inayojumuisha msaada wa bajeti na fedha za miradi ya maendeleo, ina jukumu muhimu katika ufadhili. Katika mwaka wa fedha uliokaguliwa, jumla ya makisio ya misaada ilikuwa Sh. trilioni 1.111. Hata hivyo, makusanyo halisi

yalikuwa Sh. trilioni 0.644, na kusababisha upungufu wa Sh. trilioni 0.467, sawa na upungufu wa 42%.

### iii. Mikopo Halisi kulinganisha na Bajeti

**Jedwali Na. 8** linaonesha mikopo halisi kulinganisha na makadirio ya bajeti, likitaja mikopo ya ndani, mikopo ya nje ya masharti nafuu, na mikopo ya nje isiyo ya masharti nafuu.

**Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa Mikopo**

| Aina ya Mikopo | Kiasi cha Bajeti (Sh. Trilioni) | Kiasi Mikopo iliyopokelewa (Sh. Trilioni) | (Upungufu)/ Ziada ya Mikopo (Sh. Trilioni) | % ya (Upungufu)/ Ziada ya Mikopo |
|---|---|---|---|---|
| Mikopo ya Ndani | 5.440 | 5.408 | (0.032) | (1) |
| Mikopo ya Nje Yenye Masharti Nafuu | 4.355 | 7.443 | 3.088 | 71 |
| Mikopo ya Nje Isiyo ya Masharti Nafuu | 2.101 | 3.075 | 0.974 | 46 |
| **Jumla ya Mikopo** | **11.896** | **15.926** | **4.030** | **34** |

***Chanzo**: Taarifa ya Fedha ya deni la Taifa na Mfuko Mkuu*

## 4.3 Muhtasari wa Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24

Katika mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya Sh. trilioni 40.445 iliwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya matumizi. Aidha, Serikali ilikopa Sh. trilioni 2.922 kutoka Benki Kuu, hivyo kufanya jumla ya kiasi kilichopatikana kwa ajili ya matumizi kuwa Sh. trilioni 43.367. Serikali ilitumia jumla ya Sh. trilioni 43.367 kupitia idhini ya matumizi (exchequer) kufadhili matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo, marejesho, na uhamisho wa fedha. Kiasi kilichobaki cha Sh. trilioni 3.135 hakikutolewa kupitia idhini ya matumizi (exchequer). Kiasi hiki kilijumuisha:

- Sh. trilioni 2.856 zilizotolewa moja kwa moja kwa miradi na washirika wa maendeleo (Fedha za Moja kwa Moja kwa Miradi, au D-Funds), na
- Sh. bilioni 279 za mapato ya vyanzo vya ndani yaliyokusanywa na kutumika moja kwa moja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

Uchambuzi wa matumizi ya serikali na mgao kwa taasisi za Serikali Kuu (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 1** na **Kielelezo Na. 2.**

### Kielelezo Na. 1: Matumizi ya Serikali kulingana na Wapokeaji




***Chanzo**: Ripoti za Utoaji wa Fedha kutoka kwenye Exchequer na Taarifa ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali (Consolidated Fund)*

### Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Matumizi ya Serikali kwa Makundi




***Chanzo**: Ripoti ya Utoaji wa Fedha kutoka kwenye Exchequer*

## 4.4 Utekelezaji wa Bajeti

### 4.4.1 Fedha zilizotolewa zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa Sh. bilioni 389.04

Kulingana na Kifungu cha 45(b) cha Sheria ya Bajeti sura ya 439, utoaji wa fedha kwa mafungu lazima ulingane na utendaji, bajeti ilizoidhinishwa, na upatikanaji wa fedha.

Hata hivyo, ukaguzi wangu wa utoaji fedha katika mfuko wa hazina na bajeti iliyoidhinishwa nilibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 389.04 kilitolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa katika taasisi 12. Utofauti huo unaoneshwa katika **Kiambatisho Na. II**. hali iliyosababishwa na ukosefu wa muunganisho mzuri wa Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti Kuu (CBMS) na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE). Hii imesababisha uchakataji wa data usio sahihi na utoaji wa fedha za hazina zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Ninapendekeza Serikali iongeze udhibiti katika Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti Kuu (CBMS) ili kuhakikisha kuwa umeunganishwa kikamilifu na mfumo wa MUSE. Uunganishaji huu unapaswa kuweka mipaka madhubuti ya bajeti, hivyo kuzuia utoaji wa fedha za hazina (*exchequers*) zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa kila Fungu.**

### 4.4.2 Malipo Yasiyo na Idhini ya Uhamishaji - Sh. Bilioni 35.98

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 [toleo la mwaka 2020] kinahitaji matumizi ya fedha zilizoidhinishwa kwa serikali na taasisi za umma kufanyika tu kwa mujibu wa madhumuni yaliyobainishwa na ndani ya mipaka iliyowekwa kwa mujibu wa mgawanyo wa makadirio yao.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi tisa zilifanya matumizi ya jumla ya Sh. bilioni 35.98 kwa shughuli za matumizi ya kawaida na maendeleo nje ya bajeti iliyoidhinishwa na bila kupata idhini husika ya uhamishaji wa fedha, kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. III.**

Kutumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli ambazo hazijapangwa kwenye bajeti huathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Zaidi ya hayo, hali hii inatoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa taasisi zote zinazingatia mgao wa bajeti ulioidhinishwa, na kuzuia matumizi yoyote kwa shughuli ambazo hazikupangwa.**



# SURA YA TANO

# Usimamizi wa Mapato na Deni la Serikali

## USIMAMIZI WA MAPATO NA DENI LA SERIKALI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mapungufu katika ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na changamoto za uzingatiaji wa sheria na ufanisi mdogo katika usimamizi wa mapato. Pia inatoa mapendekezo ya kuboresha ukusanyaji wa mapato. Kadhalika, sura hii inatoa muhtasari wa madeni ya umma, ikiwa ni pamoja na hali yake ya sasa, mwenendo, na uendelevu wake.

### 5.2 Utendaji wa Makusanyo ya Kodi

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya jumla ya Sh. trilioni 26.065, chini ya lengo lililowekwa la Sh. trilioni 26.725. Hii ni pungufu kwa kiasi cha Sh. bilioni 659.61, sawa na 2.5% ya malengo ya mapato yote katika Tanzania Bara.**Jedwali Na.9** linaonesha mchanganuo wa ukusanyaji wa mapato kiidara kwa Tanzania Bara.

**Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Makusanyo ya Kodi Tanzania Bara**

| Idara | Makisio (Sh. Bilioni) | Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni) | Makusanyo ziada (Pungufu) (Sh. Bilioni) | % ya Ziada/ (Upungufu) |
|---|---|---|---|---|
| A | B | C | D= (C-B) | E=(D/B) |
| Kodi za Ndani | 5,309.24 | 5,291.14 | (18.10) | (0.3) |
| Walipakodi Wakubwa | 11,984.41 | 11,314.15 | (670.26) | (5.6) |
| Ushuru na Forodha | 10,479.74 | 10,506.31 | 26.57 | 0.3 |
| **Jumla ya Makusanyo** | **27,773.39** | **27,111.6** | **(661.79)** | **(2.4)** |
| Punguza: Marejesho ya Kodi na Hamisho kwenda ZRA | 1,105.66 | 1,067.51 | (38.15) | (3.5) |
| **Jumla baada ya Marejesho ya kodi na Hamisho** | **26,667.73** | **26,044.09** | **(623.64)** | **(2.3)** |
| Ongeza: Vocha za Hazina[1] (TVC) | 57.68 | 21.71 | (35.97) | (62.4) |
| **Jumla** | **26,725.41** | **26,065.80** | **(659.61)** | **(2.5)** |

***Chanzo***: *Taarifa za Makusanyo za Mapato Zilizokaguliwa Mwaka 2023/24*

Kadhalika, Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 507.81, ikiwa ni chini ya lengo lililowekwa la Sh. bilioni 520.64. Hii ni pungufu kwa kiasi

[1] Vocha za Hazina ni matumizi yanayolipwa kupitia mfumo wa kodi ili kufidia ushuru wa uingizaji wa bidhaa kwa walipakodi wenye misamaha, ikiwemo Watumishi wa Umma, Maafisa wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Katika hali hii, TVCs zilijumuishwa kama sehemu ya tathmini ya makusanyo kwa Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa.

cha Sh. bilioni 12.83, sawa na 2.5% **Jedwali Na.10** linaonesha mchanganuo wa makusanyo ya mapato kiidara Zanzibar.

**Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa Makusanyo ya Kodi Zanzibar**

| Idara | Makisio (Sh. Bilioni) | Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni) | Makusanyo Ziada (Pungufu) (Sh. Bilioni) | % ya Ziada/ (upungufu) |
|---|---|---|---|---|
| Kodi za Ndani | 263.30 | 271.94 | 8.64 | 3.3 |
| Ushuru na Forodha | 257.34 | 235.87 | (21.47) | 8.3 |
| **Jumla ya Makusanyo** | **520.64** | **507.81** | **(12.83)** | **2.5** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2023/2024*

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Idara ya Ushuru na Forodha ilikusanya mapato juu ya lengo lililowekwa, wakati Idara ya Walipakodi Wakubwa na Idara ya Kodi za Ndani ukusanyaji ulikuwa chini ya malengo waliyowekewa. Kwa ujumla, kutotekelezwa ipasavyo kwa malengo kulisababishwa na kutofikiwa kwa ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa (*excise duty*); kodi ya zuio (*withholding tax*); Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT); kodi ya mapato ya mtu binafsi (*Individual income taxes*); ada ya ustadi na maendeleo (*Skills & Development Levy*), pamoja na kodi ya mafuta na kodi nyingine.

Uchambuzi wa mchango wa kila idara katika ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Bara umebaini kuwa Idara ya Walipakodi Wakubwa ilikuwa na 41.7%, ikifuatiwa na Idara ya Forodha na Ushuru yenye 38.8%, na Idara ya Mapato ya Ndani 19.5%. Ulinganisho wa ukusanyaji halisi wa mapato ya idara kwa mwaka wa fedha 2023/24 na 2022/23 umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3: Makusanyo ya Kodi Tanzania Bara**




***Chanzo***: *Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa Mwaka 2023/24 na 2022/23*

Kwa Zanzibar, ukusanyaji wa mapato unaonesha kwamba Idara ya Mapato ya Ndani ilichangia 53.6%, ikifuatiwa na Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa kwa 46.4%. Ukusanyaji halisi wa mapato kwa mwaka wa fedha 2023/24 na 2022/23 kwa idara hizo umeoneshwa katika **Kielelezo Na.4.**

**Kielelezo Na. 4: Makusanyo Halisi ya Kodi Zanzibar**




***Chanzo***: *Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa Mwaka 2023/24 na 2022/23*

Ulinganisho wa ukusanyaji wa mapato halisi kiidara kwa miaka ya fedha ya 2023/24 na 2022/23 unaonesha kwamba mchango wa idara zote katika ukusanyaji wa mapato umeongezeka. Kwa Idara ya Walipakodi Wakubwa, mapato yameongezeka kwa 25.3%, Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa kwa 12.7%, na kwa Idara ya Mapato ya Ndani ongezeko ni asilimia 0.07.

### 5.2.1 Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Kodi

Uchambuzi wa kiutendaji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita unaonesha kuwa ukusanyaji wa mapato umeendelea kuwa chini ya malengo yaliyowekwa, ambapo kiwango cha makusanyo ya chini ya lengo ni kati ya asilimia 2.5 hadi 13.6%. Upungufu mkubwa ulitokea katika mwaka wa fedha 2020/21, ikionesha changamoto katika kufikia malengo ya mapato.

Hali ya makusanyo ya mapato kuwa chini ya malengo yaliyowekwa inaonesha uwezekano wa kutotekelezwa ipasavyo na udhaifu wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato. Mwelekeo huu unaonesha haja ya kutathmini kwa karibu sababu zilizochangia kushindwa kufikia malengo na kuboresha usimamizi katika ukusanyaji wa kodi ili kuboresha utendaji katika ukusanyaji wa mapato.

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita umeoneshwa katika **Jedwali Na.11**.

**Jedwali Na. 11: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

| Mwaka wa Fedha | Makisio (Sh. Bilioni) | Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni) | Makusanyo Pungufu | % ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 27,246.05 | 26,573.61 | (672.44) | 2.5 |
| 2022/23 | 24,106.81 | 23,039.73 | (1,067.09) | 4.4 |
| 2021/22 | 22,191.17 | 21,303.87 | (887.30) | 4.0 |
| 2020/21 | 20,709.32 | 17,897.86 | (2,811.46) | 13.6 |
| 2019/20 | 19,451.12 | 17,930.88 | (1,520.25) | 7.8 |

***Chanzo:** Taarifa za Hesabu za Mapato za Mamlaka Zilizokaguliwa za Mwaka 2019/20 hadi 2023/24*

**Uwiano wa kodi kwa pato la taifa**

Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa ni kipimo kinachoonesha uhusiano kati ya mapato ya jumla ya kodi ya nchi na Pato la Ndani la Taifa (GDP). Uwiano mkubwa wa kodi kwa pato la taifa huashiria kuwa sehemu kubwa ya pato la taifa inakusanywa kama kodi.

Katika mwaka wa fedha 2023/24, utendaji wa Mamlaka ya Mapato ulionesha ongezeko kidogo la kiwango cha kodi kwa pato la taifa (uwiano wa kodi kwa pato la taifa) kwa 13% ikilinganishwa na 12.5% katika mwaka wa fedha 2022/23. **Kielelezo Na.5** kinaonesha uwiano wa kodi kwa pato la taifa kwa miaka minne.

**Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa**




***Chanzo:** Ripoti ya Kijalizo cha Mamlaka za Mapato za Afrika Mashariki*

**Jedwali Na.12** linaonesha ulinganisho wa uwiano wa kodi kwa pato la taifa Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki.

**Jedwali Na. 12: Uwiano wa Kodi kwa Pato la Taifa la Tanzania na Nchi Zingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Minne**

| Nchi | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| Kenya | 13.70% | 15.00% | 14.20% | 13.8% |
| Rwanda | 16.30% | 15.80% | 15.00% | 14.9% |
| Tanzania | 11.70% | 12.80% | 12.50% | 13.0% |
| Uganda | 13.00% | 13.50% | 13.70% | 13.5% |
| Burundi | 17.00% | 17.60% | 18.00% | 17.0% |

***Chanzo***: *Ripoti ya Kijalizo cha Mamlaka za Mapato za Afrika Mashariki*

Takwimu zinaonyesha ingawa uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa (tax-to-GDP ratio) umeongezeka kutoka 11.7% mwaka 2020/21 hadi 13.0% mwaka 2023/24, bado iko chini ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Hii inaashiria kwamba sehemu ndogo ya pato la uchumi wa Tanzania inakusanywa kama mapato ya kodi.

**Ninapendekeza Serikali kuimarisha ufanisi katika makusanyo ya kodi kwa kutekeleza mikakati ya kuongeza wigo wa makusanyo, kudhibiti uvujaji wa mapato, kuhamasisha utayari wa walipakodi kulipa kodi kwa hiari, na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa kodi. Hatua hizi zitachangia kuongeza ukusanyaji wa mapato na maendeleo endelevu wa uchumi wa nchi.**

### 5.2.2 Rufaa za Kodi ambazo hazijatatuliwa za Sh. Trilioni 9.83 Zinazosubiri Hukumu katika Mahakama za Rufaa za Kodi

Katika ukaguzi wa taarifa za Makusanyo za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/24 nilibaini kuwa Mamlaka ilikuwa na kesi 1,186 za kodi katika mahakama za rufaa za kodi kwa muda mrefu, zenye jumla ya Sh. Trilioni 9.83 (zikiwemo dola za Marekani 3,731,995 zilizobadilishwa kwa kiwango cha Sh. 2626.93/dola ya Marekani) kwa Tanzania Bara.

Kiasi hiki kinaashiria kupungua kwa Sh. bilioni 655.56 (6.2%) ikilinganishwa na kesi zenye kodi ya Sh. trilioni 10.49 zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita (2022/23). Kupungua kwa kesi hizi kulitokana na kusuluhishwa kwa kesi 683 katika Mahakama ya Rufaa (CAT), Tume ya Rufaa ya Kodi (TRAT), na Bodi ya Rufaa ya Kodi (TRAB). Hata hivyo, licha ya mafanikio haya, bado kuna kesi nyingi za kodi ambazo zinaweza kuchelewesha ukusanyaji wa mapato ya serikali na kuathiri mipango ya bajeti.

Uchambuzi wa kesi zilizosalia ukionesha idadi ya kesi na thamani ya kodi kwa kila mahakama na mwaka wa fedha umeoneshwa katika **Jedwali Na. 13**.

Kadhalika, katika ukaguzi wangu wa ufanisi wa kiutendaji wa TRAT na TRAB kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini kuwapo kwa upungufu wa kiutendaji katika usuluhishi wa kesi, ambapo mahakama zote zilikuwa chini ya malengo yaliyobainishwa katika Mfumo wa Bajeti wa Muda wa Kati (MTEF) wa mwaka 2023/24 – 2025/26.

(i) TRAT ilisuluhisha kesi 104 kati ya 288, sawa na 36% pekee ya lengo la mwaka.
(ii) TRAB ilisuluhisha kesi 573 kati ya 1,483, sawa na 39% pekee ya lengo la mwaka.

Viwango hivi vya usuluhishi ni vya chini sana ikilinganishwa na malengo ya MTEF ambayo yanahitaji TRAT kusuluhisha 80% na TRAB kusuluhisha 90% ya migogoro ya kodi inayowasilishwa kila mwaka.

Upungufu huu umesababishwa na ucheleweshaji wa uteuzi wa wajumbe muhimu wa tume na bodi, upungufu wa fedha za bajeti, ukosefu wa mifumo ya kufuatilia kesi na ongezeko la kesi mpya. Upungufu huu katika usuluhishi wa kesi unaonesha ufanisi mdogo unaoendelea katika mahakama za kodi. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshaji wa ukusanyaji wa mapato na kuongeza mzigo wa kesi zisizosuluhishwa.

**Ninapendekeza serikali iimarishe uwezo wa vyombo vya rufaa kwa kuvipatia vyombo hizi rasilimali fedha za kutosha Pamoja na wafanyakazi ili kuharakisha utatuzi wa kesi zinazosubiri suluhu.**

**Jedwali Na. 13: Kesi za Kodi Ambazo Hazijatatuliwa Tanzania Bara**

| Mwaka | Idadi ya Kesi | Mahakama ya Rufaa (CAT) | | Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) | | Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Sh. | Dola Za Marekani | Sh. | Dola Za Marekani | Sh. | Dola Za Marekani | Sh. | Dola Za Marekani |
| 2017/18 | 1 | - | - | - | - | 8,728,712,111 | - | 8,728,712,111 | - |
| 2019/20 | 11 | 10,221,980,312 | - | 49,729,889,875 | - | 120,395,616,621 | - | 180,347,486,808 | - |
| 2020/21 | 27 | 10,040,599,421 | - | 1,435,900,266 | - | 271,654,202,960 | - | 283,130,702,647 | - |
| 2021/22 | 97 | 121,488,155,330 | 1,997,276 | 18,272,756,934 | - | 1,218,475,002,634 | - | 1,358,235,914,897 | 1,997,276 |
| 2022/23 | 247 | 23,909,218,646 | - | 66,953,261,503 | - | 1,130,464,229,390 | 1,734,719 | 1,221,326,709,539 | 1,734,719 |
| 2023/24 | 803 | 430,249,434,867 | - | 2,714,613,945,952 | - | 3,627,152,786,575 | - | 6,772,016,167,394 | 0 |
| **Jumla** | **1186** | **595,909,388,576** | **1,997,276** | **2,851,005,754,530** | | **6,376,870,550,291** | **1,734,719** | **9,823,785,693,396** | **3,731,995** |

***Chanzo***: *Taarifa za Hesabu za Mamlaka ya Mapato Mwaka 2023/2024*

Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na kesi za kodi 98 zinazofikia Sh. bilioni 23.24 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 14**

**Jedwali Na. 14: Kesi za Kodi Zilizopo katika Mahakama za Kodi Zanzibar**

| Mwaka | Idadi ya Kesi | Bodi ya Rufani za Kodi (Sh.) | Baraza la Rufani za Kodi (Sh.) | Jumla (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 8 | 166,444,653 | 0 | 166,444,653 |
| 2021/22 | 1 | 0 | 125,366,562 | 125,366,562 |
| 2022/23 | 85 | 20,054,190,872 | 2,074,155,975 | 22,128,346,847 |
| 2023/24 | 4 | 820,042,771 | 0 | 820,042,771 |
| **Jumla** | **98** | **21,040,678,296** | **2,199,522,537** | **23,240,200,833** |

***Chanzo***: *Taarifa za Hesabu za Mamlaka ya Mapato Mwaka 2023/24*

### 5.2.3 Mapato ambayo hayakukusanywa kutokana na utumiaji wa viwango vilivyopitwa na wakati vya Ushuru wa Bidhaa kwa vinywaji vyenye kaboni - Sh. Bilioni 609.77

Ukaguzi wangu wa ripoti za uchunguzi wa kodi chini ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (Usimamizi na Viwango), Sura 147 [toleo lililorekebishwa mwaka 2019] ulibaini upungufu mkubwa katika malipo ya ushuru wa bidhaa kutoka kwa walipakodi watatu wanaozalisha vinywaji vyenye kaboni. Walipakodi hawa walitumia viwango vilivyopitwa na wakati vya Sh. 61 na Sh. 67 kwa lita. Hivyo, walisababisha ukusanyaji wa mapato wa Sh. bilioni 78.81 badala ya kiwango sahihi cha Sh. 561 kwa lita ambacho kingefanya ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa wa Sh. bilioni 688.58. Hali hii ilisababisha upungufu wa Sh. bilioni 609.77 ambazo hazikukusanywa.

Kadhalika, nilikagua watengenezaji wa vinywaji wengine wanane katika mwaka wa fedha 2023/24. Nilibaini kutozingatiwa kwa viwango sahihi katika sekta nzima, ambapo viwango vilivyopitwa na wakati bado viliendelea kutumika. Hii inaonesha haja ya kufanyika kwa uchunguzi wa kina. Aidha, inaonesha haja ya kuhimiza utekelezaji wa viwango sahihi vya ushuru, pamoja na ulipaji wa ushuru wa bidhaa ambao haukulipwa ili kuepuka upotevu mkubwa wa mapato.

Pia, nilikagua taarifa za ushuru wa bidhaa za mikoa sita ya kodi (Kinondoni, Arusha, Temeke, Tegeta, Idara ya Walipakodi wa Kati, na Pwani) na kubaini upungufu wa ushuru wa bidhaa wa Sh. bilioni 1.53. Upungufu huu ulisababishwa na ukaguzi na uchambuzi usioridhisha wa taarifa za walipakodi uliofanywa na mamlaka; hivyo, kushindwa kubaini tofauti katika taarifa zilizowasilishwa na walipa kodi. Upungufu huu unatoa fursa ya utoaji wa taarifa zisizo sahihi, hivyo kuleta upotevu wa mapato kwa serikali.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti ya TRA ihakikishe inakusanya mapato ya ushuru wa bidhaa ambayo hayakulipwa kutoka kwa walipakodi waliotumia viwango vilivyopitwa na wakati. Zaidi, ihakikishe yafuatayo: iwatake walipakodi wote kutumia viwango sahihi vya ushuru wa bidhaa, ianzishe ufuatiliaji wa kudumu, iweke adhabu kwa malipo pungufu ya kodi kwa udanganyifu, na iongeze uchunguzi katika sekta ya utengenezaji wa vinywaji ili kubaini kutotekelezwa kwa viwango sahihi vya ushuru wa bidhaa.**

### 5.2.4 Lita 14,459,706.19 za mafuta yenye thamani ya Sh. bilioni 12.55 yaliyopaswa kusafirishwa kwenda Nchi jirani kupitia bomba la mafuta la TAZAMA hayakufika katika Nchi zilizokusudiwa

Kanuni ya 104(16) ya Kanuni za Usimamizi wa Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2010, bidhaa zote zinazopaswa kusafirishwa kwenda nchi jirani lazima zitoke nchini kupitia mipaka ya forodha ili kuzuia bidhaa hizo kuuzwa katika soko la ndani ya nchi bila kulipa ushuru.

Ukaguzi wa mafuta ya petroli yaliyopaswa kusafirishwa kwenda nchi jirani kupitia Bomba la Mafuta la TAZAMA kwa kipindi cha kuanzia Januari 2023 hadi Agosti 2024, nilibaini tofauti ya lita 14,459,706.19 zenye makadirio ya kodi ya Sh. bilioni 12.55 ambazo hazikuvuka katika mipaka ya forodha kwenye nchi zilizokusudiwa. Kutowasilishwa kwa mafuta hayo katika nchi husika kunabainisha kwamba mafuta hayo yametumika bila kulipiwa kodi. Utofauti huo ulibainika baada ya kulinganisha taarifa za kiasi cha mafuta kilichoingia nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam na kiasi cha mafuta kilichopokelewa katika kituo cha Inyala, Mbeya. Tofauti ya kiasi hiki cha mafuta inaweza kuwa imetumika nchini bila kulipiwa ushuru.

Sababu kuu inayochangia tatizo hili ni kukosekana kwa ufuatiliaji kwa wakati ili kuhakikisha kuwa waagizaji wa mafuta na mawakala wa forodha wanaandaa na kuwasilisha taarifa ya mafuta yote yaliyoingizwa nchini katika mfumo wa forodha. Jambo hili lilisababisha kucheleweshwa kwa taratibu.

**Ninapendekeza Serikali kuanzisha mfumo/utaratibu wa ufuatiliaji wa taratibu za usafirishaji wa mafuta ili kuhakikisha uwajibikaji katika kila hatua ya usafirishaji na kufanya marekebisho ya mara kwa mara ya taarifa kati ya forodha kwenye kupokea mafuta na kutoa mafuta ili kubaini mapungufu na kuyashughulikia**

### 5.2.5 Mafuta Yaliyopitiliza Muda wa Kukaa Nchini Yaliyopaswa kwenda Nchi Jirani Lakini Hayakutozwa Ushuru wa Forodha

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA), 2004, bidhaa zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kwenda Nchi Jirani zinapaswa zisafirishwe kwenda nchi zilizokusudiwa au ziingizwe rasmi katika soko la ndani ndani ya muda uliowekwa. Aidha, Kanuni ya 104(16) ya Kanuni za Usimamizi wa Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2010, inazitaka bidhaa zote zinazokwenda nchi jirani kuhesabiwa kuwa zimetoka nchini kikamilifu zinapovuka mipaka ya nchi ili kuzuia ukwepaji wa kodi na uingizaji haramu wa bidhaa katika soko la ndani.

Nilikagua kiasi cha mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani katika taarifa za manifesti. Pia, nilipitia kiasi halisi cha mafuta yaliyosafirishwa kwenda nchi nyingine. Nilibaini kuwapo kwa bakaa ya lita za mafuta 1,546,614.41 zenye makadirio ya kodi ya Sh. bilioni 1.38 ambazo hazikusafirishwa kwenda nchi husika kwa zaidi ya siku 30 zilizoruhusiwa lakini ushuru wa forodha haukukusanywa.

Kadhalika, nilipitia miamala ya mafuta yaliyosafirishwa kwenda nchi jirani katika vituo vya forodha vya mipakani vya Rusumo, Mutukula, na Kabanga ambayo ilihusisha ulinganisho wa kina wa kiasi cha bidhaa zilizoingizwa nchini na kiasi halisi cha bidhaa zilizovuka mipaka hiyo kwenda Nchi husika. Uchambuzi wangu ulibaini tofauti ya kilo 826,505 za bidhaa na lita 247,299 za mafuta zenye dhamana ya jumla ya Sh. milioni 472.72. Bidhaa hizi hazikuvuka katika mipaka hiyo kwenda nchi husika.

Kushindwa kufuatilia na kutekeleza kanuni za usafirishaji wa bidhaa zinazokwenda nchi jirani kunatoa fursa ya uingizwaji haramu wa bidhaa katika soko la ndani bila kulipiwa kodi, jambo linaloweza kusababisha upotevu wa mapato kwa Serikali.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, iboreshe mifumo yake ya kidigiti kwa ajili ya ufuatiliaji wa bidhaa na mafuta yanayoingizwa nchini kwa ajili ya kwenda nchi jirani ili kuhakikisha kuwa kiasi chote kinasafirishwa kwenda nchi zilizokusudiwa. Hatua hii itasaidia kuzuia bidhaa na mafuta yanayokaa nchini kwa muda mrefu. Pia, mamlaka ihakikishe kuwa inakusanya ushuru wa forodha pamoja adhabu kwa tofauti zozote zinazobainika au kwa bidhaa na mafuta ambayo yamekaa zaidi ya muda unaoruhusiwa kisheria.**

### 5.2.6 Kutokuzingatia Sheria za Kodi

Mfumo wa bajeti wa mwaka 2023/24 unasisitiza kuzingatia sera, mikakati, na hatua mbalimbali za kiutawala katika ukusanyaji wa mapato, ikiwamo kuhakikisha matumizi sahihi ya mashine ya kutoa risiti za kielekitroni ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi, kama inavyotakiwa na Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Mashine ya Kutoa Risiti za Kielekitroni) za mwaka 2012. Zaidi ya hayo, Kifungu cha 83(A) na Kifungu Kidogo cha 4(C)(IV) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, sura ya 332, vinazitaka taasisi za serikali kushikilia asilimia mbili ya kodi ya mapato kwenye malipo kwa wasambazaji wa ndani, ili kuhakikisha kodi inakusanywa mapema na kupunguza hatari ya kuripoti mapato pungufu.

Kinyume chake, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi sita zilifanya malipo yenye jumla ya Sh. bilioni 10.28 bila kudai risiti za kielekitroni, na kodi ya zuio ya Sh. milioni 980 haikukatwa na Wizara ya Maji, kama ilivyobainishwa **Jedwali Na. 15**.

Kutokudai risiti za kielekitroni na kukata kodi ya zuio kunadhoofisha juhudi za Serikali za kuboresha ukusanyaji wa mapato, kunatoa mwanya wa ukwepaji wa kodi, na kunakwamisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kufuatilia na kuthibitisha miamala inayostahili kutozwa kodi kwa ufanisi.

**Jedwali Na. 15: Kutokuzingatia Sheria za Kodi**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| **Malipo Bila Kudai Risiti za Kielekitroni** | | |
| 1 | Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji - Wizara | 10,191,843,541 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Dodoma | 35,030,639 |
| 3 | Wizara ya Maji (Fungu Na. 49) | 19,948,000 |
| 4 | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) | 16,449,844 |
| 5 | Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) | 13,408,400 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Sumbawanga | 8,633,360 |
| **Jumla Ndogo A** | | **10,285,265,832** |
| **Malipo Yasiyokatwa Kodi ya Zuio** | | |
| 1 | Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji - Wizara | 815,079,815 |
| | Wizara ya Maji (Fungu Na. 49) | 165,009,174 |
| **Jumla Ndogo B** | | **980,088,989** |

***Chanzo***: *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua madhubuti dhidi ya taasisi zinazokiuka kanuni za kodi ili kuzuia upotevu wa mapato. Pia, iimarishe udhibiti wa ndani ili kuhakikisha malipo yanaambatana na risiti za kielekitroni na kodi ya zuio inakatwa ipasavyo.**

## 5.3 Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi

Mapato yasiyotokana na kodi ni chanzo muhimu na endelevu katika mipango ya kifedha ya serikali. Yanajumuisha mikakati ya kuongeza mapato kutoka vyanzo vingine isipokuwa kodi, kama vile ada, faini, leseni, tozo za vibali, kodi za pango, mrabaha, na mauzo ya bidhaa na huduma.

### 5.3.1 Makusanyo nje ya Mfumo wa Makusanyo

Mfumo wa bajeti wa mwaka 2023/24 unasisitiza uzingatizi wa sera, mikakati, na hatua za mbalimbali kiutawala katika ukusanyaji wa mapato, ikiwamo matumizi ya Mfumo wa Kielekitroni wa Malipo ya Serikali (GePG) kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya umma, kama inavyotakiwa na Kifungu cha 7 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi tatu zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 2.46 kama mapato yasiyo ya kodi nje ya Mfumo wa Kielekitroni wa Malipo ya Serikali (GePG), kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 16**

**Jedwali Na. 16: Taasisi Zilizokusanya Mapato Nje ya Mfumo wa Mapato**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | SUMA JKT - Sekta ya Kilimo na Viwanda | 1,355,018,000 |
| 2 | SUMAJKT - Kampuni ya Ushauri Elekezi | 983,241,000 |
| 3 | Kikosi cha Afya cha Jeshi la Polisi | 131,547,225 |
| **Jumla** | | **2,469,806,225** |

***Chanzo***: *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo wa GePG unadhoofisha uwazi, uwajibikaji, na ufanisi katika usimamizi wa mapato. Pia, huongeza hatari ya usimamizi mbaya, matumizi mabaya, au upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza Serikali na mamlaka husika zisimamie utekelezaji madhubuti wa matumizi ya mfumo wa GePG kwa ukusanyaji wote wa mapato ya umma ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.**

### 5.3.2 Madeni ya Mapato Yasiyokusanywa ya Sh. Trilioni 1.34

Mapato yasiyokuwa ya kodi yanayotokana na ada, faini, na gharama za huduma ni chanzo muhimu cha fedha kwa Serikali, kinachosaidia kuongeza mapato mengine na kusaidia bajeti kijumla. Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato haya, maafisa masuuli wanatakiwa, kwa mujibu wa Kifungu Na. 58(b) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kuhakikisha ufanisi katika ukusanyaji, kuepuka usimamizi usioridhisha, na kuhakikisha mapato haya yanachangia kikamilifu katika bajeti ya Serikali.

Uhakiki wangu wa taarifa za fedha za wizara, idara, na wakala ulionyesha kuwa Sh. trilioni 1.34 zilirekodiwa kama madeni ya mapato yasiyokuwa ya kodi lakini hazikukusanywa kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kwa mfano, Wizara ya Ardhi ilikuwa na deni la kodi ya ardhi la Sh. bilioni 201, na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilikuwa na madeni ya Sh. bilioni 352 kutokana na mauzo ya nafaka. Kutokusanywa kwa mapato haya kunachangiwa hasa na mapungufu katika mifumo ya utekelezaji, ambayo inazuia mapato hayo kugharamia bajeti na matumizi yaliyopangwa. Rejea **Kiambatisho Na. IV.**

**Ninapendekeza kwamba Serikali na mamlaka husika kuanzisha mifumo ya ukusanyaji itakayosaidia kuongeza uwezo wa kukusanya madeni, ili kuongeza uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuboresha uwezo wa kifedha wa taasisi na kufadhili bajeti ya Serikali.**

### 5.4 Usimamizi wa Deni la Serikali

Deni la Serikali linajumuisha madeni yote inayodaiwa Serikali ikiwamo ndani na nje ya nchi kupitia Serikali Kuu na wakala zake. Kwa madhumuni ya ufanisi katika usimamizi wa deni, Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kipekee ya kukopa kwa niaba ya Serikali mikopo ya nje na ndani, na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali kwa mujibu wa vifungu 3, 6, 13 na 15 vya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura ya 134.

#### 5.4.1 Mchanganuo wa Deni la Serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni 2024 lilikuwa Sh. bilioni 97,357.84 ikilinganishwa na Sh. bilioni 82,254.71 lililoripotiwa mwaka 2022/23. Kuna ongezeko la Sh. bilioni 15,103.13 (18%) ikilinganishwa na Sh. bilion 10,942.30 (15%) kwa mwaka uliopita.

Deni la Serikali linajumuisha deni la ndani na nje Sh. bilioni 31,951.56 na Sh. bilioni 65,406.28 kwa mwaka wa fedha 2023/24 mtawalia, ikilinganishwa na Sh. bilioni 28,926.37 na Sh. bilioni 53,328.33 kwa mwaka 2022/23. **Kielelezo Na. 6** kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa mwaka 2021/22 hadi 2023/24.

**Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali**




| Mwaka wa fedha | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|
| Deni la Nje | 47,272 | 53,328 | 65,406 |
| Deni la Ndani | 24,040 | 28,926 | 31,952 |
| Jumla ya Deni | 71,312 | 82,254 | 97,358 |

***Chanzo**: Hesabu za Fedha Fungu N a . 0 0 1 - deni la Serikali kwa mwaka 2021/22 hadi 2023/24*

#### 5.4.2 Mwenendo wa Deni la Ndani

Katika mwaka wa fedha 2023/24, deni la ndani liliongezeka kwa Sh. bilioni 3,025.19, sawa na 10% ya deni lililorekodiwa mwaka 2022/23. Mwelekeo wa

deni la ndani kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2023/24 umeoneshwa katika **Jedwali Na. 17**.

**Jedwali Na. 17: Mwenendo wa deni la Ndani**

| Mwaka wa Fedha | Deni | Ongezeko | |
|---|---|---|---|
| | Sh. Bilioni | Sh. Bilion | % |
| 2023/24 | 31,951.56 | 3,025.19 | 10 |
| 2022/23 | 28,926.37 | 4,886.26 | 20 |
| 2021/22 | 24,040.11 | 5,105.49 | 27 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Fedha za Deni za Mwaka 2021/22 hadi 2023/24*

### 5.4.3 Mwenendo wa Deni la Nje

Kufikia tarehe 30 Juni 2024 Deni la nje lilikuwa Sh. bilioni 65,406.28 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 12,077.95 sawa na 23% ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 53,328.33 lililoripotiwa mwaka 2022/23. Ongezeko linatokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya fedha za kigeni na mapokezi ya fedha kutokana na mikataba mipya ya mikopo. Mseto na Mwenendo wa Deni la Nje kwa miaka 2021/22 mpaka 2023/24 ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 18**.

**Jedwali Na. 18: Mwenendo na Mseto wa Deni la Nje**

| Wakopeshaji | 2023/24 | | 2022/23 | | 2021/22 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sh. Bilioni | % | Sh. Bilioni | % | Sh. Bilioni | % |
| Taasisi za Kimataifa | 43,972.38 | 67 | 33,578.24 | 63 | 28,729 | 61 |
| Nchi Marafiki | 3,675.20 | 6 | 5,163.57 | 10 | 5,208 | 11 |
| Benki za kuwezesha biashara ya Forodha | 6,193.50 | 9 | 5,655.54 | 11 | 5,973 | 13 |
| Wakopeshaji | 11,565.20 | 18 | 8,930.99 | 17 | 7,363 | 16 |
| Jumla | 65,406.28 | 100 | 53,328.33 | 100 | 47,272 | 100 |
| Ongezeko | 12,077.95 | 23 | 6,056.04 | 11 | 1,687 | 4 |

***Chanzo***: *Jedwali la Mwenendo wa Deni la Serikali kwa Mwaka 2021/22 hadi 2023/24.*

### 5.4.4 Uchambuzi wa Uhimilivu wa Deni

Katika uchambuzi wa uhimilivu wa deni la serikali wa Desemba 2024, kulingana na taarifa ya deni ya 30 Juni 2024, ilithibitishwa kuwa deni la serikali linabaki kuwa himilivu. Viashiria muhimu kama vile Uwiano wa Thamani ya Sasa ya Deni la Nje kwa Pato la Taifa (GDP) ni 23.6%, na Uwiano wa Deni la serikali kwa Pato la Taifa ni 41.1%, vyote vikiwa chini ya viwango vilivyowekwa vya 40% na 55% mtawalia. Aidha, Uwiano wa Thamani ya Sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ni 127.5%, ikiwa chini ya kiwango cha 180%. Vilevile, Uwiano wa Kulipa Deni kwa Mauzo ya Nje ni 11.7%, na Uwiano wa Kulipa Deni kwa Mapato ni 14.5%, vyote vikiwa ndani ya mipaka ya 15% na 18% mtawalia.

Ingawa viashiria hivi vinadhihirisha hali ya uhimilivu wa deni, uwiano wa Kulipa Deni kwa Mauzo ya Nje (11.7%) na Uwiano wa Kulipa Deni kwa Mapato (14.5%) unakaribia viwango vya juu vya 15% na 18%, jambo linaloashiria uwepo wa hatari katika uwezo wa kulipa madeni. Hii ina maana kwamba, iwapo kutakuwa na mabadiliko yasiyotarajiwa katika hali ya uchumi—kama vile kudorora kwa thamani ya sarafu, kupungua kwa mapato ya mauzo ya nje, au kupungua kwa mapato ya serikali—viashiria hivi vinaweza kupita viwango vya juu, na hivyo kuongeza hatari ya mkanganyiko wa deni. Ingawa hatari ya jumla ya mkanganyiko wa deni bado ni wastani, kama ilivyokuwa katika tathmini ya awali, ukaribu wa viwango hivi na mipaka yake unahitaji ufuatiliaji wa karibu na usimamizi mzuri wa deni.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iimarishe viwango vya ukwasi wa deni kwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhamasisha mauzo ya bidhaa nje ya nchi, huku ikiboresha kiwango chake cha tathmini ya sera na taasisi (Country Policy and Institutional Assessment - CPIA) ili kufikia kiwango cha 'Utekelezaji Mahiri- Strong Performer' kwa Benki ya Dunia na kuchochea ukuaji endelevu wa Pato la Taifa. Aidha, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa mapato ya mikopo ya kibiashara yanatumiwa katika miradi yenye faida kubwa ili kuchangia ukuaji thabiti wa Pato la Taifa**

# SURA YA SITA




# Usimamizi wa Ununuzi

# USIMAMIZI WA UNUNUZI

## 6.1 Utangulizi

Kifungu cha 48(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, sura ya 410, kinawataka maafisa masuuli wote kuhakikisha kuwa ununuzi wa bidhaa, kazi, au huduma unazingatia taratibu zilizowekwa chini ya sheria na kanuni zake. Aidha, kifungu cha 48(3) kinanilazimu kufanya kutathmini na kuripoti iwapo taasisi zimezingatia ipasavyo taratibu na kanuni zilizobainishwa katika sheria hiyo. Ukaguzi wangu wa ununuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24, umebaini usimamizi duni wa mikataba, kuchelewa kufanyika kwa malipo na matumizi yasiyo na tija ambayo yanaathiri utoaji wa huduma na kusababisha hasara za kifedha.

### 6.1.1 Madeni ya Wakandarasi, Washauri, na Watoa Huduma Sh. Trilioni 4.56

Kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaelekeza malipo kwa wazabuni kufanyika kwa wakati, huku kifungu cha 44.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaelekeza kuwa malipo yaliyoidhinishwa yafanyike ndani ya siku 28.

Ukaguzi wangu kwa mwaka wa fedha 2023/24 ulibaini kuwa taasisi 212 zilikuwa na madeni ya wakandarasi, washauri, na wazabuni yenye jumla ya Sh. trilioni 4.56, ambapo Sh. trilioni 3.53 hazikulipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. V.**

Sababu ya uchelewaji wa kulipa madeni haya ni uchelewaji wa mgao wa fedha zilizotengwa kwenye bajeti na Wizara ya Fedha na ukusanyaji usioridhisha wa mapato ya ndani kwa taasisi.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa inatoa fedha kwa taasisi za serikali kwa wakati na taasisi hizo ziboreshe mikakati ya ukusanyaji wa mapato yao ya ndani ili kuzuia kuongezeka kwa madeni na kuhakikisha mafanikio katika utekelezaji wa miradi.**

### 6.1.2 Riba Iliyotozwa kwa kuchelewesha Malipo - Sh. Bilioni 55.55

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) zilitozwa riba ya jumla ya Sh. bilioni 55.55 kutokana na kuchelewa kulipa madeni. Kati ya kiasi hicho, Wizara ya Ujenzi ilitozwa riba na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya kiasi cha Sh. bilioni 13.43 kutokana na kuchelewa kulipa deni lililotokana na serikali kushindwa kutoa sehemu ya

gharama ya ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni), jambo lililosababisha ongezeko la jumla ya riba inayodaiwa hadi kufikia Sh. bilioni 116.66.

Aidha, Wizara ilitozwa riba ya kiasi cha Sh. bilioni 3.38 kutokana na amri ya Mahakama ya Kimataifa ya Biashara (ICC), kuhusu mradi wa ukarabati wa barabara ya Ibanda-Uyole yenye urefu wa km 97.963, na kusababisha ongezeko la jumla ya riba ya deni hilo kufikia Sh. bilioni 20.87.

Zaidi ya hayo, TANROADS ilitozwa riba ya Sh. bilioni 38.74 kutokana na madai ya wakandarasi. kuchelewa kulipa madeni kunaongeza deni la serikali, kunaongeza gharama za miradi, na kupunguza fedha zilizotengwa kwa miradi mingine muhimu ya miundombinu.

**Ninapendekeza serikali iboreshe upangaji na utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha kuwa fedha za kutosha zinatolewa kwa wakati kwa ajili ya kulipa madeni muhimu na kuepuka malimbikizo ya riba kwa siku zijazo.**

### 6.1.3 Usimamizi Usiotosheleza wa Mikataba ya Ujenzi

Kanuni ya 114 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaelekeza kuwa taasisi nunuzi kusimamia kwa ufanisi mikataba kwa kufuatilia mienendo ya kazi, kuhakikisha zinakamilika kwa wakati na kuchukua hatua kwa mapungufu yanayojitokeza na kuhakikishe majukumu ya kimkataba yaliyowekwa yanatekelezwa kikamilifu. Mapitio yangu ya mikataba ya kazi za ujenzi yalibaini usimamizi usiojitosheleza kama inavyoelezwa hapa chini.

#### (a) Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Miradi yenye Thamani ya Sh. Trilioni 1.34

Mapitio yangu ya miradi 136 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.34 umebaini ucheleweshaji mkubwa, ambapo miradi ilikuwa nyuma kiutekelezaji kwa asilimia moja hadi 92% ikilinganishwa na muda wa kimkataba. Uchambuzi wa sekta ulibaini kuwa miradi ya barabara ilichelewa kwa 15% hadi 58%, miradi ya maji kwa 1% hadi 83%, na mradi wa sekta ya afya hadi 32%, huku sekta nyingine zikikabiliwa na ucheleweshaji wa kati ya 32% na 76%. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. VI.**

Kasi ndogo ya utekelezaji wa kazi za ujenzi inatokana na usimamizi usioridhisha wa mikataba, uwezo mdogo wa baadhi ya wakandarasi, ucheleweshaji katika kuanza kwa miradi, na uchelewaji wa upatikanaji wa fedha. Kutokamilisha miradi ndani ya muda wa mkataba kunaweza kusababisha kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hali hii huathiri utekelezaji wa miradi, hasa kwa upande wa muda, gharama, na ubora.

**Ninapendekeza kuwa Serikali iimarishe usimamizi Madhubuti wa mikataba, ihakikishe utoaji wa fedha kwa wakati, na ifuatilie utendaji wa wakandarasi ili kuzuia ucheleweshaji zaidi na hasara za kifedha**

### (b) Miradi ya Ujenzi Iliyotelekezwa - Sh. Bilioni 558.63

Nilibaini kuwa miradi 41 ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 558.63 ilitelekezwa au kusitishwa na wakandarasi. Miradi 22 ilihusiana na miundombinu ya barabara, sita ni ya sekta ya huduma za afya, 12 ya sekta ya maji, na mmoja ulikuwa katika Idara ya Huduma za Magereza (Fungu Na. 29). Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Jedwali Na. 19.**

**Jedwali Na. 19: Orodha ya Taasisi zenye Miradi Iliyotelekezwa**

| Na. | Taasisi | Idadi ya Mikataba | Jumla ya Thamani ya Mikataba (Sh.) | Sekta |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Barabara Tanzania | 22 | 507,644,240,004 | Miundombinu ya barabara |
| | **Jumla Ndogo** | **22** | **507,644,240,004** | |
| 2 | Hospitali ya Kanda, Chato | 1 | 17,705,497,182 | Sekta ya huduma za afya |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Geita | 1 | 13,213,606,303 | |
| 4 | Wizara ya Afya (Fungu Na. 52) | 1 | 2,900,000,000 | |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mount Meru | 1 | 1,504,560,281 | |
| 6 | Hospitali ya Benjamin Mkapa | 1 | 264,251,288 | |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi | 1 | 164,120,272 | |
| | **Jumla Ndogo** | **6** | **35,752,035,327** | |
| 8 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 11 | 12,201,356,964 | Sekta ya huduma za maji |
| 9 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Chato | 1 | 1,594,256,565 | |
| | **Jumla Ndogo** | **68** | **13,795,613,529** | |
| 10 | Idara ya Huduma za Magereza (Fungu Na. 29) | **1** | 1,441,214,000 | Sekta nyengine |
| | **Jumla Ndogo** | 1 | **1,441,214,000** | |
| | **Jumla Kuu** | **41** | **558,633,102,859** | |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Sababu kuu ya kutelekezwa kwa miradi hii ni kutotolewa kwa fedha za kutosha. Hali hii husababisha matatizo ya kifedha miongoni mwa wakandarasi husika. Kutelekezwa kwa miradi hiyo kunasababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi, upotevu wa rasilimali fedha, na kushindwa kupata thamani na manufaa ya fedha za serikali zilizowekezwa katika miradi hiyo.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe fedha za miradi zinatolewa kwa wakati na kwa utoshelevu. Vilevile, fedha zitolewe ili kukamilisha miradi iliyotelekezwa ili kuhakikisha thamani ya fedha ambazo tayari zimetumika.**

### 6.1.4 Malipo ya Awali kutofanyika kwa Wakati - Sh. Bilioni 141.09

Kifungu cha 10(4) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kinazitaka taasisi nunuzi kuhakikisha kuwa malipo kwa wazabuni yanafanyika kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

Nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilianza utekelezaji wa mikataba 24, ambapo wakandarasi walistahili kupokea malipo ya awali yenye jumla ya Sh. bilioni 135.05, kulingana na masharti ya mikataba hiyo. Hata hivyo, licha ya wakandarasi kutimiza matakwa ya mkataba, malipo ya Sh. bilioni 12.09 (asilimia tisa) yalichelewa kwa kipindi cha kati ya siku 14 hadi 896, huku Sh. bilioni 122.97 (91%) zikiwa bado hazijalipwa, hivyo kushindwa kutimiza matakwa ya kimkataba kwa wakati.

Aidha, nilibaini kuchelewa kuanza kwa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 64.55 kutokana na kushindwa kwa taasisi za serikali kulipa malipo ya awali ya Sh. bilioni 6.04, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 20.**

**Jedwali Na. 20: Orodha ya Taasisi zenye Miradi Iliyocholewa Kuanza**

| Na. | Jina la Taasisi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Malipo ya Awali (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Gairo | 21,140,615,426 | 3,171,092,314 |
| 2 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 41,152,388,138 | 2,672,858,221 |
| 3 | Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) | 1,096,541,845 | 100,000,000 |
| 4 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi - (Uvuvi) - (Fungu Na. 64) | 1,169,089,986 | 100,000,000 |
| | **Jumla** | **64,558,635,395** | **6,043,950,535** |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Ninahusisha suala hili na utoaji usioridhisha wa fedha zilizotengwa kwenye bajeti kutoka Wizara ya Fedha.

Ucheleweshaji wa malipo ya awali ulikwamisha wakandarasi kuleta vifaa na kuanza kazi zilizopangwa. ambapo husababisha kuchelewa utekelezaji wa miradi, uwepo wa madai ya nyongeza ya muda, kuongeza gharama, migogoro, na malipo ya riba kutokana na kuchekeweshwa kwa malipo

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe Wizara ya Fedha inatoa fedha zilizotengwa kwenye bajeti kwa utimilifu na kwa wakati ili kuepuka uvunjaji wa masharti ya mikataba.**

### 6.1.5 Miradi ya Maji yenye Malipo ya Awali Yasiyo na Dhamana - Sh. Bilioni 20.67

Aya ya 15 ya Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2022 inaelekeza kuwa malipo ya awali yatatolewa tu na taasisi nunuzi baada ya kupokea dhamana ya malipo ya awali kutoka benki inayoaminika.

Nilibaini kuwa dhamana za malipo ya awali ya Sh. bilioni 20.67 kwa mikataba 21 ya miradi ya maji zilikwisha muda wake kabla ya kurejeshwa kikamilifu kwa dhamana hizo wakati mikataba ikiendelea. Hii inatokana na dosari katika usimamizi wa mikataba, ikijumuisha ukosefu wa ufuatiliaji wa hali ya dhamana na kushindwa kuwataka wakandarasi kuongeza muda wa dhamana ya malipo ya awali. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na.21**.

**Jedwali Na. 21: Orodha ya Taasisi zenye Malipo ya Awali Yasiyo na Dhamana**

| Na. | Taasisi | Idadi ya Mikataba | Malipo ya Awali yasiyo na Dhamana (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Maji | 1 | 9,612,834,696 |
| 2 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 19 | 7,950,755,745 |
| 3 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Handeni | 1 | 3,107,193,265 |
| **Jumla** | | **21** | **20,670,783,706** |

*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Malipo ya awali yasiyo na dhamana yanaiweka serikali katika hatari ya kupoteza fedha ikiwa mkandarasi atashindwa kutekeleza wajibu wake wa kimkataba.

**Ninapendekeza kwamba serikali iimarishe mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa taasisi za serikali zinadhibiti uhalali wa dhamana za malipo ya awali na kuhakikisha nyongeza zinazohitajika zinapatikana kabla ya muda wake kuisha.**

### 6.1.6 Malipo ya Ziada kwa Wakandarasi - Sh. Milioni 773.73

Masharti ya Jumla ya Mikataba yanamtaka msimamizi wa mradi kuhakikisha kuwa vipengele vilivyothibitishwa hapo awali vinaondolewa au kurekebishwa katika malipo yanayofuata ili kuakisi maendeleo sahihi ya kazi.

Nilibaini kuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ililipa zaidi kwa kiasi cha Sh. milioni 470.32 kwa mkandarasi, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kutokana na kushindwa kupunguza kiasi kilichothibitishwa na kulipwa hapo awali kwa mkataba wa ujenzi wa jengo la ofisi ya wizara.

Pia, nilibaini kuwa Wizara ya Maji, ilipokuwa ikitekeleza mkataba wa ulazaji wa mabomba makuu ya kusafirishia maji na mtandao wa usambazaji maji katika miji mitatu (Nyashimbo, Bariadi, na Lagangabili), ilithibitisha malipo kwa kiasi kilichozidi kiwango halisi cha kazi kilichopimwa na kurekodiwa kwenye karatasi ya vipimo. Hali hii ilisababisha malipo ya ziada ya Sh. milioni 303.41.

Malipo haya ya ziada yalitokana na ukaguzi duni wa hati za madai unaofanywa na wahandisi washauri pamoja na maafisa wa wizara husika. Kutumia fedha visivyo kwa namna hii kunapunguza rasilimali zinazopatikana kwa miradi mingine muhimu na kuathiri utekelezaji wa bajeti.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe kuwa wizara zinaimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika kupitia hati za madai za wakandarasi kabla ya kutoa idhini ya malipo, na kuwadai wakandarasi kurejesha kiasi kilicholipwa zaidi.**

### 6.1.7 Kuchelewa Kupokea na Kusambaza Mbegu za Ngano na Alizeti

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kusimamia vyema ununuzi wa bidhaa, huduma, au kazi. Hii inajumuisha kufuatilia gharama na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma unafanyika kwa wakati.

Licha ya matakwa haya, nilibaini kwamba Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ilitia saini mkataba tarehe 9 Novemba 2023 kwa ajili ya kununua tani 700 za mbegu za alizeti na tani 500 za mbegu za ngano, zenye thamani ya Sh. bilioni 13.12 na Sh. bilioni 4.25, mtawalia. Muda wa kupokea mbegu, kulingana na makubaliano, ilikuwa Februari 2024. Hata hivyo, mbegu za alizeti zilipokelewa tarehe 6 Juni 2024 ikiwa zilichelewa kufika kwa miezi minne zaidi ya kipindi kilichopangwa. Ukaguzi wa kalenda ya msimu wa mazao ya (ASA) ulionesha kuwa msimu wa kupanda mbegu za ngano na alizeti ni kuanzia Januari hadi Machi.

Uhakiki nilioufanya mwezi Agosti 2024 ili kutathmini usambazaji wa mbegu ulionesha kwamba kati ya tani 500 za mbegu za ngano zilizopokelewa, tani 267 zilikuwa zimesambazwa, huku tani 232 zikiwa bado katika hifadhi. Kwa mbegu za alizeti, tani 52 zilikuwa zimesambazwa, huku tani 648 zikiwa bado zimehifadhiwa.

Ucheleweshaji huu ulisababishwa na mipango duni ya ununuzi, usimamizi hafifu wa mikataba, na ukosefu wa uratibu mzuri kati ya muda wa ununuzi na kalenda ya upandaji wa mazao. Hii imesababisha wakulima kukosa msimu wa kupanda, jambo linaloweza kusababisha kupungua kwa mavuno na mbegu zilizobaki kwenye maghala huenda zikapoteza uwezo wa kuota endapo hazitatumika kwa wakati.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe kuwa mipango ya ununuzi ya ASA inaendana na kalenda ya upandaji wa mazao, ikijumuisha tahadhari kwa uchelewaji unaoweza kutokea, na ifuatilie utendaji wa wasambazaji kupitia ripoti za maendeleo na ufuatiliaji wa hatua muhimu. Aidha, mpango madhubuti wa usambazaji wa mbegu unapaswa kutekelezwa ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu kwa wakati unaofaa.**

### 6.1.8 Taasisi Zisizo na Mipango ya Ununuzi ya Mwaka na Ununuzi Usiozingatia Mipango

Kifungu cha 49 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, kinazitaka taasisi nunuzi kuandaa mpango wa ununuzi wa kila mwaka kwa ajili ya ununuzi yote na kuunganisha bajeti yake ya ununuzi na mpango wake wa matumizi.

Nilibaini kuwa taasisi tisa za serikali zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 1.52 bila kuwa na mpango wa ununuzi wa mwaka. Vilevile, taasisi 44 hazikutekeleza ununuzi wao uliopangwa, wenye thamani ya Sh. trilioni 2.03 na dola za Marekani 223,000. Aidha, taasisi nane zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. 11.00 bilioni nje ya mipango yao ya ununuzi. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho Na VII.**

Sababu kuu ya mapungufu haya yanatokana na mipango duni na isiyo sahihi, na ukosefu wa usimamizi ndani ya taasisi za serikali. Aidha, ucheleweshaji wa utoaji wa fedha ulisababisha kuahirishwa kwa ununuzi, hali iliyozilazimu taasisi kutumia fedha kwa namna isiyopangiliwa na ya dharura.

Kutotekelezwa kwa shughuli za ununuzi kunaathiri utoaji wa huduma, kuchelewesha utekelezaji wa miradi na kudhoofisha uwazi na uwajibikaji. Zaidi ya hayo, ununuzi wa dharura wa mara kwa mara unaongeza hatari ya ukosefu wa ufanisi, udanganyifu wa bei, na matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe wizara, idara na wakala za Serikali zinaandaa mipango halisi ya ununuzi. Pia, ihakikishe zinapata fedha kwa wakati na kwamba mipango ya ununuzi inatekelezwa ipasavyo ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwenye ununuzi.**

### 6.1.9 Kuanza kwa Miradi 40 bila kuwa na Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaelekeza taasisi nunuzi kutathmini athari za kimazingira kabla ya kuanza kwa taratibu za ununuzi.

Nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ilianzisha miradi 31 ya ujenzi wa barabara yenye thamani ya Sh. trilioni 1.55 kabla ya kupata vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii kutoka kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Pia, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ilianza miradi mitano ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 16.06. Vilevile, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo ilianzisha miradi minne yenye thamani ya Sh. bilioni 1.57, yote bila kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii.

Sababu kuu ya kutotekeleza hili ni shinikizo la kuharakisha utekelezaji wa miradi likichochewa na mchakato mrefu wa upatikanaji wa vyeti vya tathmini za mazingira na kijamii. Hata hivyo, kuendelea kutekeleza miradi bila kuwa na tathmini za kimazingira sahihi kunawaweka jamii katika hatari ya matatizo kama uchafuzi wa mazingira, kuharibika kwa mifumo ya ikolojia, na hatari za kiafya. Zaidi ya hayo, marekebisho yanayofanywa kwenye miradi iliyokwishaanza ili kuzingatia tathmini hizi husababisha hasara za kifedha na ucheleweshaji katika kutekeleza miradi.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa miradi ya ujenzi katika wizara, idara na wakala za Serikali inaanza mara tu baada ya kupata vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. Hatua hii ya tahadhari ni muhimu ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi yenye tija. Aidha, husaidia kuzuia hatari za kimazingira na matumizi yasiyofaa ya fedha za umma.**

### 6.1.10 Ununuzi wenye Thamani ya Sh. Bilioni 1.96 na Mabadiliko ya Kazi za Dola za Marekani 3,890,501.55 Zilifanyika bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni

Vifungu vya 55(2), 163(4), na 185(1) vya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 vinakataza taasisi kutoa zabuni bila idhini ya bodi ya zabuni. Pia, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kinahitaji bodi ya zabuni kupitia mabadiliko yote, nyongeza au marekebisho ya mikataba inayoendelea.

Nilibaini kuwa taasisi tano zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 1.96 bila kupata idhini kutoka kwa bodi za zabuni za taasisi husika, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 22.**

**Jedwali Na. 22: Taasisi zilizofanya Ununuzi bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Utengenezaji Samani ya SUMA JKT, Chang'ombe | 1,098,652,336 |
| 2 | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza | 531,233,640 |
| 3 | Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili, Mirembe | 217,767,541 |
| 4 | Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora | 101,621,728 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Musoma | 12,282,000 |
| **Jumla** | | **1,961,557,245** |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Aidha, nilibaini kuwa Wizara ya Maji, wakati ikisimamia utekelezaji wa Miradi ya Usambazaji Maji katika miji ya Kayanga, Chato, na Geita kwa mkataba wenye thamani ya dola za Marekani 97,920,000, ilionesha mabadiliko ya kazi kwenye hati za malipo za mkandarasi Na. 1 hadi 6 yenye thamani ya dola za Marekani 3,890,501.55. Hata hivyo, mkandarasi alitekeleza kazi zilizojitokeza kwenye vipengele vya Makadirio ya gharama ya kazi (BoQ) vyenye namba za marejeo 1.11/1.28, A6.1.15-18, B6.1.6-B6.1.8a, na C6.1.6-C6.1.7 bila kupata idhini ya awali kutoka kwa Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Maji.

Vilevile, nilibaini kuwa taasisi tisa za wizara, idara na wakala za Serikali zilifanya ununuzi mdogo wenye thamani ya Sh. bilioni 1.32 lakini haukuripotiwa kwa bodi za zabuni, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 23**.

**Jedwali Na. 23: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi Mdogo bila taarifa kwa bodi ya zabuni**

| Na. | Jina la Taasisi | Thamani ya Manunuzi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Madaktari Tanganyika | 492,490,782 |
| 2 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 297,046,167 |
| 3 | Hospitali ya Benjamin Mkapa | 153,944,318 |
| 4 | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 112,083,877 |
| 5 | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 101,298,537 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi | 81,903,424 |
| 7 | Chuo cha Ardhi Tabora | 39,841,540 |
| 8 | Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi | 34,182,093 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Manyara | 14,768,500 |
| **Jumla** | | **1,327,559,238** |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Hii inatokana na ukosefu wa mifumo madhubuti ya udhibiti ya ndani na kutozingatia kanuni za ununuzi zilizowekwa. Kuendelea na ununuzi na marekebisho ya mikataba bila idhini ya bodi ya zabuni kunadhoofisha usimamizi,

kuhatarisha uwazi, na kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe wizara, idara na wakala wa Serikali, zinafuata kanuni za ununuzi kwa kuhakikisha kuwa ununuzi unaidhinishwa na Bodi za Zabuni.**

### 6.1.11 Ununuzi Uliofanywa bila Kutumia Mfumo wa Kielekitroni Sh. Bilioni 33.1

Kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kufanya ununuzi katika mfumo wa kielekitroni wa ununuzi wa umma (NeST).

Nilibaini kuwa taasisi 41 za wizara, idara na wakala za Serikali zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 33.1 bila kutumia mfumo wa NeST. Orodha ya taasisi hizo imeoneshwa katika **Kiambatisho Na VIII**

Ninahusisha suala hili na ukosefu wa ufanisi wa kiufundi, utayari wa kukubali mabadiliko, na vikwazo vya kiufundi. Kutotumia mfumo wa kielekitroni wa ununuzi wa umma kunadhoofisha lengo la Serikali la kuboresha ufanisi, kupunguza muda wa mchakato wa ununuzi, na kupunguza hasara zinazoweza kujitokeza kwa kutozingatia ununuzi kupitia mifumo.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti ili kuhakikisha matumizi ya mfumo wa kielekitroni katika michakato ya ununuzi. Pia, ichukue hatua stahiki kwa wale waliokiuka kanuni za ununuzi.**

### 6.1.12 Ununuzi wa Sh. Bilioni 30.18 uliofanyika kwa njia ya utoaji wa zabuni kwa wazabuni maaalumu na njia ya mzabuni mmoja bila kuwa na sababu za msingi

Aidha, Kanuni ya 159 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa na Kanuni ya 60 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 zinaruhusu ununuzi kwa njia ya kutumia njia ya mzabuni mmoja ikiwa kuna idhini ya bodi ya zabuni na kuwapo kwa sababu au mazingira maalumu yenye kuruhusu njia hiyo.

Aidha, Kanuni ya 152 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inaeleza kuwa taasisi inayofanya ununuzi inaweza kuweka kikomo katika utoaji wa hati za zabuni kwa idadi ndogo ya waombaji wa zabuni waliobainishwa tu ikiwa kuna sababu halali kama zilizokubaliwa katika Kanuni hizo.

Nilibaini kuwa taasisi nne za serikali zilifanya ununuzi kwa kutumia njia ya mzabuni mmoja. Pia, taasisi moja ilitumia njia ya zabuni ya utoaji wa hati za zabuni kwa idadi ndogo ya waombaji wa zabuni waliobainishwa kwa bidhaa na huduma zenye jumla ya Sh. bilioni 30.18 bila kutoa sababu mahsusi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Ununuzi za 2013. Maelezo yapo katika **Jedwali Na. 24.**

**Jedwali Na. 24: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi kwa Kutoa Zabuni kwa Wazabuni Maalumu na Njia ya Mzabuni Mmoja Bila Kuwa na Sababu Mahsusi za Kutumia Njia Hizo**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) | Njia ya Ununuzi |
|---|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Barabara Tanzania | 29,524,129,454 | Mzabuni mmoja |
| 2. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu Na. 91) | 328,536,000 | Mzabuni mmoja |
| 3. | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 289,129,500 | Utoaji wa zabuni kwa wazabuni maalumu |
| 4. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Kiomboi | 27,233,100 | Mzabuni mmoja |
| 5. | Baraza la Wataalamu wa Maabara | 13,920,320 | Mzabuni mmoja |
| | **Jumla** | **30,182,948,374** | |

*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Ukosefu wa sababu mahsusi zinazotoa uhalali wa kutumia njia ya utoaji wa hati za zabuni kwa idadi ndogo ya waombaji wa zabuni au njia ya mzabuni mmoja unatokana na upungufu katika utekelezaji wa kanuni za ununuzi na usimamizi.

Utaratibu huu huleta madhara yafuatayo: huathiri haki na uwazi katika michakato ya ununuzi; huzuia ushindani; hupunguza nafasi za kupata bidhaa zenye ubora wa juu kwa bei shindani; na huongeza hatari ya udanganyifu wa bei na mfumuko wa bei. Hivyo, hudhoofisha usimamizi bora wa rasilimali na kuathiri uwazi na thamani ya pesa katika ununuzi wa umma.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa wizara, idara na wakala za Serikali zinazingatia kikamilifu sheria za ununuzi kwa kuhakikisha kuwa kuna sababu halali wakati wa kutumia njia za ununuzi kwa njia ya mzabuni mmoja au njia ya utoaji wa hati za zabuni kwa idadi ndogo ya waombaji wa zabuni. Hali hii itaongeza ushindani, uwazi, na thamani ya fedha katika mchakato wa ununuzi.**

### 6.1.13 Ununuzi Uliofanyika bila Mikataba Sh. Milioni 420.31

Kanuni ya 164 (2)(j) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaeleza kwamba, barua ya mwaliko wa nukuu za bei na kiambatisho chochote kitakuwa na fomu ya mkataba au hati ya ununuzi wa ndani (LPO) itakayojumuisha masharti yote ya malipo.

Nilibaini kuwa taasisi nane za serikali zilifanya malipo ya Sh. milioni 420.31 kwa wazabuni wa bidhaa na huduma mbalimbali bila kuwa na mikataba au hati za ununuzi, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Orodha ya Taasisi Zilizofanya Ununuzi bila Mikataba**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Huduma za Uhamiaji (Fungu Na. 93) | 179,279,985 |
| 2 | SUMAJKT - Kampuni ya Ushonaji | 76,455,398 |
| 3 | Hospitali ya Benjamin Mkapa | 41,425,000 |
| 4 | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | 35,312,100 |
| 5 | Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora | 31,048,974 |
| 6 | Hospitali ya Kanda, Mtwara | 28,556,000 |
| 7 | Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu Na. 18) | 20,242,520 |
| 8 | SUMA JKT - Kampuni ya Usafi na Unyunyuziaji Dawa | 8,000,000 |
| **Jumla** | | **420,319,977** |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Ukosefu wa ufuatiliaji ndani ya wizara, idara na wakala za Serikali ulisababisha ununuzi wa bidhaa bila mikataba au hati za ununuzi.

Ununuzi unaofanywa bila mkataba au hati ya ununuzi unaweza kuleta migogoro ya kisheria kwa sababu ya kukosekana kwa makubaliano ya kisheria kati ya taasisi nunuzi na wazabuni.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa wizara, idara, na wakala za Serikali zinaingia mikataba rasmi na wazabuni, ikijumuisha vigezo na masharti ya kuzingatiwa na pande zote.**

### 6.1.14 Mikataba yenye thamani ya Sh. Bilioni 16.05 iliyosainiwa bila Kupekuliwa na Wanasheria

Kanuni ya 59(1) na 60(1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa na kanuni ya 2 na 3 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016 mtawalia inabainisha kuwa mikataba rasmi ambayo thamani yake ni Sh. bilioni moja na zaidi au inayofanywa kupitia zabuni ya ushindani wa kimataifa inapaswa kupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mkataba wa chini ya

Sh. bilioni moja unapaswa kupekuliwa na mwanasheria wa taasisi nunuzi kabla ya wahusika kusaini mikataba hiyo.

Nilibaini kuwa taasisi saba za wizara, idara na wakala za Serikali zilitia saini mikataba yenye thamani ya jumla ya Sh. bilioni 16.05 bila kupata maoni (kupekuliwa) ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au wanasheria wa taasisi husika. Kati ya kiasi hiki, Sh. bilioni 4.38 inahusiana na mikataba ambayo haikupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Sh. bilioni 11.66 zinahusiana na mikataba ambayo haikupekuliwa na maafisa wa sheria wa taasisi. Maelezo yanaonekana katika **Jedwali Na. 26**.

**Jedwali Na. 26: Taasisi zilizokuwa na Mikataba Isiyopekuliwa na Wanasheria**

| Na. | Taasisi | Jumla ya Gharama za Mikataba (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza | 6,249,625,540 |
| 2 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46) | 5,649,458,707 |
| 3 | SUMA JKT - Kampuni ya Ujenzi | 3,257,627,384 |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Busega | 813,827,451 |
| 5 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu | 67,551,962 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni | 10,800,009 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mount Meru | 8,036,870 |
| **Jumla** | | **16,056,927,923** |

***Chanzo***: *Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Tatizo hili linatokana na taasisi za serikali kutomshirikisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali au maafisa wa sheria wa taasisi husika.

Hali ya mikataba kutopitiwa na wanasheria kunaiweka serikali katika hatari ya kuingia makubaliano ya kisheria ambayo yanaweza kutokuwa na maslahi bora kwa umma. Hii inaweza kusababisha migogoro ya kisheria na hasara za kifedha, na kutia shaka uaminifu na uwazi katika mchakato wa ununuzi.

**Ninapendekeza kwamba taasisi za serikali ziimarishe usimamizi na kuhakikisha kwamba mikataba yote inapekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au maafisa wa sheria wa taasisi husika kabla ya kusainiwa ili kuepuka matatizo ya kisheria na matumizi yasiyo ya lazima.**

### 6.1.15 Fidia zisizolipwa kwa Watu Walioathiriwa na Miradi Sh. Bilioni 27.81

Kanuni ya 13 (1-3) ya Kanuni ya Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa ajili ya Fidia) ya mwaka 2001 inataka kiasi ambacho kitalipwa kama fidia kiwe cha haki, cha kutosha, na kilipwe kwa wakati ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya

uthamini; vinginevyo, riba ya kiwango kinachotolewa na benki za biashara kwenye amana za kudumu kitatozwa hadi fidia hizo zitakapolipwa.

Nilibaini kuwa fidia kwa Watu Walioathiriwa na Miradi (PAPs) zenye jumla ya Sh. bilioni 27.81 kwa miradi mitatu ya miundombinu ya barabara na mradi mmoja wa maji haikulipwa licha kuendelea kutekelezwa kwa miradi hiyo na kupita kwa muda wa ripoti za tathmini, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Wakati wa ukaguzi wa miundombinu ya barabara, nilibaini kwamba fidia ya Sh. bilioni 1.21 haikulipwa kwa Watu Walioathirika na Miradi (PAPs) kwa Mradi wa Barabara ya Same–Kisiwani-Mkomazi hadi Novemba 2024, licha ya ripoti ya tathmini kuwa imepitwa na muda wa miezi sita. Vilevile, fidia ya jumla ya Sh. bilioni 5.52 haikulipwa kwa waathirika 1,799 kwenye Mradi wa Barabara ya Sabasaba–Sepuka-Ndago-Kitaza, pamoja na Sh. bilioni 13.5 haikulipwa kwa waathirika 1,256 kwenye miradi mbalimbali ya miundombinu ya barabara za Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). TANROADS pia ilikuwa na deni la Sh. bilioni 6.61 kwa fidia kwa wamiliki wa ardhi hadi Septemba 2024, ambapo fedha hizi zilikuwa zimeombwa kutoka Wizara ya Fedha tangu Desemba 2023 lakini hazikutolewa.

Kwa upande mwengine, wakati wa utekelezaji wa mradi wa Handeni wa kusambaza maji kwa vijiji 27 katika Wilaya za Muheza, Handeni na Mji wa Korogwe, nilibaini kuwa watu 554 walioathiriwa na mradi (PAPs), pamoja na Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko cha Mgombezi hawajalipwa fidia ya jumla ya Sh. milioni 971.47, licha ya mradi kufikia 60% ya utekelezaji.

Ucheleweshaji huu wa malipo ya fidia unachangiwa na kuchelewa kutolewa kwa fedha kutoka Wizara ya Fedha. Kuchelewa kwa Fidia hizi kunaweza kusababisha kutozwa kwa riba au kufanya tathmini upya ili kuendana na kiwango cha malipo ya fidia. Aidha, kunaweza unasababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi na inaweza kuleta ongezeko la gharama.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa Wizara ya Fedha inatoa fedha za fidia kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba na uhitaji wa kufanya tathmini upya kwa watu waliathiriwa na miradi.**

### 6.1.16 Bidhaa na Huduma zilizochelewa kupokelewa kutoka kwa wazabuni zenye thamani ya Sh. Bilioni 6.50

Kanuni ya 242 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaeleza kuwa pale ambapo upokeaji wa bidhaa unachelewa au kuna uwezekano wa kucheleweshwa zaidi ya muda uliowekwa katika mkataba, taasisi nunuzi

itatafuta taarifa na maelezo kutoka kwa wauzaji au mawakala wao inaweza kutoza gharama ya ucheleweshaji kulingana na matakwa ya mkataba.

Nilibaini kwamba taasisi saba za serikali zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 6.50 ambazo hazikuwa zimepokelewa kwa kipindi cha kuanzia miezi miwili hadi miezi 19, licha ya mikataba kati ya taasisi hizo na wazabuni kuwa imeisha au kuzidi muda ulioongezwa wa kuwasilisha bidhaa na huduma hizo. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 27**.

**Jedwali Na. 27: Orodha ya Taasisi ambazo Zimechelewa Kupokea bidhaa zilizonunuliwa**

| Na. | Taasisi | Bidhaa | Kiasi (Sh.) | Muda Uliochelewa (Miezi) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | Mabomba ya maji | 1,897,451,234 | Miezi minane hadi 14 |
| 2 | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) | Mitambo ya usindikaji wa mbegu | 1,788,321,000 | Miezi minne |
| 3 | Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | Vifaa vya umeme na vipuri mbalimbali | 944,429,542 | Miezi saba hadi 19 |
| 4 | Wizara ya Afya (Fungu Na. 52) | Vifaa vya lishe | 765,000,000 | Miezi miwili |
| 5 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Vitabu vya sheria | 514,270,444 | Miezi miwili |
| 6 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46) | Vifaa na mashine za kujifunzia | 305,487,879 | Miezi minane |
| 7 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) (Fungu Na. 99) | Vifaa na mashine za kilimo | 293,000,000 | Miezi miwili |
| **Jumla** | | | **6,507,960,099** | |

***Chanzo**: Ripoti za Ukaguzi 2023/24*

Kuchelewa kwa mapokezi ya bidhaa zinazonunuliwa kunaonesha kwamba taasisi za serikali bado hazijachukua hatua madhubuti za kurekebisha ili kuhakikisha kwamba masharti ya mikataba yanatekelezwa na wazabuni. Hali hii inasababisha taasisi hizi kukosa uimara, hivyo kuathiri utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza kwamba taasisi za serikali ziweke mikakati ya kuhakikisha bidhaa zilizonunuliwa zinapatikana kwa wakati na kuwatoza wazabuni fidia kwa kipindi cha ucheleweshaji kulingana na masharti ya mkataba.**

### 6.1.17 Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) kuchelewesha Ununuzi na Usambazaji wa Magari 44 yenye Thamani ya Sh. Bilioni 6.8

Mkataba kati ya Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA) na Wazabuni inabainisha kuwa muda wa kimkataba wa kuwasilisha magari yaliyoagizwa na taasisi za serikali ni kati ya miezi mitatu hadi sita.

Nilibaini kuwa GPSA ilikuwa na jumla ya amana ya Sh. bilioni 6.8 kwa magari 44 ambayo hayakuwa yamewasilishwa hadi kufikia mwisho wa mwaka 2023/24. Kati ya kiasi hiki, Sh. bilioni 5.6 zilihusiana na magari 34 ambayo hayakuwa yamewasilishwa kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi miwili, huku Sh. bilioni 1.2 zikihusiana na magari 10 ambayo yalikuwa yamechelewa kuwasilishwa kwa zaidi ya miaka miwili.

Ninahusisha ucheleweshaji huo na ufuatiliaji na usimamizi mdogo kutoka kwa uongozi wa GPSA hivyo huchangia wazabuni hao kutotimiza matakwa ya mkataba. Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa magari unaathiri shughuli za taasisi, hususan katika kuwezesha huduma za usafirishaji.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe kuwa GPSA inaboresha mchakato wa ufuatiliaji na usimamizi ili kuhakikisha wauzaji wanatekeleza majukumu yao ya kimikataba na magari yanafika kwenye Taasisi za Umma kwa wakati.**

### 6.1.18 Ukosefu wa Usimamizi Madhubuti wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) katika Miradi ya Ujenzi wa Vivuko vya TEMESA Unahatarisha Ubora na Uzingatiaji wa Viwango vya Usalama

Mnamo tarehe 1 Machi 2023, kupitia Mkataba Na. AE/006/2023-2024/HQ/CS/CN-18, TEMESA iliingia makubaliano na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri zinazohusisha ukaguzi wa miradi, usimamizi, na udhibiti wa kazi za ujenzi na ukarabati wa vyombo vinane. Vyombo hivyo ni: Mv. Magogoni, kivuko kipya cha Nyamisati, kivuko kipya cha Buyagu, Mv. Bwiro-Bukondo, Mv. Kisorya-Rugezi, Mv. Nyakariro-Kome, Mv. Ijinga-Kahangala, na Teksi ya bahari mpya ya Magogoni. Mkataba huo ulikuwa na thamani ya Sh. bilioni 1.45 na ulipangwa kutekelezwa kuanzia tarehe 16 Oktoba 2023 hadi 15 Oktoba 2026.

Hata hivyo, nimebaini kuwa DMI ilipatiwa mkataba wakati tayari vyombo vitano vilikuwa katika hatua mbalimbali za ukarabati chini ya wakandarasi waliokuwa tayari wamepewa zabuni. Kutokana na hali hii, sikuweza kubaini wazi wigo wa majukumu ya DMI kwa vyombo hivyo. Hali hii imeleta ugumu kwenye tathmini ya ufanisi na majukumu ya DMI na huduma zake.

Zaidi ya hayo, nimegundua kuwa DMI haikuwa ikitembelea mara kwa mara maeneo ya ujenzi. Tangu kusainiwa kwa mkataba huo mnamo Machi 2023, DMI ilifanya ziara mbili pekee katika maeneo ya ujenzi, mnamo 11 Januari 2024 na 18 Machi 2024. Hali hii ilidhihirika katika Mv. Kisorya-Rugezi na Mv. Bwiro-Bukondo, ambapo wakandarasi walikamilisha kazi za ufungaji wa nyaya za umeme mnamo Machi 2024 bila uwepo wa DMI wala idhini yake.

Licha ya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba, DMI bado ililipwa jumla ya Sh. milioni 154.07 hadi kufikia tarehe 14 Februari 2024. Malipo haya yanaashiria uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za umma kutokana na usimamizi duni wa DMI. Zaidi ya hayo, ukosefu wa usimamizi wa kutosha ni hatari kwa ubora wa kazi za ujenzi na ukarabati, hivyo kuibua wasiwasi kuhusu iwapo vyombo hivyo vitakidhi viwango vya kiufundi na usalama kwa matumizi ya baharini.

**Ninapendekeza serikali iimarishe ufuatiliaji kwa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) ili kuhakikisha taasisi hiyo inatembelea mara kwa mara maeneo ya ujenzi na kutoa mwongozo wa kiufundi kwa wakati kwa wakandarasi. Hatua hii itasaidia kuzuia kazi duni ambayo inaweza kusababisha hasara ya fedha za umma.**

# SURA YA SABA



## Sekta ya Miundombinu

# SEKTA YA MIUNDOMBINU

## 7.1 Utangulizi

Sekta ya ujenzi ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, kwa kusaidia ukuaji wa uchumi na ustawi wa kijamii kupitia miradi ya miundombinu kama vile barabara, majengo ya umma, na mifumo ya usafiri.

Sura hii inaeleza kuhusiana na usimamizi na matumizi ya fedha za umma katika kazi za barabara, ujenzi wa majengo, na kazi za mitambo chini ya uangalizi wa Wizara ya Ujenzi na wakala zake ambazo ni; Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA). Ukaguzi wangu ulitathmini mipango ya miradi, bajeti, utekelezaji, na usimamizi kwa kuzingatia ufanisi, uwezo, na uwajibikaji. Masuala yanayohusiana na ununuzi yameelezewa kwa kina katika Sura ya Sita ya ripoti hii.

Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa kina wa matokeo ya ukaguzi na kuelezea masuala maalumu yaliyojitokeza katika utekelezaji, na usimamizi wa mipango muhimu ya miradi ya miundombinu.

## 7.2 Upekuzi Hafifu wa Mkandarasi wa Nje umesababisha Kuvunjwa kwa Mkataba na Kuchelewa Kurejeshwa kwa Sh. bilioni 13.72

Mnamo tarehe 27 Desemba 2022, Wakala wa Barabara Tanzania ilisaini mkataba Na. TRD/HQ/1015/2022/23, wenye thamani ya Sh. bilioni 38.36 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa kilomita 32 ya barabara ya Ibanda - Kiwira

Mkataba huo ulianza tarehe 31 Machi 2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Machi 2025. Baada ya mkataba huo kusainiwa, mkandarasi alipokea Sh. bilioni 3.72 zikiwa ni malipo ya awali. Hii ilikuwa baada ya kuwasilisha dhamana ya benki iliyotolewa na benki ya kigeni kutoka nchi ya Azerbaijan, iliyopokelewa kupitia benki ya kibiashara hapa Tanzania.

Hapo awali Wakala wa Barabara Tanzania ilifanya upekuzi wa mkandarasi (*due diligence*) nchini Uturuki kati ya mwezi Agosti na Septemba 2022, kwa mujibu ya matakwa ya Kanuni ya 118(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

kufikia mwezi Aprili 2024, maendeleo ya mkandarasi huyo yalikuwa 2.27% tu, hivyo kusababisha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya upekuzi mwingine wa kina wa nyaraka na uwezo wa mkandarasi. Upekuzi huu mpya ulibainisha kuwa mkandarasi alikuwa amewasilisha taarifa za uongo wakati wa mchakato wa zabuni wa awali. Uongo huo ulibainika katika vipengele vya:

taarifa za miradi aliyokamilisha, nyaraka za kugushi za Bodi ya Wakurugenzi, na hati ya kiapo cha uwakala (*power of attorney*) iliyo na saini ya kughushi ya mmojawapo wa wakurugenzi. Mapitio haya pia yalibaini kuwa upekuzi wa awali haukufanyika kwa ufanisi, kwani ulifanyika bila ya hadidu za rejea toshelevu, hivyo kushindwa kubaini makosa haya.

Aidha, kutokana na udanganyifu huo, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilitumia vifungu vya 67.1 na 67.2(i) vya Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kusitisha mkataba tarehe 09 Mei 2024. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inatakiwa kurejeshewa Sh. bilioni 13.72. Kiasi hiki kinajumuisha malipo ya awali yaliyozingatia kazi ziliyofanywa na mkandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.29, dhamana ya utendaji kazi ya Sh. bilioni 3.84, na thamani ya kazi ambazo hazijakamilika Sh. bilioni 6.59.

Hata hivyo, mkandarasi huyo amepinga kiasi hicho cha fedha na kusababisha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kulifikisha suala hilo katika Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) kwa ajili ya usuluhishi. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) iliamua kufuatilia uwezekano wa kurejeshewa madai ya dhamana ya malipo ya awali na dhamana ya utendaji kazi ya Sh. bilioni 7.56 kutoka benki mdhamini iliyopo nchini Azerbaijan. Hata hivyo, mchakato wa upatikanaji wa Kiasi hicho umekuwa mgumu kwa kuwa Benki hiyo ilitangazwa kufilisika na iko chini ya msimamizi wa ufilisi (*receivership*) tangu tarehe 24 Oktoba 2023. Ingawa dhamana hizi zilipokelewa kupitia Benki ya hapa Tanzania, jukumu la benki hii katika mchakato huu lilikuwa kuwezesha upatikanaji wa dhamana, hivyo haikubeba dhamana yoyote au kutoa udhamini wowote katika mchakato huu.

Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imemtaarifu Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na inasubiri maoni ya kisheria. Wakati huohuo, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imearifiwa kumfungia mkandarasi huyo kutokana na vitendo vyake vya udanganyifu.

Suala hili linaonesha upungufu uliopo katika Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) hususan Katika zoezi la upekuzi wa taarifa za wakandarasi wa nje. Kushindwa Kufanya upekuzi kwa usahihi kumesababisha mradi kuchelewa, mkataba kusitishwa na Hasara ya Sh. bilioni 13.72.

**Kwa wakati ujao, Wakala wa Barabara Tanzania inapaswa kuimarisha mchakato wake wa uhakiki kwa wakandarasi wa nje kwa kuandaa hadidu za rejea kikamilifu na kwa kina kabla ya zoezi la upekuzi kufanyika ili kuepuka kujirudia kwa makosa kama hayo katika siku zijazo. Pia, ninapendekeza kuwa vyombo vya uchunguzi vichunguze suala hili ili kubaini iwapo kulikuwa**

**na viashiria vya jinai wakati wa mchakato wa upekuzi wa awali uliofanyika kuthibitisha uwezo wa mkandarasi.**

## 7.3 Hasara Iliyotokana na Madai ya Ucheleweshaji Malipo na Marekebisho ya Mkataba - Sh. Bilioni 1.79

Mnamo tarehe 27 Juni 2020, Wakala Barabara Tanzania (TANROADS) iliingia mkataba na Mkandarasi, China Railway 15 Bureau Group Corporation, chini ya Mkataba Na. TRD/HQ/1052/2019/2020 kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Nachingwea – Ruangwa – Nanganga (kilomita 106) kwa kiwango cha lami, Sehemu Na. 2: Barabara ya Ruangwa - Nanganga (kilomita 53.2). Bei ya awali ya mkataba ilikuwa Sh. bilioni 50.34, ikijumuisha kodi zote za ndani, ushuru, ada, na mrabaha, isipokuwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya 18% (sawa na Sh. bilioni 8.94). Muda wa mkataba wa awali ulikuwa miezi 24, ikiwa ni pamoja na kipindi cha miezi mitatu cha maandalizi ya kazi za ujenzi. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kuanzia tarehe 20 Agosti 2020 hadi tarehe 19 Novemba 2022.

Ukaguzi wangu ulibaini gharama ya mkataba na tarehe ya kukamilika ilihuishwa mara kadhaa, na kusababisha gharama ya mkataba kurejewa na kufikia Sh. bilioni 52.13 na tarehe mpya ya kukamilika kuwa 13 Februari 2025. Marekebisho haya, kimsingi, yalihusishwa na kuchelewa kwa malipo ya awali na malipo ya muda na mabadiliko katika mawanda ya kazi. Kutokana na hali hiyo, mkandarasi alidai fidia ya Sh. bilioni 1.79, jambo ambalo Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haijalipinga. Fidia hii inaashiria upotevu mkubwa wa fedha za walipakodi ambazo zingeweza kuepukwa iwapo serikali ingetoa fedha kwa wakati kuwezesha Wakala kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati na kufanyika kwa ufanisi ungeweza kupunguza marekebisho.

**Kuzuia hasara kama hii kutokea tena, ninapendekeza kuwa serikali ihakikishe inatoa fedha kwa wakati ili kuwezesha malipo ya wakandarasi kufanyika kwa wakati, hivyo kuzuia kuongezeka kwa gharama za ziada. Aidha, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inapaswa kuimarisha mbinu zake za kubuni miradi ili kupunguza mabadiliko ya mawanda na kuepuka marekebisho mengi kwenye mikataba.**

## 7.4 Changamoto za Uendeshaji katika Mizani Minne Kumesababisha Magari 26,300 kutopimwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Mzigo wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016, magari yote yenye uzito wa jumla wa tani 3.5 au zaidi yanatakiwa kupimwa katika vituo vya kupima uzito (mizani) vilivyo kando ya mtandao wa barabara wa kimkoa na kitaifa. Hata hivyo, licha

ya masharti haya ya kisheria, nilibaini magari 26,300 yalipita bila kupimwa uzito, yakiwamo magari 1,049 katika Kituo cha Nala (Dodoma), magari 1,652 katika Kituo cha Makuyuni (Arusha), magari 671 katika Kituo cha Ndumbwe (Mtwara), na magari 22,928 katika Kituo cha Mtukula (Kagera). Hii ilitokana na changamoto za kiutendaji kama vile kukatika kwa umeme, kuharibika mara kwa mara kwa vifaa, na matatizo ya urekebishaji wa mizani. Uvunjifu huu wa sheria unaathiri utekelezaji wa kanuni za udhibiti wa mizigo na kuongeza hatari ya uharibifu wa barabara kutokana na magari yanayobeba mizigo yenye uzito uliopitiliza.

**Ninapendekeza yafuatayo kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS): itafute suluhisho la kutunza umeme la muda mrefu; iongeze matengenezo ya kuzuia uharibifu; na ifanye marekebisho ya mara kwa mara kwa vifaa vya kupima uzito ili kuhakikisha kuwa uzito wa magari unapimwa kwa usahihi na kwa njia endelevu.**

## 7.5 Mfumo wa Vibali vya Mzigo Maalumu Hauna Ufanisi na Umesababisha Taarifa za Vibali Kutokuaminika

Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Udhibiti wa Mzigo wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Mizigo Maalumu) ya mwaka 2018, mtu yeyote anayekusudia kusafirisha mzigo maalumu (wa kawaida, usio wa kawaida, hatari, usio thabiti, na mizigo mikubwa) anatakiwa kuomba kibali maalumu cha kusafirisha mzigo husika katika Wizara ya Ujenzi (Fungu Na. 98) kupitia mfumo maalumu wa maombi ya vibali vya mzigo.

Hata hivyo, nilibaini vibali 792 vilivyotolewa kutoka kwa mfumo maalumu wa maombi ya vibali katika Wizara ya Ujenzi (Fungu Na. 98) vilihakikiwa zaidi ya mara moja katika vituo 41 vya kupima uzito (mizani). Uhakiki wa nakala unaonesha kuwa wasafirishaji wametumia vibali hivyo kwa zaidi ya safari moja, na kusababisha hasara ya mapato ya serikali yenye thamani ya Sh. milioni 41.18. Kurudia kutumia vibali pia kunaonesha udhaifu katika ufanisi wa mfumo huu na kuibua shaka ya usahihi na kuaminika kwa mchakato wa kuthibitisha taarifa za vibali.

**Ninapendekeza Wizara ya Ujenzi iboreshe mfumo maalumu wa maombi ya vibali ili kuwezesha ufuatiliaji wa wakati halisi, kutambua vibali vilivyothibitishwa, na kuboresha ujumuishaji wa mfumo huo katika vituo vya kupima uzito kwa shughuli sahihi na bora zaidi.**

## 7.6 Mizani Muhimu kuharibika Mara kwa Mara na Kutokuwapo kwa Mzani wa Kudumu katika Barabara ya Mwigumbi-Bariadi (T036)

Nilibaini kuwapo kwa hitilafu za mara kwa mara kwa mizani ya Vigwaza na Makofia iliyopo chini ya Ofisi ya Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani kutokana na ukosefu wa matengenezo ya kuzuia uharibifu. Hadi kufikia wakati wa ukaguzi wangu, mwezi Novemba 2024, menejimenti ya Wakala wa Barabara ilikuwa haijatatua matatizo haya. Aidha, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara bado haijajenga mzani wa kudumu katika barabara ya Mwigumbi-Bariadi (T036) licha ya kuongezeka kwa kesi za magari kusafirisha mizigo kupita kiasi zilizobainika kupitia mzani wa kuhamishika. Ucheleweshaji huu unaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara, hivyo kusababisha gharama kubwa za matengenezo ya barabara hapo baadaye.

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara Tanzania ishughulikie matatizo ya uendeshaji katika vituo vya kupima uzito vya Vigwaza na Makofia na kuweka rasilimali za kujenga mzani wa kudumu katika Barabara ya Taifa ya Mwigumbi-Bariadi ili kudhibiti na kuzuia magari kusafirisha mizigo kupita kiasi.**

## 7.7 Kuwapo kwa Mgogoro na Watoahuduma Kumesababisha TANROADS Kukosa Taarifa za Mizani

Nilibaini katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilikuwa na mgogoro ambao haujatatuliwa na watoahuduma (Inter Consult Limited, Techno Image Limited, na Duku Telecoms and Electronics Company Limited) kuhusu upatikanaji wa taarifa za mizani kutoka katika mfumo wa mizani uitwao 'Data Bridge' katika vituo 10 vya kupima uzito (Vigwaza, Mikese, Mikumi, Njuki, Himo, Mpemba, Mingoyo, Mutukula, Makuyuni, na Nyakahura).

Mgogoro huu unatokana na haki za utambulisho za mfumo, kwani Wakala wa Barabara Tanzania inataka haki za utambulisho za msimamizi ili kuhamisha taarifa za mzani kwenye kanzidata yao ya pili baada ya kanzidata ya kwanza iliyoko kufikia kikomo.

Hata hivyo, watoahuduma wanadai kuwa kumpa Wakala wa Barabara Tanzania haki za utambulisho za msimamizi kunaweza kusababisha kunakili mfumo wao, hivyo wakala inaweza kuunda mfumo unaoshindana na mfumo wa watoahuduma. Hata hivyo, madai haya hayajathibitishwa wakati wa ukaguzi. Kutopatikana kwa taarifa hizo kumesababisha Wakala wa Barabara Tanzania kukosa taarifa za udhibiti wa mizigo iliyozidi kiwango katika vituo vya mizani 10 kuanzia tarehe 09 Januari 2024. Wakala wa Barabara Tanzania imewasilisha

suala hili katika Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) kwa ajili ya usuluhishi, lakini uamuzi bado haujafikiwa.

**Ninapendekeza Wakala wa Barabara ishirikiane kikamilifu na Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) ili kuharakisha utatuzi wa mgogoro huu wa upatikanaji wa haki za uthibitisho na watoahuduma. Hii itasaidia uhamishaji wa taarifa za mizani kufanyika kwa ufanisi bila kuathiri haki miliki za watoahuduma.**

## 7.8 Kupunguzwa kwa Bajeti na Ukosefu wa Fedha Kuliathiri Utendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania katika Usimamizi wa Miradi ya Barabara

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala wa Barabara Tanzania ilikumbana na changamoto ya kupunguzwa kwa bajeti na ukosefu wa fedha, jambo lililoathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa shughuli zake. Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kazi za barabara ilikuwa Sh. trilioni 1.09, pungufu ya Sh. bilioni 780 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita (2022/23) ya Sh. trilioni 1.87. Licha ya kupunguzwa kwa bajeti, nilibaini kati ya bajeti ya matengenezo ya mwaka huu ya Sh. bilioni 534.66, Wakala wa Barabara Tanzania ilipokea Sh. bilioni 280.47, sawa na 52% tu, kutoka kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB).

Vilevile, bajeti ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya barabara za kimkakati ya taifa iliyotengwa ni Sh. bilioni 420.88, lakini serikali ilitoa Sh. bilioni 403.40 tu. Kiasi hiki kilijumuisha Sh. bilioni 340.63 zilizotengwa kwa ajili ya malipo ya madai ya wakandarasi yaliyohakikiwa ya mwaka wa fedha 2022/23, huku Sh. bilioni 74.48 zikiwa fedha maalumu zilizotolewa kwa ajili ya janga la El-Nino na kimbunga cha Hidaya pamoja na malipo ya madai ya mashitaka. Kwa hiyo, Sh. bilioni 11.71 tu, sawa na 3% ya bajeti ya mwaka huu (2023/24), zilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za bajeti za mwaka 2023/24.

Ukosefu huu mkubwa wa fedha ulisababisha upungufu katika utekelezaji wa miradi ya barabara ya kimkakati na shughuli za matengenezo katika ofisi za mikoa za Wakala wa Barabara. Aidha, ulisababisha kuongezeka kwa madai ya wakandarasi na malipo ya riba kutoka Sh. bilioni 34.83 katika mwaka wa kifedha uliopita (2022/23) hadi kufikia Sh. bilioni 38.75 katika mwaka wa fedha 2023/24. Kadhalika, ulisababisha kusimamishwa na kutelekezwa kwa miradi muhimu ya barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 495.24, kama ilivyoelezwa kwa kina zaidi katika Sura ya Sita. Pamoja na hayo, masuala yafuatayo yalibainika:

## 7.9 Usimamizi Usioridhisha wa Wakandarasi katika Kushughulikia Upungufu wa Matengenezo ya Barabara

Pia nilibaini kuwa, kati ya bajeti ya usimamizi wa kazi za barabara zenye thamani ya Sh. bilioni 22.18 kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Wakala wa Barabara Tanzania ilipokea Sh. bilioni 10.7, sawa na 48%. Kutokana na bajeti hii ndogo ya usimamizi, Wakala wa Barabara Tanzania ilishindwa kusimamia ipasavyo mikataba 44 ya matengenezo ya barabara katika ofisi 16 za mkoa.

Ukosefu huu wa usimamizi umesababisha wakandarasi kupuuza kushughulikia kasoro sugu na mpya za barabara, kama vile uchakavu wa uso wa barabara, nyufa, matatizo ya mifereji ya maji, kushindwa kwa muundo wa barabara, mashimo, michirizi (*rutting*), vumbi, na mikwaruzo (*corrugations*) katika mtandao wa barabara kuu na za mikoa kabla ya kumalizika kwa kipindi cha matazamio.

Usimamizi huu usioridhisha unahatarisha muda mrefu wa kudumu kwa barabara na kuongeza uwezekano wa hitaji la matengenezo makubwa na yenye gharama kubwa zaidi katika siku zijazo.

**Kutokana na upungufu huu, ninapendekeza serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya Barabara. Aidha, ihakikishe fedha zinatolewa kwa wakati. Katika hali ya bajeti kutokuwa ya kutosha, serikali inapaswa kuepuka kuanzisha miradi mipya; badala yake, kipaumbele kiwe katika kukamilisha miradi inayoendelea. Mbinu hii itasaidia kupunguza ucheleweshaji wa miradi, kupunguza madai ya wakandarasi yasiyolipwa kwa wakati, na kupunguza mzigo wa kifedha kwa walipakodi unaosababishwa na ongezeko la gharama za riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo.**

## 7.10 Kutokutumika kwa Gari la Uchunguzi wa Barabara katika Tathmini ya Ubora wa Tabaka la Lami kwa ajili ya Mipango ya Matengenezo

Kutokana na uharibifu wa mara kwa mara wa sehemu za barabara zilizojengwa kwa lami kabla ya kufikia umri wao wa muundo, Wizara ya Ujenzi (Fungu Na. 98) ilinunua gari la kisasa la uchunguzi na kulikabidhi kwa Wakala wa Barabara Tanzania mnamo tarehe 17 Desemba 2021. Gari hilo lina thamani ya Sh. bilioni 1.3.

Gari hili limefungwa vifaa vyote muhimu vya tathmini na uchunguzi wa barabara za lami na lilitumika kufanya tathmini za dharura za barabara za lami katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Barabara ya Same-Himo, na Barabara ya Kimara-Kibaha yenye njia mbili (km 19.2).

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2023/24, gari hili halikutumika ipasavyo kutokana na ukosefu wa bajeti. Nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ilitenga bajeti ya Sh. milioni 548.90 kwa ajili ya tathmini za barabara za lami za jumla ya kilomita 1,410.6 katika barabara nane muhimu za mikoa minne (Arusha, Tabora, Morogoro, na Pwani). Hata hivyo, ni Sh. milioni 76.1 tu, sawa na 14%, ndizo zilizotolewa. Kutolewa huku kwa kiasi kidogo kulisababisha gari hili kutumika katika mradi mmoja tu wa barabara (Barabara ya Tabora-Mpanda – Sehemu ya 1: km 358). Kwa hiyo, barabara saba muhimu zilizobakia zenye jumla ya kilomita 1,052.6 hazikuthaminiwa kwa kutumia gari hii.

Kushindwa kufanyika kwa tathmini ya hali ya barabara za lami kumesababisha upangaji hafifu wa matengenezo ya barabara, na kusababisha uwezekano wa kutotengwa kwa bajeti inayotosheleza; hivyo, kusababisha ongezeko la uharibifu wa barabara. Zaidi ya hayo, matumizi hafifu ya gari hili yanadhoofisha uwekezaji mkubwa wa walipakodi katika ununuzi wake, hivyo kuthibitisha kuwapo kwa matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**Ninapendekeza serikali itenge na itoe bajeti inayotosha kwa ajili ya kufanya tathmini ya barabara za lami kwa kutumia gari la uchunguzi (RDSV). Tathmini hiyo ni muhimu kwa ajili ya matengenezo ya barabara na upangaji wa ujenzi wa barabara kwa siku zijazo.**

### 7.11 Upungufu wa Bajeti Kiasi cha Sh. Trilioni 1.43 kwa ajili ya Matengenezo ya Barabara Unaofanywa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

Wakati wa ukaguzi wa fedha zilizotengwa kwa shughuli za matengenezo ya barabara zinazosimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) chini ya Wizara ya Ujenzi, nilibaini udhaifu katika bajeti na utoaji wa fedha za matengenezo ya barabara kwa taasisi tekelezi, hasa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Udhaifu huu umeathiri uwezo wa wakala hizi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kadhalika, umeongeza changamoto zilizosababisha kuongezeka kwa kiwango cha uharibifu wa barabara.

Kulingana na ripoti za uchunguzi wa hali ya barabara za Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), nilibaini kuwa TANROADS na TARURA wanahitaji bajeti ya jumla ya Sh. trilioni 2.29 (TANROADS: Sh. trilioni 1.40 na TARURA: Sh. bilioni 885.08) ili kufanya shughuli za kawaida za matengenezo ya barabara na kazi za dharura, hasa kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Hata hivyo, bajeti ya matengenezo ya barabara imebaki vilevile kwa Sh. bilioni 856.79 (TANROADS: Sh. bilioni 598.13 na TARURA: Sh. bilioni 258.66) tangu mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2023/24, huku fedha halisi zilizotolewa zikiwa Sh. bilioni 405.29, sawa na 47% ya bajeti iliyoidhinishwa. Bajeti hii imesababisha upungufu mkubwa wa kifedha kwa Sh. trilioni 1.43 (TANROADS: Sh. bilioni 807.33 na TARURA: Sh. bilioni 626.41), ambao haujatatuliwa ndani ya bajeti iliyopo.

Licha ya kuongezeka kwa ushuru wa barabara na kodi ya mafuta kutoka Sh. trilioni 1.03 hadi Sh. trilioni 1.48 kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2023/24, hakuna marekebisho yoyote ya kibajeti yaliyofanyika.

**Wizara ya Fedha na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) wameshindwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, hivyo kusababisha shughuli za matengezo kukosa fedha. Hali hii ikiendelea, barabara zitaendelea kuharibika, hivyo kusababisha ongezeko la gharama za matengenezo na kupunguza kwa usalama barabarani.**

## 7.12 Upungufu katika Ukusanyaji wa Madeni katika Mradi wa Nyumba Bunju Umesababisha Kiasi cha Sh. bilioni 3.98 Kutokusanywa

Mnamo mwaka 2012, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilizindua mradi wa ujenzi wa nyumba 219 zilizopo Bunju, Dar es Salaam, ili kuziuza kwa watumishi wa umma kwa awamu. Kulingana na mikataba ya mauzo, wanunuzi walitakiwa kulipa asilimia 10 ya bei ya nyumba kama malipo ya awali, huku 90% iliyobaki kulipwa kwa awamu kwa kipindi cha miaka mitatu hadi saba. Mikataba hiyo ilieleza kuwa rejesho lolote la kila mwezi litakalochelewa kulipwalitapata adhabu ya 16% ya awamu zilizocheleweshwa. Aidha, ucheleweshaji mfululizo unaozidi miezi sita utasababisha kusitishwa kwa Mkataba wa Mauzo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, watumishi wa umma 39 walishindwa kukamilisha malipo yao yaliyobaki, kiasi cha Sh. bilioni 3.98, ucheleweshaji ukiwa kati ya mwezi mmoja hadi 53 zaidi ya tarehe za mwisho za mkataba. Licha ya kuchelewa, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) haikutoa adhabu yoyote kwa malipo yaliyochelewa wala kusitisha mikataba, hivyo kuruhusu wadaiwa kuendelea kuishi kwenye nyumba hizo. Kati yao, wadaiwa 11 walikuwa watumishi wa umma waliostaafu wakiwa na madeni ya jumla ya Sh. milioni 936.71, ambayo TBA ilishindwa kukusanya kutoka kwenye mafao ya kustaafu kutokana na upungufu uliopo kwenye mikataba.

TBA ilichukua hatua ya kuwaondoa wadaiwa sugu watatu kwa kutumia dalali wa mahakama na kutoa notisi kwa wadaiwa 15 waliokuwa na madeni yenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 839.52, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya

wadaiwa 21 waliosalia. Hadi kufikia mwezi, Februari 2025, TBA ilikuwa haijarejesha madeni yoyote kati ya yale yaliyodaiwa, hivyo kuathiri uwezo wa kifedha wa TBA na kuzuia utekelezaji wa miradi mipya ya makazi.

**Ninapendekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ichukue hatua zaidi za kisheria dhidi ya wadaiwa wote ili kuhakikisha madeni yote yanakusanywa. Hatua hii itaimarisha uwezo wa kifedha wa TBA na kuiwezesha kuwa na fedha za kuanzisha miradi mipya ya makazi.**

### 7.13 Kuchelewa Kuuzwa kwa Nyumba za Magomeni Kutokana na Mgogoro wa Bei

Mnamo Oktoba 2016, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilianzisha mradi wa ujenzi wa nyumba 644 kwa ajili ya wakazi waliokosa makazi baada ya kubomolewa kwa nyumba zao katika eneo la Magomeni Kota, Dar es Salaam. Mradi huo uliogharimu Sh. bilioni 50.19 ulikamilika mwezi Aprili 2021 na ulilenga kuuza nyumba kwa bei nafuu kupitia mkopo ndani ya kipindi cha miaka 30, huku wakinufaika na msamaha wa kodi kwa miaka mitano ya mwanzo.

Mnamo Machi 2022, TBA ilianza kusaini mikataba ya mauzo, ambapo bei ya mauzo ilipangwa kati ya Sh. milioni 48.52 na Sh. milioni 56.89 kwa kila nyumba. Hata hivyo, hadi kufikia Februari 2025, ni wakazi 173 pekee ndio waliokuwa wamesaini mikataba hiyo, huku wakazi 471 wakiwa bado hawajarasimisha makubaliano yao ya ununuzi, hii inaonesha walishindwa kumudu bei ya ununuzi.

Mgogoro huu umeonesha kuwapo kwa upungufu wa mashauriano ya kina na tathmini ya uwezo wa wanunuzi wakati wa awamu ya kupanga mradi, hivyo kuongeza muda wa kurejesha gharama za uwekezaji uliofanywa na TBA, hali inayoweza kuathiri uwezo wake wa kifedha.

**Ninapendekeza kuwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iongeze juhudi za kutatua suala hili kwa kushirikiana na taasisi husika za serikali ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu unakamilika kwa mafanikio na kuimarisha uendelevu wa kifedha wa wakala kwa muda mrefu.**

### 7.14 Vivuko vya TEMESA Kufanya Huduma ya Usafirishaji bila ya Kuwa na vyeti Vya Usalama

Kwa mujibu wa Kifungu cha 17 cha Kanuni za Usafiri wa Meli (Usalama wa Meli Ndogo, Usalama wa Meli za Mizigo za Ndani, Ukaguzi wa Usalama wa Meli Ndogo, Tafiti na Ukaguzi wa Vyombo Vinavyofanya Safari za Ndani na Pwani, Maji ya Ndani) za mwaka 2004, vyombo vyote vinavyoendeshwa na TEMESA vinapaswa kufanyiwa ukaguzi na kupewa Cheti cha Usalama na Ustahili wa Safari Baharini

na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) ili kuthibitisha kuwa vinakidhi matakwa ya kiufundi na usalama wa baharini.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa TEMESA inamiliki na kuendesha vyombo 32 bila kuwa na Cheti cha Usalama na Ustahili wa Safari Baharini kutokana na kuwapo kwa changamoto ya kisheria katika mchakato wa usajili, hususani katika tafsiri ya Sheria ya Usafiri wa Meli, Sura ya 165 pamoja na kanuni zake. Kanuni za Usafiri wa Meli (Bima ya Lazima kwa Madai ya Wahusika Wengine) za mwaka 2011, zilizotungwa chini ya Sura ya 165, zinahitaji vyombo vyote vilivyosajiliwa Tanzania pamoja na vyombo vya kigeni vilivyopewa leseni kwa ajili ya biashara ya ndani kuwa na bima ya lazima kwa madai ya wahusika wengine kama sharti la kutolewa kwa Cheti cha Usalama na Ustahili wa Safari Baharini. Hata hivyo, Kifungu cha 3 cha kanuni hizi kinatoa msamaha kwa vyombo vya serikali dhidi ya hitaji hilo.

Licha ya msamaha uliotolewa kwa vyombo vya serikali chini ya Sheria ya Usafiri wa Meli, TASAC imesisitiza kuwa vyombo vya TEMESA vinapaswa kufuata masharti ya bima ya lazima kwa madai ya wahusika wengine ili kusajiliwa na kupewa vyeti vya Usalama na Ustahili wa Safari Baharini.

TEMESA imekiri changamoto hii na imekuwa ikishirikiana kikamilifu na TASAC ili kutafuta suluhisho. Hata hivyo, hadi wakati wa kuandaa taarifa hii, Februari 2025, hakuna uamuzi uliopatikana; na vyombo vyote 32 vinaendelea kufanya kazi bila vyeti vinavyohitajika. Hali hii inahatarisha usalama wa abiria na wafanyakazi, kwani vyombo hivyo vinaweza kukosa viwango vinavyotakiwa vya kiufundi na usalama.

**Ninapendekeza kuwa TEMESA na TASAC waombe maoni au tafsiri rasmi ya kisheria kutoka kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutatua utata unaohusu utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Meli na kanuni zake. Hatua hii itafafanua ikiwa vyombo vya TEMESA vinapaswa kupitia ukaguzi wa usalama kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa abiria na wafanyakazi. Aidha, itafafanua ikiwa vinaweza kupewa Vibali vya Usalama na Ustahiliwa Safari Baharini.**

### 7.15 Kuchelewa kwa ujenzi wa Kivuko Kipya cha Nyamisati Chenye Thamani ya Sh. Bilioni 9.5

Mnamo tarehe 19 Mei 2022, Kampuni ya Dar es Salaam Merchant Group (DMG), kwa kushirikiana na KL Heavy Industry Co. Ltd, iliingia mkataba na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) chini ya Mkataba Na. AE.006/2021-2022/HQ/G/29 kwa ajili ya ujenzi na usambazaji wa kivuko kipya. Mradi huu unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 9.5 ulianza rasmi tarehe 21 Oktoba 2022 baada ya kukamilika kwa mipango yote ya kimkataba, ikiwa ni pamoja na umiliki wa eneo

la ujenzi na malipo ya awali ya Sh. bilioni 2.85, na ulitegemewa kukamiliaka tarehe 30 Agosti 2023,

Hata hivyo, kuchelewa kwa vibali vya usanifu kutoka kwa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kulisababisha TEMESA kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi kwa kampuni ya DMG kwa vipindi vitatu, hivyo tarehe mpya ya kukamilika kwa mradi ikawa 30 Oktoba 2024.

Hadi kufikia Agosti 2024, maendeleo ya ujenzi yalifikia 36% pekee, ikiwa ni chini ya kiwango kilichotarajiwa cha 90%, ambao ni sawa na ucheleweshaji wa miezi 14 (30 Agosti 2023 hadi 30 Oktoba 2024). Ucheleweshaji huu ulisababishwa na ukosefu wa nguvukazi na mkandarasi kushindwa kusambaza vifaa muhimu kwa wakati.

Matokeo ya ucheleweshaji huu yanaweza kuongeza gharama za mradi kwa upande wa usimamizi. Pia, yanaweza kuchelewesha juhudi za kuboresha usafiri wa baharini kati ya Mafia na Nyamisati.

**Ninapendekeza kuwa serikali iimarishe taratibu za usimamizi wa miradi ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa kivuko cha Nyamisati unakamilika kwa wakati. Aidha, ihakikishe mkandarasi anawajibika kwa ucheleweshaji. Hatua hii itasaidia kudhibiti gharama zisizotarajiwa, kuzuia ucheleweshaji wa miradi, na kulinda fedha za walipakodi, huku ikiendeleza azma ya serikali ya kuboresha miundombinu ya usafiri wa baharini.**

# SURA YA NANE



# Sekta ya Maji

# SEKTA YA MAJI

## 8.1 Utangulizi

Maji ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, na yanahitaji usimamizi mzuri ili kuhakikisha upatikanaji endelevu, na ubora. Serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, ambayo inakusudia kufikia lengo la usambazaji wa maji ya 85% vijijini na 95% mjini kufikia Juni 2025. Sera hiyo inalenga kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali za maji, ujenzi wa miundombinu, na kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata maji safi na salama.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa maendeleo ya sekta ya maji katika kufikia malengo hayo. Inabainisha mapungufu na mapendekezo kwa Wizara ya Maji na taasisi zake zinazohusika, ikiwa ni pamoja na Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji, na Vyombo vya Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs).

## 8.2 Kufanikisha Lengo la Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji kwa Njia Endelevu

Usimamizi endelevu wa rasilimali za maji ni muhimu ili kuhakikisha upatikanaji wa muda mrefu, usawa, na uhifadhi wa mazingira. Udhibiti mzuri, mipango, na uangalizi ni muhimu katika kudumisha usalama wa maji kwa ajili ya kaya, viwanda, na shughuli za kilimo. Hata hivyo, mapungufu kadhaa yanazuia maendeleo ya usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 8.2.1 Kuchelewa Uandaaji wa Mpango wa Kitaifa wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 inamtaka Waziri wa Maji kuhakikisha uandaaji wa Mpango wa Kitaifa wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Pamoja (IWRM) ili kuratibu uendelezaji na usimamizi wa maji, ardhi, na rasilimali zinazohusiana kwa lengo la kukuza ustawi wa kiuchumi na wa jamii kwa usawa, huku ukihakikisha uendelevu wa mifumo ya ikolojia. Hata hivyo, hadi Desemba 2024, Mpango ulikuwa bado hajandaliwa, ikiwa ni ucheleweshaji wa miaka 15 tangu sheria hiyo kuanza kutumika.

Ucheleweshaji huu umetokana na upungufu wa fedha za kuandaa mpango, hivyo kuhatarisha uendelevu wa maji katika mito, maziwa, na vyanzo vya maji vya ardhini. Pia, kunaweza sababisha upungufu wa maji na usambazaji usio na

usawa ambao unaathiri zaidi jamii za watu wa hali ya chini na sekta muhimu kama vile kilimo, viwanda, na makazi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iweke kipaumbele kwa kutenga bajeti ili kuwezesha kuandaliwa kwa Mpango wa Kitaifa wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji Kwa Pamoja ili kuhakikisha usimamizi wa rasilimali maji na uendelevu.**

### 8.2.2 Vyanzo vya Maji 2,989 Visivyohifadhiwa

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 inazitaka Bodi za maji za mabonde kuweka alama na kutangaza hifadhi ya maji ili kulinda uendelevu wake. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, kati ya vyanzo 3,339 vilivyotambuliwa vya maji, 350 tu (10.5%) vilikuwa vimehifadhiwa na 64 (1.9%) vilikuwa vimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali, hivyo vyanzo 2,989 (89.5%) havikuwa vimehifadhiwa na vyanzo 3,275 (98.1%) havikutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kasi ndogo katika kulinda vyanzo vya maji ilitokana na ukosefu wa fedha, jambo ambalo liliongeza hatari ya uvamizi, uchafuzi, na kupungua kwa maji. Bila ulinzi rasmi, vyanzo hivi vya maji vinaweza kuvamiwa na makazi yasiyo halali, ukataji miti, na matumizi kupita kiasi, jambo ambalo linaweza kudhoofisha usalama wa maji kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza kwamba Serikali itoe fedha za kutosha ili kusaidia kuweka alama na kutangaza vyanzo vya maji kwenye gazeti la Serikali ili kuzuia uvamizi na kuhakikisha uendelevu wa usambazaji maji.**

### 8.2.3 Kutodhibitiwa kwa Matumizi ya Maji na Upotevu wa Mapato ya Sh. Bilioni 2.01 Kutokana na Matumizi ya Maji wakati Vibali Vya Matumizi Vimeisha Muda Wake

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 kinahitaji kuwa watu binafsi au mashirika yanayotumia rasilimali za maji yawe na vibali vya matumizi ya maji kutoka kwenye bodi za mabonde ya maji.

Hata hivyo, bodi nne za mabonde ya maji zilikuwa na vibali 1,795 vilivyoisha muda wake. Licha ya kuisha kwa muda wa vibali hivi, wateja waliendelea kuchukua maji kutoka kwenye vyanzo bila ya uangalizi na bila kulipa ada ya matumizi ya maji hayo. Hali hii ilisababisha upotevu wa mapato ya Sh. bilioni 2.01 kutokana na ada za mwaka za matumizi ya maji.

Matumizi ya maji kwenye vyanzo vya maji bila ya udhibiti kunasababisha uchukuaji wa maji kupita kiasi, hali ambayo inahatarisha upatikanaji endelevu wa rasilimali muhimu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 28.**

**Jedwali Na. 28: Bodi za Mabonde ya Maji Zilizo na Vibali vya Matumizi ya Maji Vilivyoisha Muda Wake**

| Na. | Bodi ya Bonde la Maji | Idadi Ya Wateja | Kiasi kisichokusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ziwa Victoria | 536 | 1,405,343,432 |
| 2 | Pangani | 535 | 486,693,179 |
| 3 | Ziwa Tanganyika | 342 | 85,500,000 |
| 4 | Ziwa Nyasa | 382 | 37,665,000 |
| **Jumla** | | **1,795** | **2,015,201,611** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi*

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa bodi za mabonde ya maji zinapitia mara kwa mara vibali vya matumizi ya maji, kutoza faini kwa ukiukwaji wa sheria, na ukusanyaji wa mapato kwa muda ili kuzuia hasara na uchukuaji wa maji kupita kiasi.**

### 8.2.4 Kampuni Zinazofanya Shughuli za Uchimbaji wa Visima vya Maji bila Leseni

Kanuni za Leseni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji ya Ardhini ya mwaka 2013, kinataka kampuni ya uchimbaji maji ardhini kupata leseni halali kutoka Wizara ya Maji. Uhakiki wangu kwa kutumia kanzidata ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa mwaka 2023/24 uligundua kuwa kampuni 78 zilipatiwa leseni za biashara za uchimbaji visima vya maji ya ardhini kati ya mwaka 2020 na 2024. Hata hivyo, ni kampuni 42 tu zilikuwa na leseni halali za uchimbaji wa visima vya maji

Kukosekana kwa uratibu kati ya Wizara ya Maji na BRELA pamoja na ufuatiliaji usioridhisha vilisababisha uchimbaji wa visima vya maji bila leseni. Uchimbaji wa maji ya ardhini bila leseni unaweza kusababisha uchimbaji kupita kiasi, kupungua kwa viwango vya maji ya ardhini, na kuongezeka kwa uchafuzi, jambo ambalo linaweza kudhoofisha upatikanaji na ubora wa maji.

**Ninapendekeza kuwa Serikali iimarishe uratibu kati ya Wizara ya Maji na BRELA ili kuhakikisha kuwa kampuni zote zinazofanya shughuli za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji ya ardhini vinazingatia kanuni za leseni.**

## 8.3 Lengo la Kufikia Usambazaji wa Maji wa 95% katika Maeneo ya Mjini kufikia Mwezi Juni 2025

Kuhakikisha usambazaji wa maji wa kutosha katika maeneo ya mijini ni muhimu kwa kufanikisha maendeleo endelevu na kuboresha afya ya umma. Sera ya Kitaifa ya Maji (2002) inaweka lengo la kufikia usambazaji wa maji wa 95% katika maeneo ya mijini kufikia Juni 2025. Kulingana na taarifa ya fedha ya Wizara ya Maji kufikia tarehe 30 Juni 2024, usambazaji wa maji mjini uliongezeka kutoka 88% mnamo Juni 2023 hadi 90% mnamo Juni 2024. Hata hivyo, changamoto kadhaa zinahatarisha kufikiwa kwa lengo lililobaki, kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 8.3.1 Upungufu wa Usambazaji wa Maji kwa Lita Bilioni 26

Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 kinawataka mamlaka za maji kuchukua hatua zote muhimu ili kutoa huduma za usambazaji wa maji na usafi wa mazingira katika maeneo yao ya huduma. Hata hivyo, ukaguzi wangu uligundua kuwa Mamlaka 16 za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (WSSAs) zilikumbwa na upungufu mkubwa wa usambazaji wa maji wa lita bilioni 26.29 (71%). Jumla ya mahitaji ya maji kwa mwaka ilikuwa lita bilioni 37.21, huku uwezo wa uzalishaji uliopo ukiwa lita bilioni 10.92 tu kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 29.**

**Jedwali Na. 29: Mamlaka za Maji zilizoshindwa kukidhi Mahitaji ya Maji kwa Wateja**

| Na. | Mamlaka | Mahitaji ($m^3$/mwaka) | Uzalishaji (m3/mwaka) | Upungufu (m3/mwaka) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Handeni Trunk | 13,331,952 | 2,684,825 | 10,647,127 |
| 2 | Ifakara | 3,395,595 | 470,485 | 2,925,110 |
| 3 | Wanging'ombe | 2,613,606 | 787,998 | 1,825,608 |
| 4 | Turiani | 2,518,500 | 1,107,045 | 1,411,455 |
| 5 | Kibondo | 2,486,745 | 1,171,650 | 1,315,095 |
| 6 | Kondoa | 2,008,595 | 1,120,550 | 888,045 |
| 7 | Gairo | 1,745,795 | 547,500 | 1,198,295 |
| 8 | Songe | 1,679,382 | 71,369 | 1,608,013 |
| 9 | Mwanhuzi | 1,408,608 | 800,445 | 608,163 |
| 10 | Mpwapwa | 1,265,965 | 762,484 | 503,481 |
| 11 | Ludewa | 1,168,365 | 476,690 | 691,675 |
| 12 | Kibaya | 1,067,439 | 184,252 | 883,187 |
| 13 | Ushirombo | 1,063,884 | 328,445 | 735,439 |
| 14 | Kiomboi | 885,490 | 142,677 | 742,813 |
| 15 | Kilindoni | 323,390 | 150,380 | 173,010 |
| 16 | Maganzo | 246,448 | 114,975 | 131,473 |
| **Jumla** | | **37,209,758** | **10,921,770** | **26,287,988** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Vyanzo vya maji na miundombinu isiyotosheleza ndiyo sababu kuu za uzalishaji na usambazaji usioridhisha wa maji, hivyo kusababisha uhaba wa maji ambao uliathiri vibaya kaya, biashara na kilimo.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iweke kipaumbele na kutenga bajeti ya kutosha kuboresha miundombinu ya maji ili mamlaka za maji ziweze kukidhi mahitaji ya maji.**

### 8.3.2 Upotevu wa Maji Unaogharimu Sh. Bilioni 8.75

Maji yasiyozalisha mapato (Non-Revenue Water - NRW) ni maji yanayozalishwa na Mamlaka za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (WSSAs) ambayo hupotea kabla ya kufikia wateja. Kulingana na viwango vya EWURA, kiwango kinachokubalika cha NRW hutofautiana kulingana na daraja la WSSA, na kikomo cha juu zaidi ni 20%.

Ukaguzi wangu uligundua kuwa Mamlaka 20 za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (WSSAs) zilizidi kiwango hiki, na kusababisha hasara ya maji lita bilioni 5.97 yenye thamani ya Sh. bilioni 8.75 kwa mwaka wa fedha 2023/24 **Jedwali Na. 30.** Sababu kuu ilikuwa uvujaji wa maji kutokana na miundombinu ya zamani na kuharibika.

Viwango vya juu vya Maji yasivyo na Mapato (NRW) huongeza gharama za uendeshaji, kwani maji hutibiwa na kusambazwa bila kutoa mapato. Shida hii ya kifedha hupunguza uwezo wa WSSAs kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu na kupanua chanzo ya usambazaji wa maji.

**Jedwali Na. 30: Maji Yasiyozalisha Mapato**

| Na. | Jina la Mamlaka | Maji yaliyopotea ($m^3$) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Handeni | 1,843,664 | 2,588,546,571 |
| 2 | Bunda | 754,221 | 1,402,851,060 |
| 3 | Sengerema | 763,045 | 1,136,937,050 |
| 4 | Makonde | 374,407 | 797,861,317 |
| 5 | Mpwapwa | 416,669 | 639,265,371 |
| 6 | Chato | 384,664 | 596,959,860 |
| 7 | Ifakara | 373,569 | 423,253,972 |
| 8 | Kilwa Masoko | 239,050 | 253,431,540 |
| 9 | Wanging'ombe | 169,571 | 186,528,540 |
| 10 | Kondoa | 103,513 | 154,879,500 |
| 11 | Loliondo | 45,084 | 104,730,132 |
| 12 | Ushirombo | 49,878 | 74,817,210 |
| 13 | Ruangwa | 51,795 | 73,030,950 |
| 14 | Kibaya | 50,175 | 63,582,618 |
| 15 | Songe | 33,412 | 56,667,440 |
| 16 | Kiomboi | 51,247 | 53,296,880 |
| 17 | Kibondo | 126,872 | 52,250,484 |

| Na. | Jina la Mamlaka | Maji yaliyopotea ($m^3$) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 18 | Utete | 36,105 | 38,632,350 |
| 19 | Ludewa | 82,322 | 34,163,628 |
| 20 | Namanyere | 21,873 | 23,426,274 |
| | **Jumla** | **5,971,136** | **8,755,112,748** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi*

**Ninapendekeza kuwa Serikali iongeze fedha za ukarabati wa miundombinu ya maji na kuhakikisha ufuatiliaji wa uhakika ili kugundua uvujaji ili kupunguza hasara za Maji yasiyo na Mapato (NRW).**

### 8.3.3 Wateja Ambao Hawajaunganishiwa Mita za Kupima Matumizi ya Maji

Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ya 2019 kinazitaka mamlaka za maji kuunganisha mita za kupima matumizi ya maji kwa wateja. Hatahivyo, nilibaini wateja 2,203 katika mamlaka tatu za maji ambao hawajaunganishiwa mita za kupima matumizi ya maji.

Bila mita za kupima matumizi ya maji, matumizi ya maji yanakadiriwa badala ya kupimwa, jambo ambalo husababisha bili zisizo sahihi, upotevu wa mapato, na migogoro inayoweza kutokea kati ya wateja. Ukosefu wa mita pia hufanya kuwa vigumu kufuatilia matumizi ya maji, na hivyo kuchangia udhaifu katika usimamizi wa usambazaji. Rejea **Jedwali Na. 31.**

**Jedwali Na. 31: Wateja Wasio na Mita za Kupima Maji**

| Na. | Jina la Mamlaka | Idadi ya Wateja |
|---|---|---|
| 1 | Rujewa | 882 |
| **2** | Ludewa | 788 |
| **3** | Rombo | 533 |
| | **Jumla** | **2,203** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi*

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe mamlaka za maji zinafunga mita za kupima matumizi ya maji kwa wateja wote ambao hawana vifaa hivyo ili kuwezesha utoaji wa ankara sahihi kulingana na matumizi halisi ya maji**

## 8.4 Lengo la Kufikia Usambazaji wa Maji wa 85% katika Maeneo ya Vijijini kufikia Juni 2025

Usambazaji wa maji vijijini ni muhimu kwa afya ya umma, shughuli za kiuchumi, na kupunguza umaskini. Sera ya Kitaifa ya Maji (2002) inaweka lengo la kufikia usambazaji wa maji wa 85% katika maeneo ya vijijini kufikia Juni 2025. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, usambazaji uliongezeka kutoka 77% mnamo Juni 2023 hadi 79.6%, kulingana na taarifa ya fedha ya Wizara ya Maji. Hata hivyo, ukaguzi

wangu ulibaini changamoto kadhaa ambazo zinaweza kuzuia kufikiwa kwa lengo hili, kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 8.4.1 Matumizi Yasiyoridhisha ya Mitambo ya Uchimbaji Visima vya Maji na Kusababisha Kuchelewa kwa Mradi

Mnamo tarehe 4 Mei 2024, Wizara ya Maji ilizindua mpango wa "Kuchimba Visima 900 na Ujenzi wa Miundombinu Yake. Shabaha ya mpango huo wenye thamani ya Sh. bilioni 55.44 ni kutoa huduma za maji kwa vijiji 2,146 kufikia mwezi Oktoba 2024. Mnamo tarehe 27 Mei 2024, Wizara ilinunua na kusambaza mitambo 86 kwa RUWASA, ikiwa ni pamoja na mitambo 25 ya kuchimba visima vya maji. Mitambo hii iligharimu Sh. bilioni 29.97 na ilikuwa na lengo la kusaidia shughuli za uchimbaji wa visima vya maji katika mikoa 25 (bila kujumuisha Dar es Salaam).

Kwa mujibu wa RUWASA, muda wa wastani unaohitajika kuchimba kisima kimoja ni siku tano ikiwa rasilimali zote muhimu zinapatikana. Kwa kuzingatia dhana hii, visima 900 vingeweza kuchimbwa kuanzia mwezi Mei 2024 hadi Oktoba 2024. Takwimu hii inakidhi kikamilifu lengo la visima 900 lililowekwa kwenye mpango huu.

Hata hivyo, kufikia muda wa kukamilika kwa mpango huo, mnamo mwezi Oktoba 2024, mitambo ya uchimbaji visima vya maji ilikuwa imechimba visima 351 tu (39%), hivyo kuacha visima 549 (61%) havijachimbwa. Mnamo tarehe 23 Julai 2023, RUWASA iliingia mikataba na kampuni mbili kuchimba visima 400 kwa Sh. bilioni 10.42 ili kuharakisha maendeleo ya uchimbaji wa visima.

Pia, nilibaini kuwa mpaka kufikia mwezi Februari 2025 RUWASA ilikuwa imepokea Sh. bilioni 36.69 kutoka Wizara ya Maji na Mfuko wa Taifa wa Maji. Kiasi kilichohitajika ni Sh. bilioni 55.44 kutekeleza mpango huo tangu kuanzishwa kwake mnamo mwezi Mei 2024. Hivyo, Sh. bilioni 18.75 (34%) zilikuwa bado hazijatolewa, na kusababisha maendeleo hafifu ya ujenzi wa miundombinu ya visima.

Kwa kiasi kilichopokelewa, visima 920 (vilivyohuishwa kutoka visima 900) vilikuwa tayari vimechimbwa; ambapo visima 642 (70%) vilikuwa na maji, huku visima 278 (30%) havikuwa na maji. Pia, kati ya visima 642 vilivyokuwa na maji, miundombinu ya visima 118 tu (18%) ndiyo imekamilika na kuanza kutoa huduma za maji kwa jamii.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iboreshe mpango wa uchimbaji visima na matumizi ya mitambo ya kuchimba visima vya maji kwa kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa rasilimali muhimu kama vile wafanyakazi,**

**mafuta, na vipuri zinapatikana ili kuepuka gharama zisizo na tija na uchelewaji wa ukamilikaji wa visima.**

### 8.4.2 Kutolewa kwa Sh. Bilioni 8.32 na Mfuko wa Taifa wa Maji bila Mikataba ya Utendaji Iliyosainiwa

Kanuni ya 13 ya Kanuni za Mfuko wa Taifa wa Maji ya mwaka 2019 inahitaji Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Maji kusaini mikataba ya utendaji na taasisi za utekelezaji wa miradi ya maji kabla ya kutoa fedha kwa miradi ya maji.

Hata hivyo, nilibaini Mfuko wa Taifa wa Maji ulitoa Sh. bilioni 8.32 kwa taasisi 16 za utekelezaji wa miradi ya maji, ikiwa ni pamoja na RUWASA, bila kusaini mikataba ya utendaji, kinyume na kanuni tajwa. Udhaifu huu unaonesha udhibiti usioridhisha wa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha zilizotolewa, hivyo kuongeza hatari ya usimamizi usioridhisha na kuweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maji iliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Mfuko wa Taifa wa Maji unasaini mikataba ya utendaji na taasisi za utekelezaji wa miradi ya maji kabla ya kutoa fedha. Hatua hii itapunguza hatari ya usimamizi usioridhisha na kuhakikisha utekelezaji mzuri wa miradi ya maji.**

### 8.4.3 Upungufu wa Uendeshaji katika Vyombo vya Kutoa Huduma za Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs)

Kulingana na Kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, Chombo cha Kutoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO) kinaweza kuanzishwa kwa idhini ya wengi wa wanajamii ili kufanya usimamizi, uendeshaji, na utunzaji wa mifumo ya usambazaji wa maji katika eneo lao.

Ukaguzi wangu wa CBWSOs uligundua upungufu ufuatao ambao unaweza kuzuia kufanikisha lengo la usambazaji maji kwa 85% katika maeneo ya vijijini:

**(a) Upungufu wa Usambazaji wa Maji kwa Jamii**

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini kuwa mahitaji ya maji kwa CBWSOs nane yalikuwa $m^3$ 3,670,299 kwa mwaka, huku uwezo wao wa uzalishaji ukiwa $m^3$ 977,258 kwa mwaka. Hali hii ilisababisha upungufu wa $m^3$ 2,693,041 kwa mwaka (upungufu wa 73%). Upungufu wa usambazaji wa maji umebainishwa kwenye **Jedwali Na. 32.**

**Jedwali Na. 32: Upungufu wa Usambazaji wa Maji**

| Na. | CBWSO | Mahitaji ($m^3$/mwaka) | Uzalishaji ($m^3$/mwaka) | Upungufu ($m^3$/mwaka) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fulwe | 875,000 | 65,115 | 809,885 | 93 |
| 2 | Mvumi Mission | 911,624 | 228,125 | 683,499 | 75 |
| 3 | Mkombozi | 622,690 | 189,800 | 432,890 | 70 |
| 4 | Lwamgasa | 409,255 | 20,898 | 388,357 | 95 |
| 5 | Mahege | 182,500 | 36,500 | 146,000 | 80 |
| 6 | Mkilima | 438,000 | 317,550 | 120,450 | 28 |
| 7 | Kalengakapyo | 157,826 | 66,576 | 91,250 | 58 |
| 8 | Imuka | 73,404 | 52,694 | 20,710 | 28 |
| **Jumla** | | **3,670,299** | **977,258** | **2,693,041** | **73** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi*

Vyanzo vya maji visivyotosheleza na miundombinu duni vilikuwa sababu kuu za uzalishaji pungufu wa maji, hivyo kuzuia kaya kupata maji salama na safi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu duni, kuwekeza katika vyanzo vipya vya maji, na kuhusisha jamii katika uhifadhi wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji salama na safi.**

### (b) Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Isiyoridhisha

Ukaguzi wangu uligundua changamoto za uendeshaji na matengenezo katika Vyombo mbalimbali vya Kutoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs). Upungufu huo, kama ulivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 33** ni pamoja na tanki la maji kuvuja, vituo vya kuchotea maji ambavyo havifanyi kazi, miundombinu iliyoharibika, na visima visivyotumiwa kikamilifu.

**Jedwali Na. 33: Upungufu katika Miundombinu ya Usambazaji wa Maji**

| Chombo cha Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) | Maelezo |
|---|---|
| Makuyuni (Arusha) | Tanki kwenye chanzo limekuwa na nyufa kubwa, na kusababisha maji kuvuja. Uvujaji huu umelazimisha kiwango cha maji kudhibitiwa kwa lita 1,750 tu, ambayo ni nusu ya uwezo wake wa lita 3,500. |
| Mkombozi (Singida) | Vituo 12 vya kuchotea maji havikuwa vikifanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja. |
| Muungano (Katavi) | Tanki la maji lenye uwezo wa lita 100,000 lilikuwa likivuja kutoka chini. |
| Mvumi Mission (Dodoma) | Kisima cha Igondola na pampu ya maji na jengo la kuzalishia nishati havijaanza kutumika tangu mwaka 2015. |
| Imuka (Kagera) | Mvua kubwa iliharibu miundombinu ya vituo 20 vya kuchotea maji (DPs). |

| Chombo cha Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) | Maelezo |
|---|---|
| Kokwe (Mara) | Kati ya vituo 58 vya kuchotea maji (DPs), 15 tu vinafanya kazi, na vituo 43 havifanyi kazi. |

***Chanzo**: Taarifa ya ukaguzi*

Sababu kuu ni upungufu wa fedha, zana, na utaalamu wa uendeshaji na matengenezo, ambayo imedhoofisha uendelevu wa miradi ya maji kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iweke kipaumbele matengenezo, utunzaji, na utengaji wa rasilimali za kutosha ili kurejesha utendaji na kuhakikisha usambazaji endelevu wa maji katika jamii zilizoathirika.**

**(c) Kiwango kikubwa cha upotevu wa maji kilichosababisha hasara ya Sh. bilioni 2.05**

Maji yasiyo ya mapato (Non Revenue Water) ni kiasi cha maji ambacho huzalishwa kwa ajili ya kuuza lakini hupotea kabla ya kuwafikia wateja watarajiwa. Aya ya 5.5.3 ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 hadi 2025/26) inatoa lengo la Kitaifa la kupunguza upotevu wa maji hadi 20% ifikapo 2025/26.

Tathmini niliyoifanya nilibaini kuwa, vyombo 17 vya kijamii vya utoaji wa huduma ya maji vilikuwa na asilimia kubwa ya upotevu wa maji kuanzia 22% hadi 89%, na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 2.05 kwenye mapato ya mauzo ya maji. Hii ilichangiwa na uvujaji wa maji kutoka kwenye miundombinu chakavu na kumwagika kwa maji kutoka kwenye matanki ya kuhifadhia maji. Mchanganuo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 34.**

**Jedwali Na. 34: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vyenye kiwango kikubwa cha upotevu wa maji**

| Na. | Mkoa | Jina la chombo | Uzalishaji (m3) | Mauzo (m3) | Upotevu (m3) | % ya upotevu | Hasara (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Katavi | Wangogo | 1,138,070 | 218,000 | 920,070 | 81 | 1,388,445,400 |
| 2. | Katavi | Mmasi | 153,126 | 20,140 | 132,986 | 87 | 205,188,840 |
| 3. | Katavi | Ndui/nyaki | 74,102 | 8,000 | 66,102 | 89 | 102,261,312 |
| 4. | Mara | Sukuchiwasa | 79,016 | 23,752 | 55,264 | 70 | 79,414,368 |
| 5. | Morogoro | Ngerengere | 89,705 | 65,248 | 24,457 | 27 | 53,193,975 |
| 6. | Arusha | Makilenga | 343,921 | 268,259 | 75,663 | 22 | 51,450,619 |

| Na. | Mkoa | Jina la chombo | Uzalishaji (m3) | Mauzo (m3) | Upotevu (m3) | % ya upotevu | Hasara (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | Mara | Nyamongo | 81,229 | 52,414 | 28,815 | 35 | 34,578,000 |
| 8. | Mwanza | Shiwasa | 46,371 | 28,330 | 18,041 | 39 | 27,061,500 |
| 9. | Morogoro | Dutumi | 52,512 | 39,384 | 13,128 | 25 | 24,384,000 |
| 10. | Mwanza | Busisi | 38,785 | 27,533 | 11,252 | 29 | 16,878,000 |
| 11. | Singida | Matonya | 41,314 | 32,229 | 9,085 | 22 | 15,898,760 |
| 12. | Arusha | Mbuga nyekundu | 57,600 | 44,998 | 12,602 | 22 | 15,752,700 |
| 13. | Mara | Grumet | 17,465 | 10,566 | 6,899 | 40 | 12,418,200 |
| 14. | Mara | Kyabarakiko | 6,926 | 1,576 | 5,350 | 77 | 8,024,900 |
| 15. | Mwanza | Luwasa | 13,806 | 8,516 | 5,290 | 38 | 7,935,000 |
| 16. | Pwani | Gwata | 13,760 | 8,927 | 4,833 | 35 | 4,128,000 |
| 17. | Pwani | Makip | 13,500 | 9,121 | 4,379 | 32 | 3,240,000 |
| Jumla | | | | | | | **2,050,253,574** |

*Chanzo*: *Taarifa ya Ukaguzi*

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kupitia RUWASA ihakikishe matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu ya maji ili kupunguza uvujaji wa maji na kuimarisha usimamizi wa karibu ili kupunguza matumizi ya maji yasiyoidhinishwa. Zaidi ya hayo, vifungwe vifaa vya kudhibiti maji kumwagika kutoka kwenye matenki ya kukusanyia maji na kuhakiki ubora wa mita za maji ili kuhakikisha bili za maji zinazotozwa zinaendana na matumizi halisi.**

### (d) Gharama za Uendeshaji Zimezidi Mapato katika CBWSOs

Uchambuzi wa kifedha ulibaini kuwa gharama za uendeshaji zilizidi mapato hadi 138%, jambo ambalo lilileta mzigo kwa uendelevu wa CBWSOs . Hii ilitokana na usimamizi usioridhisha, gharama kubwa za matengenezo, na ukusanyaji wa mapato ulio duni **Jedwali Na. 35**.

**Jedwali Na. 35: Orodha ya CBWSOs zenye Gharama za Uendeshaji Zilizozidi Mapato**

| Na. | CBWSO | Mapato (Sh.) | Matumizi (Bila Uchakavu wa mali) (Sh.) | Hasara (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkombozi | 104,204,604.00 | 120,274,292.00 | 16,069,688.00 | 15 |
| 2 | Mahege | 3,104,000.00 | 7,395,173.00 | 4,291,173.00 | 138 |
| 3 | Fulwe | 76,606,000.00 | 80,392,631.54 | 3,786,631.54 | 5 |
| 4 | Nkimwankoi | 105,692,413.59 | 108,419,339.57 | 2,726,925.98 | 3 |
| 5 | Sinaki | 46,661,977.54 | 48,996,673.00 | 2,334,695.46 | 5 |
| 6 | Mkongoro II | 32,940,200.00 | 33,822,055.34 | 881,855.34 | 3 |

| Na. | CBWSO | Mapato (Sh.) | Matumizi (Bila Uchakavu wa mali) (Sh.) | Hasara (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Igamba Group | 12,173,123.53 | 12,558,528.67 | 385,405.14 | 3 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi*

**Ninapendekeza kuwa Serikali iboreshe njia za kukusanya mapato ya CBWSOs kwa kupunguza gharama, kuboresha miundombinu ya maji, kuimarisha usimamizi wa kifedha, na kutekeleza mifumo ya ufuatiliaji ili kuhakikisha huduma za kusambaza maji zinakuwa endelevu na maji yapatikane kwa uhakika.**

**(e) 15,606 Mita za maji Hazikuhakikiwa na Wakala wa Vipimo**

Kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Vipimo na Mizani (Cap 340) kinahitaji vyombo vyote vya kupimia kuchunguzwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo na Mizani (WMA), huku kifungu cha 21(1) kikilazimisha kutiwa alama ya uthibitisho ili kuzuia udanganyifu.

Hata hivyo, Mita 15,606 katika CBWSOs 37 hazikuchunguzwa wala kuthibitishwa na WMA. Hii ilitokana kukosekana kwa uelewa na mapungufu ya rasilimali ambayo yalizuia CBWSOs kushirikiana na WMA.

Kutothibitishwa kwa mita kunaweza kusababisha ankara za maji zisizo sahihi, na kusababisha upotevu wa mapato kutokana na malipo ya chini au migogoro ya wateja kuhusu malipo ya kupita kiasi. Zaidi ya hayo, ankara za maji zisizoaminika zinaweza kudhoofisha imani ya umma katika shughuli za CBWSOs.

**Napendekeza kuwa Serikali, kupitia RUWASA, ihakikishe kuwa vipima vyote vya maji katika CBWSOs vinachunguzwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo na Mizani (WMA) ili kuhakikisha kiwango halisi cha maji yanayosambazwa, na hivyo kutoa ankara za maji halisi kwa wateja.**

**(f) Mapato yasiyokusanywa ya thamani ya Sh. bilioni 3.74 yatokanayo na ankara za maji**

Kifungu cha 35 (5) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinaeleza kuwa, kuanzia tarehe ya kusajiliwa kwa chombo cha watoa huduma ya maji, watumiaji wa maji wanaopata huduma kutoka kwenye chombo hicho husika watalazimika kulipia huduma hiyo kwa kutumia kiwango kitaka chotozwa na chombo husika. Zaidi ya hayo, Kifungu cha 38 (a) cha Sheria hiyo hiyo kinaeleza kuwa, chanzo kikuu cha mapato cha vyombo vya kijamii vya utoaji wa

huduma za maji ni gharama za maji zinazolipwa na kila mtumiaji anayepata huduma za maji kutoka kwenye chombo husika.

Nilifanya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa vyombo 160 na kubaini kuwa mapato ya Sh. bilioni 3.74 hayakukusanywa kutoka kwenye ankara za maji zilizotolewa kwa wateja waliopata huduma za maji kutoka vyombo 121 kwa mwaka wa fedha 2023/24. Mchanganuo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. IX**

Upungufu huu wa mapato huzuia uwezo wa CBWSOs kugharamia shughuli muhimu, ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi, matengenezo ya vifaa, na uboreshaji wa huduma, na hatimaye kuathiri uendelevu wa utoaji wa huduma za maji

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kama msimamizi wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji, iweke mikakati na mbinu madhubuti za kukusanya mapato zitakazohakikisha wateja wanaopatiwa huduma za maji na vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji wanalipa ankara zao ili mapato hayo yasaidie kuboresha miundombinu ya maji na kufanya huduma za maji ziwe endelevu.**

### (g) Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji kutofikia lengo la kutoa huduma za maji kwa jamii

Kanuni ya 24(1) & (2) ya Kanuni za Maji Safi na Usafi wa Mazingira (Usajili na Uendeshaji wa Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji) za Mwaka 2019 inatoa wajibu kwa kila chombo cha watoa huduma ya maji kuwafikia wanufaika wake wote ndani ya eneo la huduma kama ilivyoainishwa kwenye cheti cha usajili wa chombo husika. Cheti cha usajili hueleza vijiji ambavyo chombo kinapaswa kuhudumia.

Usajili wa vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji unavipa mamlaka ya kutoa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira kwenye eneo la huduma lililo chini ya mamlaka yake.

Wakati wa ukaguzi nilipitia usajili wa vyombo 160 vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji na kuhakiki maeneo yaliyofikiwa na huduma za maji na nilibaini kuwa, vyombo 21 vilikuwa na vijiji 349 vilivyosajiliwa chini yake kwa madhumuni ya kusambaza huduma ya maji safi. Ingawa, ni vijiji 206 tu sawa na 59% ndivyo vilikuwa vimefikiwa na huduma za maji, huku vijiji 143 sawa na 41% vikiwa havina huduma za maji safi. Mchanganuo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 36.**

**Jedwali Na. 36: Vyombo vya Kijamii vya Utoaji wa Huduma za Maji ambavyo Havikufikia Lengo la Kusambaza Maji Vijijini**

| Na. | Mkoa | Jina la chombo | Jumla ya vijiji | Vijiji vinavyopata huduma ya maji | Vijiji visivyo na huduma ya maji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shinyanga | Mwanya | 23 | 2 | 21 |
| 2. | Kagera | Kasharunga | 21 | 7 | 14 |
| 3. | Kagera | Nyinenshamba | 23 | 10 | 13 |
| 4. | Tabora | Ilasa | 35 | 23 | 12 |
| 5. | Shinyanga | Ilogi | 16 | 4 | 12 |
| 6. | Tabora | Umwai | 26 | 16 | 10 |
| 7. | Morogoro | Ngerengere | 24 | 16 | 8 |
| 8. | Tabora | Choma | 21 | 13 | 8 |
| 9. | Shinyanga | Mwamasa | 19 | 11 | 8 |
| 10. | Tabora | Igogo | 9 | 3 | 6 |
| 11. | Shinyanga | Nyabuki | 9 | 3 | 6 |
| 12. | Tabora | Kamawinu | 12 | 8 | 4 |
| 13. | Shinyanga | Mwabulya | 21 | 17 | 4 |
| 14. | Tabora | Chamilaga | 11 | 8 | 3 |
| 15. | Geita | Uyovu | 13 | 10 | 3 |
| 16. | Geita | Runzewe-Mashariki | 6 | 3 | 3 |
| 17. | Shinyanga | Bulyanhulu | 6 | 4 | 2 |
| 18. | Shinyanga | Kata Ya Ngaya | 9 | 7 | 2 |
| 19. | Shinyanga | Bunnema | 21 | 19 | 2 |
| 20. | Shinyanga | Buka | 14 | 13 | 1 |
| 21. | Shinyanga | Songambele-Shinyanga | 10 | 9 | 1 |
| | **Jumla** | | **349** | **206** | **143** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Ukosefu wa huduma za kutosha za maji umesababishwa na uchache na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji, hivyo kuathiri sehemu kubwa ya wakazi wa vijiji husika. Hali hii ni kikwazo katika upatikanaji wa maji safi na salama na inahatarisha afya za wananchi, mifugo, shughuli za kilimo, na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, iweke mikakati madhubuti ya usimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa kuridhisha wa maji katika maeneo ambayo vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji vimepangiwa kutoa huduma za maji, hivyo kufikia malengo ya kitaifa ya kufikisha huduma za maji na usafi wa mazingira kwa wananchi wote.**

### (h) Mita za maji hazijafungwa kwenye vituo vya usambazaji (DPs)

Kifungu cha 33(1)(d) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kinavitaka vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji kufunga mita

za maji ili kupima kwa usahihi kiasi cha maji yanayotolewa kwenye mabomba ya umma, watumiaji binafsi, au vituo vyovyote vya kusambaza maji vilivyotengwa ili kuhakikisha ufuatiliaji makini, utozaji bili kwa ufanisi, na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji. Hii ni muhimu kwa kukuza uwazi, kuzuia upotevu wa maji, na kuhakikisha kwamba, watumiaji wanatozwa malipo ya haki kwa matumizi yao ya maji.

Tathmini niliyoifanya ilibaini kuwa mita za maji 8,050 hazikufungwa kwenye vituo vya usambazaji kwenye vyombo 24 vya kijamii vya utoaji wa huduma ya maji kutokana na uhaba wa fedha za ununuzi wa mita za maji, na wakati mwingine, watumiaji walikuwa wakipinga kufungiwa mita, wakihofia gharama kubwa na kutoelewa faida za upimaji, kama vile malipo ya haki na usimamizi bora wa rasilimali. Mchanganuo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 37**.

**Jedwali Na. 37: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji visivyofunga mita za maji**

| S/Na. | Mkoa | Jina la chombo | Idadi ya mita zisizofungwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Morogoro | Mang'ula | 3,961 |
| 2. | Njombe | Imalinyi Kidugula | 720 |
| 3. | Ruvuma | Kiambwso | 665 |
| 4. | Njombe | Lugawaso | 641 |
| 5. | Kigoma | Mukaka | 469 |
| 6. | Arusha | Kimasakina | 439 |
| 7. | Arusha | Makilenga | 304 |
| 8. | Kigoma | Ubukaka | 235 |
| 9. | Njombe | Nuliyai | 210 |
| 10. | Kigoma | Ilafasha | 110 |
| 11. | Geita | Imalabupina- Nanda | 108 |
| 12. | Geita | Lulembela | 93 |
| 13. | Njombe | Matamba | 39 |
| 14. | Kigoma | Ilakoze | 22 |
| 15. | Kigoma | Kidahwe - Matendo | 22 |
| 16. | Tabora | Ilasa | 3 |
| 17. | Tabora | Kinamwaka | 2 |
| 18. | Tabora | Nanga | 1 |
| 19. | Tabora | Ziba | 1 |
| 20. | Tabora | Chamilaga | 1 |
| 21. | Tabora | Mwaisaka | 1 |
| 22. | Arusha | Kiwango | 1 |
| 23. | Arusha | Mbuga Nyekundu | 1 |
| 24. | Arusha | Olmulo | 1 |
| **Jumla** | | | **8,050** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Kushindwa kufunga mita za maji kwa wateja na kwenye vituo vya maji vya umma kunazuia ukadiriaji wa matumizi sahihi ya maji, na hivyo kusababisha upotevu wa mapato kutokana na matumizi ya maji yasiyofuatiliwa.

**Napendekeza kuwa, Serikali kupitia RUWASA itenge bajeti ya ununuzi na uwekaji mita za maji kwa kila kituo cha usambazaji ili kuwezesha utoaji sahihi wa ankara kulingana na matumizi halisi ya maji. Zaidi ya hayo, kuwe na kampeni za uhamasishaji wa jamii ili kuwaelimisha watumiaji kuhusu faida za mita za maji, ikiwa ni pamoja na utoaji ankara za maji kwa haki na kuimarika kwa huduma.**

## 8.5 Lengo la Kutoa Maji Safi na Salama

Kupata maji safi na salama ni haki ya msingi ya binadamu na ni msingi wa afya ya umma. Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama ni muhimu kwa kuzuia magonjwa yanayosambazwa kwa maji, kuboresha ubora wa maisha, na kusaidia maendeleo endelevu. Hata hivyo, ukaguzi wangu uligundua upungufu katika mfumo wa usambazaji wa maji. Upungufu huo unaweza kudhoofisha lengo hili, hivyo kuhatarisha afya za binadamu.

### 8.5.1 Matumizi ya Maji ya Mabwawa bila Kupimwa Ubora

Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2018 inakataza matumizi ya maji kwa ajili ya kunywa bila kufanyiwa uchunguzi wa ubora. Hata hivyo, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria iliruhusu matumizi ya maji kutoka kwenye mabwawa tisa kwa madhumuni ya matumizi ya wanakijiji bila kufanyiwa uchunguzi, hivyo kukiuka kanuni hiyo.

Mabwawa hayo ni New Sola, Manchira, Nyankanga, Tagota, Mwadila, Zebeya, Ilambambasa, Igumangobo, na Malya. Sababu kuu ni kutofuatwa kwa kanuni. Matumizi ya maji yasiyopimwa ubora kutoka kwenye mabwawa yanaweza kuhatarisha afya za watumiaji.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria inapima ubora wa maji kwa vyanzo vyote vya maji vya Mabwawa kabla ya kuruhusu matumizi ya maji husika. Pia, ihakikishe inafuata matakwa ya Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2018.**

### 8.5.2 Ufuatiliaji Usioridhisha wa Ubora wa Maji katika Migodi ya Dhahabu Unaohatarisha Afya ya Jamii

Ufuatiliaji wa ubora wa maji katika migodi ya dhahabu unahusisha kuchunguza sifa za maji, kemikali, na baiolojia za maji kwa maeneo ya ndani na yaliyo karibu na migodi. Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria inatakiwa kufanya ufuatiliaji mara nne kwa mwaka wa ubora wa maji katika vituo vya utafiti vilivyowekwa katika maeneo ya migodi ya dhahabu.

Hata hivyo, katika mwaka wa 2023/24, ufuatiliaji wa ubora wa maji ulifanywa mara moja tu katika migodi ya dhahabu ya North Mara, Bulyanhulu, Buzwagi, na Geita, badala ya mara nne. Upungufu huu ulitokana na uhaba wa fedha, jambo ambalo lilidhoofisha uwezo wa Bodi kufuatilia na kupunguza hatari za uchafuzi

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria inatenga fedha za kutosha za ufuatiliaji wa mara kwa mara wa ubora wa maji katika migodi ya dhahabu ili kuzuia uchafuzi maji na kulinda afya za jamii.**

### 8.5.3 Kutofanya Vipimo vya Ubora wa Maji

Kanuni ya 6(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Ufuatiliaji Ubora wa Maji) ya mwaka 2018 inaelekeza utoaji wa cheti cha upimaji ubora wa maji na mamlaka husika mara tu itakapothibitishwa kuwa ubora wa maji ni salama kwa matumizi ya binadamu. Zaidi ya hayo miongozo ya uendeshaji na matengenezo ya skimu za maji vijijini na vifaa vya usafi wa mazingira ya mwaka 2021 inaelekeza skimu za maji kupima Ubora wa maji ghafi na yaliyosafishwa yanayosambazwa kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulifichua kuwa CBWSOs 11 zilishindwa kutekeleza mpango wa utaratibu wa ufuatiliaji wa ubora wa maji. Mchanganuo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 38**.

**Jedwali Na. 38: Vyombo vya kijamii vya utoaji wa huduma za maji visivyofanya vipimo vya ubora wa maji**

| Na. | Mkoa | Jina la chombo |
|---|---|---|
| 1. | Mara | Kibara |
| 2. | Mara | Mwibagi |
| 3. | Mara | Bulisumakwi |
| 4. | Mara | Sukuchiwasa |
| 5. | Mara | Kyabarakiko |
| 6. | Mara | Grumet |
| 7. | Mara | Sirari |
| 8. | Katavi | Mmasi |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Katavi | Ndui/Nyaki |
| 10. | Ruvuma | Kiambwso |
| 11. | Singida | Riftvalley |

***Chanzo***: *Taarifa ya Ukaguzi*

Zaidi ya hayo, katika CBWSO ya Wangogo (Mkoa wa Katavi), matokeo ya majaribio yalithibitisha kuwa maji ya kisima yalishindwa kufikia viwango vya ubora, lakini bado yaliendelea kusambazwa kwa jamii. Tatizo hili lilitokana na upungufu wa bajeti ya kuyasafisha maji na uangalizi usioridhisha wa RUWASA, jambo ambalo liliongeza hatari ya magonjwa yanayosababishwa na maji.

**Ninapendekeza Serikali kupitia RUWASA ianzishe programu ya kina ya ufuatiliaji wa ubora wa maji, pamoja na matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu na uboreshaji ili kuzuia uchafuzi. Kwa maji yasiyo salama, vyanzo mbadala vya maji salama vitafutwe, na udhibiti mkali wa kanuni za ubora wa maji uhakikishwe ili kudumisha utii na kulinda afya ya jamii.**

### 8.5.4 Kuchelewa kwa Miaka Sita katika Kuhuisha Miongozo ya Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa

Miongozo ya Kitaifa ya Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa (2018) inaweka miongozo ya kufanya majaribio, viwango vya ubora, na majukumu ya wahusika. Jedwali 7.1 la miongozo hiyo linaagiza kuwa Wizara ya Maji ipitie na kuhuisha miongozo hiyo kila baada ya miaka mitatu.

Hata hivyo, kufikia Desemba 2024, miongozo hiyo haijpitiwa na kuhuishwa kwa miaka sita, hasa kutokana na ukosefu wa fedha. Miongozo ambayo imepitwa na wakati inaweza kudhoofisha viwango vya ubora wa maji, na kufanya ufuatiliaji usioridhisha katika kulinda afya ya umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe Wizara ya Maji inatenga rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya kupitia na kuhuisha Miongozo ya Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa.**

### 8.5.5 Ukosefu wa Uangalizi wa Maabara Binafsi za Upimaji wa Ubora wa Maji

Aya ya 4.2.2(i) ya Sera ya Kitaifa ya Maji (2002) inahitaji ufuatiliaji na tathmini ya utaratibu wa ubora wa maji ili kudumisha viwango vya maji salama ya kunywa.

Hata hivyo, ukaguzi ulibainu Wizara ya Maji haina hifadhidata au utaratibu wa uangalizi na udhibiti wa maabara binafsi za kupima maji. Pengo hili

limesababisha kutofautiana katika tathmini za ubora wa maji na michakato ya upimaji wa maji usio na udhibiti.

Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji), 2018 hazitaji kwa uwazi kuwa Wizara idhibiti maabara binafsi za maji, jambo ambalo limesababisha ukosefu wa uwajibikaji na usawa katika upimaji wa maji.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji ipitie Kanuni za Usimamizi wa Rasilimali za Maji ili kujumuisha jukumu la kufanya uangalizi na udhibiti wa maabara binafsi za upimaji wa ubora wa maji. Hii itahakikisha usawa katika upimaji na utoaji wa taarifa za uchunguzi wa ubora wa maji.**

# SURA YA TISA



## Sekta ya Afya

# SEKTA YA AFYA

## 9.1 Utangulizi

Sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, kwani ina mchango mkubwa kwenye ustawi wa umma na tija ya kiuchumi. Mifumo bora ya afya inahitaji ugawaji mzuri wa rasilimali, usimamizi thabiti, na uzingatiaji wa viwango vya udhibiti vilivyowekwa ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Sura hii inaangazia masuala ya ufanisi yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa shughuli za sekta ya afya. Ukaguzi huo ulijumuisha sehemu mbalimbali za mifumo ya afya, zikiwamo Hospitali za Rufaa za mikoa na Hospitali Maalumu, pamoja na majukumu na ufanisi wa Mabaraza ya Afya, Bodi za Afya, na Wizara ya Afya katika kutekeleza majukumu yao husika.

Yafuatayo ni masuala yaliyobainishwa pamoja na mapendekezo yake kama ifuatavyo:

## 9.2 Ukosefu wa Kiunzi cha Kisheria cha Utoaji na Upandikizaji wa Viungo Vya Binadamu

Muongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu Kanuni za Utoaji na upandikizaji wa Seli, Tishu, na Viungo vya Binadamu (2010) unapendekeza kwamba nchi wanachama ziunde viunzi vya kisheria vya kitaifa ili kudhibiti utoaji na upandikizaji wa viungo. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa Tanzania haina kiunzi cha kisheria kusimamia utoaji na upandikizaji wa viungo vya binadamu kama vile figo, uboho wa mfupa, na vipandikizi vya sikio (cochlear implants).

Kukosekana kwa kiunzi cha kisheria huongeza hatari ya matibabu kufanyika bila kuzingatia taratibu, kanuni na viwango, na pia kunaweza kusababisha kuwepo kwa biashara haramu ya viungo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya upandikizaji wa viungo. Hali hii inatokana na ucheleweshaji wa kuandaa sheria muhimu zinazohitajika.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Afya, iharakishe uanzishaji wa kiunzi cha kisheria cha kusimamia utoaji na upandikizaji wa viungo vya binadamu na kuhakikisha inazingatia mahitaji ya shirika la afya duniani haraka iwezekanavyo.**

## 9.3 Ucheleweshaji wa Kupitishwa na Utekelezaji wa Miundo Mipya ya Taasisi kwa Hospitali za Rufaa za Kanda

Serikali inaendesha hospitali za kanda za Benjamin Mkapa, Mbeya, Chato, na Mtwara ili kutoa huduma maalumu za afya. Ili kuhakikisha utoaji wa huduma unafanyika kwa usawa na kwa mujibu wa viwango, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliielekeza Wizara ya Afya tarehe 19 Julai 2022 kutekeleza muundo sanifu wa hospitali hizi. Hatua hii ilihusisha kuandaa orodha ya kazi, kuandaa maelezo ya majukumu ya kazi, kuendesha programu za uhamasishaji kwa wafanyakazi, na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji ifikapo tarehe 18 Oktoba 2022. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 26 Februari 2025, utekelezaji ulikuwa haujakamilika kutokana na kukosekana kwa agizo rasmi la uanzishwaji (establishment order) na mfumo wa kisheria wa kuidhinisha muundo huo.

Kwa sasa, Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa ndio pekee inayofanya kazi kama taasisi inayojitegemea yenye muundo kamili na ulioidhinishwa, huku hospitali za rufaa za kanda za Mbeya, Chato, na Mtwara zikifanya kazi chini ya miundo isiyo sawa, na kukosa vitengo muhimu vya usimamizi na Idara muhimu.

Wizara ya Afya iliomba idhini ya kuifanya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya kuwa taasisi inayojitegemea (semi-autonomous), lakini haikujumuisha hospitali za rufaa za kanda za Chato na Mtwara. Hali hii imeendelea kuchelewesha uanzishwaji wa muundo sanifu kwa hospitali hizo. Kutokuwiana huku kunaweza kupelekea utoaji wa huduma usio sawa, kupungua kwa ufanisi wa kazi, na kushuka kwa morali ya wafanyakazi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Afya, iweke kipaumbele na kufuatilia kwa karibu mchakato wa kuanzisha muundo sanifu ili kuhakikisha utekelezaji wa mfumo uliopitishwa katika hospitali zote za kanda. Pia, iharakishe uwasilishaji na uidhinishaji wa maagizo rasmi ya uanzishwaji wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, Chato, na Mtwara ili kuzipatia hadhi ya kisheria. Hatua hii itahakikisha hospitali zote zinafanya kazi chini ya muundo mmoja, hivyo kukuza usawa na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya.**

## 9.4 Kutofanyika kwa Tathmini huru ya Utendaji wa Hospitali

Mwongozo wa Usimamizi saidizi wa ndani (ISS) na Tathmini Huru ya Utendaji wa Hospitali (EHPA) kwa Hospitali za Rufaa (Februari 2018) inahitaji Wizara ya Afya kufanya tathmini huru angalau mara moja kwa mwaka. Tathmini hii inahakikisha

kuwa hospitali zinatoa huduma za afya zenye ubora, salama, na zenye ufanisi, huku zikihamasisha maboresho endelevu .

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha wa 2023/24, tathmini huru ya utendaji wa hospitali haikufanyika katika Hospitali nne za Rufaa za mkoa ambazo ni Amana, Iringa, Morogoro, na Njombe. Hali hii ilitokana na uwajibikaji hafifu wa Wizara ya Afya katika kuhakikisha kuwa tathmini huru za utendaji wa hospitali inatekelezwa kama inavyohitajika. Kutokufanyika kwa tathmini huru kunaweza kuathiri utambuzi wa maeneo yenye mafanikio, changamoto, na yanayohitaji maboresho katika utoaji wa huduma za afya.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na menejimenti ya hospitali tajwa, ihakikishe kuwa tathmini huru za utendaji wa hospitali zinafanyika.**

## 9.5 Upotevu wa Mapato Kutokana na Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Afya ya Kiasi cha Sh. Bilioni 9.64

Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395, kinaeleza kuwa mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo kwa madai yasiyo na sababu ya msingi ya kuzingatia sheria na kanuni zinazohusu malipo ya madai yaliyotolewa chini ya sheria. Vifungu 40 na 41 vya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya vinatoa fursa kwa mtoa huduma za afya kukata rufaa kulingana na masharti ya Mfuko.

Tathmini yangu ya hospitali za rufaa za mikoa, za kibingwa, na za kanda imebaini kuwa hospitali 29 zilikuwa na madai yaliyokataliwa yenye jumla ya Sh. bilioni 9.64 kutokana na changamoto mbalimbali, zikiwamo, kutokuwa wa idhini stahiki, nambari zisizo sahihi za magonjwa, kutokufuata miongozo ya matibabu na nyaraka zenye makosa na zisizokamilika. Changamoto hizi zilitokana na ukosefu wa kutosha wa uhakiki wa ubora wa madai ya huduma ambazo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya haifadhili. Aidha, kiasi kilichokataliwa kimeongezeka kwa Sh. milioni 702.41 (8%) ikilinganishwa na kiasi cha Sh. bilioni 8.94 kilichoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita. Hii inaonesha kuwa Menejimenti haijatekeleza mapendekezo yangu ya kushughulikia suala hili kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. X**

Kukataliwa kwa madai ya bima ya afya kunapunguza mapato ya hospitali na kunakwamisha juhudi za serikali za kutoa huduma bora na endelevu za afya kwa jamii.

**Ninapendekeza kuwa watoa huduma za afya waimarishe mifumo ya udhibiti wa ubora wa ndani kabla ya kuwasilisha madai kwa lengo la kuhakikisha**

**uzingatiaji wa kanuni na sheria za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kupunguza kukataliwa kwa madai. Aidha, Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa hospitali zinafanya maboresho na kufuata taratibu za kukata rufaa kwa madai yanayostahili ili kupata mapato yaliyokataliwa.**

## 9.6 Kuchelewa kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kulipa madai ya hospitali

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Mfuko wa taifa wa Bima ya Afya (NHIF) sura ya 395, kinahitaji Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kulipa madai kwa watoahuduma ndani ya siku sitini baada ya kupokea madai hayo.

Ukaguzi wangu uliofanyika katika kupima muda wa kushughulikia madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya katika hospitali ulibaini kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2023/24, hospitali sita zilikuwa na madai yenye jumla ya Sh. bilioni 5.63 ambayo NHIF haikuyalipa kwa wakati. Malipo hayo yalicheleweshwa kwa muda wa siku 60 hadi 120 zaidi ya tarehe zilizopangwa

**Jedwali Na. 39: Ucheleweshaji wa kulipwa kwa madai ya mfuko wa taifa wa bima ya afya**

| Na. | Jina la Hospitali | Idadi ya siku za ucheleshwaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Benjamin Mkapa | Siku 60 | 3,695,379,433 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Dodoma | Kuanzia siku 90 mpaka 120 | 789,183,891 |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni | Kuanzia siku 30 mpaka 60 | 391,993,663 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Musoma | Siku 120 | 349,726,578 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi | Kuanzia siku 60 mpaka 90 | 207,295,867 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala | Kuanzia siku 60 mpaka 90 | 198,419,919 |
| | Jumla | | **5,631,999,351** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti mwaka 2023/24*

Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa ufanisi katika kuandaa na kuwasilisha fomu za madai kwenda mfuko wa taifa wa bima ya afya, pamoja na ukosefu wa utekelezaji wa masharti ya mikataba kati ya Hospitali na mfuko wa taifa wa bima ya afya. Ucheleweshaji wa kutolewa kwa fedha huathiri uwezo wa kifedha wa hospitali wa kutoa huduma za afya kwa jamii.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na menejimenti ya hospitali, ifanye mazungumzo na mfuko wa taifa wa bima ya afya ili kuhakikisha kuwa madai yanalipwa kwa wakati kama inavyotakiwa**

**na Sheria. Aidha hospitali ziandae na kuwasilisha fomu za madai kwa usahihi na kwa wakati kwa mfuko wa taifa wa bima ya afya.**

## 9.7 Mapato ambayo Hayajakusanywa kutoka kwa Makampuni ya Bima ya Afya na Mifuko ya Fidia - Sh. Bilioni 6.81

Kulingana na Kanuni ya 57(2) ya Kanuni ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanakumbushia kwa haraka malipo yaliyochelewa na kuchukua hatua zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na hatua za kisheria pale inapohitajika.

Ukaguzi wa taarifa za madai ya bima kwa mwaka wa fedha 2023/24 ulibaini kuwa hospitali 14 za rufaa za mikoa zilikuwa na mapato ya Sh. bilioni 6.81 ambayo hayajakusanywa kutoka kwa kampuni za bima za afya na mifuko ya fidia, ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kampuni za bima za Assemble na Strategies, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF). Madai haya ya kurejeshewa gharama za matibabu yalikuwa hayajalipwa kwa hadi miezi 12, hali inayoashiria upungufu katika ufuatiliaji na usimamizi wa hospitali katika kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati kulingana na makubaliano, kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XI.**

Malipo ya huduma za kitabibu yaliyochelewa kwa muda mrefu yanaweza kusababisha vikwazo katika mtiririko wa fedha kwa hospitali, hivyo kusababisha ugumu wa kukidhi gharama za uendeshaji na kuzuia kupokea wagonjwa ambao ni wanachama kutoka makampuni yao ya bima ambayo hayajalipa madai yao.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti za hospitali kutekeleza mkakati wa ukusanyaji wa deni unaojumuisha ufuatiliaji wa kawaida, kukumbushia na mawasiliano ya wazi na wateja kuhusu majukumu ya malipo na vipindi vya malipo.**

**Aidha, Wizara ya Afya inapaswa kuanzisha mfumo wa kufuatilia na kuhakiki madai ya hospitali, ili kuhakikisha kuwa malipo yanakusanywa kwa wakati. Katika hali ambapo kuna ucheleweshaji wa mara kwa mara, adhabu za kisheria na za kimkataba zinapaswa kutekelezwa ili kuwajibisha makampuni ya bima na kuzuia usumbufu katika mtiririko wa fedha wa hospitali na utoaji wa huduma.**

## 9.8 Kutoteketezwa kwa Dawa zilizokwisha Muda wake wa Matumizi

Kanuni ya 10 ya Kanuni ya chakula, dawa na vipodozi ya Tanzania ya mwaka 2015, inamtaka Mkuu au Mfamasia wa Hospitali kuanzisha mchakato wa kuteketeza bidhaa zisizofaa.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa hospitali 11 kati ya 34 zilikuwa na dawa zilizokwisha muda wake zenye thamani ya Sh. bilioni 1.41. Dawa hizo zilikuwa zimehifadhiwa bila kuteketezwa kwa kipindi cha hadi miaka mitano. Rejea **Jedwali Na. 40**.

**Jedwali Na. 40: Kutoteketezwa kwa Dawa Zilizopita Muda**

| Na. | Jina la hospitali | Kiasi (Sh.) | Muda uliopita baada ya kuisha muda wake (miaka) |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Singida | 3,414,126 | 5 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tabora | 619,259,382 | 5 |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana | 1,312,322 | 4 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba | 129,787,992 | 4 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Iringa | 94,747,453 | 4 |
| 6 | Hospitali ya Kibong'oto | 57,488,908 | 4 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Morogoro | 87,134,751 | 2 |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tanga | 69,617,141 | 2 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Njombe | 328,290,326 | 1 |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songwe | 764,075 | 1 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sumbawanga | 20,448,845 | 1 |
| **Jumla** | | **1,412,265,321** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti mwaka 2023/24*

Hali hii ilitokana na uingizwaji wa dawa mpya, ununuzi wa dawa kwa wingi ambazo hazitumiki mara kwa mara na zenye muda mfupi wa matumizi, na mchakato mrefu wa kupata idhini ya kuteketeza dawa. Dawa zilizopitwa muda wa matumizi zinaweza kuwa hatari kwa mazingira na afya ya wafanyakazi na kusababisha hasara kwa Hospitali.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Wizara ya Afya na kwa kushirikiana na menejimenti za hospitali, (a) kushauriana na Wizara ya Fedha ili kupata idhini na miongozo ya kuteketeza dawa zilizopitwa muda, na (b) kuhakikisha kuwa dawa zinazonunuliwa ni zile zinazohitajika na hospitali na zilizo na maisha marefu.**

## 9.9 Watoahuduma wa Afya na Shule zinazotoa Huduma bila Leseni

Katika kuhakikisha kuwa wataalamu wa afya, watoa huduma wa tiba asili, na vyuo wanazingatia masharti ya leseni, hatua hii ni muhimu kwa utoaji wa huduma bora za afya, usalama wa wagonjwa, na usimamizi wa kanuni za udhibiti. Sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Wataalamu wa Matibabu, Meno na Afya ya Mwaka 2017, Kanuni za Mafunzo ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010,

pamoja na Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala (Usajili wa Wataalamu na Vituo vya Afya) G.N 411 ya Mwaka 2008, zinawataka watoa huduma na taasisi zote za mafunzo kupata na kuhuisha leseni zao ili kuendesha shughuli zao kihalali.

Hata hivyo, ukaguzi wa mwaka wa 2023/24 ulibaini ukiukwaji wa sheria hizi katika sekta ya afya. Wataalamu wa afya 84 katika hospitali za rufaa za mikoa saba, wakiwemo madaktari, wataalamu wa mionzi ambao walikuwa wakifanya kazi bila leseni zilizohuishwa kutoka Baraza la madaktari (MCT) na Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania (TAEC).

**Jedwali Na. 41: Hospitali za Rufaa za mikoa zilizo na Wataalamu wa Afya bila Leseni za Kufanya Kazi**

| Na. | Jina la hospitali | Idadi ya wataalamu | Kundi la wataalamu |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Katavi | 20 | Madaktari |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Morogoro | 20 | Madaktari |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Ligula | 14 | Madaktari |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tabora | 9 | Madaktari |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tanga | 8 | Madaktari |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Manyara | 8 | Wataalamu wa mionzi watatu na Madaktari watano |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sumbawanga | 5 | Madaktari watatu na madaktari wa meno wawili |
| | **Jumla** | **84** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti mwaka 2023/24*

Pia, Vyuo 50 vinavyotoa mafunzo ya uuguzi na ukunga havikuhuisha leseni zao kama inavyotakiwa na Kanuni ya 6 ya Kanuni za Ufundishaji wa Uuguzi na Ukunga ya 2010 katika wa mwaka wa fedha 2023/24. Watoahuduma wa dawa za tiba asili hawakuhuisha leseni zao kinyume na sheria ya hivyo kusababisha ukosefu ya mapato ya Sh. Milioni 304.97 kwa baraza kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 42.**

**Jedwali Na. 42: Watoahuduma bila Leseni Halali**

| Kundi | Mwaka ambao leseni zimekwisha muda | Idadi ya watendaji | Kiwango | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Watendaji | 2019 | 161 | 100,000 | 16,100,000.00 |
| | 2020 | 194 | 100,000 | 19,400,000.00 |
| | 2021 | 818 | 100,000 | 81,800,000.00 |
| | 2022 | 628 | 100,000 | 62,800,000.00 |
| | 2023 | 598 | 100,000 | 59,800,000.00 |
| Wauzaji wa tiba asili | 2015 | 265 | 75,000 | 19,875,000.00 |
| | 2022 | 8 | 75,000 | 600,000.00 |
| | 2023 | 8 | 75,000 | 600,000.00 |

| Kundi | Mwaka ambao leseni zimekwisha muda | Idadi ya watendaji | Kiwango | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| Vituo | 2017 | 79 | 250,000 | 19,750,000.00 |
| | 2021 | 24 | 250,000 | 6,000,000.00 |
| | 2022 | 52 | 250,000 | 13,000,000.00 |
| | 2023 | 21 | 250,000 | 5,250,000.00 |
| **Jumla** | | | | **304,975,000** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti mwaka 2023/24*

Mapungufu haya yanatokana na kukosekana kwa ufanisi wa mifumo ya ndani ya Wizara ya Afya na vyombo vinavyohusika vya udhibiti katika ufuatiliaji na kuhakikisha utekelezaji wa sheria. Kuruhusu wataalamu wasio na leseni kufanya kazi kunaweza kuhatarisha usalama wa wagonjwa. Zaidi ya hayo, vyuo zinazofanya kazi bila leseni zilizohuishwa zinadhoofisha uhalali na uaminifu wa programu za mafunzo zinazotolewa. Pia, kutohuisha leseni kunasababisha upotevu wa mapato kwa mabaraza yanayotokana na ada za kuhuisha leseni.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na menejimenti za hospitali, baraza la madaktari, na baraza la tiba asili na tiba mbadala, iimarishe udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha kuwa wataalamu wote wa afya wanasajiliwa na wanayo leseni halali za kufanya kazi. Zaidi ya hayo, iimarishe utekelezaji wa kusasisha leseni kupitia ufuatiliaji mkali na kuweka vikwazo kwa shule zisizofuata kanuni.**

# SURA YA KUMI



# Sekta Nyingine

## SEKTA NYINGINE

### 10.1 Utangulizi

Shughuli za Maendeleo ya Tanzania zinaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, ambayo inalenga kuboresha kiwango cha maisha, amani na utulivu, utawala bora, jamii yenye elimu na inayojifunza, pamoja na uchumi shindani kwa ajili ya maendeleo endelevu. Ili kufikia malengo haya, mageuzi mbalimbali yamefanyika yakihusisha sekta kama kilimo, mifugo na uvuvi, madini, nishati, elimu, na ardhi, hivyo kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Sura hii inaangazia masuala muhimu yaliyobainika katika sekta nyingine za Elimu, Madini, Nishati, Ardhi, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii. Inaangazia maeneo yanayohitaji uangalizi wa haraka na mageuzi.

### 10.2 Madini na Nishati

Sekta za madini na nishati zina mchango mkubwa katika kusaidia uchumi na kuchochea maendeleo ya jumla ya Tanzania. Wizara ya Nishati ina jukumu la kusimamia usimamizi wa rasilimali za nishati na petroli, uongezaji thamani katika petroli, kuendeleza miundombinu ya mafuta na gesi, ununuzi wa mafuta kwa pamoja, mipango ya umeme mijini na vijijini, pamoja na maslahi ya wazawa katika vyanzo vya nishati na petroli vinavyoweza kuhuishwa au kutohuishwa. Wizara ya Madini inatekeleza jukumu lake la kusimamia na kudhibiti masuala yote yanayohusiana na sekta ya madini kwa mujibu wa Amri ya Rais iliyochapishwa katika Tangazo la Serikali (GN) Na. 432 lililotolewa tarehe 20 Oktoba 2017. Pia, ina wajibu wa kuandaa, kutekeleza, na kufuatilia sera zote zinazohusiana na sekta ya madini.

Ukaguzi wangu kwenye sekta hizi umebaini upungufu unaoweza kuathiri utendaji na ufanisi wa sekta ya nishati na madini kama ilivyobainishwa katika aya zifuatazo:

#### 10.2.1 Kuchelewa Kutekelezwa kwa Ulinganifu wa Bei za Mafuta kwa Kampuni za Uagizaji wa Mafuta

Ulinganifu wa bei za mafuta unalenga kufanya bei ya mafuta kuwa sawa hata kama gharama ya kushusha mafuta ni nafuu zaidi katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na bandari nyingine kama Mtwara na Tanga.

Kanuni ya 14A ya Marekebisho ya Kanuni za Petroli (Ununuzi wa Pamoja kwa Jumla) za mwaka 2024 inataka gharama za bidhaa zote zinazoletwa kupitia

Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja kwa Jumla ziwe sawa ili kuhakikisha matumizi bora ya bandari zote zinazoingiza mafuta. Gharama ya kushusha bidhaa ni jumla ya bei ya bidhaa ya mafuta mara baada ya kufika katika kituo kilichoteuliwa na Kampuni za Uagizaji wa Mafuta (*Oil Marketing Companies* - OMC).

Mwezi Machi 2024, Mamlaka ya Ununuzi wa Pamoja wa Mafuta ya Petroli (PBPA) ilianzisha mchakato wa ulinganifu wa bei ili kusawazisha bei za mafuta katika bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara. PBPA inafidia gharama za juu za kushusha mafuta zilizoingiwa na Kampuni za Uagizaji wa Mafuta (OMCs) katika bandari ghali zaidi, kama Mtwara na Tanga, kwa kutumia michango kutoka kwa OMCs zinazofaidika na gharama za chini za kushusha mafuta katika bandari nafuu kama Dar es Salaam. Michango hii inapaswa kukusanywa kupitia akaunti maalumu kwa ajili ya kuweka kiasi cha ziada kinachokusanywa kutoka kwa OMCs. Utaratibu huu unahakikisha kuwa bei za mafuta zinakuwa sawa kote nchini.

Mapitio yangu yamebaini kuwa tangu mchakato wa ulinganifu wa bei uanze mwezi Machi 2024, PBPA bado haijakusanya michango kutoka kwa OMCs wala kutoa fidia kwa OMCs wanaokabiliwa na gharama za juu za kushusha mafuta katika bandari kama Mtwara na Tanga. Mamlaka ya Ununuzi wa Pamoja wa Mafuta ya Petroli (PBPA) ilieleza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ndiyo yenye jukumu la kukokotoa kiwango cha makusanyo na kubaini kiasi cha marejesho. PBPA itakusanya na kulipa fidia kwa kuzingatia kiwango kinachowekwa na EWURA, ambacho bado hakijakamilika.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Taratibu za Kawaida za Uendeshaji (SOPs), PBPA inapaswa kukusanya takwimu za kila mwezi za meli zote za bidhaa za petroli zilizoshushwa na kukokotoa gharama ya wastani ya kushusha mafuta.

Ucheleweshaji huu unatokana na udhaifu wa PBPA katika kutekeleza michakato ya kukokotoa gharama za kushusha mafuta kwenye bandari na kukusanya michango ya OMCs, jambo linaloathiri mchakato wa ulinganifu wa bei, pia ukosefu wa kipengele maalumu katika kanuni na taratibu za uendeshaji (SOPs) kinachoelekeza muda wa kulipa fidia.

Kuna hatari kuwa Kampuni za Uagizaji wa Mafuta zinazofanya kazi katika bandari zenye gharama kubwa kubeba gharama za juu bila kupata fidia, jambo linaloweza kupunguza faida zao na pengine kuzuia ushiriki wao endelevu katika biashara ya mafuta. Hali hii, hatimaye, inaweza kuathiri bei za mafuta kote nchini.

**Ninapendekeza kwamba uongozi wa PBPA uharakishe mchakato wa ulinganifu wa bei za mafuta kwa kukokotoa viwango husika vya makusanyo**

**na kutekeleza malipo ili kuwezesha fidia kwa wakati kwa Kampuni za Uagizaji wa Mafuta ambazo zilikuwa na gharama za juu za kushusha mafuta. Taratibu na kanuni za Uendeshaji (SOPs) zinapaswa kurekebishwa ili kujumuisha muda maalumu wa malipo ya fidia kwa makampuni husika.**

### 10.2.2 Hasara ya Dola za Marekani milioni 147 kutokana na Kufutwa kwa Leseni Hodhi za Madini

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kinamruhusu Waziri kuingia katika makubaliano ya kimaendeleo na wamiliki wa leseni za madini, ikijumuisha haki za madini, shughuli za uchimbaji, hisa isiyo na gharama ya serikali, ushiriki wa serikali, na ufadhili wa kifedha.

Baada ya mabadiliko ya sheria hiyo mwaka 2017, kifungu cha 10 kinataka Serikali kuwa na angalau 16% ya hisa ambazo hazina gharama zisizoweza kupunguzwa katika kampuni za uchimbaji madini, kulingana na aina ya madini na kiwango cha uwekezaji. Zaidi ya hayo, Serikali itakuwa na haki ya kumiliki hadi 50% ya hisa, kulingana na matumizi ya kodi yaliyosamehewa ambayo yangetozwa kwa kampuni ya uchimbaji madini.

Ili kutekeleza masharti haya, Kifungu cha 11 (kilichorekebishwa) kinataka makubaliano yote ya madini yaliyofikiwa kabla ya kuanza kutumika kwa kifungu hiki yatabaki kuwa na nguvu, kulingana na masharti ya Sheria ya Mikataba ya Utajiri wa Asili na Rasilimali (mapitio na majadiliano ya masharti yasiyofaa) ya mwaka 2017. Hii inamaanisha kuwa serikali inaweza kurejea na kujadiliana tena masharti katika mikataba ya zamani ikiwa yatabainika kuwa hayafai au hayana manufaa.

Mwaka 2017 Serikali ilifuta leseni hodhi za wamiliki 12 wa leseni za madini. Hatua hii ilisababisha migogoro ya kisheria, ambapo wahusika watatu walioathirika waliwasilisha kesi katika Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID). Kutokana na migogoro hiyo, jumla ya madai yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 147 yalitatuliwa nje ya mahakama, huku serikali ikiwa tayari imelipa Dola za Marekani milioni 117 (Sh. bilioni 306.14), na kubaki na deni la Dola za Marekani milioni 30 ambalo halijalipwa. Matokeo haya yanaonesha hatari kubwa za kifedha, ikijumuisha uwezekano wa malipo yasiyo na tija yanayotokana na mchakato huo.

Sababu kuu ya migogoro hii ya kisheria na madeni ni utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 kuhusisha mikataba ya nyuma, hivyo kusababisha kufutwa kwa leseni hodhi za madini zilizotolewa kabla ya 2017.

**Ninapendekeza kuwa marekebisho yajayo ya sheria za madini yasitekelezwe kwa kuhusisha makubaliano au mikataba iliyoingiwa zamani kabla ya mabadiliko husika. Badala yake, sheria mpya zinapaswa kutumika na kutekelezwa kuanzia kipindi mabadiliko yalipotokea ili kuwa na uhakika wa kisheria na kulinda haki za wawekezaji.**

## 10.3 Ardhi, Kilimo, Mifugo na Utalii

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepewa mamlaka ya kuwezesha usimamizi madhubuti wa ardhi na huduma za maendeleo ya makazi kwa ajili ya ustawi wa kijamii na kiuchumi wa jamii ya Tanzania. Usimamizi wa ardhi unachukua nafasi muhimu katika kuimarisha uzalishaji wa kilimo, rasilimali za mifugo na uvuvi, pamoja na kusimamia rasilimali za asili na kukuza utalii.

Sehemu hii inalenga kuangazia upungufu unaoathiri malengo ya usimamizi madhubuti wa ardhi, usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kilimo, ongezeko la thamani katika kilimo, udhibiti endelevu wa rasilimali za mifugo na uvuvi, pamoja na uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za asili na za kitamaduni. Aidha, inahusisha uendelezaji wa utalii, huku ikitoa mapendekezo yenye manufaa.

Tathmini yangu ya utendaji wa sekta hizi kupitia Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, pamoja na taasisi na mashirika yanayohusiana na wizara hizi imebaini yafuatayo:

### 10.3.1 Kasi Ndogo katika Kutatua Migogoro ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 246

Kufuatia migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya jamii na Serikali, mnamo Januari 2019, Ofisi ya Rais iliwaelekeza mawaziri wanane wa sekta ambazo zimeathiriwa na migogoro ya matumizi ya ardhi kuwasilisha mapendekezo yatakayotoa suluhisho la kudumu kwa migogoro hiyo.

Wizara hizo ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ulinzi, na Wizara ya Fedha. Maelekezo hayo yalilenga maeneo yaliyo hatarini kukumbwa na migogoro kama vile maeneo ya ufugaji, kilimo, ulinzi na usalama, hifadhi za misitu, hifadhi za wanyamapori, vyanzo vya maji, na maeneo ya uhifadhi wa mazingira.

Mapitio yangu yalibaini kuwa Kamati ya Mawaziri wa Sekta ilifanya uchambuzi wa vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi katika mikoa yote ya Tanzania na kubaini vijiji 975 vyenye migogoro hiyo. Kamati iliwasilisha ripoti yenye mapendekezo kwa Serikali na mnamo tarehe 23 Septemba 2019, Baraza la Mawaziri lilitoa maamuzi na maelekezo kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji hivyo 975. Zoezi hilo lilipaswa kukamilika mwaka 2022.

Hata hivyo, licha ya Kamati ya Mawaziri wa Kisekta kuwa na mpango wa utekelezaji wa kutatua migogoro iliyosalia ifikapo Juni 2024, nilibaini kuwa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 729 (75%) imetatuliwa, huku migogoro ya vijiji 246 (25%) bado haijatatuliwa. Hii ni kutokana na baadhi ya wananchi kutokubaliana na mapendekezo ya serikali ya kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao, jambo ambalo limechelewesha mchakato.

Maoni yangu ni kuwa, kutotatuliwa kwa migogoro ya matumizi ya ardhi za vijiji ni hatari kwa usimamizi wa rasilimali za nchi, kama vile mbuga za taifa, hifadhi za misitu, na vyanzo vya maji. Pia, kunaweza kusababisha ukuaji mdogo wa uchumi na usalama hafifu katika nchi.

**Ninapendekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta, waandae mikakati inayowezekana kutatua migogoro iliyosalia ya matumizi ya ardhi, ikishughulikia masuala ya wananchi na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za nchi.**

### 10.3.2 Kutofikiwa kwa Lengo la Urasimishaji wa Vipande 500,000 vya Ardhi na Tathmini ya Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Miaka 10 ya Urasimishaji Ardhi

Vifungu vya 56-60 vya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na kifungu cha 23 cha Sheria ya Upangaji Miji ya mwaka 2007 kinatoa mamlaka ya kisheria kwa ajili ya urasimishaji wa makazi yasiyopangwa.

Kwa upande mwingine hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi kwa mwaka 2023/24 katika Aya ya 70 iliweka malengo ya Wizara ya Ardhi kurasimisha vipande 500,000 vya ardhi ndani ya mwaka huo. Vilevile, hotuba hiyo ilionesha kuwa Wizara ya Ardhi inakusudia kutathmini utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Miaka 10 ya Urasimishaji na Uzuiaji wa Makazi yasiyopangwa, ambayo ilianza mwaka 2013 hadi 2023. Tathmini hii inalenga kubaini mafanikio na changamoto za programu hiyo na kutoa mapendekezo bayana jinsi ya kushughulikia urasimishaji wa makazi yasiyopangwa nchini.

Mapitio yangu ya ripoti ya utekelezaji wa urasimishaji kwa mwaka 2023/24 ilionesha kuwa Wizara ya Ardhi haijatekeleza tathmini ya programu ya miaka 10 na imefanikiwa kupima na kuidhinisha vipande 222,545 (44.5%) vya ardhi kati ya lengo lililowekwa.

Ninahusisha udhaifu huu na mikakati isiyojitosheleza ya Wizara ya Ardhi katika kusimamia na kudhibiti urasimishaji pamoja na ukosefu wa rasilimali za kifedha za kutosha kusaidia zoezi la tathmini.

Kutofanikiwa kwa lengo lililowekwa la urasimishaji kunaleta hatari ya kuongezeka kwa makazi yasiyopangwa ambayo yanaweza kuwanyima wananchi huduma bora za miundombinu na mazingira salama. Vilevile, kushindwa kutathmini programu hiyo kunazuia wizara kubaini kwa utimilifu mafanikio na changamoto za mpango huo, jambo ambalo lingetoa miongozo bora ya jinsi ya kusimamia urasimishaji wa makazi yasiyopangwa nchini.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Ardhi ihakikishe rasilimali fedha za kutosha inapatikana. Pia, itafiti njia bora na za ufanisi ili kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa miaka kumi wa Programu ya Kitaifa ya Urasimishaji na Uzuiaji wa Makazi yasiyopangwa 2013-2023. Vilevile, iandae mikakati inayofaa ili kuboresha upungufu uliobainishwa.**

### 10.3.3 Kuchelewa Kutekeleza Mradi wa Ardhi Namba 4951

Tume ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi ya Taifa inatekeleza mradi wa ardhi namba 4951 ili kuboresha mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya 38 na vijiji 1,520. Vijiji hivyo vipo kando ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Reli ya Kisasa, Mtambo wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, Kanda ya Magharibi, na wilaya zinazopakana na Tanzania na nchi nyingine. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miaka saba ya fedha, kuanzia 2018/19 hadi 2024/25.

Katika ukaguzi wangu wa andiko la mradi la Januari 2018, nilibaini kuwa mradi huu ungehusisha kuandaa Mipango ya Mfumo wa Matumizi ya Ardhi kwa wilaya 38 na mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 1,520 katika maeneo yanayokabiliwa na uharibifu mkubwa wa bioanuai na mazingira, migogoro ya matumizi ya ardhi, na ukosefu wa usalama wa umiliki. Pia, nilibaini kuwa mradi huu ungetekelezwa kwa kutumia bajeti ya serikali ya Sh. bilioni 32.21 ndani ya kipindi cha miaka saba ya fedha.

Hata hivyo, nilibaini ucheleweshaji katika utekelezaji wa mradi. Hadi tarehe 30 Juni 2024, tume ilikuwa imeandaa mipango miwili tu ya Mfumo wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya (DLUFPs) (5%) kati ya 38, hivyo kuacha mipango 36 (95%) ambayo

haikuandaliwa. Aidha, kati ya mipango 1,520 ya Mfumo wa Matumizi ya Ardhi ya Vijiji (VLUFPs), tume ilikuwa imeandaa mipango 782, na kuacha mipango 738 ambayo haikuandaliwa

Ucheleweshaji huu ulisababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha kutoka serikalini. Hadi tarehe 30 Juni 2024, tume ilikuwa imepokea Sh. bilioni 11.47 (36%) pekee kati ya bajeti jumla ya Sh. bilioni 32.21. Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi huu unaleta hatari za uharibifu wa mazingira, migogoro ya ardhi na ukosefu wa usalama wa umiliki ardhi, jambo linalosababisha maendeleo duni ya kiuchumi na hatari za kijamii na kibaolojia.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili kutekeleza mradi na kufikia manufaa yanayotarajiwa bila kuchelewa.**

### 10.3.4 Changamoto katika Kufikia Malengo ya Udahili na Malengo ya Utoaji Mikopo kwa Vijana katika Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT-YIA)

Mnamo Agosti 2022, Wizara ya Kilimo ilizindua programu ya "Jenga Kesho iliyo Bora: Mipango ya Vijana kwa Kilimobiashara (BBT-YIA)" ili kushughulikia changamoto ya ushiriki mdogo wa vijana katika sekta ya kilimo, hivyo kuongeza mchango wao katika sekta hii. Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora inajumuisha kipindi cha miaka minane (kuanzia 2022/23 hadi 2029/30). Lengo kuu la kimkakati ni kutoa mafunzo kwa vijana 1,500,000 katika kilimo, uelewa wa kifedha, na ujasiriamali. Pia, inalenga kuboresha ujuzi wa vitendo wa vijana 20,000 kupitia programu za mafunzo ya kazi, na kuwaongoza na kuwafundisha vijana 15,000 wanaoanzisha kilimobiashara kupitia programu za kuanzisha biashara hadi mwaka 2030.

Programu hii inakadiriwa kugharimu Sh. bilioni 356.199 (sawa na Dola za Marekani milioni 148.41). Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inachangia 24% ya bajeti, huku 76% iliyobaki inatolewa na washirika wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), na sekta binafsi.

Tathmini yangu ya mpango kazi wa BBT-YIA kwa mwaka 2023/24 ilibaini kuwa wizara ilikusudia kudahili kundi la pili la vijana 1,000 na kutoa mikopo kwa vijana 100 kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ifikapo tarehe 30 Juni 2024. Hata hivyo, hadi tarehe 15 Septemba 2024, hakuna vijana waliodahiliwa kujiunga na programu hii kwa mwaka 2023/24, huku mikopo ikitolewa kwa vijana 35 pekee, hali inayoashiria upungufu katika kufikia malengo yaliyowekwa. Hii inatokana na ukosefu wa fedha za kutosha na zisizo na uhakika kwa ajili ya programu hii, pamoja na uelewa mdogo au uhitaji duni miongoni

mwa vijana wanaostahili kupata mikopo ya kilimo. Jambo hili linachangiwa na mikakati dhaifu ya kuwafikia na kuwahamasisha walengwa wa mpango huo.

Aidha, nilibaini kasi ndogo katika utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2023/24, ambapo shughuli 15 kati ya 59 zilichelewa kutekelezwa. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. XII.**

Kushindwa kufikia malengo ya kudahili na kutoa mikopo kwa vijana kunakwamisha malengo ya programu ya kuwashirikisha vijana katika kilimo biashara.

**Ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali: ihakikishe fedha za kutosha zinapatikana ili kusaidia programu hii kwa kuboresha ushirikiano na mawasiliano na mashirika ya ufadhili; iandae mpango wa dharura wa kutambua vyanzo mbadala vya fedha, na kurekebisha mpango kazi wa programu ili uendane na rasilimali zilizopo; na iimarishe mawasiliano na kampeni za uhamasishaji ili kuwajulisha na kuwahimiza vijana wanaostahili kutumia fursa za mikopo ya kilimo biashara.**

### 10.3.5 Kutofanya Kazi kwa Masoko ya Upili ya Mifugo yenye Thamani ya Sh. Milioni 502.58.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza majukumu yake kulingana na dira ya Sekta ya Mifugo: "Kuwa na Sekta ya Mifugo inayohusisha biashara kwa kiwango kikubwa, ya kisasa, na endelevu, ikitumia mifugo bora na yenye tija kubwa ili kuhakikisha usalama wa chakula, kuimarisha kipato cha kaya na taifa, na kulinda mazingira."

Tathmini yangu ya Idara ya Maendeleo ya Uzalishaji na Masoko ilibaini kuwa, kati ya miaka ya fedha 2020/21 na 2021/22, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilijenga masoko sita ya upili ya mifugo kwa jumla ya gharama ya Sh. bilioni 6.06. Hata hivyo, masoko matatu (Buhigwe – Kigoma, Kileo – Moshi, na Nata – Nzega) yenye thamani ya Sh. milioni 502.58 hayajaanza kufanya kazi kwa zaidi ya miaka minne kutokana na ukosefu wa tathmini ya kina iliyotakiwa kufanyika kabla ya kupendekeza ujenzi wa masoko hayo.

Ninaamini kwamba bila ya kuwa na mifumo imara ya usimamizi wa miradi na fedha za umma, pamoja na nia ya mgawanyo sahihi wa rasilimali kwa wakati, Serikali itaendelea kupata hasara kutokana na matumizi yasiyo na tija ambayo yangeweza kuepukwa kwa kufanya maamuzi sahihi kwa wakati na mahali panapofaa.

**Ninapendekeza kwamba Wizara Mifugo na Uvuvi itatue changamoto zinazozuia matumizi ya masoko yaliyojengwa. Ili kuepuka matumizi yasiyo na tija, ni muhimu kuwa na mifumo imara ya usimamizi wa miradi na fedha za umma pamoja na mgawanyo wa rasilimali kutokana na uhitaji na kwa wakati.**

### 10.3.6 Kuchelewa kulipwa fidia ya Sh. Bilioni 21.95 kwa Migogoro ya Ardhi Iliyotatuliwa

Kanuni ya 13 ya Sheria ya Ardhi (Thamani ya Ardhi kwa Madhumuni ya Fidia) ya mwaka 2001 inataka fidia ya ardhi ilipwe ndani ya miezi sita baada ya uthibitisho wa tathmini.

Mnamo Januari 2019, Wizara ya Maliasili na Utalii iliunda kamati ya kutatua migogoro ya ardhi ya maliasili katika vijiji 975 katika mikoa 26. Kati ya mwaka 2021 na 2023, vijiji tisa katika maeneo sita vilifanyiwa tathmini ya fidia yenye jumla ya Sh. bilioni 68.43 ili kumaliza migogoro ya ardhi kati ya jamii zinazozunguka maliasili. Hata hivyo, ni vijiji sita pekee kutoka maeneo mawili vilivyopokea fidia ya sehemu ya Sh. bilioni 46.48, hivyo kuacha kiasi cha Sh. bilioni 21.95 hakijalipwa kwa vijiji vitatu vilivyosalia katika maeneo manne.

Upungufu huu wa malipo ya fidia uliotokana na uchache wa fedha kutoka serikalini unaweza kusababisha malalamiko, ongezeko la uvamizi, na uwezekano wa kutozwa riba kwa kuchelewesha malipo ya fidia kwa zaidi ya miezi sita.

**Ninapendekeza kwamba Serikali itoe kipaumbele cha kutoa fedha za kutosha ili kulipa fidia kamili kwa vijiji vilivyosalia, hivyo kuzuia malalamiko na uvamizi, huku ikiepuka gharama za ziada za riba.**

### 10.3.7 Maombi Yasiyokaguliwa kwa ajili ya Malipo ya Fidia ya Sh. Bilioni 4.83

Kanuni za 3, 4, na 5 za Kanuni za Uhifadhi wa Wanyama Pori (Fidia kwa Uharibifu wa Wanyama Hatari) za mwaka 2011 zinahitaji watu ambao mazao au mifugo yao imeharibiwa na wanyama hatari kuripoti tukio hilo kwa afisa mtendaji wa kijiji aliye karibu ndani ya siku tatu. Pia, wanapaswa kuomba malipo ya fidia kwa mkurugenzi wa wanyama pori kwa kutumia fomu maalumu iliyotolewa ndani ya siku saba. Kisha, mkurugenzi anapaswa kufanya ukaguzi ili kutathmini uhalali wa kupokea fidia.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini kwamba Mfuko wa Ulinzi wa Wanyama Pori Tanzania ulipokea maombi 35,287 ya malipo ya fidia kutokana

na uharibifu uliosababishwa na wanyama hatari. Hata hivyo, ni waombaji 14,944 (42%) pekee waliofanyiwa ukaguzi na kulipwa fidia zao, huku waombaji 20,343 (58%) wenye maombi ya Sh. bilioni 4.83 yakibaki bila kukaguliwa. Hali hii ilisababishwa na upungufu wa wafanyakazi na fedha kwa ajili ya mchakato wa uhakiki. Kuchelewa kwa ukaguzi kunazuia fidia kutolewa kwa wakati, kunaathiri ushahidi au uthibitisho wa tukio, na kudhoofisha ufanisi wa mchakato wa fidia kwa waathirika.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe Mfuko wa Ulinzi wa Wanyama Pori unatenga fedha za kutosha na kuongeza wafanyakazi ili kuharakisha ukaguzi wa maombi ya fidia na kupunguza mrundikano wa maombi ambayo hayakaguliwi.**

### 10.3.8 Uvamizi wa Hekta 3,000 katika Shamba la Msitu wa Korogwe

Kifungu cha 26(g) cha Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inazuia kukaliwa kwa hifadhi za misitu bila idhini, isipokuwa ikiwa makubaliano, leseni, au kibali kitatolewa kwa mujibu wa Sheria hiyo.

Ukaguzi wangu kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulionesha kwamba jamii imevamia hekta 3,000 kati ya 10,805 za Shamba la Msitu wa Korogwe na kufanya shughuli za kilimo. Licha ya uvamizi huu, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kutatua tatizo hili, jambo ambalo linahatarisha shughuli za shamba hilo na kuonesha upungufu katika utekelezaji wa ulinzi wa ardhi.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania inadhibiti shughuli haramu, inashirikiana na taasisi nyingine kuzuia uvamizi, kuanzisha mfumo imara wa ufuatiliaji, na kuongeza uhamasishaji kwa umma ili kulinda hifadhi za misitu.**

### 10.3.9 Upanuzi na Ujenzi Usioidhinishwa wa Eneo la Burudani katika Msitu wa Meru

Mnamo tarehe 21 Aprili 2023, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ilisaini makubaliano ya miaka mitano na M/s RITUNGU Tours and Safaris Ltd ya kusimamia maeneo ya burudani katika Hifadhi ya Msitu ya Meru katika Kanda ya Kaskazini, ikijumuisha mgahawa, baa, na viwanja vya michezo, kwa muda unaoisha tarehe 20 Aprili 2028. Makubaliano hayo hayakubainisha kiasi cha fedha kitakacholipwa na mwekezaji.

Ukaguzi wangu kwenye uwekezaji huu ulibaini kasoro zifuatazo:

- Mwekezaji alikuwa akifanya shughuli za burudani katika Hifadhi ya Msitu ya Meru tangu 2021, miaka miwili kabla ya makubaliano rasmi kusainiwa, ikimaanisha kuwa shughuli za uwekezaji zilifanyika bila mkataba halali kuwapo.

- Mwekezaji alikuwa akifanya shughuli za michezo, ikiwamo kuendesha pikipiki za magurudumu manne kwa zaidi ya kilometa 10 hivyo kuzidi eneo lililoruhusiwa la mita za mraba 3,500 kama ilivyobainishwa katika masharti ya makubaliano.

- Mwekezaji alijenga miundombinu ya kudumu kwa kutumia saruji, hivyo akakiuka Kifungu IX cha Masharti ya Makubaliano (TOR), ambacho kinabainisha wazi kuwa ujenzi uwe wa miundombinu ya muda mfupi kwa kutumia mbao.

Kasoro hizi zinadhihirisha upungufu wa mifumo ya ufuatiliaji na udhibiti inayolenga kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya makubaliano. Jambo hili linaathiri ustawi wa kifedha wa eneo la burudani na uendelevu wake wa muda mrefu.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kwamba Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania inaimarisha ufuatiliaji na utekelezaji wa masharti ya mkataba ili kulinda ustawi wa kifedha na kiutendaji wa eneo la burudani la msitu wa Meru.**

## 10.4 Elimu, Sayansi na Teknolojia

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kuandaa na kutekeleza sera za elimu, sayansi, teknolojia, na maendeleo ya ujuzi. Pia inasimamia mafunzo ya ufundi kupitia Kitengo cha Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Zaidi ya hayo, Kitengo cha Uthibiti Ubora wa Shule (SQA) cha wizara kinahakikisha kwamba viwango vya elimu vinafikiwa na kwamba elimu bora inatolewa kupitia ukaguzi wa shule za serikali na binafsi.

Mapitio yangu ya utendaji wa Wizara katika kuboresha Maendeleo ya Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Uthibiti Ubora wa Shule (SQA) yalibaini mambo yafuatayo;

### 10.4.1 Kusimama kwa Ujenzi wa Vituo 63 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23 na 2023/24, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilitenga Sh. bilioni 95.78 kwa ajili ya Awamu ya

Kwanza ya ujenzi wa vituo 63 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya (DVTCs) na Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa kimoja (RVTC). Halmashauri za wilaya zilipewa jukumu la kutoa ardhi inayoweza kufikiwa na miundombinu muhimu, ikiwa ni pamoja na maji, umeme na barabara. Awamu ya ujenzi ilijumuisha kujenga majengo tisa ya uendeshaji katika kila DVTC na majengo 23 katika RVTC, na mradi uliopangwa kukamilika ifikapo Desemba 2023.

Hata hivyo, kufikia tarehe 30 Juni 2024, ni Sh. bilioni 44.81 pekee (sawa na 46.78% ya kiasi kilichotengwa) zilizokuwa zimetolewa, jambo ambalo liliwezesha ununuzi wa vifaa na kuanza kwa shughuli za awali za mradi. Licha ya hayo, ukaguzi wa eneo la mradi uliofanyika mwezi Oktoba 2024 ulibaini kuwa ujenzi ulikuwa umesimama tangu Juni 2024, huku maendeleo ya ujenzi yakiwa kati ya 17% na 35%. Mradi huo ulikuwa umechelewa kwa zaidi ya miezi 10 kutoka tarehe ya mwisho ya kukamilika. Aidha, nilibaini kuwa miundombinu muhimu bado inakosekana, ambapo DVTC nane hazina barabara za kufikika, 37 hazina huduma za maji, na 41 hazina umeme. Ukosefu huu wa huduma za msingi unaweza kuathiri ufanisi wa vituo hivi mara baada ya kukamilika. Zaidi ya hayo, vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa kwa wingi, ikiwemo mifuko 10,127 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 199.93, viliharibika na kuwa hazifai kwa matumizi baada ya kukaa muda mrefu bila kutumika katika DVTC 21. Tatizo hili lilihusishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha, hali inayozua wasiwasi kuhusu uwezo wa mradi kukamilika kwa wakati na uwezekano wa hasara zaidi za kifedha.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Fedha, ihakikishe utoaji wa fedha kwa wakati ili kukamilisha kazi za ujenzi. Wizara ya Elimu, kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa, itoe miundombinu muhimu ili kuwezesha kuanza kwa shughuli za vituo kwa wakati mara baada ya kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya ujenzi.**

### 10.4.2 Ofisi za Kanda za Uthibiti Ubora wa Shule Ambazo Hazijaanzishwa

Ofisi za Ofisi za Uhakikisho wa Ubora wa Shule zina jukumu muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wa viwango vya elimu na utoaji wa elimu bora katika shule za msingi na sekondari kote Tanzania.

Mapitio yangu ya Muundo Mpya wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ulioidhinishwa tarehe 11 Aprili 2023, yalibaini kuanzishwa kwa Ofisi za Uthibiti Ubora za Mikoa na kutambuliwa rasmi kwa Ofisi za Uthibiti Ubora za Wilaya. Ofisi za Uthibiti Ubora za Kanda ziliondolewa katika muundo, na wafanyakazi na rasilimali zao zilihamishiwa katika Ofisi za Wilaya.

Nilibaini kuwa Wakuu wa Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya wameteuliwa rasmi na kutambuliwa kwa stahili zinazostahili. Hata hivyo, uanzishwaji wa Ofisi za Uthibiti Ubora wa Mikoa, ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha viwango vya elimu na utoaji wa elimu bora katika ngazi ya mikoa, bado haujakamilika. Zaidi ya hayo, Maafisa wa Uthibiti Ubora wa Mikoa bado hawajateuliwa.

Kuchelewa kuanzishwa kwa Ofisi za Uthibiti Ubora wa Mikoa na uteuzi wa maofisa kunatokana na uhaba wa rasilimali fedha. Ucheleweshaji huu unahatarisha uratibu na ufuatiliaji wa ufanisi wa shughuli katika ngazi ya mkoa, ambayo ni muhimu katika kuendeleza maendeleo ya elimu nchini Tanzania.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iharakishe uanzishaji wa Ofisi za Uthibiti Ubora katika ngazi ya Mkoa ili kuhakikisha viwango vya elimu vinazingatiwa na utoaji wa elimu bora.**

SURA YA KUMI NA MOJA



# Usimamizi wa Mifuko Maalumu na Mifuko Mingine

# USIMAMIZI WA MIFUKO MAALUMU NA MIFUKO MINGINE

## 11.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa usimamizi wa Mifuko Maalumu na Mifuko ya Uwezeshaji, ikilenga changamoto na upungufu katika usimamizi wake. Mifuko Maalumu, imeanzishwa na Katiba, hutumia fedha zilizotengwa kwa madhumuni maalumu, huku Mifuko ya Uwezeshaji ikiundwa kupitia Sheria na Kanuni za taasisi husika, ikitumia fedha kutoka kwa vyanzo vilivyobainishwa katika Sheria na Kanuni husika za kuanzishwa.

Ukaguzi wangu wa mifuko hii ulibaini upungufu kama inavyoelezwa hapa chini:

## 11.2 Mifuko Maalumu

### 11.2.1 Ada/Tozo za Mafuta ambazo hazijapelekwa kwenye Mifuko Maalumu Sh. trilioni 1.14

Ibara ya135(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba fedha zilizotengwa kwa madhumuni maalumu hazipaswi kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kanuni za Petroli (Uwekaji wa Ada ya Petroli) za mwaka 2015, Kanuni za Mfuko wa Taifa wa Maji za mwaka 2019, Sheria ya Barabara na Ada za Mafuta, sura ya 220, na Sheria ya Reli, 2017, Sura ya 170 zinaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukusanya ada na tozo za mafuta kwenye dizeli na petroli na kuziwasilisha kwenye akaunti husika za Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF), Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) na Mfuko wa Reli (RF).

Ukaguzi wangu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2023/24 ulibaini kuwa jumla ya Sh. trilioni 2.59 zilikusanywa na TRA kwa niaba ya Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF), na Mfuko wa Reli kisha kuhamishiwa Wizara ya Fedha. Hata hivyo, Wizara ya Fedha ilihamisha Sh. trilioni 1.44 pekee kwenda mifuko hiyo husika, hivyo salio la Sh. trilioni 1.14, sawa na 44% ya jumla ya fedha zilizokusanywa, bado halijapelekwa kwenye mifuko husika.

**Jedwali Na. 43: Ada/Tozo za Mafuta kwa mwaka 2023/24**

| Jina la Mfuko | Ada/Tozo za mafuta zilizokusanywa na TRA na kuhamishiwa Wizara ya Fedha (Sh.) | Kiasi Kilichopelekwa kwenye Mifuko (Sh.) | Kiasi Kisichopelekwa kwenye mifuko (Sh.) |
|---|---|---|---|
| RFB | 1,485,104,391,713 | 836,723,932,251 | 648,380,459,462 |
| RF | 500,526,466,822 | 236,072,543,892 | 264,453,922,930 |

| Jina la Mfuko | Ada/Tozo za mafuta zilizokusanywa na TRA na kuhamishiwa Wizara ya Fedha (Sh.) | Kiasi Kilichopelekwa kwenye Mifuko (Sh.) | Kiasi Kisichopelekwa kwenye mifuko (Sh.) |
|---|---|---|---|
| REA | 415,816,809,570 | 267,416,857,248 | 148,399,952,322 |
| NWF | 194,223,192,376 | 106,757,292,181 | 87,465,900,195 |
| **Jumla** | **2,595,670,860,481** | **1,446,970,625,572** | **1,148,700,234,909** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Fedha za TRA na Taarifa za Ukaguzi wa Mifuko Maalumu*

Kutowasilishwa kwa kiasi chote cha makusanyo ya tozo na ada za mafuta kumevunja matakwa ya katiba na kudhoofisha uwezo wa mifuko na wakala kugharimia miradi ya maji, barabara, reli na umeme vijijini. Hali hii imesababisha kuchelewa kwa maendeleo ya miundombinu na kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa miradi.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe uwasilishaji wa haraka na kamili wa ada/tozo za mafuta kwa mifuko maalumu ili kuwezesha ufadhili wa miradi ya maji, barabara, reli, na umeme vijijini hapa nchini.**

## 11.3 Mifuko ya Uwezeshaji

### 11.3.1 Wingi wa Mifuko ya Uwezeshaji na Changamoto ya Usimamizi

Hadi kufikia mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ilikuwa na mifuko 59, inayosimamiwa na Wizara, Serikali za Mitaa, Mamlaka za Udhibiti, na Mashirika ya Umma. Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya mifuko ina majukumu yanayofanana, hali inayosababisha kujirudia kwa kazi, ongezeko la gharama za kiutawala, na changamoto katika usimamizi wa fedha. Mifano ya Mifuko hiyo ni: Mfuko wa wanawake na vijana ulioko wizarani na ulioko Mamlaka za serikali za mitaa na kuna Mfuko wa maendeleo ya Vijana uko Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Ili kuongeza ufanisi, usimamizi wa fedha na uwajibikaji, ninapendekeza Serikali;**

**(a)** **Kuunganisha mifuko yenye majukumu yanayofanana ili kupunguza gharama za kiutawala na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa fedha. Hii itaruhusu njia rahisi katika kugawa rasilimali za kifedha huku ikihakikisha uwezeshaji wa kiuchumi wenye matokeo zaidi.**

(b) **Ianzishe mamlaka au utaratibu wa kuratibu mifuko yote ya Serikali ili kuhakikisha kuna uwiano wa matumizi ya fedha, uratibu wa miradi, na uwajibikaji wa fedha zinazokusanywa kwa kuweka jukumu la**

**kuratibu na kusimamia mifuko yote ya uwezeshaji kwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC).**

### 11.3.2 Mfuko wa Utafiti na Maendeleo ya Kilimo haujafanya kazi

Mfuko wa Utafiti na Maendeleo ya Kilimo umeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 26 (1) & (2) cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ya mwaka 2016, kwa lengo la kuwezesha na kuunga mkono utafiti wa kilimo pamoja na majukumu mengine ya taasisi. Mfuko huu unapata fedha zake kutoka kwenye mgao wa bajeti uliotengwa na bunge pamoja na ruzuku.

Mapitio yangu ya shughuli za TARI kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 yalibaini kuwa mfuko ulianzishwa mnamo Juni 2023, lakini haujaanza kufanya kazi licha ya kuidhinishwa kwa kanuni za taasisi zinazohusiana na uendeshaji wake mwezi huo huo. Sababu kuu ni kuchelewa kutekelezwa kwa taratibu za uendeshaji na mfumo wa kiutawala unaohitajika kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko. Hali hii imeathiri uwezo wa taasisi kuwezesha na kuunga mkono utafiti wa kilimo, Jambo linaloweza kuathiri miradi ya utafiti inayoendelea na ile inayotarajiwa kuanza katika siku zijazo.

**Ninapendekeza kwamba TARI na Wizara ya Kilimo wahakikishe Mfuko unaanza kufanya kazi kwa kuharakisha taratibu za uendeshaji na za kiutawala, ikiwamo uteuzi wa wajumbe wa kamati na kupata rasilimali na wafanyakazi wa kutosha ili kusimamia mfuko kwa ufanisi.**

### 11.3.3 Ufanisi Usioridhisha wa Mfuko wa Amana wa Mazingira

Kifungu cha 213 na 214 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kimeanzisha Mfuko wa Taifa wa Amana wa Mazingira, ambao hupata mapato yake kutoka kwa mgao wa bajeti wa Bunge, michango, ruzuku, mapato kutoka kwa miradi inayofadhiliwa, na tozo za ada zitakazowekwa. Malengo ya mfuko ni: kujenga uwezo, kuunga mkono utafiti wa mazingira, kutoa tuzo, kutoa machapisho, na kutoa udhamini wa masomo. Malengo mengine ni: kufadhili programu za jamii kupitia ruzuku, na kufadhili mikutano ya Kamati ya Ushauri ya Mazingira ya Taifa.

Nilifanya tathmini ya kuwapo kwake na utekelezaji wa mfuko wakati wa ukaguzi wangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Licha ya kuanzishwa kwake mwaka 2006, nilibaini kuwa mfuko huu haukufanikiwa kukusanya mapato ya kufadhili shughuli zake zilizokusudiwa. Aidha, mfuko umebaki bila kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 17, hasa kutokana na kushindwa kutekeleza utaratibu wa kukusanya mapato uliowekwa.

Hali hii imekwamisha mfuko kufikia malengo yake na kuzuia utekelezaji wa malengo ya serikali katika sekta ya mazingira.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ifikirie kufunga mfuko huu usiofanya kazi, au kuchukua hatua mahsusi zinazohitajika kuufanya ufanye kazi kwa kutumia vyanzo vilivyowekwa vya kukusanya mapato na kuhakikisha unafanya kazi kwa ufanisi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.**

### 11.3.4 Uanzishaji na Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Uchimbaji Madini (EMDF)

Kwa mujibu wa tamko la Katibu Mkuu katika taarifa za fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Uchimbaji Madini (EMDF) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, mfuko huu ulianzishwa kwa msingi wa Sheria ya Uwezeshaji ya Taifa ya mwaka 2004. Sheria hii inatoa miongozo ya kuanzisha mifuko ya uwezeshaji ili kusaidia utekelezaji wa mipango mbalimbali ya uwezeshaji wa kiuchumi.

Mfuko ulianzishwa rasmi na iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2012 ili kusaidia wachimbaji wadogo na wa kati na kukuza mafunzo ya ujasiriamali katika sekta ya madini. Mfuko pia unasaidia kujenga uwezo kwa maafisa wa serikali wanaosimamia na kuendesha sekta hiyo na kukuza mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa taifa.

Mapitio yangu ya uendeshaji wa mfuko yalibaini yafuatayo:

a) Uanzishwaji wa EMDF haukufuata kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Uwezeshaji wa Kiuchumi ya Taifa ya mwaka 2004, ambacho kinahitaji kila taasisi au shirika linalotaka kufanya shughuli za kiuchumi kwa mujibu wa sheria hii kuwasilisha ombi la usajili kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji wa Kiuchumi la Taifa. Kifungu cha 28 kinahitaji Katibu Mtendaji, baada ya kuridhika na maudhui ya ombi, kusajili taasisi au shirika na kutoa cheti cha usajili. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa hakuna nyaraka wala hati zinazoelezea kwa uwazi uanzishaji wa mfuko, madhumuni yake, chanzo cha ufadhili na taratibu za uendeshaji.

b) Awali, mfuko ulitegemea michango kutoka kwa kampuni za uchimbaji, kama ilivyobainishwa katika makubaliano ya maendeleo ya uchimbaji kati ya serikali na kampuni za uchimbaji. Hata hivyo, baada ya marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017, ambayo yalifuta makubaliano haya, EMDF imekuwa na changamoto ya kupata chanzo cha fedha cha kuaminika na endelevu. Kwa sasa, mfuko unafanya kazi kwa salio la benki linaloendelea kupungua ambalo limefika Sh. milioni 178.47, kama

ilivyooneshwa katika taarifa za fedha za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024.

Kwa maoni yangu, bila nyaraka za uhakika za uanzishaji na mfumo wa kisheria, EMDF inakosa msingi wa kuwapo kwake. Jambo hili linafanya kuwa vigumu kupata vyanzo vya fedha vinavyoweza kutegemewa, hivyo kudhoofisha manufaa ya mfuko kwenye maendeleo ya uchimbaji wa madini.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Madini ifanye tathmini upya ya umuhimu wa mfuko huu. Ikiwa bado unahitajika, unapaswa kuanzishwa tena kwa kufuata mfumo wa kisheria unaofaa, ambapo madhumuni ya mfuko, vyanzo vya fedha, na taratibu za uendeshaji zitafafanuliwa kwa uwazi. Ikiwa mfuko hauhitajiki, unapaswa kufutwa.**

### 11.3.5 Madeni ya mikopo yanayokabiliwa na hatari ya kutorejeshwa - Sh. bilioni 2.58

Aya ya 6.1 ya Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wa Mei 2022 inabainisha kwamba kipindi cha kurejesha mikopo hakitazidi miezi 36 kuanzia tarehe mkopo ulipotolewa kwa vikundi vya vijana.

Mapitio yangu ya Mfuko katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira, na Watu Wenye Ulemavu (OWM-KVAU) yalibaini madeni ya mikopo yasiyolipwa yenye jumla ya Sh. bilioni 5.02 kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa (ambazo zinawajibika kutoa mikopo kwa vijana) hadi tarehe 30 Juni 2024. Hasa, Sh. bilioni 2.58 (51%) ya kiasi hiki kilikuwa hakijalipwa kwa kipindi cha kati ya miaka 3 hadi 21.

Ninahusisha udhaifu huu na kushindwa kwa menejimenti kufuatilia vyema mikopo iliyotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa ili itolewe kwa vijana. Kushindwa kukusanya mikopo kutoka kwa vikundi vya vijana na watu binafsi kumekwamisha utoaji wa mikopo mipya kwa vikundi vingine vya vijana vinavyohitaji, na hatimaye kukwamisha lengo la mfuko la kusaidia shughuli za kiuchumi za vijana na kupunguza ukosefu wa ajira.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya OWM-KVAU ufanye ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya mchakato wa utoaji mikopo na urejeshaji wake kwenye ngazi ya halmashauri. Aidha, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wanufaika ili kurejesha mikopo ambayo haijalipwa kwa muda mrefu.**

### 11.3.6 Mikopo Iliyotolewa kwa Vikundi vya Vijana Kabla ya Kufanya Mafunzo na Ushauri - Sh. Bilioni 1.28

Aya ya 4.1.2 Ya Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wa mwaka 2022 inataka wanufaika wa mikopo kufanyiwa mafunzo ya awali kuhusu huduma za maendeleo ya biashara, ujasiriamali, na usimamizi wa kifedha kabla ya kutolewa kwa fedha. Kamati ya kiufundi ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana inaweza kushirikiana na wadau wengine au kuajiri wataalamu wa mafunzo inapohitajika. Mafunzo ya baada ya ufadhili na ushauri wa wanufaika yatatolewa ili kuhakikisha uwezo wa vijana kurejesha mikopo na kufanya vizuri.

Kinyume chake, ukaguzi wangu ulibaini kwamba katika mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Watu Wenye Ulemavu (OWM-KVAU) ilitoa mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 1.28 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kabla ya wanufaika kupata mafunzo na ushauri muhimu. Ninahusisha tatizo hili na ukosefu wa ufuatiliaji na tathmini, kwani wizara ilishindwa kutekeleza shughuli hizi muhimu.

Kwa maoni yangu, kutoa mikopo bila kutoa mafunzo ya maendeleo ya biashara kunaongeza hatari ya wanufaika kutosimamia vyema fedha hizo, na kufanya urejeshaji wa mikopo kuwa changamoto. Hali hii itasababisha kutofikiwa kwa malengo ya mfuko.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya OWM-KVAU itoe mafunzo na ushauri kwa wanufaika wa mikopo kabla ya kutoa mikopo. Hii itachangia kujenga uwezo na kuimarisha ujuzi wa kibiashara kwa wanufaika. Pia, ihakikishe kwamba fedha hazitumiki kwa shughuli zilizo nje ya malengo ya mikopo husika. Vilevile, itoe kipaumbele kwenye ufuatiliaji na tathmini.**

## 11.4 Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa

### 11.4.1 Upungufu katika Usimamizi na Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Taifa wa Maafa

Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu Na. 37) inasimamia Mfuko wa Taifa wa Maafa, ulioanzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022. Lengo kuu la mfuko ni kusaidia kuzuia maafa, kupunguza, kujiandaa, kukabiliana, na shughuli za uokoaji, ili kuhakikisha mbinu kamili na iliyoratibiwa ya usimamizi wa maafa nchini Tanzania. Kazi za usimamizi wa maafa hutekelezwa katika ngazi mbalimbali, kuanzia ngazi ya mtaa na kata, kuendelea hadi kamati za udhibiti wa maafa za wilaya na mikoa, na hatimaye kuratibiwa katika ngazi ya kitaifa na Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa. Taratibu hizi za uratibu wa

ngazi mbalimbali zinahakikisha ugawaji bora wa rasilimali, kujipanga kukabiliana na maafa, na juhudi za uokoaji kufuatia matukio ya maafa.

Mapitio ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika usimamizi wa masuala yanayohusiana na maafa yalibaini upungufu na changamoto kubwa katika matumizi ya Mfuko wa Taifa wa Maafa kama inavyofafanuliwa hapa chini:

### 11.4.2 Fedha ambazo hazijatumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyoathiriwa na mafuriko ya matope Hanang, Sh. Bilioni 7.01

Mnamo tarehe 3 Desemba 2023, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang katika Mkoa wa Manyara ilikumbwa na janga la mafuriko ya matope. Kuanzia Desemba 2023 hadi Juni 2024, Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa jumla ya Sh. bilioni 15.49, ambapo Sh. bilioni 4.36 zilitolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, wakati Sh. bilioni 11.13 zilitolewa kwa taasisi nne za serikali katika Mkoa wa Manyara (TARURA, BAWASA, TANESCO, na RUWASA) kwa ajili ya kurejesha miundombinu mbalimbali iliyoharibiwa na mafuriko ya matope. Mbali na urejeshaji upya wa miundombinu, serikali pia ilipanga kujenga nyumba 109 (73 zikiwa zimetolewa na serikali na 36 na Shirika la Msalaba Mwekundu la Tanzania).

Hadi tarehe 04 Oktoba 2024, taasisi hizi (TARURA, BAWASA, TANESCO, na RUWASA) zilikuwa zimetumia Sh. bilioni 4.12, huku Sh. bilioni 7.01 zikiwa hazijatumiwa. Kushindwa kutumia fedha hizi kulitokana kwa kiasi kikubwa na kuchelewa kwa michakato ya ununuzi ya taasisi hizi. Jambo hili lilisababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya kazi na ukosefu wa malengo ya mradi ambayo yangehakikisha miradi inamalizika kwa wakati. Ucheleweshaji huu unadhoofisha juhudi za kurejesha miundombinu muhimu na huduma za jamii, ikiwa ni pamoja na miradi ya maji, umeme, na barabara.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kushirikiana na Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya Mkoa wa Manyara, iimarishe ufuatiliaji kwa taasisi zilizopewa fedha ili kuhakikisha utekelezaji mzuri na ujenzi wa miundombinu na huduma zilizoathiriwa na mafuriko ya matope wilayani Hanang unakamilika kwa wakati.**

### 11.4.3 Kutokuombwa kwa Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Miradi ya Dharura Baada ya Maafa Kulikosababisha Ongezeko la Gharama ya Sh. Milioni 252.86

Nilibaini kwamba tarehe 29 Februari 2024, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang iliiajiri Kampuni ya Ujenzi ya Suma JKT Construction Company Limited kujenga nyumba 73 kwa ajili ya wahanga wa mafuriko ya matope kwa gharama ya Sh. bilioni 1.66, ambapo Sh. milioni 252.86 zilitengwa kwa ajili ya VAT. Ingawa M/S

Suma JKT ilikamilisha mradi kwa mafanikio, nilibaini kwamba kiasi kikubwa cha Sh. milioni 252.86, sawa na 15.25% ya jumla ya gharama za mradi, kilitumiwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Kiasi hiki kingeweza kuokolewa na kutumika kujenga nyumba nyingine 11, hivyo kuongeza idadi ya wanufaika, endapo Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ingeomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Hali hii imepunguza fursa ya kuongeza ufanisi wa juhudi za kurejesha huduma za jamii baada ya maafa.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kushirikiana na watekelezaji wa miradi ya maafa, ihakikishe kuwa ombi la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani linapelekwa TRA ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya maafa.**

### 11.4.4 Hasara ya Kifedha ya Sh. Milioni 118 kutokana na Ujenzi wa Visima Visivyotoa maji na Vyenye Maji Machafu

Nilibaini kwamba RUWASA mkoa wa Manyara ilitumia Sh. milioni 57 kuchimba visima vitatu ambavyo havikutoa maji. Aidha, RUWASA ilitumia Sh. milioni 60.95 kwa visima viwili ambavyo vilitoa maji yenye madini mengi na yenye uchafu, yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu. Pia, nilibaini kwamba menejimenti ya RUWASA ilitegemea ripoti ya uchunguzi wa mfumo wa maji iliyopitwa na wakati na haukufanya uchunguzi wa kina. Jambo hili lilisababisha hasara ya Sh. milioni 118.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya RUWASA ihakikishe inatumia njia za kisasa kufanya utafiti wa kihydrolojia ya uwepo wa maji chini ya aridhi kabla ya kuanza miradi ya uchimbaji wa visima. Hii itasaidia kutambua vyanzo vya maji vinavyofaa na kuepuka uwekezaji katika maeneo yasiyo na maji au yenye uchafu.**

### 11.4.5 Hatari ya Kutumika Vibaya kwa Sh. Milioni 41 kutokana na Kuingizwa kwa Vitu Visivyohusika katika Kandarasi ya Mradi wa Ugavi wa Maji

Nilibaini kwamba tarehe 23 Septemba 2024, RUWASA Manyara iliiajiri kampuni ya JISHAM & Construction Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya ugavi wa maji katika vijiji vya Gabadaw, Kinyamburi, Sarjanda, Basodagwaruq, na Nangwa kwa bei ya Sh. bilioni 1.25. Ukaguzi wa mkataba huu ulibaini vitu viwili visivyohusiana na kandarasi hii (maboksi matano ya vifaa vya kutendea kazi vyenye thamani ya Sh. milioni 1 na pikipiki tano zenye thamani ya Sh. milioni 40) ambavyo havikuwa na uhusiano na mradi wa maji. Kuingizwa kwa vitu hivi kumechangiwa na ukaguzi usio madhubuti wa Maelezo ya Vipimo (BOQ)

uliofanywa na RUWASA Manyara. Hali hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi zinazofikia Sh. milioni 41. Hadi wakati wa kukamilisha ripoti ya ukaguzi mnamo Februari 2025, RUWASA ilikuwa haijamlipa mkandarasi Sh. milioni 41.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya RUWASA ufanye mapitio ya mkataba ili kuondoa vitu vyote visivyohusiana na mkataba huu. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba rasilimali zinatumika pekee kwa ajili ya mradi wa ugavi wa maji kama ilivyokusudiwa.**

### 11.4.6 Ucheleweshaji wa Ujenzi wa Shule ya Awali na Msingi unaosababishwa na Serikali

Wakati wa kupitia taarifa za maafa, nilibaini kwamba serikali ilipanga kujenga shule mpya ya msingi na ya awali katika wilaya ya Hanang kwa thamani ya Sh. milioni 546.39. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi mnamo Novemba 2024, nilibaini kwamba vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 101.57 vilikuwa vimenunuliwa na kuhifadhiwa, lakini serikali ilikuwa haijatoa kiasi kilichobaki cha Sh. milioni 444.83. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ushahidi kwamba serikali ilianza mchakato wa kupata mkandarasi wa kujenga shule hizo, jambo ambalo limesababisha kuchelewa zaidi kwa utekelezaji wa mradi huu.

**Ninapendekeza Serikali itenge kiasi kilichobaki cha Sh.444.83 milioni kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ili kuharakisha mchakato wa kupata mkandarasi. Pia, iweke muda maalumu wa utekelezaji ili kuhakikisha ujenzi wa shule za msingi na awali unafanyika kwa wakati.**

### 11.4.7 Kuchelewa Kusambaza Vifaa kwa Taasisi zenye Uhitaji - Sh. Milioni 231.06

Kanuni ya 26(3)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022 inataka fedha au msaada kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa maafa zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Endapo fedha au msaada unabaki bila kutumika, unapaswa kupelekwa kwenye kituo cha kuhifadhi misaada ya kibinadamu au kama itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ilipokea jumla ya mabati 14,823 yenye thamani ya Sh. milioni 419.69 na mifuko 22,973 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 324.42 kusaidia ujenzi wa shule ya awali na soko la mbogamboga na vituo vya afya katika eneo la Warret. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi mwezi, Septemba 2024, nilibaini kuwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni

231.06 vikiwa ni mabati 6,014 yenye thamani ya Sh. milioni 170.27 na mifuko 4,305 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 60.79 vilikuwa havijatumika kwa ajili ya kukamilisha majengo husika. Vifaa hivi vilikuwa vimehifadhiwa katika maghala ya Warret na bohari ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.

Vifaa hivi vilitokana na michango ya wadau mbalimbali. Hata hivyo, kucheleweshwa kwa ugawaji wa vifaa hivi kwa taasisi zinazohitaji kutasababisha uharibifu, au wizi. Hali hii inadhihirisha usimamizi usiofaa wa rasilimali zilizotolewa kwa ajili ya kurejesha miundombinu na huduma zilizoathiriwa na maafa.

**Ninapendekeza Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kubaini na kugawa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 231.06 kwa miradi au taasisi nyingine zenye uhitaji kwa kuzingatia Kanuni ya 26(3)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022.**

# SURA YA KUMI NA MBILI



# Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

# BALOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI

## 12.1 Utangulizi

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania ili kulinda na kukuza maslahi ya taifa nje ya nchi. Hili linatekelezwa kupitia balozi zake za nje, misheni za kudumu na balozi mwakilishi wa Tanzania aliyeidhinishwa. Balozi hizi ni muhimu katika kukuza maslahi ya Tanzania nje ya nchi, kuwezesha biashara na uwekezaji, na kudumisha uhusiano wa kidiplomasia.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali ilitenga kiasi cha Sh. bilioni 161.01 kwa ajili ya kugharamia shughuli za balozi 43 za nje, ambapo Sh. bilioni 148.84 (92%) zilitolewa. Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yanayohusiana na ukaguzi wa kifedha na uzingatiaji wa sheria uliofanywa katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na balozi zake za nje. Maeneo muhimu yaliyokaguliwa ni diplomasia ya uchumi, usimamizi wa mapato na bajeti, usimamizi wa matumizi, na usimamizi wa mali.

## 12.2 Diplomasia ya Uchumi

Aya ya 28 ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 inaeleza kuwa diplomasia ya uchumi inahusisha mawasiliano na ushirikiano na nchi nyingine, mashirika ya kiserikali, na taasisi za kimataifa. Tangazo la Serikali Na. 385 la tarehe 07 Mei 2021 linaitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutekeleza majukumu mbalimbali ya kidiplomasia ili kuendeleza maslahi ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi ya Tanzania, huku ikizingatia utu wa binadamu, usawa, uhuru, na mamlaka ya kujitawala.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kupitia kifungu cha bajeti Na. 1021—Idara ya Diplomasia ya Uchumi inatekeleza shughuli za diplomasia ya kiuchumi chini ya Lengo C (kuimarisha uwezo wa taasisi kutimiza majukumu yake) na lengo E (kukuza maslahi ya jamii na kiuchumi). Jumla ya Sh. milioni 641.67 zilitengwa na kupokelewa katika ngazi ya Wizara, ambapo sh. milioni 529.32, sawa na 82% zilitumika.

### 12.2.1 Nchi Tatu Hazikuweza Kutoa Huduma kwa Uwiano Sawa na Walizopatiwa na Serikali ya Tanzania

Utoaji huduma kwa uwiano sawa (*reciprocity*) katika kidiplomasia kunahusu makubaliano baina ya nchi mbili kupeana huduma kwa uwiano usawa. Ibara ya

2 ya mkataba wa Vienna wa uhusiano wa kidiplomasia wa mwaka 1961 inahitaji kuwapo kwa makubaliano baina ya nchi mbili kuhusu uhusiano wa kidiplomasia.

Serikali ya Tanzania iliipatia Jamhuri ya Uturuki ekari 5 za ardhi katika eneo la Mtumba-Dodoma lililotengwa kwa ajili ya majengo ya balozi mbalimbali. Aidha, nilibaini Ubalozi wa Tanzania - Ankara haujapatiwa ardhi nchini Uturuki licha ya barua za kukumbusha zilizotumwa tangu Machi na Novemba 2024. Vilevile, licha ya nchi ya Kuwait kupatiwa ardhi na Serikali ya Tanzania Kiwanja Namba 61, Kitalu A, Eneo la Ihumwa, Dodoma, nilibaini kuwa Ubalozi wa Tanzania - Kuwait haujapatiwa ardhi nchini Kuwait licha ya barua ya kukumbusha iliyotumwa mnamo tarehe 10 Januari 2023.

Kutoshughulikiwa kwa suala hili kunazorotesha utoaji wa huduma kwa uwiano usawa, uhusiano wa kidiplomasia na kunaongeza gharama za uendeshaji kwa balozi za Tanzania kuendelea kukodi majengo ya ofisi na makazi. Ushirikiano imara wa kidiplomasia ni muhimu katika kuhakikisha masilahi ya Tanzania yanazingatiwa.

**Ninapendekeza kuwa serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, iendelee kuwasiliana na mamlaka za nchi husika ikiwamo kufanya mazungumzo ya kidiplomasia ili kuharakisha utoaji wa ardhi kwa Ubalozi wa Tanzania huko Ankara na Kuwait. Pia, ifuatilie kufutwa kwa masharti ya viza kwa watanzania wanaoingia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.**

### 12.2.2 Kukosekana kwa Miongozo ya Uendeshaji wa Madarasa ya Kiswahili katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

Aya ya 26 ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 inalenga kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi iliyothabiti.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kiasi cha Sh. milioni 142.47 kilitengwa kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha madarasa ya Kiswahili balozini bila kuwa na miongozo rasmi au mfumo rasmi wa uendeshaji wa madarasa haya ya Kiswahili. Hii ilijumuisha kukosekana kwa sera inayohusu uundaji wa mtaala, vigezo vya walimu, ratiba za madarasa, na mgawanyo wa fedha.

Kwa mfano, uendeshaji wa madarasa ya Kiswahili katika Ubalozi wa Tanzania - Paris umekuwa ukisimamiwa na Watanzania waishio ughaibuni (*diaspora*). Vilevile, Ubalozi wa Tanzania - Roma unasimamia madarasa ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na malipo ya walimu, ambapo katika mwaka wa 2023/24, Sh. milioni

18.57 za ada za madarasa ya Kiswahili zilizokusanywa zilihamishiwa katika mfuko mkuu wa serikali.

Kukosekana kwa miongozo kumesababisha kukosekana kwa ubora sawa wa ufundishaji na usimamizi wa madarasa ya Kiswahili, hivyo kuzorotesha ufanisi wake kama chombo cha kidiplomasia na utamaduni. Kuandaa miongozo ya uendeshaji wa madarasa ya Kiswahili ni muhimu ili kuweka viwango sawa, uwajibikaji, na uendelevu wa programu za lugha ya Kiswahili katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

**Ninapendekeza kuwa serikali ihakikishe Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaandaa, kusambaza, na kutekeleza miongozo ya uendeshaji wa madarasa ya Kiswahili balozini ili kuboresha ubora na uwiano wa programu za kiswahili katika kuimarisha utamaduni na diplomasia.**

### 12.2.3 Ukosefu wa Wataalamu Balozini

Aya ya 26 ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 inalenga kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi iliyothabiti.

Katika ukaguzi wangu wa tange za watumishi balozini kuhusianisha na shughuli zilizopo katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, nilibaini uhitaji wa wataalamu wafuatao:

(i) Katika Ubalozi wa Tanzania – Brasilia, nilibaini ukosefu wa wataalamu wa biashara, kilimo na utalii ambao ni muhimu katika kuendeleza diplomasia ya kiuchumi na kutumia fursa zinazopatikana nchini Brazil.

(ii) Katika Ubalozi wa Tanzania - Jakarta, nilibaini ukosefu wa wataalamu ambao ni muhimu katika kuratibu wa kusimamia fursa zinazopatikana katika sekta za kilimo, viwanda, biashara, na madini.

(iii) Ubalozi wa Tanzania - Paris, haukuwa na afisa mratibu wa masuala yanayohusu Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambaye anatakiwa kuiwakilisha Tanzania kama mwanachama wa bodi ya utendaji kwa kipindi cha mwaka 2023-2025. Aidha, nilibaini ukosefu wa mchumi atakayeratibu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ambayo ni lengo kuu la sera ya mambo ya nje.

(iv) Katika Ubalozi wa Tanzania – Algiers, nilibaini ukosefu wa mtaalamu katika sekta ya mafuta na gesi, hii inazuia Tanzania kunufaika kwani Algiers ni nchi inayoongoza katika kusafirisha mafuta kwenda barani

Afrika kupitia kampuni ya Sonatrach. Kukosekana kwa mtaalamu kunazuia juhudi za Tanzania kujiendeleza kiuchumi katika sekta ya nishati.

(v) Ubalozi wa Tanzania - Doha, ulihitaji mtaalamu wa uchumi na biashara ili kuwezesha ukuaji wa ushirikiano wa biashara na uwekezaji. Kwa kuzingatia uchumi imara wa Qatar, ukosefu wa nafasi hii, ulizuia utangazaji wa sekta ya utalii, kilimo na fursa za uwekezaji na hivyo ulichelewesha ushughulikiaji wa maombi ya uwekezaji Tanzania na mazungumzo baina ya pande mbili.

(vi) Zaidi ya hayo, Ubalozi wa Tanzania Roma ulihitaji Mwakilishi wa Kudumu wa Kilimo kwa mashirika ya kimataifa ambayo ni Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Chakula Duniani (WFP) na Shirika la Kimataifa la Fedha kwa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Kwa sasa, Jukumu la ushiriki katika mikutano ya mashirika haya linafanywa na mwambata kilimo ambaye hana haki ya kupiga kura kwenye mikutano hiyo inayofanya maamuzi, hii unazuia uwezo wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika maamuzi na kukosa fursa mbalimbali za kifedha.

Kukosekana kwa wataalamu balozini kunatokana na uhaba wa fedha na kutokuwa na uwiano kati ya mahitaji ya watumishi na vipaumbele vya kidiplomasia na kiuchumi katika balozi za Tanzania Nje ya Nchi. Uhaba wa fedha na ukosefu wa wataalamu unazuia Tanzania kushiriki kikamilifu katika masuala ya uhusiano baina ya nchi mbili na baina ya mashirika ya kimataifa na hivyo kuzuia fursa za kiuchumi na kidiplomasia.

**Ninapendekeza kuwa serikali iongeze bajeti ya balozi za Tanzania nje ya nchi ili kushughulikia ukosefu wa wataalamu ili kuendana na majukumu yaliyopo balozini na, ikiwezekana, kuongeza wataalamu waliobainishwa hapo juu.**

## 12.3 Usimamizi wa Mapato na Bajeti

### 12.3.1 Uchelewaji wa Kuwasilishwa Fedha za Matumizi Balozini

Shughuli za balozini hufadhiliwa na mapato kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kifungu cha 44(3) cha Sheria ya Bajeti, sura ya 439, kinahitaji afisa masuuli kutumia bajeti kulingana na mpango wa mtiririko wa fedha wa mwaka.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa bajeti iliyoidhinishwa kwa balozi 43 kwa mwaka wa fedha 2023/24 ilikuwa Sh. bilioni 161.01. Hata hivyo, Sh. bilioni 148.89,

sawa na 92%, ndizo zilizotumwa balozini katika mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, nilibaini kuwa fedha za matumizi balozini zilitumwa kwa kuchelewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ikiwa na uchelewaji wa mwezi mmoja mmoja kwa mwaka mzima. Uchelewaji huu uliathiri uwezo wa kifedha wa balozi za Tanzania nje ya nchi katika kutimiza majukumu kwa wakati, ikiwa ni pamoja na malipo ya kodi, ada za shule, gharama za uendeshaji ofisi, na posho za wafanyakazi.

Kwa mfano, nilibaini Ubalozi wa Tanzania - Beijing ulilipa faini ya Sh. milioni 42.39 kwa sababu ya ucheleweshaji wa malipo ya kodi kutokana na ucheleweshaji wa kupokea fedha kutoka wizarani.

**Ninapendekeza kwamba Serikali itengeneze mpango Madhubuti wa kutenga na kulinda fedha "*ringfence*" zilizopangwa kwa ajili ya Balozi ili kuhakikisha zinapewa kipaumbele na kutolewa kwa wakati. Hii itawawezesha Balozi kutekeleza majukumu yake muhimu kama vile kulipa kodi za pango, ada za masomo, gharama za uendeshaji, na posho za wafanyakazi bila kukwama. Utoaji wa fedha kwa wakati ni muhimu kwa kudumisha utoaji bora wa huduma za kidiplomasia na kuhifadhi taswira ya nchi kimataifa**

### 12.3.2 Fedha Zilizotumwa kwa ajili ya Ukarabati Balozini Kutotumika kwa Muda Mrefu Sh. bilioni 2.08

Kifungu cha 44(3) cha Sheria ya Bajeti, sura ya 439, kinahitaji maafisa masuuli kutumia bajeti kulingana na mpango wa mtiririko wa fedha wa mwaka.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mnamo tarehe 21 Desemba 2023, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilituma jumla ya Sh. bilioni 3.14 kwa balozi mbili kwa ajili ya ukarabati na ununuzi wa samani bila kuwa na maandalizi ya mpangokazi wa matumizi ya fedha hizo. Hivyo, nilibaini kuwa Sh. bilioni 2.08 zilibaki katika akaunti za amana kwa miezi 14 hadi mwezi Februari, 2025 bila kutumika. Maelezo ya fedha zisizotumika yanaonekana kwenye **Jedwali Na.44.**

**Jedwali Na. 44: Fedha za Ukarabati Zilizotumwa katika Balozi**

| Maelezo | Fedha zilizotumwa (Sh.) | Fedha Zilichobaki (Sh.) |
|---|---|---|
| Ukarabati na ununuzi wa samani katika Ubalozi wa Kudumu wa Umoja Mataifa - Geneva | 1,934,068,330 | 1,934,068,330 |
| Ukarabati na ununuzi wa samani katika Ubalozi wa Tanzania - London | 1,214,099,741 | 152,919,766 |

| Maelezo | Fedha zilizotumwa (Sh.) | Fedha Zilichobaki (Sh.) |
|---|---|---|
| Jumla | **3,148,168,071** | **2,086,988,096** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

Hii ilitokana na ukosefu wa maelekezo ya kina na mpangokazi wa utekelezaji wa ukarabati balozini kabla ya fedha kutumwa. Maoni yangu ni kwamba, kuna hatari ya kuongezeka kwa gharama za ukarabati itakayotokana na uendelevu wa uharibifu wa majengo, ambayo ingeweza kuepukika.

**Ninapendekeza kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ihakikishe:**

a) **inaandaa mpangokazi wa utekelezaji wa miradi balozini kabla ya fedha kutumwa balozini; na**
b) **inaanza na kukamilisha ukarabati bila kucheleweshwa zaidi.**

## 12.4 Usimamizi wa Mali

### 12.4.1 Uchelewaji wa Kupata Idhini ya Kuondoa Mali Chakavu Balozini

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) ya mwaka 2024 inahitaji taasisi za serikali kupata idhini ya kuondoa mali chakavu kutoka kwa Katibu Mkuu - Hazina.

Tarehe 7 Oktoba 2021, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha alitoa waraka wenye Kumb. Na. FA.48/185/01 unaoelezea taratibu za kufuata za kuondoa mali chakavu balozini, zikihitaji uundwaji wa bodi ya uhakiki na kupata idhini kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa balozi 21 zilikuwa na vifaa vya ofisi na magari chakavu vilivyohitaji kuondolewa licha ya kuwapo kwa maombi kadhaa ya idhini ya kuondoa yaliyotumwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kati ya Januari 2019 na Oktoba 2024.

Pia, nilibaini kuwa katika Ubalozi wa Tanzania - Roma, Serikali ya Italia ilitenga nafasi tatu za usajili wa magari ya kidiplomasia kwa Ubalozi wa Tanzania. Hivyo, kushindwa kuondoa gari lisilofanya kazi lenye namba ya usajili wa kidiplomasia CD 0058 DE kumefanya ubalozi kushindwa kupata gari lingine, kwani nafasi zote zilizotolewa za magari ya kidiplomasia zimejazwa. Maelezo ya mali zilizochakaa yameoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XIII.**

Hii ilitokana na taratibu za kupata idhini kutoka kwa Katibu Mkuu wa Hazina kuchukua muda mrefu. Hali hii ilisababisha vifaa hivi chakavu kujaza nafasi za ofisi, kuleta hatari kwa usalama, na kuzuia ununuzi wa vifaa vipya.

**Ninapendekeza kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane na Wizara ya Fedha kutoa muongozo utakaowezesha balozi za Tanzania nje ya nchi kuondoa mali chakavu kwa wakati ambazo ni vifaa vya Tehama, samani za ofisi na magari na ikiwezekana kuwapatia mamlaka ya kuondoa mali zilizochakaa.**

### 12.4.2 Gharama Kubwa Zinazotumika Kulipa Kodi ya Pango katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi Sh. Bilioni 22.63

Kanuni ya 11(3)(c) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2021 inawapa mamlaka maafisa masuuli kusimamia na kulinda fedha na rasilimali za umma zilizo chini yao. Hii inajumuisha kukagua na kulinda vifaa na mali zote zinazomilikiwa na idara zao.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kati ya balozi 43 zilizokaguliwa, balozi 39 zililipa Sh. bilioni 22.63 kwa ajili ya kodi ya ofisi na makazi kwa mwaka wa fedha 2023/24, sawa na 14% ya bajeti ya mwaka ya balozi.Kwa miaka mitatu mfululizo, balozi hizo 39 zililipa jumla ya Sh. bilioni 56.56, malipo ambayo yangeweza kuepukwa kama Balozi zikipatiwa uwezo wa kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na ukarabati,huku fedha hizo kwa ajili ya malipo ya kodi zikitumika kurejesha mikopo. Maelezo yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 45** hapa chini:

**Jedwali Na. 45: Mwenendo wa Ulipaji wa Kodi za Pango kwa Miaka Mitatu**

| Na. | Mwaka wa Fedha | Kiasi Kilicholipwa (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | 2023/24 | 22,636,286,299 |
| 2 | 2022/23 | 18,463,447,500 |
| 3 | 2021/22 | 15,466,352,294 |
| **Jumla** | | **56,566,086,093** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Fedha*

Hii imetokana na Serikali kushindwa kukarabati majengo chakavu na kuendeleza viwanja vilivyotolewa na nchi wenyeji kwa balozi za Tanzania nje ya nchi. Maoni yangu ni kwamba, kuendelea kulipa kodi za pango kunapunguza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na majukumu ya kimsingi ya ubalozi.

**Ninapendekeza kuwa serikali itenge fedha au kufanya tathmini ya uwezekano wa kupata mikopo ya majengo itakayowezesha kujenga au**

**kununua majengo ya ubalozi, hivyo kupunguza gharama kubwa za kodi ya pango.**

## 12.5 Makubaliano Baina ya Nchi Mbili

### 12.5.1 Vihatarishi Vinavyotokana na Kukosekana kwa Hati Sanifu ya Makubaliano ya Uwekezaji Baina ya Nchi Mbili

Tangazo la Serikali Na. 407 A na B (GN Na. 407) linaipa mamlaka Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji (Fungu Na. 11) kuongoza, kuratibu, na kufuatilia majadiliano ya uwekezaji wa kimataifa kwa niaba ya serikali. Hii inajumuisha kuingia katika mikataba ya uwekezaji baina ya nchi mbili, yanayolenga kulinda na kukuza uwekezaji unaofanywa na wawekezaji wa kigeni kwa kuweka masharti yanayohusu ulinzi wa kisheria, taratibu za utatuzi wa migogoro, na masuala mengine yanayohusiana na uwekezaji.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Tanzania ilikuwa imesaini mikataba 30 ya uwekezaji baina ya nchi mbili (BITs) na mataifa mbalimbali. Hata hivyo, mikataba hii yote iliandaliwa na nchi washirika badala ya serikali kupitia Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji (POPI). Kutegemea mikataba iliyoandaliwa na nchi za kigeni kunaongeza hatari ya kuwepo kwa masharti yasiyofaa, kwani yanaweza kuzingatia zaidi maslahi ya nchi hizo badala ya malengo ya kimkakati ya Tanzania. Kutokulingana kwa maslahi haya kunaweza kusababisha masharti ya uwekezaji ambayo hayaendani kikamilifu na malengo ya muda mrefu ya kiuchumi na kisera ya nchi.

**Ninapendekeza serikali, kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, isanifu hati za makubaliano baina ya nchi mbili ambayo itaendana na vipaumbele vya uwekezaji wa kitaifa. Hii itahakikisha kuwa mikataba ijayo italenga maslahi ya pande zote mbili na kutoa haki kwa wageni na kulinda maslahi ya kiuchumi ya Taifa.**

# SURA YA KUMI NA TATU




# Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mishahara na Mafao ya Wastaafu

# USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU, MISHAHARA NA MAFAO YA WASTAAFU

## 13.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya upungufu uliyobainika wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa rasilimaliwatu, mishahara, na uandaaji wa mafao ya wastaafu katika taasisi mbalimbali za Serikali Kuu.

Pia inajumuisha mapendekezo ya kuboresha usimamizi wa rasilimaliwatu katika sekta ya umma. Hatua hizi zinalenga kuboresha ufanisi wa uendeshaji na kuhakikisha kwamba taasisi za umma zinatekeleza vyema majukumu yao

## 13.2 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Usimamizi madhubuti wa rasilimaliwatu ni muhimu kwa taasisi za umma. Unahakikisha kuwa kuna nguvu kazi yenye ujuzi na hamasa inayosababisha kutoa huduma zenye ubora. Pia, kuboresha na kuhamasisha uwajibikaji, na kuunga mkono malengo ya taasisi. Upungufu katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu unaweza kusababisha ufanisi duni na changamoto za upangaji wa nguvu kazi. Upungufu niliyobaini katika taasisi za umma na mapendekezo ya kuboresha ufanisi wa uendeshaji yanajadiliwa katika aya zifuatazo.

### 13.2.1 Kutowasilisha Makato ya Kisheria ya Sh. Bilioni 1.34 kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi

Kanuni Na. 12(4) ya Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (za Jumla) za mwaka 2018, na Kifungu Na. 12(7) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, zinawataka waajiri wanaochangia kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kulipa kiasi kinachodaiwa ndani ya mwezi mmoja baada ya kumalizika kwa mwezi unaohusiana na michango hiyo.

Vivyo hivyo, Kifungu Na. 9 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa ya mwaka 1999 na Kifungu Na. 84 (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332, Toleo la Marekebisho la mwaka 2019) zinahitaji kulipwa kwa wakati kwa makato, na adhabu hutolewa kwa ucheleweshaji wowote.

Katika Ukaguzi wangu kwa mwaka wa fedha 2023/24 nilibaini kuwa taasisi 20 hazikuwasilisha makato ya michango ya wanachama ya hifadhi za jamiii, michango ya bima ya afya, na kodi ya PAYE (Pay-As-You-Earn) yenye jumla ya Sh. bilioni 1.03 kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa kipindi kati ya mwaka

mmoja hadi 21. Hii inaonesha upungufu wa Sh milioni 25.78 ikilinganishwa na Sh. bilioni 1.06 iliyoripotiwa kwa taasisi 17 katika mwaka uliopita, kama ilivyobainishwa kwenye **Jedwali Na. 46**.

Aidha, nilibaini kuwa Balozi za Tanzania zilizopo Bujumbura na Kinshasa hazikuzingatia matakwa ya nchi husika kwa kushindwa kuwasilisha makato ya kisheria ya mishahara yenye jumla ya Sh. milioni 33.71 na Sh. milioni 277.89 mtawalia. Hii inasababisha jumla ya makato ya kisheria ambayo hayajalipwa kufikia TZS bilioni 1.34 kwa taasisi 20 na balozi mbili.

**Jedwali Na. 46: Orodha ya Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Makato ya Kisheria ya Mishahara**

| Na. | Taasisi | Mlipwaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Bunda | TRA | 105,366,373 |
| | | PSSSF | 183,111,635 |
| 2 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Busega | NSSF na PSSSF | 34,236,400 |
| 3 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Chato | PSSSF | 54,687,069 |
| 4 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Ifakara | PSSSF | 14,172,598 |
| 5 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Igunga | PSSSF | 115,651,793 |
| 6 | Chombo cha Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii Imuka | Mifuko ya Pensheni | 4,056,000 |
| 7 | Shule ya Sekondari Jitegemee | NSSF | 2,104,944 |
| 8 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Kasulu | PSSSF | 65,170,195 |
| 9 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Kilwa Masoko (KIMUWASA) | PSSSF | 2,918,600 |
| 10 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Kondoa | PSSSF | 72,117,579 |
| 11 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Uwanda wa Makonde | PSSSF | 47,073,000 |
| 12 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Mugango/Kiabakari (MKWASSA) | NHIF | 1,142,700 |
| 13 | Chombo cha Watoahuduma ya Maji Ngazi ya Jamii Nkimwankoi | PSSSF | 5,040,000 |
| 14 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Orkesument | PSSSF | 57,554,485 |
| 15 | Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) | NHIF | 1,846,200 |
| | | PSSSF | 6,154,000 |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Singida | TRA | 2,037,600 |
| | | NHIF | 532,800 |
| | | PSSSF | 5,328,000 |
| 17 | Kampuni ya Ushauri ya SUMAJKT | TRA | 12,705,000 |

| Na. | Taasisi | Mlipwaji | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 18 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Tunduru | NSSF na PSSSF | 26,205,564 |
| 19 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Ushirombo (UWSSA) | PSSSF | 567,000 |
| 20 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Wanging'ombe | PSSSF | 215,470,590 |
| **Jumla** | | | **1,035,250,125** |

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24

Ninahusisha hali hii na upungufu wa fedha na ukosefu wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji kwa ajili ya kuwasilisha makato ya kisheria kwa wakati. Kutozingatia takwa hili kunahatarisha usalama wa kifedha wa watumishi, kunachelewesha upatikanaji wa mafao ya kustaafu wanayostahili, na kunaweka taasisi katika hatari ya faini na adhabu. Pia, kushindwa kuwasilisha makato hayo kumesababisha adhabu ya Sh. milioni 83.38 kwa taasisi nne. Taasisi hizo ni Mamlaka za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Chato, Wanging'ombe, Tunduru na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kilwa Masoko (KIMUWASA). Fedha hizi zingeweza kutumika kwa shughuli nyingine za uendeshaji.

**Ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali, kupitia maafisa masuuli husika: itekeleze mifumo madhubuti ili kuhakikisha makato ya kisheria yanawasilishwa kwa wakati; itenge fedha kwa ajili ya madhumuni hayo, na ilipe kiasi kilichosalia bila kuchelewa zaidi.**

### 13.2.2 Upungufu katika Uandaaji na Utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi wa Umma

Kanuni Na. G 1 (8) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, zinataka taasisi za serikali kuendesha programu za utangulizi na maelekezo kwa watumishi wapya.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 17 hazikuendesha programu za utangulizi na uelekezi kwa watumishi wapya 434. Orodha kamili ya taasisi hizi imeainishwa kwenye **Jedwali Na. 47**.

**Jedwali Na. 47: Orodha ya Taasisi Zilizoshindwa Kufanya Programu za Utangulizi na Uelekezaji**

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Kipindi cha Ajira |
|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 123 | Julai 2023 hadi Juni 2024 |
| 2 | Wizara ya Maji (Fungu Na. 49) | 64 | Septemba 2023 hadi Machi 2024 |

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Kipindi cha Ajira |
|---|---|---|---|
| 3 | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | 35 | Agosti 2023 |
| 4 | Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) | 34 | Julai 2023 hadi Juni 2024 |
| 5 | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | 26 | Februari hadi Juni 2024 |
| 6 | Taasisi ya Maji | 20 | Julai 2023 hadi Juni 2024 |
| 7 | Mamlaka ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Mugango/Kiabakari (MKWASSA) | 17 | Julai 2023 hadi Juni 2024 |
| 8 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika (LNBWB) | 15 | Januari 2024 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe | 15 | Julai 2023 hadi Machi 2024 |
| 10 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini | 15 | Agosti 2022 |
| 11 | Bodi ya Filamu Tanzania | 13 | Septemba 2023 |
| 12 | Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi | 12 | Julai 2023 hadi Juni 2024 |
| 13 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga | 12 | Julai 2023 hadi Machi 2024 |
| 14 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | 11 | Julai 2023 hadi Machi 2024 |
| 15 | Taasisi ya Ardhi Morogoro | 8 | Desemba 2023 hadi Mei 2024 |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Sumbawanga | 7 | Julai 2023 hadi Machi 2024 |
| 17 | Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) | 7 | Julai hadi Agosti 2023 |
| **Jumla** | | **434** | |

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24

Vikwazo vya bajeti vinazuia hasa kufanyika kwa Kozi za Utangulizi na Uelekezaji, jambo linaloathiri vibaya tija ya watumishi, utendaji, na utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia maafisa masuuli husika, kuweka kipaumbele katika kutoa mafunzo ya utangulizi na uelekezi kwa watumishi wapya ili kuwapatia watumishi hao viwango vya kimaadili na miongozo muhimu kwa ajili ya utekelezaji majukumu yao.**

### 13.2.3 Taarifa zisizo Sahihi za Watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS)

Kanuni Na. 110 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001, inawapa maafisa masuuli jukumu la kuhifadhi taarifa sahihi za malipo ya stahiki za watumishi ndani ya mamlaka zao na kuzihuisha mara kwa mara ili kuhakikisha usahihi wake.

Aidha, Waraka Na.1 (Kumb. Na. CAC.44/472/01/A) wa tarehe 24 Mei 2021 na Barua ya Uanzishaji (Kumb. Na. CFC.26/205/01/AR/71) ya tarehe 30 Mei 2022 zinahitaji waajiri kuhuisha taarifa za watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) ili kuhakiki usahihi wa taarifa.

Nilibaini kuwapo kwa taarifa zisizo sahihi za watumishi katika taasisi nane, ambapo watumishi 283 walikuwa na taarifa zisizokamilika na za zamani katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS). Tofauti hizi zilionekana katika tarehe za kupandishwa cheo, tarehe za uthibitisho, sifa za kielimu, na tarehe ya kuzaliwa ambazo haziendani kati ya Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na. 48**.

**Jedwali Na. 48: Orodha ya Taasisi Zenye Taarifa Zisizo Sahihi za Watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS)**

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Tofauti za Taarifa |
|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Maji (Fungu Na. 49) | 143 | Tarehe za kuzaliwa zilizo kwenye mfumo hazifanani na zile zilizo kwenye Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN). |
| 2 | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | 62 | |
| 3 | Wizara ya Uchukuzi | 31 | |
| 4 | Wizara ya Nishati | 9 | |
| 5 | Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji (Fungu Na. 11) | 4 | |
| 6 | Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu (ADEM) | 25 | Kutofautiana kwa tarehe za kuzaliwa kati ya Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), na hadhi ya vyeo vya watumishi haijahuishwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS). |
| 7 | Bodi ya Maji ya Bonde la Wami Ruvu | 5 | Tarehe ya uthibitisho na kupandishwa cheo inaonesha mwaka 1900, hakuna namba ya jalada binafsi la mtumishi na |

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Tofauti za Taarifa |
|---|---|---|---|
| | | | kutokamilika kwa taarifa za kituo cha kazi. |
| 8 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania | 4 | Watumishi wasio na namba za mtihani wa kidato cha nne. |
| | **Jumla** | **283** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

Kasoro hizi zinatokana na upungufu wa kuhuisha taarifa za watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS). Taarifa zisizo sahihi za watumishi katika HCMIS zinaweza kusababisha kuachishwa kazi watumishi kabla ya muda wa kustaafu, kuendelea kwa ajira baada ya umri wa kustaafu, pamoja na kuathiri maamuzi kuhusu kupandishwa vyeo vya watumishi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia maafisa masuuli wa taasisi husika, ihakikishe taarifa za watumishi katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) zinahuishwa mara kwa mara na kuwa sahihi.**

### 13.2.4 Watumishi Wanaokaimu katika Nafasi ya Uongozi kwa zaidi ya Miezi Sita

Kanuni Na. D.24 (3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, zinahitaji kwamba mtumishi wa umma asitumikie nafasi ya kukaimu uongozi kwa zaidi ya miezi sita na kwamba mamlaka ya uteuzi ikamilishe mchakato wa uteuzi ndani ya kipindi hiki.

Nilibaini kuwa taasisi 15 zilikuwa na watumishi 106 wanaokaimu katika nafasi za uongozi kwa kipindi cha miezi saba hadi miezi 84, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali 49**.

**Jedwali Na. 49: Orodha ya Taasisi zenye Watumishi Wanao Kaimu katika Nafasi ya Uongozi kwa Zaidi ya Miezi Sita**

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Kipindi cha Kukaimu (Miezi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Huduma za Magereza | 24 | 8 hadi 49 |
| 2 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 21 | 12 hadi 36 |
| 3 | Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 14 | 7 hadi 37 |
| 4 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa | 13 | 26 |
| 5 | Wakala wa Ununuzi wa Umma (GPSA) | 9 | 60 |
| 6 | Tume ya Mipango | 5 | 9 hadi 12 |
| 7 | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 4 | 8 hadi 84 |

| Na. | Taasisi | Idadi ya Watumishi | Kipindi cha Kukaimu (Miezi) |
|---|---|---|---|
| 8 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | 3 | 15 |
| 9 | Bodi ya Usajili wa Wathamini | 3 | 14 |
| 10 | Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika | 2 | 48 |
| 11 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 2 | 10 hadi 24 |
| 12 | Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | 1 | 15 |
| 13 | Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) | 2 | 9 hadi 22 |
| 14 | Tume ya Taifa ya UNESCO | 2 | 9 hadi 10 |
| 15 | Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala (TAHPC) | 1 | 9 |
| **Jumla** | | **106** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

Tatizo hili limeonekana mara kwa mara katika kaguzi zilizopita. Hata hivyo, linaendelea kuwapo kutokana na ucheleweshaji wa kupata vibali vya ajira na uhamisho wa watumishi kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mchakato mrefu wa uchunguzi, na ukosefu wa ufuatiliaji wa kutosha kutoka kwa uongozi wa taasisi husika kwa mamlaka ya uteuzi hali ambayo inazidi kuibua matatizo. Maoni yangu ni kwamba ucheleweshaji wa uteuzi na kupandishwa vyeo kwa watumishi kwa wakati unaathiri morali ya watumishi, maamuzi, uwajibikaji, na utendaji wa taasisi kwa ujumla.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ichukue hatua za haraka kutatua tatizo hili kwa kuhakikisha uteuzi wa watumishi ambao wamekuwa wakikaimu katika nafasi za uongozi kwa muda mrefu. Aidha, pale ambapo watumishi wanaokaimu hawakidhi vigezo vinavyohitajika, uteuzi mpya unahitajika kujaza nafasi hizo.**

### 13.2.5 Stahiki za Watumishi Zisizolipwa zenye Thamani ya Sh. Bilioni 274.80

Kanuni Na. E.23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, zinahitaji kwamba mtumishi wa serikali anapopandishwa cheo au kuteuliwa katika nafasi ya juu, anakuwa na haki ya malimbikizo ya mshahara. Pia, aya ya 4 ya Waraka wa Hazina Na. 1 wenye Kumb. Na. CBE.187/209/01''B''/51 wa tarehe 7 Februari 2023, inahitaji waajiri wote kusimamia taratibu za malipo ya mshahara ili kuepuka malimbikizo ya mshahara.

Nilikagua taarifa za kifedha za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 na kubaini kuwa taasisi 205 zilirekodi madai ya watumishi yenye jumla ya Sh. bilioni 274.80, ikionesha ongezeko la Sh. bilioni 27.61 ikilinganishwa na mwaka uliopita kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. XIV.**

Kuongezeka kwa madai ya watumishi kunatokana na ukosefu wa fedha na ucheleweshaji wa kuidhinishwa madai na Ofisi ya Rais – Usimamizi wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa maoni yangu, madai ya watumishi yasiyolipwa yanaongeza mzigo wa madeni kwa Serikali, yanawakatisha tamaa, na kuathiri motisha kwa watumishi.

**Ninapendekeza kwamba taasisi hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Fedha kuharakisha idhini na malipo ya stahiki za watumishi zinazodaiwa.**

### 13.2.6 Ukosefu wa Muundo wa Utumishi Ulioidhinishwa

Kanuni Na. D.6 (2) ya Kanuni za Kudumu za Huduma za Umma za mwaka 2009, zinataka kwamba watumishi lazima wawe na sifa zilizobainishwa katika Muundo wa Utumishi Ulioidhinishwa kwa kada husika kabla ya kuteuliwa, kupandishwa cheo, au kuhamishwa kwa nafasi yoyote katika utumishi wa umma.

Nilibaini kwamba taasisi saba hazikuwa na Muundo wa Utumishi Ulioidhinishwa kwa vipindi vinavyotofautiana kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 41. **Jedwali Na. 50** linaorodhesha taasisi zinazokosa Mpango wa Huduma Ulioidhinishwa.

**Jedwali Na. 50: Orodha ya Taasisi zisizo na Muundo wa Utumishi ulioidhinishwa**

| Na. | Taasisi | Tarehe ya Kuanzishwa Taasisi |
|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Mafunzo ya Ufugaji Nyuki | Agosti 2010 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato | Septemba 2022 |
| 3 | Utafiti wa Jiolojia Tanzania | Mei 2018 |
| 4 | Shirika la Magereza | 1983 |
| 5 | Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Rujewa | Juni 2024 |
| 6 | Kampuni ya Ulinzi ya SHIMA | Februari 2021 |
| 7 | Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mji wa Mbulu | 2002 |

**Chanzo:** Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24

Tatizo hili linatokana hasa na ucheleweshaji wa kupata idhini kutoka kwa mamlaka husika. Bila Muundo wa Utumishi ulioidhinishwa, watumishi katika

ngazi mbalimbali wanabaki na hofu kuhusu haki zao kuhusiana na uteuzi, kupandishwa cheo, na uhamisho. Hali hii inaweza kupunguza utendaji na morali ya watumishi, hivyo kuathiri ufanisi wa taasisi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora na taasisi husika, ziandae na kupata idhini ya Muundo wa Utumishi.**

### 13.2.7 Upungufu wa Watumishi wa Umma

Kanuni Na. D.7 na D.8 (1) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, linaelezea majukumu ya Sekretarieti ya Ajira katika kujaza nafasi za ajira katika huduma za umma na taratibu zitakazofuatwa wakati wa mchakato wa ajiri.

Nilibaini upungufu wa watumishi wa umma katika taasisi mbalimbali za Serikali. Mapitio ya orodha ya mahitaji ya watumishi na nafasi zilizo wazi katika taasisi 39 za serikali yalionesha upungufu wa watumishi 2202 ikilinganishwa na idadi inayohitajika ya watumishi 4490. Upungufu huu unazuia kufikiwa kwa malengo ya ufanisi yaliyowekwa na taasisi za Serikali Kuu. Kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. XV.**

Ninahusisha tatizo hili na ucheleweshaji katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kujaza nafasi za wazi na kutoa vibali vya ajira.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ihakikishe kuwa nafasi za wazi zinajazwa haraka.**

### 13.2.8 Masurufu Yasiyorejeshwa - Sh. bilioni 2.28

Kanuni ya 103 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inahitaji kurejeshwa kwa fedha za masurufu zilizotolewa au kurejeshwa kwa fedha za masurufu zilizocheleweshwa kutoka kwa mshahara wa mfanyakazi.

Kinyume chake, nilibaini kuwa wafanyakazi katika taasisi tisa hawajarejesha fedha za masurufu zenye jumla ya Sh. bilioni 2.28. Licha ya tarehe ya mwisho ya marejesho kupita, taasisi hizo hazijarejesha kiasi hicho kutoka kwenye mishahara yao. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 51.**

**Jedwali Na. 51: Orodha ya Taasisi Zenye Masurufu Yasiyorejeshwa**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Chuo cha Ardhi - Morogoro | 793,522,469 |
| 2 | Fungu Na. 34: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 669,182,774 |
| 3 | Fungu Na. 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 357,610,120 |
| 4 | Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji | 209,276,250 |
| 5 | Mkataba wa Kugawana Uzalishaji wa Nishati (MEM-PSA) wa Wizara ya Nishati | 139,150,902 |
| 6 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) | 44,040,000 |
| 7 | Ubalozi wa Tanzania - Jakarta | 37,345,700 |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Dodoma | 33,428,000 |
| 9 | Fungu Na. 32: Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 5,441,034 |
| | **Jumla** | **2,288,997,249** |

***Chanzo***: *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti Mwaka 2023/24*

Hii inaonesha ukosefu wa utekelezaji wa udhibiti wa kifedha, ambao unaathiri usimamizi bora wa fedha za umma na kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**Ninapendekeza Serikali iimarishe udhibiti wa kifedha ili kuhakikisha fedha za masurufu zinarejeshwa kwa wakati kulingana na kanuni. Aidha, ihakikishe kiasi kilichobaki kinarejeshwa kutoka kwa mishahara ya maafisa wanaohusika, malipo yao, au haki nyingine kama inavyohitajika.**

## 13.3 Ukaguzi wa Awali wa Mafao ya Wastaafu Yaliyoandaliwa kwa Malipo

Ukaguzi wa awali wa mafao ya kustaafu yanayolipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ni utaratibu unaotekelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 143(2)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa). Katiba inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuidhinisha malipo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kuthibitisha ibara ya 136 imezingatiwa.

### 13.3.1 Mawanda na Lengo la Ukaguzi wa awali

Ukaguzi wa awali wa mafao ya kustaafu unahusisha mafao ya kustaafu ya watumishi wa umma yanayolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ikijumuisha pensheni, kiinua mgongo kwa baadhi ya maafisa wa Serikali.

Ukaguzi huu unalenga kuhakikisha usahihi, uzingatiaji wa sheria, na ustahiki wa malipo ya mafao kabla ya kufanyika kwa malipo. Hii husaidia kuzuia makosa, udanganyifu, na hasara za kifedha, huku ikikuza uwazi na uwajibikaji.

### 13.3.2 Utekelezaji wa Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wangu wa awali ulianza na majalada 81 ya wastaafu ikiwa ni bakaa kutoka mwaka wa fedha 2022/23, na majalada 1,950 yaliwasilishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24, na kufanya jumla ya majalada 2,031 kupatikana kwa ajili ya ukaguzi wa awali. Kati ya hayo, majalada 1,789 yalifanyiwa ukaguzi na kuidhinishwa, huku 125 yakirejeshwa kwa waajiri kwa ajili ya marekebisho kutokana na hoja zilizobainika. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, majalada yaliyosalia yalikuwa 117.

## 13.4 Matokeo ya ukaguzi wa awali wa majalada

Ukaguzi wa awali wa majalada ya mafao ya kustaafu kwa mwaka wa fedha 2023/24 ulibaini changamoto kadhaa, kama zinavyofafanuliwa kwenye aya zifuatazo:

### 13.4.1 Kukosewa kwa ukokotoaji wa mafao na Waajiri

Uhakiki wangu wa majalada 1,789 yaliyoidhinishwa kwa malipo ulibaini makosa katika majalada 30 (asilimia mbili), ikiwa ni pamoja na makosa katika hesabu ya kipindi cha utumishi, mishahara iliyotumika, michango ya mwajiri na mwajiriwa iliyowasilishwa kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii kimakosa, na makosa mengine tofauti. Hata hivyo, makosa hayo yalirekebishwa na majalada hayo niliyaidhinisha kwa malipo.

Miongoni mwa majalada 30 ya mafao ya wastaafu yaliyokokotolewa kimakosa, majalada 17 (57%) yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa Sh. milioni 244.38 na majalada 13 (43%) yalikokotolewa kwa kiwango pungufu kwa Sh. milioni 26.17. Muhtasari wa idadi ya majalada na makosa yaliyobainika umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 52**.

**Jedwali Na. 52: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa**

| Na. | Aina ya Kosa | Mafao yaliyozidi | | Mafao yaliyopungua | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Majalada | Kiasi (Sh.) | Idadi ya Majalada | Kiasi (Sh.) |
| 1 | Muda wa utumishi usio sahihi | 13 | 222,793,909 | 10 | 22,340,915 |
| **2** | Makosa mbalimbali katika ukokotoaji | 1 | 46,607 | 1 | 1,955,537 |
| 3 | Mishahara iliyokosewa | 3 | 21,542,225 | 2 | 1,873,996 |

| Na. | Aina ya Kosa | Mafao yaliyozidi | | Mafao yaliyopungua | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Majalada | Kiasi (Sh.) | Idadi ya Majalada | Kiasi (Sh.) |
| **Jumla** | | **17** | **244,382,741** | **13** | **26,170,447** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi*

Sababu zilizobainishwa ni mapungufu katika kukokotoa mafao kutokana na makosa katika hesabu, tafsiri isiyo sahihi ya sera za mafao, dosari za ujazaji wa taarifa, na kutokuwapo kwa uhakiki wa kutosha wa uthibitisho ili kutambua na kurekebisha makosa wakati wa mchakato wa ukokotoaji.

Bila ukaguzi wangu wa awali, Serikali ingeweza kupata hasara ya Sh. milioni 244.38 kutokana na ukokotozi uliozidi kiasi stahiki, na wastaafu wangepata mapunjo ya jumla ya Sh. milioni 26.17.

Mapungufu yaliyobainishwa yanaonesha mchango mkubwa wa ukaguzi wa awali wa mafao na malipo mengine yanayolipwa moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hii pia inadhihirisha udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani na changamoto kwa maafisa masuuli, hali inayoweza kusababisha athari za kifedha kwa Serikali na wastaafu.

**Ninapendekeza Serikali kuboresha mifumo ya uthibitishaji na kutoa mafunzo endelevu kwa wafanyakazi kuhusu sera za mafao na njia sahihi za ukokotoaji. Vilevile, ni muhimu kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa maafisa masuuli ili kuhakikisha usahihi, uwajibikaji na kuzuia makosa katika mchakato wa ukokotoaji wa mafao.**

### 13.4.2 Ucheleweshwaji wa Uandaaji na Uwasilishwaji wa Taarifa za Mafao

Kwa mujibu wa Kanuni ya 88 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, waajiri na waajiriwa wanawajibika kuhifadhi kumbukumbu za ajira kwa usahihi ili zitumike kama rejea wakati wa ukokotoaji wa mafao ya kustaafu kwa mwajiriwa husika.

Vilevile, Kanuni Na. F. 48 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, ikisomwa sambamba na Kanuni ya 32(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, inamtaka mtumishi wa umma anayekaribia kustaafu kuwasilisha taarifa kwa maandishi kwa mamlaka ya uteuzi kupitia taratibu rasmi, angalau miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu, akieleza nia yake ya kustaafu.

Katika ukaguzi wa awali wa mwaka 2023/24, nilibaini kuwa waajiri walichelewa kuandaa na kuwasilisha majalada ya mafao ya wastaafu 339 ambayo ni sawa na 17% ya majalada yote yaliyopokelewa. Ucheleweshaji huo ulikuwa kati ya mwaka mmoja hadi miaka 15.

Kucheleweshwa kwa malipo ya mafao ya kustaafu kunaathiri kwa kiasi kikubwa ustawi wa maisha ya wastaafu, kwani wengi wao hutegemea mafao hayo kugharamia mahitaji yao ya kila siku. Muhtasari wa majalada ya mafao ya kustaafu na kiwango cha ucheleweshaji umeoneshwa katika **Jedwali Na. 53**.

**Jedwali Na. 53: Majalada yaliyochelewa kuandaliwa na kuwasilishwa**

| Muda wa ucheleweshwaji wa majalada | Idadi ya Majalada |
|---|---|
| Hadi miaka miwili | 224 |
| Hadi miaka 5 | 51 |
| Hadi miaka 15 | 64 |
| **Jumla** | **339** |

**Chanzo:** Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Maafisa masuuli, ihakikishe maandalizi na uwasilishwaji wa majalada ya mafao ya kustaafu kwa wakati katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hatua hii itasaidia kuepuka ucheleweshaji wa uchakataji wa mafao ya wastaafu, ambao unaathiri ustawi wao katika jamii.**

### 13.4.3 Majalada Yaliyohojiwa hayajarudishwa kuidhinishwa

Ukaguzi wa awali wa majalada ya mafao ya kustaafu hufanywa kwa kuzingatia vigezo vitatu muhimu: ustahiki wa mlengwa, ukamilifu wa nyaraka zilizowasilishwa, na usahihi wa ukokotoaji wa mafao.

Katika mchakato huu, endapo kutabainika makosa, tofauti, au dosari zozote, jalada hurudishwa kwa mwajiri kwa ajili ya kurekebisha hoja husika. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma (GN Na. 47 ya 2009), waajiri wanapaswa kushughulikia hoja hizo na kuwasilisha majibu ndani ya siku 21 tangu tarehe ya kupokea jalada.

Wakati wa ukaguzi, majalada 125 ya mafao ya kustaafu yalihojiwa na kurudishwa kwa waajiri. Kati ya hayo, majalada 85 yalihusu wastaafu waliokuwa kwenye masharti ya kawaida ya kazi ambayo sasa hayastahili kuhakikiwa na kulipwa, kufuatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2023. Miongoni mwa majalada yaliyosalia, 40 yalirudishwa kwa ajili ya marekebisho, lakini hadi tarehe 30 Juni 2024, hayakuwa yamewasilishwa tena kwa ajili ya uhakiki.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia maafisa masuuli, ishughulikie kwa wakati hoja za ukaguzi wa awali au itafute ufafanuzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapobidi. Aidha, Serikali inapaswa kuwachukulia hatua Maafisa Rasilimaliwatu kwa kuchelewesha uchakataji na uwasilishaji wa majalada ya pensheni.**

# SURA YA KUMI NA NNE




# Usimamizi wa Mali

# USIMAMIZI WA MALI

## 14.1 Utangulizi

Mfumo imara wa usimamizi wa mali katika taasisi unaleta manufaa nane muhimu: ufanisi bora katika utekelezaji wa majukumu, kuokoa gharama, kupunguza hatari zinazoweza kujitokeza, kufanya maamuzi bora, kuongeza matumizi ya mali kwa muda mrefu, kuboresha ufuatiliaji wa mali, kuongeza uimara, na faida ya ushindani kupitia kuboresha maisha ya mali na kuhakikisha utendaji bora wakati wote wa matumizi ya mali.

Serikali imetoa Nyaraka, Miongozo na Kanuni mbalimbali kuhusu usimamizi wa mali na kusisitiza utekelezaji na uzingatiaji wa taratibu hizi. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini baadhi ya masuala ya kutofuata taratibu na sheria ambayo yanajadiliwa katika sura hii.

## 14.2 Taasisi Zinazofanya kazi bila Mpango wa Matengenezo ya Mali

Kwa mujibu wa Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma), za Mwaka 2024, maafisa masuuli wanapaswa kuandaa mpango wa matengenezo kwa mali za umma.

Lengo la mpango wa matengenezo ni kuweka mali katika hali ya kufanya kazi kwa matumizi yaliyokusudiwa, kuhakikisha utoaji wa huduma bora, na kuboresha matumizi ya kiuchumi ili kuongeza manufaa ya kila taasisi.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini taasisi 31 zilifanya kazi bila Mpango wa Matengenezo ya Mali. Jumla ya gharama za ununuzi wa mali hizo ni Sh. trilioni 2.77, na thamani yake katika taarifa za fedha ni Sh. trilioni 2.35, na walitumia Sh. bilioni 28.29 kwa ukarabati na matengenezo ya mali hizo katika mwaka 2023/24.

Pia, balozi 14 zenye mali za thamani ya Sh. bilioni 129.11 na thamani ya mali hizo kwa sasa katika taarifa za fedha ni Sh. bilioni 104.93 zilitumia gharama ya Sh. milioni 710.91 kwenye matengenezo ya mali hizo bila kuwa na mpango wa matengenezo ya mali na zilishindwa kuhifadhi rekodi sahihi za ukarabati na matengenezo ya mali zao.

Taratibu hizi ziliathiri ufanisi wa utendaji wa shughuli zao na zilihusishwa na ukosefu wa usimamizi bora. Angalia **Kiambatisho Na. XVI** na **Kiambatisho Na XVII.**

Bila kuwa na mpango wa matengenezo wa mali, serikali inajiweka hatarini kukutana na madhara makubwa kama vile vifaa kushindwa kufanya kazi mara kwa mara, kupungua kwa uzalishaji, gharama za matengenezo kuongezeka, hatari za usalama, changamoto za utekelezaji wa sheria, ongezeko la mali zisizoweza kutumika, na muda mfupi wa maisha ya mali. Hali hii inaweza kuathiri vibaya ufanisi wa uendeshaji wa serikali na uthabiti wake wa kifedha.

**Napendekeza serikali, kupitia Wizara ya Fedha, kusisitiza maandalizi na utekelezaji mpango wa usimamizi wa mali kwa ajili ya wizara zote, idara, wakala wa serikali, na taasisi nyingine na kutunza taarifa zinazohusiana na matengenezo ya mali.**

## 14.3 Mali zisizokuwa na Nambari ya Utambulisho Sh. Bilioni 9.92

Kanuni ya 3 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) za mwaka 2024 inahitaji Maafisa Masuuli kutoa nambari ya kipekee au nambari kwa kila mali ya umma inayonunuliwa kwa mujibu wa sheria husika au kufuata muundo uliowekwa katika jedwali la kwanza la Kanuni hizi.

Ingawa taasisi nyingine za serikali zimefanya vyema katika eneo hili, niliona kwamba mali zenye thamani ya Sh. bilioni 9.92 kutoka kwa taasisi 15 na Sh. milioni 81.45 kutoka kwa balozi tano hazina nambari za utambulisho wa mali zinazohitajika kwa mujibu wa kanuni. Tazama **Jedwali Na. 54** na **Jedwali Na. 55** kwa taasisi nyingine za serikali na balozi, mtawalia.

**Jedwali Na. 54: Taasisi zenye Mali Zisizokuwa na Nambari ya Utambulisho**

| Na. | Jina la Taasisi | Gharama (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Maswa | 3,152,099,707 |
| 2 | Huduma za Mashtaka za Taifa - NPS | 1,677,107,009 |
| 3 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Turiani | 1,655,508,258 |
| 4 | Kampuni ya Magereza | 1,117,703,858 |
| 5 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Busega | 835,627,330 |
| 6 | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Taifa (TALIRI) | 539,085,000 |
| 7 | Kitengo cha Matibabu cha Polisi | 331,551,000 |
| 8 | Chuo cha Utumishi wa Umma | 233,939,208 |
| 9 | Hospitali ya Kijeshi ya Lugalo | 123,330,000 |
| 10 | Kampuni tanzu ya Jeshi la Polisi | 73,054,725 |
| 11 | Bodi ya Maji ya Bonde la Maji la Ndani | 43,050,000 |
| 12 | Mfuko wa Utamaduni na Sanaa wa Tanzania | 28,266,325 |
| 13 | Chombo cha watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii-Mvumi | 24,434,500 |
| 14 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Namanyere | 5,000,000 |
| 15 | Chombo cha watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii-Imuka | 3,300,000 |

| Na. | Jina la Taasisi | Gharama (Sh.) |
|---|---|---|
| | **Jumla** | **9,843,056,920** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za 2023/24*

**Jedwali Na. 55: Balozi zenye Mali zisizokuwa na Nambari ya Utambulisho**

| Na. | Jina la Taasisi | Gharama (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Ubalozi wa Jakarta | 32,691,900 |
| 2 | Kamisheni ya Juu ya Kuala Lumpur | 22,130,706 |
| 3 | Ubalozi wa Tanzania - Brussels | 15,104,435 |
| 4 | Ubalozi wa Tanzania katika The Hague | 8,608,228 |
| 5 | Kamisheni ya Juu ya London | 2,922,617 |
| | **Jumla** | **81,457,886** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Kutoweka misimbo ya mali ya serikali huongeza hatari ya matumizi mabaya bila kutambuliwa na kuzuia kufuatilia mienendo ya mali husika. Hii inachangiwa na utendakazi duni wa wakuu wa idara zinazohusika.

**Ninapendekeza kwamba serikali iendelee kutilia mkazo suala la kuweka misimbo kwa mali zinazomilikiwa na umma na taasisi husika ili kuhakikisha kwamba mali zote za sasa na mpya zinazopatikana zinanakiliwa mara moja ili kuepusha matumizi mabaya na kuimarisha udhibiti unaofaa.**

## 14.4 Mali Zilizotelekezwa kwa muda Mrefu bila Matengenezo au Kuuzwa

Kanuni ya 23 na 24 za Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) za mwaka 2024 zinahitaji Maafisa Masuuli kuomba na kupendekeza uondoaji na uuzaji wa mali kwa wakati muafaka wakati inapoonekana kuwa haiwezekani kifedha kuzirekebisha, zimeisha muda, hazitumiki, ni za kale, au zisizoweza kutengenezeka.

Nilibaini uwepo wa mali zisizotumika, vitu vilivyochakaa, magari yaliyosimama muda mrefu, pikipiki, vifaa vya kilimo, vifaa vya TEHAMA, vifaa vya kutibua udongo na samani za ofisi ambazo hazikutengenezwa wala kuuzwa. Hata hivyo, sikuona maboresho katika eneo hili ikilinganishwa na mwaka uliopita. Licha ya juhudi za serikali, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali 34 ziliripoti udhaifu huu, ikilinganishwa na 27 kwa mwaka 2022/23. Mali hizi zimebaki bila kutumika kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 15. Tazama maelezo katika **Kiambatisho Na. XVIII.**

Ninaamini kuwa mali zilizopitwa na wakati zipo kwa sababu ya michakato mirefu ya kuidhinisha uuzwaji ama kuteketezwa kwake na kutopatikana fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo muhimu. Kuchelewa kuuza mali

zisizotengenezeka kama vile magari, mitambo na vifaa visivyoweza kutumika hupelekea kuharibika kwa vifaa hivyo na kupunguza fedha ambayo ingeweza kupatikana pale ambapo vingeuzwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa kuna fedha za kutosha na kuunda mipango ya matengenezo ya mali zinazofanya kazi ili kuimarisha maisha ya mali hizo yawe marefu sambamba na kurahisisha mchakato wa uondoshaji wa mali zisizotumika.**

## 14.5 Mali za kudumu kutoingizwa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali-GAMIS

Wizara ya Fedha ilianzisha Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) ili kusimamia orodha za mali katika taasisi za umma na kuboresha utoaji wa hesabu.

Mnamo tarehe 15 Julai 2021, Wizara ya Fedha ilitoa Waraka wa Hazina Na. 2 kwa mwaka 2021/22 kuhusu usimamizi wa kielektroniki wa mali za umma kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) ukiwataka maafisa masuuli kuhakikisha kuna matumizi sahihi ya Mfumo na muda wa mwisho wa kujiunga ulikuwa tarehe 31 Agosti 2021. Masharti haya yalisisitizwa na Kanuni ya 4 ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) za mwaka 2024, na Maelekezo ya Hazina (Kumb. Na. KA.32/233/01/174) ya tarehe 12 Juni 2024, ambayo yalihitaji maafisa masuuli kutekeleza kwa haraka kanuni hizi.

Uhakiki wangu ulibaini kuwa taasisi nyingi za serikali zimeshasajili orodha za mali kwenye mfumo wa kielektroniki, isipokuwa taasisi chache ambazo bado hazijaingiza taarifa zao kwenye mfumo. Mali zilizonunuliwa kwa thamani ya Sh. trilion 1.83 na zikiwa zimebakisha thamani ya kitabuni ya Sh. trilioni 1.37 kutoka kwa Wizara 47, Idara, Wakala, Mamlaka na Bodi za Maji, na Hospitali za Rufaa za Mikoa hazikuandikishwa katika Mfumo (GAMIS). Hii ni ongezeko la taasisi 14 (42%) ikilinganishwa na taasisi 33 zilizoripotiwa katika mwaka 2022/23. Rejea **Kiambatisho Na. XIX** kwa maelezo zaidi

Pia, nilibaini kuwa balozi 12 zenye mali za thamani ya Sh.125.92 bilioni na thamani ya kitabuni ya Sh.111.50 bilioni ambazo hazijarekodi mali zao katika mfumo, yaani, GAMIS. Tazama **Jedwali Na. 56** kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 56: Balozi ambazo hazikuongeza au kurekodi mali za Serikali katika Mfumo**

| Na. | Jina la Ubalozi | Thamani ya Asili (Sh.) | Thamani ya Kitabuni (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ubalozi wa Tanzania Paris | 48,845,354,725 | 41,519,900,976 |

| Na. | Jina la Ubalozi | Thamani ya Asili (Sh.) | Thamani ya Kitabuni (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 2 | Ubalozi wa Tanzania Nairobi | 28,983,302,699 | 28,364,441,363 |
| 3 | Ubalozi wa Tanzania Geneva | 16,128,861,931 | 14,652,934,113 |
| 4 | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa- DRC | 14,017,744,385 | 13,440,746,806 |
| 5 | Ubalozi wa Tanzania New Delhi | 13,211,946,941 | 11,460,102,811 |
| 6 | Ujumbe wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Umoja wa Mataifa-Vienna | 1,242,148,054 | 962,115,838 |
| 7 | Ubalozi wa Tanzania Doha | 943,916,484 | 436,893,159 |
| 8 | Ubalozi wa Tanzania Havana, Cuba | 712,474,574 | 355,732,909 |
| 9 | Ubalozi wa Tanzania Kuala Lumpur | 953,793,891 | 307,618,949 |
| 10 | Ubalozi wa Tanzania Algiers | 218,764,771 | - |
| 11 | Ubalozi wa Tanzania Jakarta | 579,061,450 | - |
| 12 | Ubalozi wa Tanzania Lusaka | 83,528,103 | - |
| **Jumla** | | **125,920,898,008** | **111,500,486,924** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Pamoja na mali ambazo hazijasajiliwa kwenye mfumo, taasisi hizi zilianzisha rejista za mali za ndani ili kuandaa taarifa za fedha, na hivyo kuboresha usahihi licha ya mapungufu ya mfumo. Hii ilichangiwa na kutokuwa na mafunzo ya kutosha katika uendeshaji wa mfumo.

**Ninapendekeza serikali iwape mafunzo watumishi kuhusu GAMIS na kuhakikisha mali zote zimerekodiwa kwenye mfumo. Maafisa Masuuli wanapaswa kutekeleza miongozo ya usimamizi wa mali, kuhakikisha taasisi zinatumia mifumo kwa ajili ya usimamizi bora na utunzaji sahihi wa kumbukumbu.**

### 14.6 Kutokuwapo kwa Hati za Kumiliki Viwanja Vinavyomilikiwa na Serikali

Kanuni ya 3(4) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali ya Umma) 2024 inamtaka Afisa Masuuli kupata umiliki halali wa mali ya umma na kutoa uthibitisho wa umiliki. Kifungu cha 29(1)(a)(b)(c) cha Sheria ya Ardhi Sura. 113 (Iliyorekebishwa mwaka 2019) inasema kwamba Kamishna anapotoa haki za umiliki, mwombaji lazima apokee "cheti cha umiliki," bila kujali umiliki wa sasa. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa idadi ya taasisi za serikali zisizo na Hati za Kumiliki za viwanja vyao ni karibu sawa na idadi ya mwaka wa fedha 2022/23. Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini kuwa taasisi 18 hazikuwa na hati miliko za viwanja 336. Nahusisha kukosekana kwa Hati za umiliki wa viwanja vinavyomilikiwa na serikali na ufuatiliaji usioridhisha kwa Kamishna wa Ardhi. Tazama **Jedwali Na. 57** kwa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 57: Orodha ya Taasisi zenye Viwanja Vinavyokosa Hati Miliki**

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Viwanja |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Huduma za Magereza | 193 |
| 2 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Vituo vya Mafunzo ya Ufundi vya Wilaya) | 39 |
| 3 | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa-NIDA | 30 |
| 4 | Huduma za Mashtaka za Kitaifa - NPS | 19 |
| 5 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Kondoa | 15 |
| 6 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 10 |
| 7 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Mbinga Mjini | 10 |
| 8 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Rujewa | 4 |
| 9 | Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania | 3 |
| 10 | Mamlaka ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira-Ushirombo | 3 |
| 11 | Tume ya Madini | 2 |
| 12 | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (Vituo vya Kilimanjaro Magharibi na Buhuri Tanga) | 2 |
| 13 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Wanging'ombe | 1 |
| 14 | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 1 |
| 15 | Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru | 1 |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | 1 |
| 17 | Mamlaka ya Huduma ya Maji Na Usafi Wa Mazingira-Kasulu | 1 |
| 18 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Soko la Upili la Mifugo Kizota | 1 |
| **Jumla** | | **336** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi*

Bila Hati Miliki ya Kutumia Ardhi, hakuna ushahidi wa kisheria wa umiliki au haki ya kutumia ardhi. Ukosefu huu unanyima umiliki wa kisheria wa mali, na hivyo kuleta ugumu katika juhudi za kuuza, kuweka dhamana, au kuiendeleza. Zaidi ya hayo, unakwamisha juhudi za kuuza mali na kuongezea hatari ya kufukuzwa, huku ikionyesha hali tete ya umiliki wa ardhi.

**Ninapendekeza kwamba serikali, kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kushirikiana na Maafisa Masuuli wote ambao hawajaweza kupata Hati ya Kumili na Haki ya Kutumia Ardhi kwa viwanja vilivyomo katika mamlaka yao ili kupata Hati Miliki zao.**

## 14.7 Kutofanyiwa maamuzi kwa mali zilizokabidhiwa katika eneo lililodhibitiwa la Mererani

Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali ya Umma) 2024 inamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha matumizi bora ya mali ya umma. Ikiwa mali itasalia bila kutumika kwa muda wa miezi sita, afisa lazima aripoti kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa hatua zaidi. Kanuni ya 7(2) inaeleza kuwa iwapo Katibu Mkuu atakuta mali hiyo haina kazi kwa zaidi ya miezi sita na ofisa hajaripoti, Katibu anaweza kuhamisha au kutoa mali hiyo kwa taasisi nyingine zitakazoweza kuzitumia.

Mwaka 2020, mali zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya Tanzanite One iliyopo Mirerani Kitalu C zilihamishiwa Tume ya Madini kupitia mkataba uliosainiwa ukihusisha Tume ya Madini, Tanzanite One na STAMICO, huku Tume ya Madini ikiteuliwa kuwa msimamizi wa mali hizo.

Nilitembelea Eneo Linalodhibitiwa la Mirerani (MCA) na kukagua taarifa ya makabidhiano na uhamishaji wa mali zilizokabidhiwa Serikalini na M/s Tanzanite One na kubaini kuwa Tume ya Madini iliitaarifu Wizara ya Fedha kuhusu mali hizo tarehe 21 Desemba 2022. Hata hivyo, hakuna maamuzi au maagizo yaliyotolewa kuhusu matumizi, uhamisho au uondoaji wa mali hizo katika eneo hilo. Kwa hivyo, mali hizo hazijatumika kwa zaidi ya miaka minne. Tazama maelezo kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 58.**

**Jedwali Na. 58: Mali zilizokabidhiwa kwa serikali ambazo hazijafanyiwa maamuzi**

| Na. | Mali | Idadi ya Mali |
|---|---|---|
| 1 | Magari na Mitambo | 42 |
| 2 | Bunduki ya risasi nyingi | 40 |
| 3 | Vifunga/mihuri | 39 |
| 4 | Risasi | 30 |
| 5 | Transifoma | 18 |
| 6 | Vifaa vya chumba cha udhibiti | 14 |
| 7 | Bastola | 8 |
| 8 | Jenereta | 7 |
| 9 | Mashine ya mkandamizo wa hewa | 7 |
| 10 | Mashine ya kupandisha na kushusha | 7 |
| 11 | Pampu | 7 |
| 12 | Vyuma vya mazoezi | 6 |
| 13 | Vifaa vya mazoezi | 6 |
| 14 | HT/D swichi za bodi | 5 |
| 15 | Vipande vya ziada vya vifaa | 4 |
| 16 | Pikipiki | 3 |

| Na. | Mali | Idadi ya Mali |
|---|---|---|
| 17 | Bunduki | 3 |
| 18 | Nyaya (Kebo) | 2 |
| 19 | Uniti ya Mwanga wa jua | 1 |
| 20 | Ganda la kuwekea risasi | 1 |

***Chanzo****: Taarifa ya Ukaguzi*

Kuahirisha maamuzi kuhusu matumizi au uuzaji wa mali hizi kunazidisha hatari ya kupoteza thamani ya hizo mali na kupelekea kutofaa tena kwa matumizi kutokana na kasi ya ukuaji wa kiteknolojia.

**Ninapendekeza serikali kupitia Wizara ya Fedha, itathmini hali na thamani ya mali hizi na kutoa maagizo ya haraka kuhusu matumizi, uhamisho au uuzaji wake.**

## 14.8 Majengo Chakavu

Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) za mwaka 2024 inamtaka Afisa Masuuli kuandaa na kutekeleza mpango wa matengenezo ya mali za umma kwa utaratibu ulioonyeshwa katika fomu jedwali la nne.

Nilibaini kuwa hospitali tatu na balozi tano zilikuwa na majengo na miundombinu iliyoharibika, kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 59**.

**Jedwali Na. 59: Majengo chakavu katika Hospitali na Balozi**

| Na. | Jina la Ubalozi | Hali ya Jengo |
|---|---|---|
| 1 | Ubalozi wa Tanzania-Lusaka | Jengo la Makazi ya Balozi lina hali isiyoridhishaa |
| 2 | Ubalozi wa Tanzania-Nairobi | Jengo la Makazi ya Balozi lina hali isiyoridhishaa |
| 3 | Ubalozi wa Tanzania-New Delhi | Hali isiyoridhishaa ya jengo la Ubalozi na majengo ya nyumba za makazi za ubalozi |
| 4 | Ujumbe wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Umoja wa Mataifa - New York | Kufungwa kwa Jengo la Balozi la Mount Vernon kutokana na uharibifu (30 Overhill Road, MT. Vernon, NY 10552, BLOCK 2144, LOT 01) -NY |
| 5 | Ubalozi wa Tanzania-Paris | Hali isiyoridhishaa ya majengo ya Balozi na nyumba za makazi |
| | **Hospitali** | **Majengo yaliyoharibika** |
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Dodoma | Wadi 1, Wadi 2, Wadi 16, Wadi 17, Wadi 13 na Wadi 14, Chumba cha mazoezi ya viungo, Maabara, Wadi 5, Wadi 10, Wadi 6, Chumba za tiba za meno, CSSD, Wadi 4, Wadi 12 |

| Na. | Jina la Ubalozi | Hali ya Jengo |
|---|---|---|
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Mbeya | Jengo la Wazazi |
| 3 | Hospitali ya Mirembe | Chumba cha maiti na sehemu ya kufulia nguo |

***Chanzo:*** *Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti za 2023/24*

Uchakavu huo ulichangiwa hasa na bajeti isiyotosha iliyotengwa kwa shughuli za maendeleo ya hospitali na balozi.

Majengo na miundombinu iliyotelekezwa, sakafu zisizo imara, na nyaya zilizo wazi zina hatari kubwa kwa watu wanaoishi na kufanya kazi kwenye mazingira hayo. Utunzaji hafifu wa mali na majengo ya serikali na balozi zetu unaathiri moja kwa moja thamani ya mali zilizozunguka balozi zetu na unaweza, kuchochea shughuli za uhalifu ama kuwa makazi ya wahalifu.

**Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na Wizara ya Fedha, ninapendekeza serikali iendelee kutenga fedha za maendeleo katika bajeti ya kila mwaka ili kukarabati miundombinu na majengo yaliyoharibika au kujenga mpya.**

# SURA YA KUMI NA TANO



# Majukumu ya Utawala na Uangalizi

# MAJUKUMU YA UTAWALA NA UANGALIZI

## 15.1 Utangulizi

Utawala bora na uangalizi thabiti ni nguzo imara za taasisi za umma zinazowajibika, zenye uwazi na ufanisi. Miundo ya utawala huweka mwelekeo na kufafanua aina ya uongozi, huku uangalizi ukihakikisha utii wa sheria, sera, na taratibu bora. Kwa pamoja, huimarisha uwajibikaji, hudumisha imani ya umma, na kuboresha usimamizi na mgawanyo wa rasilimali. Zinapotekelezwa kwa ufanisi, mifumo hii huongeza utendaji kwa kufafanua wazi majukumu na wajibu, huku zikihakikisha uzingatiaji wa viwango vilivyowekwa.

Sura hii inawasilisha matokeo ya tathmini yangu kuhusu majukumu ya utawala na uangalizi katika wizara, idara, na wakala za serikali. Inaangazia maeneo makuu matatu: uundaji na utekelezaji wa miundo ya utawala, mgawanyo wa mamlaka na majukumu, pamoja na utekelezaji wa majukumu ya uangalizi. Aidha, sura hii inabainisha maeneo yanayohitaji maboresho na inatoa mapendekezo mahsusi.

## 15.2 Tathmini ya Majukumu ya Utawala

Utawala bora huanzia kwenye bodi imara za usimamizi. Miundo muhimu kama vile bodi za usimamizi, kamati za ukaguzi, vitengo vya ukaguzi wa ndani, na kamati za usimamizi wa vihatarishi ina mchango mkubwa katika kuhakikisha utoaji mzuri wa huduma, maamuzi sahihi, uwajibikaji, na uzingatiaji wa sheria na kanuni. Bodi hizi zinapaswa kuundwa kwa mujibu wa sheria, kuteuliwa ipasavyo, na kufanya kazi kikamilifu. Upungufu wowote katika uundwaji au utendaji wake unaweza kudhoofisha utawala na kuathiri uwezo wa taasisi kufanikisha malengo yake.

Tathmini yangu kuhusu miundo ya utawala na bodi imebaini upungufu ufuatao:

### 15.2.1 Kutokuwapo kwa Bodi za Usimamizi

Licha ya matakwa ya kisheria yanayohitaji kuundwa kwa bodi za usimamizi kama vile bodi za wakurugenzi, bodi za wadhamini, mabaraza ya usimamizi, au bodi za ushauri za wizara, taasisi 17 hazijaunda bodi hizo. Hali hii inazifanya taasisi husika kuendesha shughuli zake bila uangalizi unaostahili. Orodha ya taasisi zenye upungufu huu imeoneshwa katika **Jedwali Na. 60**

**Jedwali Na. 60: Taasisi Zisizo na Bodi za Usimamizi**

| Na. | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Chunya |
| 2 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Gairo |
| 3 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Itumba Isongole |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Kilindoni |
| 5 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Kishapu |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Loliondo |
| 7 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Ludewa |
| 8 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Maganzo |
| 9 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Mbinga |
| 10 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Namanyere |
| 11 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Namtumbo |
| 12 | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (NFA) |
| 13 | Kituo cha Afya cha Police |
| 14 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Songe |
| 15 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Tunduru |
| 16 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Turiani |
| 17 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Utete |

*Chanzo*: *Taarifa ya Ukaguzi*

### 15.2.2 Bodi za Usimamizi Zilizomaliza Muda Wake

Aidha, nilibaini kuwa bodi za usimamizi za taasisi sita zilikuwa zimemaliza muda wake wa uteuzi bila kuteuliwa bodi mpya. Hali hii ilisababisha taasisi husika kuendelea kujiendesha bila usimamizi madhubuti. Taasisi hizo zimebainishwa katika **Jedwali Na. 61.**

**Jedwali Na. 61: Taasisi zenye Bodi Zilizokwisha Muda wake**

| Na. | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1 | Chuo cha Mafunzo ya Misitu (FTI) |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala |
| 3 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Mwanhuzi |
| 4 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira - Namanyere |
| 5 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi |
| 6 | Chuo cha Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi (PWTI) |

*Chanzo*: *Taarifa ya Ukaguzi*

### 15.2.3 Kuwapo kwa Idadi Ndogo ya Wajumbe katika Tume ya Marekebisho ya Sheria Tanzania

Ukaguzi wangu wa Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Tanzania ulibaini kutokuzingatiwa kwa masharti ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Tanzania ya mwaka 1980 kinachotaka tume hiyo kuundwa na mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine wasiopungua wanne.

Nilibaini kuwa, hadi wakati wa Ukaguzi mwezi Novemba 2024, Tume ilikuwa na Mwenyekiti pamoja na wajumbe wawili pekee, hivyo kusababisha upungufu wa wajumbe wawili. Ninachukulia kwamba upungufu huu unaweza kuathiri utendaji wa Tume na uwezo wa kufikia akidi ya vikao endapo mjumbe mmoja atakosekana, kwani akidi inayohitajika ni angalau wajumbe watatu.

Changamoto hizi, zikiwamo ukosefu wa bodi na kamati pamoja na upungufu wa wajumbe, zinatokana na ucheleweshaji wa teuzi na upungufu wa rasilimalifedha kwa uendeshaji wa bodi hizo.

Ni maoni yangu kuwa kutokuwapo kwa bodi, upungufu wa wajumbe, na ucheleweshaji wa teuzi kunadhoofisha usimamizi madhubuti, ufanisi wa maamuzi ya kimkakati, na utendaji wa taasisi kwa ujumla.

**Ninapendekeza kwamba Maafisa Masuuli, kwa kushirikiana na mamlaka za uteuzi, waharakishe mchakato wa kuanzishwa kwa bodi na uteuzi wa wajumbe wa bodi hizo kwa taasisi hizi ili kuimarisha usimamizi. Kwa Mamlaka za Maji ambazo hazina rasilimali za kutosha kugharamia uendeshaji wa bodi, Wizara inaweza kufikiria kubadilisha muundo wa taasisi hizo ili kuwezesha uwepo wa bodi zinazotoa miongozo ya kimkakati na kuhakikisha uwajibikaji.**

### 15.2.4 Upungufu katika Uteuzi na Muundo wa Baraza la Kitaifa la Uongozi la Mpango wa Kujitathmini kwa Nchi za Afrika (APRM) - Tanzania

Ukaguzi wa Mpango wa Kujitathmini kwa Nchi za Afrika (APRM) - Tanzania ulibaini kasoro katika muundo wa Baraza la Kitaifa la Uongozi, lililoanzishwa chini ya Ibara ya 16 ya Mkataba wa APRM. Awali, baraza hilo liliundwa na wajumbe 20 walioteuliwa mwaka 2006. Hata hivyo, kufikia sasa, baraza limebakiwa na wajumbe wanne, bila uteuzi mpya wa kujaza nafasi zilizotokana na vifo na kustaafu kwa wajumbe wa awali.

Aidha, nilibaini kuwa wajumbe waliobaki wamehudumu kwa miaka 18 bila ukomo wa muda wa kuhudumu, kwani barua zao za uteuzi hazikubainisha muda wa kuhudumu. Vilevile, hakuna hadidu za rejea zinazosimamia uteuzi wa wajumbe, muda wa kuhudumu, akidi, na matakwa ya kimuundo. Kutokana na hilo, haifahamiki idadi sahihi ya wajumbe wanaopaswa kuwamo katika baraza na akidi inayotakiwa kwa vikao. Licha ya umuhimu wake katika kusimamia utulivu wa kisiasa, ukuaji wa uchumi, na maendeleo endelevu, APRM Tanzania haijapewa kipaumbele kinachostahili, hali ambayo imedhoofisha uwezo wake wa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Ni maoni yangu kuwa kasoro hizi zinadhoofisha utendaji wa Baraza na uwezo wa APRM Tanzania kufikia malengo yake.

**Ninapendekeza Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kushirikiana na APRM Tanzania, iweke hadidu za rejea zitakazosimamia uendeshaji wa Baraza la Kitaifa la Uongozi na kuhakikisha uteuzi wa idadi stahiki ya wajumbe.**

### 15.2.5 Kutokuwapo kwa Kamati za Ukaguzi

Kama sehemu ya mapitio yangu, nilibaini kwamba licha ya matakwa ya Kanuni 30 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inayotaka taasisi za umma kuwa na kamati za ukaguzi zitakazosimamia mifumo ya udhibiti wa ndani, kupitia mipango ya ukaguzi na ripoti za utendaji, pamoja na kusimamia mchakato wa tathmini ya vihatarishi, taasisi tano zilikuwa hazina kamati za ukaguzi. Taasisi hizi ni: Kampuni ya Ulinzi ya SHIMA, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira - Makete, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songwe, Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori ya Pasiansi, na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bukoba.

### 15.2.6 Kutokuwapo kwa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Licha ya umuhimu wa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika kutathmini mifumo ya udhibiti wa ndani, utekelezaji wa sheria, na kusimamia vihatarishi, nilibaini taasisi tano ambazo hazikuanzisha vitengo vya ukaguzi wa ndani. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Maji ya Kilindoni, Mamlaka ya Maji ya Mugango Kiabakari, Kampuni ya Ulinzi ya SHIMA, Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi (TPFCS), na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira – Tunduma.

Upungufu huu unatokana na kuchelewa kwa uteuzi wa wajumbe wa kamati za ukaguzi, upungufu wa rasilimalifedha, na kutokupewa kipaumbele kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani.

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa kamati za ukaguzi na vitengo vya ukaguzi wa ndani kunapunguza uwezo wa kushughulikia upungufu unaojitokeza katika usimamizi wa rasilimalifedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, na kupunguza uwezo wa taasisi katika kufanya tathmini huru ya mifumo ya udhibiti na uzingatiaji wa sheria mbalimbali. Aidha, kunaathiri utendaji wa bodi za utawala katika kutekeleza majukumu yao.

**Ninapendekeza maafisa masuuli waanzishe kamati za ukaguzi na vitengo vya ukaguzi wa ndani ili kuimarisha usimamizi wa fedha, kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani, na kuzisaidia bodi za usimamizi katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi kwa ufanisi.**

### 15.2.7 Kutokuwapo kwa Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi

Katika sehemu ya usimamizi, na kwa mujibu wa Aya ya 2.4 ya Mwongozo wa Mwaka 2023 wa Uandaaji na Utekelezaji wa Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma, taasisi za umma zinatakiwa kuanzisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa taasisi 19 hazikutayarisha wala kutekeleza mifumo hiyo. Kutokuweka kipaumbele kwa hatua za udhibiti wa vihatarishi kumesababisha kutokuwapo kwa mifumo hii. Orodha ya taasisi hizo imo katika **Jedwali Na. 62.**

**Jedwali Na. 62: Taasisi zisizo na Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi**

| Na. | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1 | Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF) |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma |
| 3 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita |
| 5 | Bodi ya Bonde la Maji - Ziwa Nyasa |
| 6 | Wizara ya Kilimo |
| 7 | Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo |
| 8 | Chombo cha Watoahuduma ya Maji Mkongoro II |
| 9 | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) |
| 10 | Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza |
| 11 | Jeshi la Magereza |
| 12 | Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji |
| 13 | Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini |
| 14 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga |
| 15 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Bombo Tanga |
| 17 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika |
| 18 | Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) |
| 19 | Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi |

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi*

Kukosekana kwa mifumo ya usimamizi wa vihatarishi kunaweza kuziweka taasisi hizo katika hatari zisizodhibitiwa, na kusababisha hasara za kifedha, kuathiri utendaji kazi, na kukosa uwezo wa kufikia malengo ya kimkakati.

**Ninapendekeza kuwa taasisi hizi ziandae na kutekeleza mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kutambua vihatarishi na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.**

## 15.3 Tathmini ya Ukasimishaji wa Mamlaka na Majukumu kwa Menejimenti

Mbali na kuanzishwa kwa bodi za usimamizi, utawala bora unategemea mgawanyo mzuri wa majukumu kwa menejimenti na maafisa watendaji. Maafisa

hawa husimamia shughuli za kila siku, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utoaji wa huduma bora na kuzingatia sera na kanuni zilizowekwa. Mgawanyo sahihi wa majukumu unawezesha bodi za usimamizi kujikita katika kufanya maamuzi ya kimkakati na kusimamia ufanisi katika utendaji.

Katika tathmini ya utawala na usimamizi, nilipitia uteuzi wa watendaji wakuu pamoja na utekelezaji wa majukumu waliyokasimiwa. Tathmini yangu ya ukasimishaji wa majukumu ilibaini upungufu ufuatao:

### 15.3.1 Kutokuwapo kwa Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka 14 za Majisafi na Usafi wa Mazingira

Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 kinaelekeza kuwa kila Mamlaka ya Maji iwe na mkurugenzi mtendaji aliyeteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya maji kusimamia shughuli za kila siku za mamlaka.

Hata hivyo, ukaguzi wa mamlaka 82 za majisafi na usafi wa mazingira ulibaini kuwa mamlaka 14 (17%) zinafanya kazi bila wakurugenzi watendaji, huku nafasi hizi zikikaimiwa na maafisa wengine. Zaidi ya hayo, mamlaka 10 kati ya 14 hazikuwa na bodi za wakurugenzi, jambo linaloongeza ukubwa wa tatizo katika utendaji. Orodha ya mamlaka hizo ipo katika **Jedwali Na. 63**.

**Jedwali Na. 63: Orodha ya Mamlaka zisizo na Wakurugenzi Watendaji**

| Na | Jina la Mamlaka ya Maji | Kuwapo kwa Wakurugenzi Watendaji | Kuwapo kwa Bodi ya Wakurugezi |
|---|---|---|---|
| 1 | Itumba Isongole | x | x |
| 2 | Kibaya | x | |
| 3 | Kilindoni | x | x |
| 4 | Kilwa Masoko | x | |
| 5 | Kishapu | x | x |
| 6 | Loliondo | x | x |
| 7 | Ludewa | x | x |
| 8 | Lushoto | x | |
| 9 | Maganzo | x | x |
| 10 | Namanyere | x | x |
| 11 | Namtumbo | x | x |
| 12 | Rujewa | x | |
| 13 | Songe | x | x |
| 14 | Turiani | x | x |

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi*

Kutokuwapo kwa wakurugenzi watendaji katika mamlaka hizi kumechangiwa na upungufu wa makusanyo katika mamlaka hizo, hivyo kushindwa kugharamia matumizi yanayojumuisha stahiki zinazohitajika katika nafasi hizo. Pengo hili la

uongozi pamoja na kutokuwapo kwa bodi za usimamizi huweza kusababisha usimamizi duni, hatimaye kuathiri utendaji na uendelevu wa Mamlaka hizo.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji kuteua wakurugenzi watendaji wa mamlaka hizi na kuziwezesha kifedha na kwa rasilimaliwatu ili kuimarisha utendaji na ukusanyaji wa mapato, hivyo kuhakikisha uendelevu wa majukumu yao.**

### 15.3.2 Kutokuwapo kwa Maafisa Mashtaka wa Wilaya katika Wilaya 31

Kifungu cha 5(3) cha Sheria ya Huduma za Mashtaka ya Taifa, sura ya 430 kinamtaka Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuteua maafisa sheria kusimamia masuala ya mashtaka katika kila mkoa na wilaya, watakaojulikana kama maafisa mashtaka wa mikoa na wilaya. Maafisa hawa pia watatumika kama wenyeviti wa Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzisha ofisi za mashtaka katika wilaya 108 pekee kati ya 139, sawa na 77%. Hali hii inazifanya wilaya 31, sawa na 23%, kutokuwa na maafisa mashtaka wa wilaya na hivyo kuathiri usimamizi wa haki kwa wananchi. Ukaguzi ulibaini kuwa upungufu huu unatokana na uhaba wa rasilimalifedha na watu, jambo ambalo limekwamisha uanzishwaji wa ofisi za mashtaka katika wilaya zilizobaki.

Kutokuwapo kwa maafisa hao kunaathiri utoaji wa huduma kwa umma, kuchelewesha mashtaka ya jinai, kuongeza mlundikano wa kesi, kudhoofisha uwakilishi wa serikali katika mahakama za wilaya, na kuathiri utendaji kazi wa Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, itoe kipaumbele katika kuteua maafisa mashtaka wa wilaya katika wilaya zilizobaki na kutenga rasilimali muhimu ili kuimarisha huduma za mashtaka katika ngazi ya wilaya.**

## 15.4 Tathmini ya Majukumu ya Usimamizi

Ikiwa miundo ya utawala inaweka msingi wa uwajibikaji na uelekeo wa kimkakati, ufanisi wake unategemea usimamizi mzuri ulio na ufanisi, ikiwamo kufanya vikao vya kisheria. Kwa kuzingatia umuhimu wa bodi, kamati za ukaguzi, na vitengo vya ukaguzi wa ndani katika kusimamia uadilifu, utendaji kazi wao kupitia vikao vya mara kwa mara unachangia kuboresha usimamizi.Katika kutathmini majukumu ya usimamizi, nilibaini upungufu ufuatao:

### 15.4.1 Kutokufanyika kwa Idadi Inayotakiwa ya Vikao vya Bodi

Ukaguzi ulibaini kuwa bodi za taasisi 10 hazikufanya vikao kwa idadi inayohitajika kisheria, kama ilivyobainishwa katika taratibu zao za utawala. Upungufu huu unadhoofisha uwezo wa bodi katika kutoa usimamizi bora na miongozo ya kimkakati. Idadi ya vikao vilivyofanywa na bodi za taasisi hizo imebainishwa katika **Jedwali Na. 64**.

**Jedwali Na. 64: Taasisi zenye Idadi Ndogo ya Vikao vya Bodi**

| Na. | Jina la Taasisi | Vikao vya Bodi kwa mwaka 2023/24 |
|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Amana | Bodi ya Hospitali haikufanya vikao vyote vinne vilivyohitajika. |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | Bodi ya Hospitali ilifanya vikao viwili tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 3 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa | Bodi ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 4 | Bonde la Ziwa Tanganyika | Bodi ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 5 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbulu | Hakukuwa na vikao vya bodi kutokana na kuchelewa kwa uteuzi wa wajumbe wa bodi uliofanyika mwezi Aprili 2024. |
| 6 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Bodi ya Ushauri ya Mfuko wa Mikopo ya Nyumba haikufanya kikao chochote licha ya kutakiwa kufanya vikao vinne. |
| 7 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugango-Kiabakari | Bodi ilikaa vikao vitatu pekee kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 8 | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa | Kamati ya Uongozi ya Mamlaka haikufanya vikao vya robo mwaka vilivyohitajika katika mwaka. |
| 9 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini | Bodi ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 10 | Kituo cha Jemolojia Tanzania | Bodi ya Ushauri ya Wizara ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi*

### 15.4.2 Kutokufanyika kwa Idadi Inayohitajika ya Vikao vya Kamati za Ukaguzi

Licha ya Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kuzitaka kamati za ukaguzi kukutana kila robo mwaka, ukaguzi umebaini kuwa kamati za ukaguzi za taasisi tisa hazikutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kutofanya vikao vinavyotakiwa vya kila robo mwaka. Orodha ya taasisi husika na idadi ya vikao imetolewa katika **Jedwali Na. 65**.

**Jedwali Na. 65: Taasisi zenye Upungufu katika Kamati za Ukaguzi**

| Na | Jina la Taasisi | Upungufu katika Kamati za Ukaguzi |
|---|---|---|
| 1 | Bodi ya Maji ya Bonde la Ndani | Kamati ya Ukaguzi haikufanya vikao vyake vya kila robo mwaka. |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni | Kamati ya Ukaguzi ya Hospitali ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 3 | Wizara ya Maji | Kamati ya Ukaguzi ya Wizara ilifanya vikao vitatu tu kati ya vinne vilivyohitajika. |
| 4 | Hospitali ya Afya ya Akili ya Mirembe | Kamati ya Ukaguzi ya Hospitali haikufanya vikao vyake vya kila robo mwaka. |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mount Meru | Kamati ya Ukaguzi ya Hospitali ilifanya vikao viwili tu kati ya vinne vilivyohitajika na haikuitia tathmini ya usimamizi wa vihatarishi. |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga | Kamati ya Ukaguzi ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika na haikupitia taarifa za fedha kabla ya kutolewa. |
| 7 | Wakala wa Majengo Tanzania | Kamati ya Ukaguzi ya Wakala ilifanya kikao kimoja tu badala ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 8 | Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) | Kamati ya Ukaguzi ya Tume ilifanya kikao kimoja tu kati ya vikao vinne vilivyohitajika. |
| 9 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wanging'ombe | Kamati ya Ukaguzi ya Mamlaka haikufanya vikao vya kila robo mwaka kama inavyotakiwa. |

***Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi*

Upungufu huu umesababishwa na ucheleweshaji wa uteuzi, kushindwa kufikia akidi ya vikao, na uhaba wa fedha za kugharamia shughuli za kamati na bodi.

Kwa maoni yangu, kutofanyika kwa vikao kama inavyotakiwa kunaathiri ufanisi wa bodi na kamati katika kudhibiti mifumo ya ndani, kufuatilia ripoti za ukaguzi, kusimamia vihatarishi, kufanya maamuzi sahihi ya kimkakati, na kutoa miongozo. Hali hii inaweza kusababisha kushuka kwa utendaji wa taasisi husika.

**Ninapendekeza bodi na kamati za ukaguzi zitimize kikamilifu wajibu wao kwa kufanya vikao vinavyotakiwa ili kuimarisha utawala bora, huku maafisa masuuli wakihakikisha utekelezaji wa ratiba za vikao unazingatiwa ipasavyo.**

### 15.4.3 Upungufu katika Utekelezaji wa Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi

Licha ya matakwa ya Muongozo wa mwaka 2023 wa Kuandaa na Kutekeleza Mifumo ya Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma unaozitaka taasisi hizo kuanzisha na kuimarisha mchakato wa usimamizi wa vihatarishi, ukaguzi wangu ulibaini upungufu katika utekelezaji wake ndani ya taasisi 18. Upungufu huu ni pamoja na ukosefu wa vitengo maalumu vya usimamizi wa vihatarishi,

kutofanyika kwa tathmini za vihatarishi, kutokuwapo kwa rejista za vihatarishi au matumizi ya rejista ambazo hazijahuishwa, pamoja na kushindwa kufanya ufuatiliaji wa vihatarishi kwa vipindi vinavyohitajika. Upungufu huu umebainishwa katika **Kiambatisho Na. XX**.

Upungufu huu unatokana na kutopewa kipaumbele na utekelezaji usioridhisha wa usimamizi wa vihatarishi. Hali hii inaweza kuathiri ufanisi wa taasisi, kudhoofisha mifumo ya udhibiti wa fedha, na kuongeza hatari ya ubadhirifu pamoja na usimamizi duni wa rasilimali.

**Ninapendekeza yafuatayo kwa taasisi hizi: ziimarishe usimamizi wa vihatarishi kwa kuanzisha vitengo maalumu; zifanye tathmini za vihatarishi mara kwa mara; zihuishe rejista za vihatarishi, na zitekeleze mifumo endelevu ya ufuatiliaji na tathmini. Menejimenti inapaswa kutenga rasilimali za kutosha na kuteua wasimamizi mahususi ili kuimarisha juhudi za kupunguza athari zinazoweza kutokea.**

# SURA YA KUMI NA SITA



# siasa

## Vyama vya Siasa

# VYAMA VYA SIASA

## 16.1 Utangulizi

Vyama vya siasa vina jukumu muhimu katika kukuza demokrasia, utawala, na utulivu wa kisiasa. Uendeshaji wa vyama vya siasa unahitaji usimamizi mzuri wa fedha, kufuata miundo ya utawala, na ukidhi wa mahitaji ya kisheria ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, na ufanisi. Mifumo madhubuti ya uangalizi ni muhimu katika kudumisha uadilifu wa kifedha, kudumisha mifumo ya udhibiti wa ndani, na kulinda mali za vyama.

Katika ukaguzi wa vyama 19 vya siasa kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini masuala muhimu yanayohitaji kuchukuliwa hatua. Masuala haya yameelezwa kwa kina katika sehemu hii:

## 16.2 Taarifa za Kifedha

### 16.2.1 Kuchelewa Kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu cha 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, sura ya 258 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinataka vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka.

Ukaguzi wangu ulibaini, vyama viwili vya siasa, Chama cha Kidemokrasia cha Muungano (UDP) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), vilichelewa kuwasilisha taarifa za fedha kwa makadirio ya kati ya siku 29 hadi 34. Uongozi wa vyama vya siasa ulieleza kuwa uchelewaji huo ulitokana na kuchelewa kwa mchakato wa uandaaji wa taarifa za fedha.

**Ninapendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa achukue hatua stahiki kuhakikisha kuwa vyama vya UDP na CHADEMA vinawasilisha taarifa zao za fedha kufikia tarehe 30 Septemba kila mwaka.**

## 16.3 Usimamizi wa Mapato na Bajeti

### 16.3.1 Mapato Kiasi cha Sh. Milioni 133.26 Hayakukusanywa

Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa (ya mwaka 2019) kinasema kuwa mapato na rasilimali za vyama vya siasa vilivyosajiliwa yanatokana na ada za uanachama, michango ya hiari, mapato ya uwekezaji, ruzuku ya serikali, na misaada kutoka kwa vyanzo vingine vyovyote.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa vyama kumi vya siasa vilipanga kukusanya jumla ya Sh. milioni 236.87 kutoka kwa michango ya wanachama na ruzuku. Kati ya hizo, Sh. milioni 103.61 zilikusanywa sawa na 44% na kushindwa kukusanya kiasi cha Sh. milioni 133.26 (56%). Upungufu mkubwa zaidi ulitokea Chama cha Kidemokrasia (DP) (Sh. milioni 52.45, sawa na 95% hazikukusanywa) na Chama cha Wafanyakazi Tanzania (TLP) (Sh. milioni 10.00, sawa na 95% hazikukusanywa). Maelezo yanaoenekana kwenye **Jedwali Na. 66.**

**Jedwali Na. 66: Vyama vya Siasa Vilivyokusanya Mapato Pungufu**

| Na. | Chama cha Siasa | Bajeti (Sh.) | Kiasi Kilichokusanywa (Sh.) | Upungufu (Sh.) | % ya Kutofikia Ukusanyaji (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Democratic Party (DP) | 55,310,000 | 2,860,769 | 52,449,231 | 95 |
| 2 | Alliance for Democratic Change (ADC) | 70,000,000 | 49,050,000 | 20,950,000 | 30 |
| 3 | Chama Cha Demokrasia Makini (DM) | 25,800,000 | 8,365,500 | 17,434,500 | 68 |
| 4 | Union for Multiparty Democracy (UMD) | 30,000,000 | 16,875,000 | 13,125,000 | 44 |
| 5 | Tanzania Labor Party (TLP) | 10,500,000 | 500,000 | 10,000,000 | 95 |
| 6 | Alliance for Africa Farmers Party | 14,924,000 | 6,179,000 | 8,745,000 | 59 |
| 7 | Chama cha Ukombozi wa Umma | 11,500,000 | 7,675,000 | 3,825,000 | 33 |
| 8 | Chama cha Kijamii (CCK) | 3,600,000 | 62,400 | 3,537,600 | 98 |
| 9 | African Democratic Alliance (ADA), TADEA | 7,650,000 | 5,753,496 | 1,896,504 | 25 |
| 10 | National League for Democracy (NLD) | 7,590,000 | 6,290,000 | 1,300,000 | 17 |
| **Jumla** | | **236,874,000** | **103,611,165** | **133,262,835** | |

*Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi*

Hii ilitokana na wanachama wa vyama vya siasa kushindwa kulipa ada zao za usajili za kila mwezi na ufuatiliaji usioridhisha wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kutohuishwa kwa taarifa za wanachama kwenye rejista. Kushindwa

kukusanya mapato kwa mujibu wa bajeti kunavikwamisha vyama vya siasa kutimiza shughuli zao zilizopangwa na kufikia malengo yao ya kisiasa.

**Ninapendekeza kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuvisimamia vyama vya siasa kuhuisha taarifa za wanachama kwenye rejista na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuwawezesha wanachama kuwasilisha ada zao za usajili wa kila mwezi.**

### 16.3.2 Michango ya Wanachama yenye Thamani ya Sh. Milioni 31.7 Haikuwasilishwa katika Akaunti za Benki za Vyama vya Siasa

Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, sura ya 258 (iliyorekebishwa mwaka 2019), kinataka kila chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kisheria kufungua akaunti ya benki ya chama ambayo mapato yote yanayopatikana kutokana na ada za uanachama, michango ya hiari, misaada, ruzuku, au mapato ya uwekezaji yanapaswa kuwasilishwa benki.

Licha ya pendekezo langu katika miaka iliyopita, nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2023/24 vyama vinne vya siasa vilikusanya jumla ya Sh. milioni 31.7 bila kuwasilisha katika akaunti za benki za vyama husika. **Jedwali Na. 67** linaonesha orodha ya vyama vya siasa ambavyo havikuwasilisha mapato kwenye akaunti za benki.

**Jedwali Na. 67: Vyama vya Siasa ambavyo Havikuwasilisha kwenye Akaunti za Benki Michango ya Wanachama Wake**

| Na. | Chama cha Siasa | Kiasi Kisichowasilishwa Benki (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | National Convention for Construction and Reform (NCCR Mageuzi) | 26,226,000 |
| 2. | Chama cha Kijamii (CCK) | 2,882,400 |
| 3. | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA) | 2,175,000 |
| 4. | National League for Democracy (NLD) | 460,000 |
| **Jumla** | | **31,743,400** |

***Chanzo:*** *Vitabu vya Fedha na Taarifa za Benki*

Hali hii ilitokana na mazoea ya muda mrefu ya kutumia fedha zinazokusanywa na kuepuka gharama za uendeshaji wa akaunti za benki, hivyo kusababisha akaunti za benki kutotumika. Kushindwa kuwasilisha fedha za makusanyo ya michango ya wanachama katika akaunti za benki kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha. Pia, kunaweza kusababisha hali ya kutofautiana kwa kumbukumbu za kihasibu. Zaidi, kunaondoa uwazi katika utendaji.

**Ninapendekeza kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe makusanyo ya fedha yanawasilishwa kwa wakati katika akaunti za benki za vyama vya siasa.**

### 16.3.3 Kutolipwa kwa Deni la Muda Mrefu la Sh. Milioni 135

Kifungu cha 5 cha makubaliano ya mikopo kati ya NCCR-Mageuzi na wakopeshaji mbalimbali kilitaka chama kurejesha fedha bila riba ndani ya miezi 28.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kati ya tarehe 15 Februari 2020 na 18 Julai 2020, NCCR-Mageuzi iliingia mikataba na wakopeshaji watano, ikiwa na jumla ya Sh. milioni 135 kwa ajili ya kusaidia gharama za maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Hata hivyo, mikopo hiyo haijarejeshwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (miezi 60).

Hii ilisababishwa na uhaba wa kifedha unaokikabili chama cha NCCR-Mageuzi. Kushindwa kulipa mikopo ya muda mrefu kunakiuka masharti ya makubaliano, hivyo kuharibu sifa ya kukopeshwa na kupunguza uwezo wa kupata mikopo mingine baadae.

**Ninapendekeza kuwa chama cha NCCR-Mageuzi kitafute fedha na kuandaa mpango wa ulipaji wa deni la Sh. milioni 135. Pia, kifanye majadiliano na wakopeshaji kuhusu kurekebisha masharti ya malipo.**

## 16.4 Utawala

### 16.4.1 Nafasi za Viongozi wa Juu wa Vyama vya Siasa Zilizo Wazi

Ibara ya 27 ya Katiba ya NCCR-Mageuzi ya mwaka 2020 inawatambua Makamu Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa kutoka Zanzibar na Katibu Mkuu Msaidizi kutoka Bara kama viongozi wa juu wa chama ambao husimamia shughuli za chama na kusaidia majukumu ya Katibu Mkuu.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa chama cha NCCR–Mageuzi kilikuwa na nafasi za wazi za Makamu Mwenyekiti kutoka Zanzibar na Katibu Mkuu Msaidizi kutoka Bara tangu Agosti 2023. Hii ilisababishwa na viongozi waliokuwepo kuteuliwa na kupangiwa majukumu mengine, huku wakiacha nafasi zao katika chama zikiwa wazi.

Uchelewaji wa muda mrefu wa kuitisha vikao vya kamati kuu kwa ajili ya kuteua viongozi umesababisha ukosefu wa uongozi madhubuti na kuchelewesha maamuzi muhimu na muelekeo ndani ya chama. Kukosekana kwa viongozi wa juu wa chama kunahatarisha uchelewaji wa kufanya maamuzi, kunapunguza ari

ya kazi na kunaathiri ufanisi wa shughuli ambayo inaathiri uwezo wa chama katika kufikia malengo yake.

**Ninapendekeza kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe NCCR-Mageuzi inateua Katibu Mkuu Msaidizi kutoka Tanzania Bara na Makamu Mwenyekiti kutoka Zanzibar bila kuchelewa zaidi.**

### 16.4.2 Kutokufanyika kwa Mikutano ya Kisheria ya Vyama vya Siasa

Kanuni ya 24(1) ya Kanuni za Baraza la Vyama vya Siasa ya mwaka 2019 inavipa mamlaka vyama vya siasa kufanya mikutano miwili, ya Halmashauri Kuu na miwili ya Kamati Kuu ya Taifa ili kuhakikisha utawala bora na maamuzi ya kimkakati.

Ukaguzi ulibaini kuwa vyama vya Demokrasia Makini (DM) na National Reconstruction Alliance (NRA) vilishindwa kufanya mikutano ya Halmashauri Kuu na Kamati Kuu ya Taifa.Hii ilisababishwa na uhaba wa fedha za kuendeshea mikutano.

Kushindwa kufanya mikutano ya kisheria kunachelewesha mchakato wa kutoa maamuzi muhimu ya vyama, hivyo kuathiri mfumo wa utawala, mipango ya kimkakati na ufanisi wa shughuli za vyama.

**Ninapendekeza kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe kuwa vyama vya Demokrasia Makini (DM) na National Reconstruction Alliance (NRA) vinatenga fedha za kutosha kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya kisheria kwa wakati.**

### 16.4.3 Kutokuteuliwa kwa Wajumbe wa Bodi za Wadhamini

Bodi ya Wadhamini wa vyama vya siasa kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 21(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, sura ya 318 (iliyorekebishwa mwaka 2019), inasimamia mali, uwekezaji, na shughuli zozote za biashara za chama. Usajili wa Bodi ya Wadhamini unazingatia Sheria ya Usajili wa Bodi ya Wadhamini, sura ya 318, ambayo husimamiwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa vyama vya Alliance for Democratic Change (ADC) na Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) havijawahi kusajili Bodi ya Wadhamini wala kuwasilisha taarifa za matumizi na kulipa ada ya mwaka, hii inakiuka matakwa ya Kifungu cha 2 cha Sheria ya Usajili wa Bodi ya Wadhamini, sura ya 318, kinachohitaji Bodi ya Wadhamini kusajiliwa na RITA. Vile vile, Chama cha TLP kilishindwa kuwasilisha taarifa za matumizi kwa Wakala wa

Usajili, Ufilisi na Udhamini licha ya kutozwa Sh. 108,000 mnamo Oktoba 2020 kwa kutokidhi matakwa ya sheria kwa miaka iliyopita.

Aidha, nilibaini kuwa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF) iliisha muda wake tangu tarehe 11 Juni 2022 na wajumbe wapya hawakuteuliwa, hii inakiuka Ibara ya 101 (1) ya Katiba ya CUF ya mwaka 2019 inayotaka Bodi ya Wadhamini kuteuliwa na Baraza Kuu la Taifa kwa muda wa miaka mitano. Uchelewaji huu ulitokana na uhaba wa fedha za kuendeshea mikutano ya Baraza Kuu la Taifa.

Kushindwa kusajili Bodi ya Wadhamini wa vyama vya ADC na CHAUMMA kunaathiri utawala bora na kuleta athari za kisheria, wakati kutoteua kwa Bodi ya Wadhamini wa CUF kumeongeza hatari za matumizi yasiyoidhinishwa na kutokidhi matakwa ya katiba yake.

**Ninapendekeza kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa asimamie:**

a. **Vyama vya siasa vya ADC na CHAUMMA kuchukua hatua za haraka kukamilisha usajili wa Bodi za Wadhamini RITA na kuwasilisha taarifa za matumizi kwa wakati pamoja na kulipa ada ya mwaka ili kutii matakwa ya kisheria; na**
b. **CUF kupata fedha za kufanya mkutano wa Baraza Kuu la Taifa ili kuteua Bodi mpya ya Wadhamini.**

## 16.5 Usimamizi wa Mali

### 16.5.1 Usajili wa Mali za Vyama vya Siasa kutumia Majina ya Watu Binafsi

Ibara ya 26(7)(a) ya Katiba ya NCCR Mageuzi ya mwaka 2020 inaipa majukumu Bodi ya Wadhamini kusimamia mali zote za Chama, zisizohamishika na zinazohamishika.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Kiwanja Namba 37 chenye jengo kilichopo Ilala, Dar es Salaam, kilichonunuliwa mwaka 1998 na chama cha NCCR Mageuzi chenye thamani ya pamoja na jengo Sh. milioni 145.06, kilisajiliwa kwa jina la mtu binafsi badala ya Bodi ya Wadhamini, licha ya mapendekezo yangu ya awali kuhusu usajili sahihi wa mali. Zaidi ya hayo nilibaini kuwa chama cha CUF kina magari 10 yenye thamani ya Sh. milioni 274.93, yaliyonunuliwa kati ya mwaka 2012 na 2015 lakini magari haya yalisajiliwa kwa majina mbalimbali ya watu binafsi.

Hii ilisababishwa na changamoto katika mchakato wa usajili na kuleta hatari ya migongano kisheria juu ya umiliki wa mali hizo na kupunguza uwajibikaji. Pia,

inadhoofisha mfumo wa utawala bora wa vyama na kunaweza kuhatarisha utulivu wa kifedha hivyo kuathiri uendelevu wa shughuli zao.

**Ninapendekeza kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe vyama vya NCCR-Mageuzi na CUF vinahamisha umiliki wa mali kutoka kwa watu binafsi kwenda kwa Bodi zao za Wadhamini.**

## Kiambatisho Na. I: Hati za Ukaguzi na Hitimisho la Utekelezaji wa Sheria

| Na. | Jina la Taasisi/Ripoti | Hati 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu Na. 1: Deni la Serikali | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 2 | Fungu Na. 3: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 3 | Fungu Na. 4: Ofisi ya Rais – Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka (RAMD) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 4 | Fungu Na. 5: Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 5 | Fungu Na. 6: Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 6 | Fungu Na. 7: Ofisi ya Msajili wa Hazina | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 7 | Fungu Na. 10: Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 8 | Fungu Na. 11: Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 9 | Fungu Na. 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 10 | Fungu Na. 13: Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 11 | Fungu Na. 14: Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 12 | Fungu Na. 15: Tume ya Usuluhishi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 13 | Fungu Na. 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 14 | Fungu Na. 18: Tume ya UNESCO ya Taifa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 15 | Fungu Na. 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 16 | Fungu Na. 20: Ofisi ya Rais - Ikulu | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 17 | Fungu Na. 21: Hazina | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 18 | Fungu Na. 22: Huduma za Jumla | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 19 | Fungu Na. 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 20 | Fungu Na. 24: Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 21 | Fungu Na. 25: Ofisi ya Waziri Mkuu – Ofisi Binafsi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 22 | Fungu Na. 26: Ofisi ya Makamu wa Rais – Ofisi Binafsi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 23 | Fungu Na. 27: Msajili wa Vyama vya Siasa | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 24 | Fungu Na. 28: Jeshi la Polisi Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 25 | Fungu Na. 29: Jeshi la Magereza | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 26 | Fungu Na. 30: Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 27 | Fungu Na. 31: Ofisi ya Makamu wa Rais | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |

| Na. | Jina la Taasisi/Ripoti | Hati 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 28 | Fungu Na. 32: Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 29 | Fungu Na. 33: Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 30 | Fungu Na. 34: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 31 | Fungu Na. 35: Huduma za Mashtaka ya Taifa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 32 | Fungu Na. 37: Ofisi ya Waziri Mkuu | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 33 | Fungu Na. 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 34 | Fungu Na. 39: Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 35 | Fungu Na. 40: Mahakama | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 36 | Fungu Na. 41: Wizara ya Katiba na Sheria | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 37 | Fungu Na. 42: Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 38 | Fungu Na. 43: Wizara ya Kilimo | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 39 | Fungu Na. 44: Wizara ya Viwanda na Biashara | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 40 | Fungu Na. 46: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 41 | Fungu Na. 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 42 | Fungu Na. 49: Wizara ya Maji | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 43 | Fungu Na. 50: Wizara ya Fedha | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 44 | Fungu Na. 51: Wizara ya Mambo ya Ndani | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 45 | Fungu Na. 52: Wizara ya Afya | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 46 | Fungu Na. 53: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 47 | Fungu Na. 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 48 | Fungu Na. 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 49 | Fungu Na. 58: Wizara ya Nishati | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 50 | Fungu Na. 59: Tume ya Marekebisho ya Sheria | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 51 | Fungu Na. 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 52 | Fungu Na. 62: Wizara ya Uchukuzi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 53 | Fungu Na. 64: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 54 | Fungu Na. 65: Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu (PMO-LYED) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 55 | Fungu Na. 66: Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 56 | Fungu Na. 67: Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 57 | Fungu Na. 68: Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 58 | Fungu Na. 69: Wizara ya Maliasili na Utalii | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |

| Na. | Jina la Taasisi/Ripoti | Hati 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 59 | Fungu Na. 91: Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 60 | Fungu Na. 92: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 61 | Fungu Na. 93: Idara ya Uhamiaji Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 62 | Fungu Na. 94: Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Umma | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 63 | Fungu Na. 96: Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 64 | Fungu Na. 98: Wizara ya Ujenzi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 65 | Fungu Na. 99: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 66 | Fungu Na. 100: Wizara ya Madini | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 67 | Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 68 | Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 69 | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 70 | Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 71 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 72 | Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania (TACAF) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 73 | Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki (EASTC) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 74 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 75 | Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 76 | Mamlaka ya Serikali Mtandao | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 77 | Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 78 | Taasisi ya Jiolojia Tanzania (GST) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 79 | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 80 | Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 81 | Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 82 | Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 83 | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 84 | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 85 | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 86 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 87 | Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 88 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 89 | Wakala wa Majengo Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 90 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 91 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 92 | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |

| Na. | Jina la Taasisi/Ripoti | Hati 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 93 | Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 94 | Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 95 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 96 | Wakala wa Huduma za Umeme, Mitambo na Elektroniki Tanzania (TEMESA) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 97 | Chuo cha Maji | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 98 | Wakala wa Vipimo (WMA) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 99 | Mfuko wa UKIMWI | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 100 | Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji (IDF) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 101 | Wizara ya Maji - Mfuko wa Maji wa Taifa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 102 | Mfuko wa Mikopo ya Wafanyakazi Hazina | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 103 | Mfuko wa Pembezoni wa Kilimo (AGITF) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 104 | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 105 | Mfuko wa Maendeleo ya Madini | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 106 | Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 107 | Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 108 | Mfuko wa Usimamizi wa Maafa ya Taifa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 109 | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 110 | Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 111 | Mfuko wa Maendeleo ya Haki za Wazalishaji wa Mimea | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 112 | Bodi ya Mfuko wa Barabara | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 113 | Wizara ya Ujenzi - Akaunti ya Mfuko wa Barabara | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 114 | Mfuko wa Misitu Tanzania | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 115 | Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania (TWPF) | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 116 | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 117 | Ubalozi wa Tanzania Windhoek, Namibia | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi na baadhi ya upungufu |
| 118 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 119 | Ubalozi wa Tanzania – Abuja, Nigeria | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 120 | Ubalozi wa Tanzania – Harare, Zimbabwe | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 121 | Ubalozi wa Tanzania - Kuala Lumpur, Malaysia | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 122 | Ubalozi wa Tanzania - London | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 123 | Ubalozi wa Tanzania - Lusaka, Zambia | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 124 | Ubalozi wa Tanzania - New Delhi, India | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 125 | Ubalozi wa Tanzania – Ottawa, Canada | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 126 | Ubalozi na Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Vienna | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |

| Na. | Jina la Taasisi/Ripoti | Hati 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake 2023/24 | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Bajeti 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 127 | Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa - Geneva | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 128 | Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa - New York | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 129 | Ubalozi wa Tanzania Havana - Cuba | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 130 | Ubalozi wa Tanzania Seoul - Korea | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 131 | Ubalozi wa Tanzania The Hague | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 132 | Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 133 | Ubalozi wa Tanzania Algiers | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 134 | Ubalozi wa Tanzania Ankara | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 135 | Ubalozi wa Tanzania Beijing, China | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 136 | Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 137 | Ubalozi wa Tanzania Brasilia, Brazil | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 138 | Ubalozi wa Tanzania Brussels, Ubelgiji | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 139 | Ubalozi wa Tanzania Bujumbura, Burundi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 140 | Ubalozi wa Tanzania Cairo, Misri | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 141 | Ubalozi wa Tanzania Doha | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 142 | Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 143 | Ubalozi wa Tanzania Jakarta, Indonesia | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 144 | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 145 | Ubalozi wa Tanzania Kuwait | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
| 146 | Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 147 | Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 148 | Ubalozi wa Tanzania Moroni, Komoro | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 149 | Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 150 | Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 151 | Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 152 | Ubalozi wa Tanzania Paris, Ufaransa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya upungufu | Imekidhi |
